

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**Kikao cha Kumi na Saba - Tarehe 3 Julai, 2003**

*(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**HAZI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa Mwaka 2001/2002 (*The Annual Report and Accounts of the Capital Markets and Securities Authority for the year 2001/2002*)

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 160

**Sifa ya Mji**

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA** aliuliza:-

Kwa kuwa baadhi ya Makao Makuu ya Wilaya za Tanzania hayana hadhi ya Mji, mfano Mbinga - Mkoani Ruvuma:-

(a) Je, ni sifa zipi na utaratibu upi ufuatwe ili baadhi ya makazi yenye watu wengi hususan Makao Makuu ya Wilaya na maeneo mengine maarufu ya biashara kama vile Makambako, Wilaya ya Njombe, Mkoa wa Iringa kupewa hadhi ya daraja la Mji unaostahili?

(b) Je, ni mamlaka zipi zinahusika katika kuhakikisha kuwa kila makazi ya watu yenye sifa za kuwa Mji yanapewa hadhi inayostahili kwa wakati muafaka ili kuzuia uharibifu wa mazingira na kulinda afya za wakazi wake?

(c) Je, ni nini faida ya kijiji kupandishwa hadhi kisheria na kuwa mji mdogo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI  
ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mbunge wa Mbinga Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, makazi yenyewe watu wengi hususan Makao Makuu ya Wilaya ili yaweze kupewa hadhi ya kuwa Mji mdogo au Mji, yanapaswa kuwa na sifa mbalimbali kama ifuatavyo:-

Kwanza, ni eneo kufikia vigezo vinavyotambulika mara nyingi inakuwa ni idadi ya watu, uwezo wake kiuchumi na kadhalika na hivyo kupata hadhi ya kuwa Mji.

Pili, ni eneo kuwa kituo chenye shughuli nyingi za kibashara, kiuchumi na viwanda. Tatu, eneo linaloweza kuijendesha lenyewe, katika kutoa huduma za kijamii kama elimu na afya. Nne, eneo kuwa kituo cha utawala na tano eneo kuwa ni Kituo na au makutano ya miundombinu ya usafiri na usafirishaji kama barabara, reli, bandari na kiwanja cha ndege.

Mheshimiwa Spika, utaratibu unaofuatwa ili eneo lenye makazi yenyewe watu wengi kuweza kupata hadhi ya kuwa mji, umeelezwa na kufafanuliwa kwenye Kifungu cha 27 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Namba 7 ya mwaka 1982 na Kifungu cha 5 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Miji) Namba 8 ya mwaka 1982. Kwa mujibu wa sheria hii, maamuzi na utekelezaji wa suala hili hufanywa na Baraza la Madiwani wa Halmashauri husika na kuwasilisha maombi rasmi kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kuititia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Aidha, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, Ofisi yangu inaandaa taratibu na mahitaji yatakayowezesha upangaji wa madaraja ya Halmashauri kwa maana ya Halmashauri za Miji, Manispaa na Jiji.

(b) Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Halmashauri za Wilaya na Miji ndizo zinazohusika kisheria katika kuhakikisha kuwa makazi ya watu yenyewe sifa za kuwa mji yanapewa hadhi ya Mji inayostahili kama vile hadhi ya kuwa Mji Mdogo, Mji, Manispaa au Jiji. Mamlaka nyingine inayohusika ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa ambaye kwa mujibu wa sheria za Serikali za Mitaa anahusishwa katika kuhakikisha sheria na sera zinafuatwa na zinatkelezwa kikamilifu. Hata hivyo, mwaka huu Ofisi yangu inakusudia kama ilivyokwishesha kuyatangaza maeneo kama 88 kuwa Halmashauri za Miji midogo.

(c) Mheshimiwa Spika, faida ya kijiji kupandishwa hadhi kisheria na kuwa Mji Mdogo ni eneo hilo husika kuwa na mabadiliko ya kisheria ya mfumo wa uongozi, utawala, utendaji na uendeshaji wa shughuli za Serikali za Mitaa na kupata huduma za mipango Miji.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Katika baadhi ya Halmashauri pamoja na Wilaya ya Mbinga kuna maeneo ambayo yanatambuliwa na Halmashauri kama Miji Midogo kwa mfano Kigonsera, Maguu, Itembo, *Mambabay* na kadhalika na watu wanaamini hivyo. Nini tofauti ya hiyo Miji Midogo na Mamlaka ya Miji Midogo kwa sababu maeneo hayo tayari vimepimwa na watu wanatozwa kodi kama vile kwenye miji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, tofauti iliyopo kati ya maeneo hayo ambayo yanaitwa Miji Midogo katika maeneo fulani fulani katika Wilaya na haya ambayo nimeeleza hapa kwa maana ya Mamlaka za Miji Midogo ni ya kisheria. Miji Midogo ambayo kule Mbinga mnata Miji Midogo kwa mujibu wa taratibu zetu bado ni vijiji. Kwa hiyo, kuitwa Miji Midogo ni kukosa tu neno zuri ambalo lingeweza kufaa kutumika. Kwa hiyo, kwa kweli kimsingi nadhani taratibu nilizozieleza ndio zinakuwezesha wewe kupata Mji Mdogo, Mji, Manispaa ama Jiji.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Swali la kwanza, hivi sasa Kijiji cha Makambaku kina watu zaidi ya 51,000, katikati ya Nyanda za Juu kina *Railway Siding* na hivi sasa ninavyoongea watu wamejaa kutoka Kenya, Comoro, Kongo, Zambia, Zanzibar lakini ni kijiji. Kwa maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri kina sifa zote za kuwa Mji Mdogo. Kwa kusubiri vijiji hivyo hivyo vilete mapendekezo kupitia Madiwani wao na kwa sababu vijiji hivi ndio chanzo cha fedha kwa Halmashauri ya Wilaya ile kutakuwa na mgawanyiko, kwa hiyo mnachelewesha vijiji hivi kuzidi kuharibika na kuwa na kama Mwanjelwa na baadaye kushindwa kuendesha miji. Je, isingekuwa vizuri mahali pengine uamuza uwe unatoka toka Serikali Kuu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili.

**SPIKA:** Hapana, una swali moja tu. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli sasa hivi Makambaku ni kijiji kikubwa sana lakini kama tulivyoeleza hapa juzi, Makambaku ni moja kati ya vijiji 88 ambavyo Waziri wa Nchi kwa kutumia mamlaka yake ameamua kikitangaza kama Mji Mdogo na kwa kutambua kwamba Halmashauri nyingi zinasita kukubali kuanzisha Miji Midogo katika Halmashauri zake, ndio maana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais ameamua kwamba kila wakati atakapoona inafaa atatumia mamlaka hayo kuanzisha Miji Midogo mahali pote.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa vile Serikali imeazimia kuunda Mamlaka ya Miji Midogo 88 ifikapo Januari mwaka 2004, Bunge lijalo la mwezi Oktoba, Serikali iko tayari kutupa sisi Wabunge na wananchi Waraka

unaoelezea miundo, ikama na hatma za mali inayoondosheka na isiyoondesheka za Halmashauri mama?

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumhakikishia kwamba mara utaratibu utakapokamilika, tutatoa taarifa kwa kila Mamlaka ya Mji tuliyioianzisha ili muweze kuona kama unavyosema muundo, ikama, mali zitakazokuwa zimekwenda kwenye Mamlaka hizo na kwa ujumla mambo mengine yote yanayohusika na uanzishwaji wa Miji Midogo, Miji na mambo mengine. Tutajitahidi ili kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge kuweza kufuatilia kwa karibu zaidi.

Na. 161

### **Wananchi Wanaoishi Mabondeni**

**MHE. PETER KABISA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inawataka wananchi wa Kata za Mzimuni, Kigogo na Magomeni wanaoishi mabondeni wahame kutokana na kero ya mafuriko ya mara kwa mara nyakati za masika na kwa kuwa wananchi wa maeneo hayo kwa upande wake na kwa kulitambua hilo wamegundua kuwepo kwa mifereji ya makalvati kwenye Mto Msimbazi yaliyokuwa yamewekwa kwa lengo la kupitisha maji hivyo wakaamua kuchanga fedha kwa ajili ya kupanua mfereji/mto huo ili maji yaweze kupita bila kusababisha mafuriko na kuwafanya watulie kwenye maeneo yao:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba inalo jukumu la kuunga mkono juhudi za wananchi hao kwa kushirikiana nao kitaalam na katika hali na mali ili waweze kuondoa kero hiyo?

(b) Kwa kuwa wananchi wenyewe wameamua kumaliza kero hiyo ya mafuriko kwa kupanua Mto/mfereji wa kupitisha maji, je, Serikali haioni kwamba kwa sasa isitishe amri ya kuwashamisha wananchi hao na badala yake Serikali na wananchi wa maeneo hayo waendelee na juhudi za kutengeneza kitaalam mfereji huo?

(c) Kwa kuzingatia maelezo ya sehemu a na b ya swali hili, je, kwa nini Serikali sasa isifute amri yake ya kuapeleka wananchi hao Mahakamani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Peter Kabisa, Mbunge wa Kinondoni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji *The Township and Country Planning Ordinance Cap.378* na Mpango kamambe wa Jiji la Dar es Salaam wa mwaka 1978, maeneo ya mabondeni ni maeneo tete (*hazardous*) na hayafai kwa makazi ya binadamu. Kwa hali hii, Serikali haitaunga mkono juhudi zozote za wananchi

kutaka kuendelea kuishi katika maeneo hayo na badala yake wanatakiwa kuyahama maeneo hayo mara moja.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la sehemu (a), maeneo ya mabondeni yaliyopo pale Dar es Salaam ni ya hatari na hayafai kwa kuwa makazi ya binadamu. Kwa sababu hiyo, Serikali haipo tayari kusitisha amri yake ya kuwataka wote wanaoishi mabondeni kuhama kwenye maeneo hayo kwa usalama wao lakini vile vile usalama wa mali zao.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ina jukumu la kuhakikisha usalama wa wananchi wake na kwa kuwa wananchi wanaoishi mabondeni wanahatarisha maisha yao na pia wanakiuka amri halali, Serikali haitafuta azma yake ya kuwapeleka wananchi hao Mahakamani ili kuikoa maisha yao na pia nguvukazi ya Taifa.

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo na ombi.

Mheshimiwa Spika, maeneo niliyoyazungumzia ni maeneo ambayo maji ya mafuriko hayagusi lakini vile vile ni kwamba wahamiaji katika maeneo hayo waliachwa na Serikali bila amri ya kuondoka kwa maana hiyo walidhani wamehamia katika makazi hayo kihalali kwa maana kwamba pamekuwa na makosa mawili kosa la Serikali kuwaacha wakienda maeneo hayo bila kuwaambia wasiende lakini kosa la pili Serikali hiyo hiyo ambayo inadhamira ya kuondoa kero za wananchi haiko tayari kuzungumza na wananchi ili kuwaelimisha. Naomba Serikali iendelee kuwasaidia wananchi kwa kukaa nao ili kuwasaidia kukaa katika maeneo ambayo mafuriko hayafiki.

**SPIKA:** Ni kipindi cha maswali sio maombi lakini Mheshimiwa Waziri amesikia ombi lako. Haya ni maswali ya Dar es Salaam nilimwona Mheshimiwa Dr. Makongoro Mahanga. (*Kicheko*)

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa suala la wakazi wanaoishi mabondeni katika Jiji la Dar es Salaam sio la Jimbo la Kinondoni tu ni karibu Majimbo mengi zikiwepo Kata za Segerea, Vingunguti, Tabata, Buguruni kwenye Jimbo langu la Ukonga, Jangwani, Mchikichini na Upanga Magharibi kwenye Kata za Mheshimiwa Iddi Simba na kwa kuwa wananchi hawa wanaoishi mabondeni sasa hivi wamefikia zaidi ya 200,000 na kujaribu kuwashamisha kutoka kwenye mabonde yale ni ndoto za alinacha...

**SPIKA:** Sasa swali.

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Je, Serikali haioni kwamba ni muda muafaka kubuni mradi madhubuti wa kuwawezesha kuendelea kuishi pale kwa kurekebisha sheria, kufanya *regularization* ili kudhibiti mafuriko kwa sababu suala hili linawezekana?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Jiji la Dar es Salaam lina maeneo mengi ambayo yana mabonde na tofauti ya mabonde haya ni kiwango cha hasara ambayo inajitokeza kila wakati mafuriko yanapotokea. Kwa sasa Serikali haina mpango wowote wa kuanzisha mradi wa aina ambayo Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, anasema na hadi hapo tutakapokuwa tumefikia hapo kwa kweli tutaendelea kuomba wananchi wanaoishi katika mabonde wahame kwa sababu taratibu ndivyo zinavyosema. Jambo hili sio alinacha kwa sababu tayari tunapambana nao Mahakamani, kwa hiyo, kama hapanabudi tutaendelea hivyo ili mradi jambo hili tulifikishe mahali pake.

Na. 162

### **Kuunda Chama Kikuu cha Ushirika - Dodoma**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa Vyama Vikuu vya Ushirika ni muhimu sana na kwa kuwa Mkoa wa Dodoma hakuna Chama Kikuu cha Ushirika baada ya Chama Kikuu cha Ushirika (*CRCU*) kufilisika:-

- (a) Je, ni Vyama vya Ushirika vingapi vinatakiwa ili kuunda Chama Kikuu cha Ushirika?
- (b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba kuundwa kwa Chama Kikuu cha Ushirika kutasaidia sana wakulima wa Mkoa wa Dodoma kupata soko la uhakika la kuuza mazao yao?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, ninapenda kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uundaji wa Vyama vya Ushirika hutegemea nia ya wanachama ambao katika kufanikisha kutekeleza azma yao huamua kwa hiari yao kutatua matatizo yao kwa pamoja. Jukumu la Serikali katika kuwawezesha wananchi wake kupiga vita umaskini kwa kuzingatia dhana ya umoja ni kuwahamasisha ili waunde na au wajunge katika Vyama vya Ushirika kulingana na mahitaji yao.

Aidha, ili kuwedesha hali hii kufanyika kwa kuzingatia taratibu, Serikali imeweka mazingira kwa njia ya sera, sheria na kanuni ambayo huwedesha uendeshaji wa vyombo hivi kwa misingi ya kidemokrasia. Serikali haiwezi kulazimisha kuunda Chama chochote cha Ushirika bila shughuli endelevu ya kufanya.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa napenda kujibu swalii la Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Idadi ya Vyama vya Ushirika vya Msingi vinavyohitajika katika kuunda Chama Kikuu ni Vyama visivyopungua viwili kulingana na Kifungu cha 24(2) cha Sheria ya Ushirika Na.15 ya mwaka 1991 na Marekebisho yake ya mwaka 1997.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana na wazo la Mheshimiwa Mbunge kwamba kuundwa kwa Chama Kikuu cha Ushirika kunaweza kusaidia wakulima wa Mkoa wa Dodoma kupata soko la uhakika la kuuza mazao yao. Hata hivyo, jambo la msingi ambalo Serikali inahimiza ni kwa wakulima kuunda kwanza Vyama imara vya Msingi ambavyo iwapo itahitajika ndivyo vitawezekuamua kuunda Chama Kikuu chenyehu kujimudu kiuchumi na ambacho kitakidhi haja za wanachama wake.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Mkoa wa Dodoma hauna Vyama vya Msingi vya Mazao. Vilivyopo ni vikundi vya uzalishaji ambavyo kimsingi vinaweza kuwa katika hatua ya awali ya kuunda ushirika utakaoweza kusajiliwa endapo vitakidhi vigezo vilivyowekwa katika sheria. Idadi ya kutosha ya wanachama, mitaji imara na uongozi madhubuti ni baadhi ya vigezo muhimu vinavyowezesha kuwa na ushirika imara kuanzia katika ngazi ya msingi, Vyama Vikuu na ngazi nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa kuwa si lazima Chama Kikuu kiwe cha mazao ya kilimo, Mkoa Dodoma unazo fursa nyingi za kuanzisha Vyama vya Msingi vyenye shughuli nyingine kama vile ufugaji, Akiba na Mikopo, kilimo cha zabibu na kadhalika ambavyo hatimaye vinaweza kuungana na kuanzisha Vyama Vikuu kama itabidi.

Mheshimiwa Spika, kwa ufahamisho Mheshimiwa Mbunge, Mkoa wa Dodoma umeonyesha maendeleo mazuri katika kuanzisha na kuendeleza Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo ambapo hadi sasa vipo jumla ya Vyama 47 vinavyofanya kazi zake vizuri sana.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ushirika na Masoko.

(a) Kwa kuwa Chama Kikuu cha Ushirika cha Mkoa wa Dodoma (*CRCU*) kilikuwa na mali kwa mfano magari na majengo, je, baada ya kufilisika mali hizo alikabidhiwa nani?

(b) Kwa kuwa kuna watu waliohusika kufilisi Chama hiki, je, Serikali ilichukua hatua gani kwa watu waliofilisi Chama hiki na kusababisha wananchi wa Mkoa wa Dodoma kukosa mahali pa kuuza mazao yao?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa na uchungu juu ya kufilisika kwa Chama Kikuu cha Ushirika ambacho kilikuwa kinahudumia wakulima wa Mkoa wa Dodoma pamoja na mimi mwenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini suala la mali zilikabidhiwa kwa nani, kwa kweli Chama kilipofilisika maana yake ni kwamba kilikuwa mufilisi kwa hiyo, hakikuwa na mali ya kukabidhiwa kwa mtu mwengine isipokuwa mali zake sasa zilitakiwa ziuzwe ili ziweze kulipia madeni kwa wale wote waliokuwa wanakidai.

Mheshimiwa Mbunge kama anakumbuka nilipokuwa najibu swalii lingine linalofanana na hili kutoka kwa Mheshimiwa Khalid Suru, nilisema kwamba mali za *CRCU* zilikwishauzwa na utaratibu wa kulipa madeni ni kuzingatia vigezo kwamba wanatangulia taasisi za fedha na wadai wengine. Hata hivyo, kuuzwa kwa mali zile hadi sasa bado hazijakidhi madeni yote ambayo *CRCU* ilikuwa inadaiwa.

Mheshimiwa Spika, pili, juu ya watu ambao walifilisi Vyama vya Ushirika hususani *CRCU*, kufilisika kwa *CRCU* kulitokana na sababu nyingi mojawapo ilikuwa ni madeni makubwa ambayo yalikuwa yamelimbikizwa na Benki na hata hivyo baadhi ya watu waliohusika na kufilisi *CRCU*, Serikali inaendelea kuwafuatilia hatua kwa hatua ili waweze kuchukuliwa hatua.

**SPIKA:** Huu ni ushirika Mkoani Dodoma, kwa hiyo, nampa nafasi Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga, Mikoa mingine subirini zamu yenu. (*Kicheko*)

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swalii dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema viko Vyama vya Msingi vya aina nyingine ambavyo vinaweza vikaungana vikawa Chama Kikuu, je, atakubaliana na mimi ni vema sasa Serikali ikaviandalia mazingira ya kuanzishwa Chama Kikuu cha Ushirika?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, napenda nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mazingira niliyoyaelezea kwamba Vyama hivi vya aina nyingine vinaweza kuungana na kuanzisha Chama Kikuu cha Ushirika kwa kadri zinavyohitaji hivyo ndivyo tunavyofanya sasa hivi kuelimisha, kuhamasisha pamoja na kuwaandaa wananchi ili kuanzisha ushirika wa mahitaji yao. Kwa hiyo, Serikali inafanya hivyo.

Na. 163

### **Elimu ya Ushirika**

**MHE. GWASSA A. SEBABILI** aliuliza:-

Kwa kuwa kutohana na kuvunjika kwa Vyama Vikuu nchini mwaka 1972 watumishi wa Idara ya Ushirika wakati huo wengi waliachishwa kazi, kufukuzwa kazi, kustaafu na wengine kujunga na mashirika yasiyo ya Kiserikali au kujajiri wenyewe na kwa kuwa wale wachache waliobaki katika utumishi wameonekana wamechoka na upo uhaba mkubwa sana wa vitendea kazi maofisini na vijiji na kwa kuwa kutohana na mapungufu tajwa hapo juu elimu ya ushirika haijulikani vijiji waliko wakulima ambao pamoja na kughubikwa na bei mbaya ya mazao yao leo wanakabiliwa na udhalimu wa wanunuvi binafsi wa mazao wanaovamia vijiji wakati wa msimu wa mavuno na kuwabana ka bei ndogo zaidi kwa sababu ya kuwa wajinga wa shughuli za ushirika na hivyo wakulima vijiji na hata mijini wamekata tamaa ya kuendeleza kilimo na kukimbilia shughuli za biashara ndogo ndogo ambazo nazo wengi hawana utaalim nazo hivyo wakulima sasa wanababaika:-

Je, Serikali inayo mikakati gani madhubuti na ya makusudi ya kumkomboa mkulima wa Tanzania?

#### **NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gwassa Sebabi, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa mabadiliko kadhaa ambayo yamekuwa yakinke wa kwenye sekta ya ushirika kwa nyakati mbalimbali yakiwemo yale ya kuvunjwa kwa Vyama vya Ushirika mwaka 1976 na siyo 1972 kama alivyokuwa amesema Mheshimiwa Mbunge, yamekuwa ni moja ya vyanzo vya baadhi ya matatizo sugu yaliyoukumba ushirika nchini likiwemo na la elimu duni ya ushirika. Serikali pia inatambua tatizo la upungufu wa watumishi wa Idara ya Ushirika ambalo linatokana na upunguzaji (*retrenchment*) wa watumishi wa Serikali uliofanyika mwaka 1994.

Mheshimiwa Spika, matatizo hayo pamoja na mengine kadhaa yalikwisha bainishwa na Kamati Maalumu ya Rais ya mwaka 2000 juu ya kufufua, kuimarisha na kuendeleza ushirika nchini na kuyawekea mkakati madhubuti wa kuyatatua chini ya mpango maalum wa utekelezaji ambao Wizara yangu inaufutilia na kuutekeleza hatua kwa hatua.

Baadhi ya mikakati iliyopo kwenye mpango huo ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha Vyama vya Ushirika vya Msingi ili kuwawezesha wanachama kumiliki Vyama vyao wao wenyewe.

(ii) Kuongeza mitaji katika Vyama vya Ushirika; mkakati unaolenga kuviwezesha Vyama vya Ushirika kujenga mitaji inayokidhi mahitaji ya Vyama hivyo katika kuwashudumia wanachama wao kiuchumi na kijamii.

(iii) Kuimarisha taasisi za Serikali zinazohusika na maendeleo ya ushirika ambazo ni Idara ya Ushirika, Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika

(COASCO) na Chuo cha Ushirika Moshi ili ziweze kutoa huduma zinazotakiwa kwa ufanisi zaidi.

(iv) Kuimarisha elimu na mafunzo ya ushirika shirikishi kwa wanachama, viongozi na watendaji ambayo ilianzishwa rasmi mwaka 1998 ambayo lengo lake ni kujenga elimu bora ya kufufua, kuimarisha na kuendeleza ushirika ndani ya soko huru.

(v) Kuongeza idadi ya watumishi wa Idara ya Ushirika ili kuimarisha ukaguzi na ushauri juu ya maendeleo ya ushirika.

Mheshimiwa Spika, juhudui zetu sote zinahitajika katika kuhakikisha kuwa wananchi wetu wanajiunga na Vyama vya Ushirika na kushiriki kikamilifu katika kuvitumia na kuvisimamia.

**MHE. GWASSA A. SEBABILITY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kukubali kwamba kuna upungufu wa watumishi nchi nzima kuhusu elimu ya ushirika, kwa kuwa Wilaya ya Ngara ina watumishi wawili tu wanaokaa Ofisi ambao hawana hata usafiri, je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubali kwamba sasa wakati umefika aitumie Wilaya hii watumishi zaidi ili kuendeleza elimu ya ushirika na kupunguza adha ya wanunuzi binafsi kuendelea kuwasumbua wakulima wa kahawa na mazao mengine?

(ii) Kwa kuwa Wilaya ya Ngara ndio inayotoa *organic coffee* na hii imevutia vizuri sana soko la kahawa nchini na kwa kuwa sasa Wilaya ya Ngara inajenga kiwanda cha kukoboa kahawa ili kuweza kuwapa wananchi wake bei nafuu kuliko ilivyo hivi sasa, Mheshimiwa Waziri atakubali kuliambia Bunge lako tatizo la *KCU* kukalia mgao wa wananchi wa wakulima wa Ngara umefikia wapi ili kuwaongeza ari ya kuendeleza zao la kahawa?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza kuhusu watumishi, kama nilivyosema Serikali ilishabaini tatizo la upungufu wa watumishi na nilipokuwa najibu swali lingine linalofanana na hili nilisema tulibaini idadi ambayo itatakiwa kukidhi mahitaji ya sasa hivi ya kuimarisha ushirika nchini ni kiasi cha watumishi 300 na baadhi ya Halmashauri za Wilaya zimeshaanza kuajiri kutegemeana na mahitaji waliyonayo.

Napenda nimshauri Mheshimiwa Mbunge kwa kuitia mamlaka zinazohusika ambazo ni Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Idara Kuu ya Utumishi Serikalini, Halmashauri yake ya Ngara inaweza ikabainisha idadi ya watumishi ambao wanahitajika kwa sababu nafasi hizo zilikwishaombwa na kimsingi Serikali ilikwishakubali.

Mheshimiwa Spika, la pili kuhusu mali za *KCU*, kwanza nipongeze kwamba sasa hivi kule Ngara wanatarajia kujenga kiwanda cha kahawa kukidhi hii *organic coffee*

ambayo inazalishwa kule ni jambo la kupongezwa na ni vizuri sana lakini tatizo la mali za *KCU* nilishawahi kujibu swali hili hapa Bungeni la Mheshimiwa Gwassa Sebabili, nikasema tatizo hili lilikuwa likishughulikiwa na Serikali kwa kulifatilia kwa karibu na nilishalitaarifu Bunge hili kwamba tulikuwa tumeshapeleka timu ya wataalam wetu kwenda kuliangalia kwa karibu zaidi ili kujua mgawanyo huo utakuwaje kwa sababu yamekuwepo mabadiliko ya mara kwa mara kutegemea Vyama vyta Ngara vilivyokuwa vinamilikishwa aidha *KCU* na wakati mwingine vikaenda Biharamulo.

Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba taarifa ya timu yetu inaandaliwa, muda si mrefu tutawasiliana na Mheshimiwa Mbunge ili aweze kuelewa hatua hii inakwendaje.

Na. 164

### **Barabara ya Mkoa Itokayo Utende - Ras Mkumbi**

**MHE. HALIMA O. KIMBAU (k.n.y. MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH)** aliuliza:-

Je, Serikali ina mipango gani ya kuimarisha miundombinu ya barabara hasa ile ya kutoka Utende kupitia Kiegeani, Kitomondo, Kilindoni, Dongo, Ndagoni, Buleni, Kirogwe, Jimbo Kanga, Bweni hadi Ras Mkumbi yenyen urefu wa km 70 ambayo haijafanyiwa matengenezo kwa takribani miaka miwili?

### **NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mbunge wa Mafia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ye Utende - Kilindoni - Ras Mkumbi ni barabara ya Mkoa inahudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mkoa wa Pwani. Barabara hii imekuwa ikifanyiwa matengenezo ya kawaida na ya dharura kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2000/2001, Wizara yangu ilifanya matengenezo ya kawaida na ya dharura kwenye barabara hiyo kwa gharama ya shilingi milioni 12. Mwaka wa fedha 2001/2002, kiasi cha shilingi milioni 18,2 kilitumika kwa ajili ya matengenezo ya kawaida na dharura ya barabara hiyo na katika mwaka wa fedha 2002/2003, Ofisi ya Meneja wa *TANROADS* Pwani kwa kushirikiana na Mhandisi wa Wilaya ya Mafia na uongozi mzima wa Wilaya ya Mafia imeifanyia matengenezo ya kawaida barabara hiyo kwa kutumia kiasi cha shilingi milioni 40.4.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Wizara yangu imepanga kutumia jumla ya shilingi milioni 10.5 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida ya barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kuifanya matengenezo ya kawaida barabara ya Utende - Kilindoni - Ras Mkumbi yeny urefu wa kilometra 70 kadri ya upatikanaji wa fedha ili kuifanya iendelee kupitika muda wote.

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naishukuru Serikali kwa kutumia milioni zote hizo kwa kipindi chote lakini nina swali moja la nyongeza. Matengenezo haya ya kawaida hayawezi kufanyika kikamilifu bila kuwa na vifaa vinavyostahili kutumika wakati wa matengenezo.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, atakubaliana na mimi kwamba sasa umefika wakati wa Wilaya ya Mafia kupata vitendea kazi vya matengenezo ya barabara bila kutegemea vitendea kazi kutoka *TANROADS* Mkoa wa Pwani? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, matatizo yanayotukabili Mafia ni mawili. Moja kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba hakuna mitambo ya kutengenezea barabara. Mbili, molamu iliyopo Mafia haina *standard* ya kuweza kutengeneza barabara ngumu. Kwa hiyo hii inatupa tabu sana.

Je, Mheshimiwa Waziri sasa upo tayari Mafia ipate mitambo yake yenyewe? Mimi ningefurahi sana kuwapa Mafia mitambo kama ningekuwa na uwezo, lakini nadhani uwezo huo upo mikononi mwao wenyewe kupanga na kuangalia jinsi gani ya kuweza kupata mitambo hiyo.

Na.165

### **Barabara ya Mikumi - Kilosa**

**MHE. CHRISTOPHER S.WEGGA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Mikumi - Kilosa inahitaji matengenezo kwa kuwekewa changarawe kwani imeshapita miaka kumi bila matengenezo yoyote hasa ikizingatiwa kwamba ni barabara kuu inayounganisha Wilaya na Wilaya:-

(a) Je, ni lini Serikali itatengeneza barabara hiyo?

(b) Kwa kuwa Serikali ina mipango kabambe ya kuboresha barabara zetu, je, Serikali haioni umuhimu wa kuitengeneza barabara niliyoitaja hapo juu kwa kiwango cha lami ili kuleta maendeleo katika Mikoa na Wilaya kwa ujumla?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Christopher Wegga, Mbunge wa Mikumi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara ya Mikumi - Kilosa yeny urefu wa kilomita 78 ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wizara yangu kuitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Spika, barabara hii imekuwa ikipatiwa matengenezo ya kawaida na ya maeneo korofi (*spot improvement*) kama ifuatavyo:-

Mwaka wa fedha wa 2000/01, Wizara yangu ilitumia jumla ya shilingi milioni 17.1 kuifanya matengenezo ya kawaida na ya maeneo korofi barabara hii. Mwaka 2001/02, imetumia shilingi milioni 14.4 kwa matengenezo ya kawaida na ya maeneo korofi na mwaka wa fedha 2002/03, imetumia shilingi milioni 20 kuifanya matengenezo ya kawaida barabara hii. Barabara hii kwa sasa hali yake ni nzuri na inapitika bila taabu.

(b) Mheshimiwa Spika, katika dhana ya kuleta maendeleo katika Mikoa na Wilaya kwa ujumla, Wizara yangu kwa sasa imeshaanza uchunguzi wa awali kwa kuijenga barabara nzima ya Mikumi - Kilosa - Dumila - Turiani - Mziha - Handeni hadi Korogwe. Tayari awamu ya kwanza ambayo ni upimaji wa awali (*preliminary survey*) imeshafanyika. Hatua inayofuata ni pamoja na kutafuta fedha kwa ajili ya usanifu kamili wa barabara nzima. Aidha, suala la kujengwa kwa kiwango cha lami au la litategemea upembizi yakinifu na usanifu utakaofanyika.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swal la nyongeza. Kwa kuwa barabara hiyo sasa imetambuliwa na Wizara kutokana na jibu hili. Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kupokea shukrani za watu wa Jimbo la Mikumi?

La pili, kwa kuwa zipo barabara ndogo ndefu zeny ngazi ya Wilaya kutoka Kilosa mpaka Mbamba, Ruaha Mbuyuni mpaka Wering'ombe kutoka Ulaya mpaka Malolo. Je, atasaidia kidogo fedha ili ziweze kutengenezeka na hizo barabara ndogo ndogo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, wakati anauliza swal hilo nilinong'ona na mwenzangu hapa Mheshimiwa Mizengo Pinda na yeye akasema katika utaratibu wa kawaida basi atapeleka fedha katika utaratibu huo huo. (*Makofii*)

Na. 166

#### **Mchango wa Kuimarisha Sekta ya Uchukuzi**

**MHE. LEONARD N. DEREFA** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa wadau wa shughuli mbalimbali kama vile wanunuzi wa mazao huchangia maendeleo ya mazao husika na kwa kuwa usalama barabarani kwa hivi sasa ni tatizo kubwa linaloangamiza maisha ya Watanzania na mali zao.

Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuboresha Sheria Na. 30 ya Mwaka 1973 na kuwataka wadau wa sekta ya uchukuzi wakati wa kununua Leseni za Usafirishaji wawe wakichangia asilimia mbili mpaka tano ya thamani ya Leseni kisha fedha hizo ziwekwe katika Mfuko wa Kamati ya Usalama Barabarani na kisha zigawiwe Mikoani ili zisaidie kupambana na tatizo linaloangamiza Watanzania na mali zao?

#### **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Leonard Derefa, Mbunge wa Shinyanga Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usalama Barabarani Na. 30 ya 1973 ilielekeza kuundwa kwa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani na pia ilitoa majukumu kwa Baraza hilo yanayohusu kupambana na ajali za barabarani. Kwa bahati mbaya sheria hiyo haikutoa vianzio mapato vya Baraza. Kwa hiyo, Baraza hili halina vianzio vya mapato vya kisheria vya kuliwezesha kutekeleza majukumu hayo kwa ufanisi. Katika kulitafutia Baraza mapato, Wizara yangu imekasimu madaraka ya kukusanya fedha zitokanazo na ukaguzi wa magari wakati wa kipindi cha maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani kwa Baraza hilo pamoja na Kamati za Usalama Barabarani za Mikoa. Maadhimisho haya hufanyika pote nchini kila mwaka mwezi Septemba. Mwaka huu maadhimisho haya Kitaifa yatafanyika katika Mkoa wa Singida.

Aidha, Baraza na Kamati za Mikoa hukusanya michango ya hiari kutoka kwa wadau mbalimbali. Hata hivyo Wizara yangu inakiri kuwa bado fedha zinazopatikana ni kidogo na haziliwezeshi Baraza kutekeleza majukumu yake ya kutoa elimu kwa umma kupitia Redio, magazeti na *Television* kwa ufanisi. Lengo la elimu hii ni kuongeza uelewa wa jamii kuhusu sheria za barabarani ili kupunguza ajali.

Kwa msingi huu, ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Mbunge kwamba wadau wa sekta ya uchukuzi na usafirishaji wachangie asilimia mbili hadi tano ya thamani ya Leseni zao ni mzuri na Wizara yangu itaufanyia kazi ikishirikiana na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi na wadau wengine kupitia Mamlaka Kuu ya Leseni kwa kuzingatia Sheria ya Usafirishaji Na. 1 ya Mwaka 1973.

Na. 167

#### **Simu Mji Mdogo wa Laela**

**MHE. PONSIANO D. NYAMI (k.n.y. MHE. CHRISANT M. MZINDAKAYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa dunia ina maendeleo makubwa ya kisasa kuhusu mawasiliano katika simu za mdomo na kwa kuwa Laela sasa imefikia hadhi ya kuwa Mji Mdogo:-

Je, Serikali inaweza kuishauri Kampuni ya Simu (*TTCL*) kuanzisha mawasiliano ya simu huko Laela?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu uliofanywa katika Mji Mdogo wa Laela kuhusu biashara ya simu umebaini kwamba Mji Mdogo huo una jumla ya wateja 50 ambaao wanahitaji huduma ya mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Spika, katika awamu ya pili ya mpango wa *TTCL* wa maendeleo wa mwaka 2003/04, Mji Mdogo wa Laela umepangiwa kupata mtambo wa mawasiliano ya simu wa kisasa aina ya digital wenye uwezo wa kuhudumia jumla ya wateja 128. Kasi ya utekelezaji wa mpango huo itategemea mapato ya Kampuni.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa huu Mji wa Laela ni muhimu sana kwa kuwekewa simu kama Mheshimiwa Waziri alivyosema. Je, kwa wakati huu isingekuwa ni rahisi kufunga zile simu zinazoitwa *wireless* ili kusudi angalau wananchi wa pale waweze kupata mawasiliano?

La pili, kwa kuwa Mkoa wa Rukwa unapakana na nchi jirani na vile vile kuna Mikoa mingine kama vile Kigoma, Kagera, Mbeya, Ruvuma, Mtwara na Mara nayo imepakana na nchi jirani na kiusalama Mikoa ya mipakani inapata matatizo makubwa ya wakimbizi au majambazi na vyovoyote itakavyokuwa. Je, isingekuwa vizuri Serikali kuititia *TTCL* ikahakikisha kwamba katika maeneo yote haya ya pembezoni kunawekwa simu ambazo zitawenza kusaidia wananchi pale wanapopata matatizo kutoa taarifa mahali panapohusika?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nakubaliana naye kwamba Mji wa Laela una umuhimu wa kuwekewa simu kama Mji mingine vile vile. Lakini napenda nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba hivi sasa tunachokifanya kule ni kuondoa zile *Absolute Analogy Transmission System* ambazo hazifanyi kazi na za miaka mingi ziwekwe nyingine mpya ndiyo tuweze kuweka hiyo mitambo mingine ikiwemo na ya Namanyere. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pili, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kuititia Kampuni ya Simu tunayo malengo ya kuona mipakani kote tunaweka simu ili ziweze kusaidia kiusalama na pia kusaidia mahitaji ya wananchi wa sehemu hizo. (*Makofii*)

Na. 168

**Mahitaji ya Umeme - Wilayani Sengerema**

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA (k.n.y. MHE. DR. JAMES M. WANYANCH) aliuliza:-**

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais alipotembelea Mji wa Mugumu Wilayani Serengeti Oktoba, 2000 aliahidi kuwa Mji huo utapatiwa umeme kabla ya mwaka 2005 na kwa kuwa Shirika la SIDA limeshatoa fedha kwa ajili ya kazi hiyo bado haijaanza:-

(a) Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kupeleka umeme kwenye Mji huo Wilayani Serengeti?

(b) Je, ni lini kazi ya kupeleka umeme katika Wilaya hiyo itaanza na itachukua muda gani kukamilika?

(c) Je, ni Vijiji gani vitakavyopatiwa umeme katika awamu ya kwanza?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mbunge wa Serengeti, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tayari Serikali imekwishaanza kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya Mwaka 2002. Serikali ilitia saini makubaliano na Serikali ya Sweden ya kupata fedha za kutekeleza mradi wa kupeleka umeme Mji wa Mugumu Wilayani Serengeti. Sasa hivi mshauri wa kitaalam wa mradi (*Consultant*) wa Kampuni ya SWECO International AB anajiandaa kuanza kazi kwa ajili ya awamu ya kwanza ya mradi. Inategemewa kwamba kabla ya mwisho wa mwezi Julai, 2003 kazi hii itakuwa imeanza ambapo ni pamoja na kuandaa na kutangaza zabuni za kupata Mkandarasi wa kufanya kazi za ujenzi wa mifumo ya umeme ikiwemo laini ya umeme kutokea kitu cha umeme cha Bunda hadi Mji wa Mugumu na vitongoji vyake.

(b) Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza ambayo inahusu Mshauri wa kitaalam kama nilivyosema awali, inatarajiwa kuchukua muda usiozidi miezi sita. Hivyo inatarajiwa kwamba kama hapatakuwa na kasoro zitakazojitokeza basi kazi ya ujenzi wa mifumo ya umeme ikiwemo laini ya kilovolti 33 itaanza mwezi Desemba, 2003 yaani mwishoni mwa mwaka huu.

(c) Mheshimiwa Spika, inategemewa kuwa Vijiji vifuatavyo vitapatiwa umeme katika awamu hii ya kwanza navyo ni Ingamba, Kisangura, Nyakibere, Bushera, Kawangala, Mugeta, Nyabisingisi, Motukeri, Nyichoka, Fort Ikoma, Isenye, Nata, Tabora B na Rung'abure.

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa kukosekana kwa umeme katika Mji wa Mugumu, Makao Makuu ya Wilaya ya Serengeti kunachelewesha sana maendeleo ya Mji huu ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya kwa muda mrefu na kwa sababu Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba katika kipindi hiki cha 2000-2005 umeme utakuwa umepatikana Serengeti. Je, Waziri anaweza kutoa tamko kwamba ahadi hii ya Rais itatekelezwa katika kipindi hiki cha 2000-2005?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi fedha zimepatikana, kazi imeshaanza kwa maana ya kumpata *consultant* na napenda nirudie kusema kwamba kama ambavyo Mheshimiwa Rais alivyowaahidi wananchi wa Serengeti umeme utapatikana kabla ya mwaka 2005 kama hakutajitokeza kasoro ambazo zipo nje ya uwezo wa Serikali na uwezo wa kibinadamu kwa ujumla. Lakini ahadi hii ipo na imeshaanza kutekelezwa katika muda huu ambao imeahidiwa. (*Makofit*)

Na. 169

### **Uchumi wa Tanzania na Sekta ya Madini**

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI** aliuliza:-

Kwa kuwa uchumi wa Tanzania kwa kiwango kikubwa unategemea sekta ya madini:-

(a) Je, ni kiasi gani cha Dhahabu, Almasi, *Green Garnet* na *Tanzanite* kimezalishwa kwa mwaka 2001/2002?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kimepatikana kwa mauzo ya madini yaliyotajwa kwenye sehemu (a) ya swali hili kwa mwaka 2001/2002?

(c) Je, ni kwa nini takwimu za sekta hiyo muhimu kiuchumi haziwasilishwi Bungeni na kujadiliwa au kuletwa kama taarifa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Major Jesse Makundi*, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kiasi cha madini ya Dhahabu, Almasi, *Green Garnet* na *Tanzanite* kilichozaalishwa kwa mwaka 2001/02 ni kama ifuatavyo:-

Dhahabu mwaka 2001 ni tani 29.5, mwaka 2002 tani 43.3. Almasi karati 254,271 mwaka 2001 na mwaka 2002 ni karati laki 239.7. *Green Garnet* ni kilo 523.7 mwaka 2001 na mwaka 2002 ni kilo 785. *Tanzanite* ni 5,473 kwa mwaka 2001 na mwaka 2002 ni 6,460. Orodha hii ambayo ina takwimu zingine ninayo na Mheshimiwa Mbunge atapatiwa baada ya kujibu swali hili.

(b) Mheshimiwa Spika, jumla ya fedha zilizopatikana kutokana na mauzo ya madini hayo ni dola za Kimarekani milioni 308.87 kwa mwaka 2001 na dola milioni 458.28 kwa mwaka 2002. Kwa mujibu wa takwimu kutoka Benki Kuu ya Tanzania na takwimu ambazo na sisi tunazo, hivi sasa sekta ya madini inachangia asilimia 2.8 ya Pato la Taifa.

(c) Mheshimiwa Spika, takwimu zimekuwa zikiwasilishwa hapa Bungeni kila mwaka kama kiambatanisho cha hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nishati na Madini na kwa maana hiyo basi kuambatanishwa huko kunatoa fursa kwa Waheshimiwa Wabunge kuweza kujadili takwimu hizi na kujadili suala zima hili.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Mwenyezi Mungu ameipa Tanzania utajiriwa madini kama alivyozipa nchi zingine utajiri wa mafuta. Je, Serikali inadhibitije utajiri huu wa madini na kuona kwamba hayatoki nje bila urasimu na kwamba kila kinachopatikana kwenye machimbo hayo kinakuwa ni halali na kamili kwa ajili ya matumizi ya Tanzania hii? (*Makofi*)

La pili, kwa kuwa Rais amewateua viongozi wa ngazi za juu sana katika Kampuni ya Meremeta kuongoza Kampuni hii je, kama kukitokea tatizo lolote au ubovu wowote nani atamnyooshea mwingine kidole? (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu udhibiti wa madini. Suala zima la uchimbaji wa madini na biashara ya madini unatawaliwa na Sheria ya Madini ya mwaka 1998 na taratibu za madini za mwaka 1999 pamoa na sheria mbalimbali zinazohusu uchimbaji na biashara na hasa biashara ya madini kwa maana ya kodi mbalimbali ambazo ni sheria za nchi yetu.

Kupitia sheria hii na kupitia usimamizi wa Wizara ya Nishati na Madini na usimamizi wa Wizara ya Fedha inategemea na sekta yenyewe kama inahusu mambo ya fedha na kadhalika, upo udhibiti wa madini yetu yanayochimbwa katika sehemu mbalimbali. Wakati Mheshimiwa Waziri wa Fedha anatoa hotuba yake hapa halafu ikarejewa pia wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anatoa hotuba yake hapa ilielezwa baadhi ya mipango ya kuendeleza udhibiti wa suala hili la madini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge hakutaja ni madini gani katika yale ambayo tumeyajibu hapa si rahisi kuanza kueleza katika kila aina ya madini udhibiti mahsusuna unaofanyika.

Lakini ningependa nichukue nafasi hii nitoe mfano wa *Tanzanite* ambao Serikali imechukua hatua madhubuti kabisa na kulitangaza lile eneo la Mererani kama ni *controlled area* ukawekwa mfumo maalum wa kuhakikisha kwamba uchimbaji wa madini unaendeshwa katika utaratibu ambao utakuja kuipatia faida kubwa nchi yetu. Hata katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha alitaja pia mwelekeo wa

Serikali wa jinsi ya kushughulikia *Tanzanite* hapa nchini. Sasa hii ni aina ya mifano ambayo tunaweza tukaitoa katika suala zima la udhibiti wa madini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, kwamba Mheshimiwa Rais ameteua viongozi wa ngazi za juu na kwamba pakitokea tatizo nani atamnyooshea mwagine kidole. Jibu lake ni jepesi aliyeteua ndiye ambaye anaweza kuchukua hatua zozote. Hakuna mtu ambaye ana uwezo wa kiutawala mkubwa zaidi kuliko yehe Mheshimiwa Rais ambaye ameteua. (*Makofî*)

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wachimbaji wakubwa kama wa *Kahama Gold Mine* wamemilikishwa asilimia mia moja na Serikali kutochukua hisa hatu moja je, Serikali haioni kwamba Mikataba kama hii ni kuwadhulumu Watanzania na je, ina mpango wa kubadilisha hiyo Mikataba? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda ieleweke kwamba suala la uchimbaji madini katika nchi yetu linahusisha wachimbaji wakubwa na wadogo wadogo. Hii ndiyo sera ya Serikali inayotokana na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Sasa inawezekana kuna Vyama ambavyo hii siyo sera yao lakini kwa upande wa Serikali hii ndiyo sera tunayoitekeleza. Kuhusu suala la Mikataba nilizungumza hapa wiki iliyopita kuhusu masuala ya Mikataba na nadhani Mheshimiwa Mbunge pengine asubiri tu wakati tutakapotoa hotuba yetu ya bajeti tunaweza tukalielezea zaidi suala hili la madini. (*Makofî*)

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kupitia vyombo vya habari tunesikia kwamba kampuni moja ya *Jay Pool* ambayo inashughulika na madini ya *Tanzanite* imeandikia Serikali barua kwamba mpango huu tulipitisha juzi juzi isitishe, ule mpango wa kuchonga madini hapa hapa nchini hasa hiyo *Tanzanite*. Tunesikia habari hiyo na sisi tulipitisha bajeti hapa juzi kukubali kwamba ni vema na tunaunga Serikali mkono kwamba uchongajji ufanyike hapa na ni ajira kwa watu wetu. Sasa wale wanasesma tukifanya hivyo ni mbaya kwa sababu tunaaua ajira kwa watu wao.

Swali, je, Serikali kweli imepata barua hiyo na kama imepata barua hiyo itapingana na uamuzi wa Bunge au itatii uamuzi wa Bunge ambao umeshapita hapa? (*Makofî*)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tumepata barua kutoka kwa *Jewellers Association* wa *Jay Pool* huko India ambao ndiyo wachorongaji wakubwa wa *Tanzanite* hapa duniani. Wana wasiwasi kwamba hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ambayo ilikuwa kwa Kiswahili lakini kwa Kiingereza ilipotafsiriwa kwenye magazeti ilikuwa na maana kwamba uuzaji wa *Tanzanite* iliyochorongwa utasitishwa

mara moja. *In fact* kwenye magazeti wao wanasesma tarehe moja Julai, ambapo kwa kweli Waziri alisema: “Serikali ya Tanzania au Tanzania itasitisha uuzaji wa *raw Tanzanite* kwa muda siyo tarehe moja Julai. (*Kicheko*)

Nadhani ndivyo na Waziri wa Fedha yupo, natumaini haikusemwa kwamba tarehe 1 Julai, ndiyo itasitishwa. Tumewajibu kwa kuwaambia kwamba hiyo ndiyo azma na ndiyo sera ya Serikali katika kuongeza *value* ya mazao yetu siyo madini na korosho na kila kitu. Nia yetu ni kuongeza *value* ili tuweze kuuza mazao ambayo yanatuongezea fedha za kigeni na ajira hapa hapa nchini.

Kwa hiyo, tutajiandaa tupate wawekezaji na tumewaandikia tukawaambia wawekezaji wowote kutoka India au popote pale na wa hapa Tanzania wenyе nia ya kuingia kwenye biashara hiyo Serikali itawapa vivutio vyote vile ambavyo tunatoa kwenye sekta nyininge za madini.

Mheshimiwa Spika, katika uwekezaji hasa huu amba ni wa fedha nyingi kama Serikali isipotoa kauli ambazo zina uhakika mnaanza ku-disturb *the fiscal regime* ambayo ipo na watu wanaanza kuwa na wasiwasi kwamba hii nchi unawekeza leo, kesho wanabadilisha au wanavuruga. Kwa hiyo, tumewahamasisha waje wawekeze na wachonge hapa nchini, halafu tuuze *Tanzanite* ambayo imechongwa na yenye thamani kubwa ili tusipate hasara kama tulivyokuwa tukiipata siku za nyuma. (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kuongezea tu kwa majibu mazuri kabisa ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Serikali haina utaratibu wa kutii barua ambazo zinatoka nje kwa hatua hizi na hizo barua. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu ahsante sana na hiyo ndiyo imetufikisha mwisho wa kipindi cha maswali. Sasa kuna tangazo moja la Kikao cha Kamati. Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii wakutane leo tarehe 3 Julai, 2003 kwenye Ukumbi wa mikutano chumba namba 56 kuanzia saa 4.30 asubuhi, Kamati ya Huduma za Jamii.

Baada ya tangazo hilo, napenda kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge yafuatayo, moja, kwa kuwa *weekend* hii itakuwa ndefu ni vizuri mkajua mapema ili muweze kujipangia utawala binafsi utakavyokuwa. Ninachotaka kueleza ni kwamba Semina iliyopangwa kufanyika siku ya Jumamosi ingedhaminiwa na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi wameahirisha, wenyewe wamesema hawajawa tayari. Kwa hiyo, mnawenza kupanga utawala binafsi kuanzia Jumamosi, Jumapili na Jumatatu. Kwa sababu siku ya Jumatatu ndiyo Sabasaba yenyewe. Kwa hiyo, Semina ya Jumamosi haitakuwepo.

La pili, nifikishe salaam za mgeni wetu wa jana Mheshimiwa Rais wa Malawi, Dr. Bakili Muluzi, anasema nifikishe ujumbe Bungeni kwamba alifurahishwa sana na mapokezi, alifurahishwa sana na umakini wa Waheshimiwa Wabunge katika kumsikiliza yeye. Aliniomba nifikishe salaam hizo na sasa nimezifikasiha. (*Makofi*)

## HOJA ZA SERIKALI

### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2003/2004 Wizara ya Ujenzi**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. SAMWEL M. CHITALILO:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

**SPIKA:** Endelea tu *Hansard* inakusikia.

**MHE. SAMWEL M. CHITALILO:** Vile vile mimi binafsi napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa na kuingia Bungeni hapa kwa kupitia Vyama mbalimbali. (*Makofi*)

Vile vile napenda kutoa shukrani zangu za pekee kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, pamoja na Naibu Waziri wake na watumishi wote akiwemo Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa pekee vilevile napenda kuishukuru Wizara ya Ujenzi kwa kuona umuhimu wa kutengeneza barabara ya kutoka Dodoma hadi huko sasa karibu na Mwanza na sehemu zingine kwa kiwango cha lami. (*Makofi*)

Vile vile napenda kuishukuru Wizara ya Ujenzi kwa mwaka 2002 na mwaka 2001 kwa kuona umuhimu wa barabara za Jimbo la Buchosa, ambazo ziliwa hazijatengenezwa zaidi ya miaka ya 30. Lakini kwa kiwango kikubwa sasa barabara hizo zimetengenezwa kwa kiwango cha changarawe, barabara ya kuanzia Luchiri kwenda Bukokwa na kutoka Bukokwa hadi Nyehunge na Nyehunge hadi Isaka. Natumaini kwamba kipindi hiki kidogo kilichobaki cha Isaka hadi Kaunda kitakuwa kimemalizika ndani ya muda mfupi, ninayo imani hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani zangu, lakini bado ninawasilisha kilio changu kikubwa cha barabara ya kutokea Nyakalilo kwenda Lushamba yenyе urefu wa kilomita 32, ni kwamba barabara hii zaidi ya miaka 35 sasa haipitiki kabisa, wananchi wa Buchosa wanapita kwa baiskeli na akinamama wanaokwenda hospitali kwa ajili ya kujifungua, wanajifungulia njiani au aidha, wanakufa kabla ya kufika kwenye hospitali. Barabara hii kwanza ni barabara muhimu ya uchumi ndani ya Jimbo la Buchosa na kwa Mkoa mzima wa Mwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, barabara hii napenda kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba ilikuwa imesahaulika. Kwanza ilikuwa imepelekwa Mkoani kwamba itatengenezwa na Mkoa wa Mwanza, lakini ghafla mwaka 2002 au mwaka 2001 ikawa imeamuliwa kwamba barabara hii ni ya Wilaya. Kwa sababu ilikuwa imesahaulika kwa muda mrefu

ni kwamba uwezo wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema haitaweza kabisa kuitengeneza barabara ile na gharama yake ni zaidi ya milioni mia mbili na kitu kwa hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu bahati nzuri yuko hapa mwaka 2000 wakati ule wa uchaguzi. Ahadi ya kwanza ilikuwa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba barabara ile itatengenezwa mara moja tu baada ya Chama Tawala cha CCM kushinda. Vile vile alikuja Mheshimiwa Rais baada ya muda mfupi, wakati ule ule wa mwaka 2000, akatoa ahadi kwenye barabara ile ile itokayo Nyakalilo kwenda Lushamba yenyeki kilomita 32 kwamba itatengenezwa haraka sana iwezekanavyo.

Baada ya uchaguzi kumalizika, alikuja Mheshimiwa Waziri Mkuu tukawa naye katika kijiji cha Bukokwa akaahidi kwamba barabara ile itatengenezwa haraka iwezekanavyo. Kwa hiyo, matumaini ya wananchi wa Buchosa ni matumaini kwa Mheshimiwa Rais wao na Mheshimiwa Waziri Mkuu wao, lakini hivi sasa barabara hii bado haijatengenezwa na bado sioni kama ipo kwenye mkakati wa kuitengeneza.

Mheshimiwa Spika, vile vile Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa John Magufuli, alipofika kwenye *Road Board* ile ya Mkoa wa Mwanza aliwambia na kuwaagiza wajumbe watokao Halmashauri ya Sengerema kwamba wamwandikie *write up*, waandike mchanganuo vizuri kabisa na wampelekee ili aweze kuishughulikia barabara hiyo mapema. Lakini cha ajabu mchanganuo umeandikwa na ukapelekwa, baadaye tena Wizara ya Ujenzi ikarudisha mchanganuo huo kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema. Wakisema kwamba barabara ile ni ya Halmashauri siyo ya Mkoa. Lakini kwa kipindi kirefu ilikuwa inaeleweka kwamba ni barabara ya Mkoa.

Sasa *special request* yangu hapa ni kwamba izingatiwe ahadi ya Mheshimiwa Rais na ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba barabara hii itengenezwe mapema iwezekanavyo. Ninaona kwamba wananchi wa Buchosa hivi sasa kama kuna watu wengine wanakuwa na maadui huko pembeni basi na mimi mnanijengea uadui ndani ya wananchi wangu wanaonipenda na walionipa kura. Naomba barabara hii itengenezwe haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Sawa.

**MHE. SAMWEL M. CHITALILO:** Mheshimiwa Spika, sipendi kurudia rudia nimetumwa na wananchi wa Buchosa na wenyewe wanisikie kabisa kwamba mimi sasa nimefikisha mawazo haya. Kama ahadi za Mheshimiwa Rais, unazitengua wewe, waambie wewe, siyo mimi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sina mengine zaidi. Naunga mkono hoja hii asilimia mia moja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Lakini Mheshimiwa Mbunge, kwa siku zijazo kumbuka kuzungumza na Spika siyo kuzungumza na Waziri moja kwa moja.

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia katika hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, mimi niungane na wenzangu wote walioipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri inazozifanya na kwa kweli sote tunazona na katika hilo hakuna ubishi ni kwamba Wizara inafanya kazi vizuri na kwa kweli niipongeze Serikali kwa ujumla kwa sababu hasa tulipoanza kuweka vipaumbele katika sekta mbalimbali mafanikio yanaanza kuonekana katika Wizara zote zile ambazo tumeziweka kuwa Wizara za vipaumbele. Nadhani katika kila Wizara moja moja tunaweza tukaonyesha kitu kinachofanyika kwa kukiona na kwa kukigusa. Kwa hiyo, naungana na wenzangu kuipongeza Serikali sana. Awali kabisa nipende kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mimi nitapenda niongelee mambo mawili tu kama muda utaniruhusu. La kwanza, niungane kabisa na Kamati ya Miundombinu iliyotoa taarifa yake hapa jana na kwa kweli niwapongeze wajumbe wote wa Kamati ya Miundombinu wakiongozwa na Mwenyekiti wao Profesa Henry Mgombelo.

Mimi si Mjumbe wa Kamati hiyo. Lakini kwa kweli nime-share na wao wazo moja kwamba kuna haja ya kuangalia upya uendeshaji wa barabara zetu katika nchi hii. Kwa maana ya kumkabidhi nani hasa azitengeneze barabara kwa pamoja. Ninaungana na Kamati ya Miundombinu katika ukurasa wa 10 kipengele cha 5.9.2 kwamba sasa tuangalie uwezekano ama tunampa *TANROADS* barabara zote aziendeshe mpaka kule vijijini au tuangalie ni jinsi gani tufanye ili tumpe mtu mmoja azifanye kwa uzuri na standard inayokubalika nchi nzima. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tunaona barabara zile ambazo ziko mikononi mwa *TANROADS* kwa kweli zinakuwa barabara nzuri. Lakini barabara zile ambazo kwa kweli ziko katika Mamlaka zingine ubora wake unakuwa kwa kweli si nzuri sana na hii nafikiri tulipewa majibu juzi hapa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwamba Halmashauri zetu nyingi hazina wataalam.

Kwa hiyo, tuliangalie hilo na tulifanyie kazi. Tuangalie uwezekano wa kuipa *TANROADS* barabara zote hizi. Ama wale Wahandisi wetu walioko katika Halmashauri basi wawe ni sehemu ya *TANROADS* katika ngazi ya Wilaya. Nilitaka ni-share na Kamati ya Miundombinu kuhusu wazo hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni juu ya upandishaji wa hadhi wa barabara zetu nchini. Kwa sababu barabara zetu zina madaraja, kuna hadhi ya Wilaya, kuna hadhi ya Mkoa na kuna hadhi ya Kitaifa. Kama hatufanyi hilo la kwanza basi tuangalie utaratibu wa upandishaji wa hizi barabara. Sisi katika Mkoa wa Shinyanga tumeshapeleka mapendekezo ya barabara zetu nyingi sana kupandisha hadhi kwa sababu zinakidhi vigezo vile na zipo nyingi sana. Barabara ambazo zimekidhi vigezo vyote vya kupandishwa hadhi kutoka katika Halmashauri kwenda katika ile ngazi ya Mkoa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini jibu tulilonalo katika kikao chetu cha *Road Board* cha Mkoa ni kwamba inahitajika sheria ipitiwe upya. Sasa ni mwaka juzi sijui sheria kupitiwa upya inachukua muda gani. Lakini hili lisipofanyiwa kazi vizuri nafikiri litatuchelewesha kuleta maendeleo ya nchi hii. Kuna barabara ambazo kwa kweli zina umuhimu wa pekee na zina sababu mahsus. Nitatoa mfano wa barabara moja au mbili.

Kuna barabara hii ya Nyang'hwale, Chelajomu, hii ni barabara ambayo kwa kweli ikiwekwa vizuri itaimarisha uchumi wa Mkoa na kwa bahati nzuri au kwa sababu nyingine kwa upande wa Mkoa wa Mwanza wana barabara ya Mkoa inayotoka nafikiri Busisi inakuja kuishi Nyakologo mpakani, halafu kunakoendelea inakuwa ni barabara ya Halmashauri ambayo si nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nasisitiza kwamba kuwepo basi uwiano wa mitandao hii ya Kimkoa. Unakuwa na mtandao wa Mkoa, unakwenda kuishia mpakani mwa Mkoa, halafu kunakoendelea hakuna barabara ya Mkoa, tuliziweka barabara hizi kwa sababu mbalimbali kwa kuzingatia vigezo. Sasa sijui inachukua muda gani kuirekebisha hii sheria ili hizi barabara ziweze kupandishwa hadhi na ziweze kufanyiwa kazi. Ningependa tuambiwe kwamba sheria italetwa hapa lini, na sisi tuko hapa kwa ajili ya kuzirekebisha sheria na kuzitunga kwa manufaa ya wananchi siyo kwa manufaa yetu. Kwa hiyo, nashauri kabisa kwamba kama tatizo ni sheria basi iletwe haraka ili kwamba hizo barabara ziweze kupandishwa hadhi.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya mwaka huu sijaona popote ile *terminology* ambayo tulikuwa tukiitumia siku za nyuma ya *BOT*, kujenga barabara ku-*operate* na baadaye kuhamisha *build operate and transfer*. Sasa sijui imekwama wapi na tatizo ni nini, hakuna watu wanaojitolea kufanya hizi kazi jamani.

Mheshimiwa Spika, mimi nilitaka nilizungumzie hili kwa sababu nilikuwa na hoja ambayo nataka niilete hapa kuhusu ujenzi na utumiaji wa barabara. Kule Jimboni kwangu kuna barabara moja inatoka Busoka, Sengese, Kakola inaelekea mpaka Geita, na hii barabara hadhi yake haijulikanijulikani. Hii barabara si ya Wilaya, si Mkoa na si ya Taifa, ipo ipo tu, hata ukarabati wake unabaki haueleweki, nani anaitengeneza.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna mtumiaji mmoja au wawili wakubwa sana wanaitumia hii barabara hii. Sisi katika *Road Board* kule Shinyanga tulipokaa tukasema tuwashawishi hawa wenzetu waiweke katika hadhi inayokubalika ili waitengeneza kwa kiwango cha lami na mimi naamini kuna uwezo wa kufanya hivyo, tumewashawishi lakini nasikitika kusema walikataa kata kata, wakasema si kazi yetu kuitengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kweli barabara ile imekuwa kero kwa wananchi wangu wa vijiji vyote nilivyovitaja kwa sababu mbili au tatu. Ile barabara imekuwa na msongamano wa magari na malori, kila aina ya magari, makatapila na takataka zote zinazosafiri kwenye barabara. Wananchi wangu wote wa vijiji vile kuanzia Busoka, Tombo, Sengese, Runguya, Kakola, Bugarama wanakabiliwa na wimbi la vumbi kila

siku. Sasa sijui nilikuwa najaribu kufanya utafiti na Daktari wangu wa Wilaya kuona kama hakuna ongezeko la maradhi yanayosababishwa na vumbi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kilichonifanya nitaje uwezekano wa kuendelea na huu mtindo wa *BOT* ni sababu hii. Ninaamini kabisa kuwa uwezo wa kuitengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami na ninashangaa sheria zetu zinatwambia, kwa mfano, barabara ile haina hadhi ya Taifa, haina hadhi ya Mkoa na haina hadhi ya Halmashauri, sheria zinasema kwamba barabara za aina ile uzito uwe tani 10 na kurudi chini. Lakini malori yanayopita katika barabara ile ni ya tani 40, tani 50. Ile barabara inapoharibika yale malori yanaweza kuhimili kupita kwenye njia mbovu kama ile, lakini magari yetu madogo madogo yanayowabeba akinamama na Mheshimiwa Mbunge yanapata shida kweli kupita katika barabara ile. Sasa hakuna muda maalum uliowekwa kwa ajili ya kuikarabati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla waangalie uwezekano na ni uwezekano wa kimsingi kwamba hiyo barabara itengenezwe kwa kiwango cha lami na wanaweza. Nitatoa mfano yaliyowezekana katika mtindo wa *BOT*, katika Wizara zingine, labda tutachukua uzoefu katika Wizara ya Nishati na Madini, wale watu waliweza kujenga hii grid ya umeme kutoka Shinyanga mpaka kule wanakofanya kazi kwa makubaliano. Wamekubaliana na Wizara ama *TANESCO* kwamba katika matumizi ya umeme huo basi watakuwa wanapunguziwa bei ili kufidia gharama walizotengeneza gridi hiyo kwenda kule kwenye mgodi wao. Pia sijui Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kama na wenyewe walifanya hivyo, lakini hawa watu wameweza kujenga Kituo cha Polisi kikubwa sijui kwa matumizi gani. Lakini nafikiri ni kwa matumizi ya kulinda mali zao, lakini kwa mtindo huo wameweza kujenga, sasa wanatumia barabara hii.

Mheshimiwa Spika, mimi nasema kwanza wanaitumia barabara hii kinyume cha sheria kwa sababu ile barabara mimi naamini inatakiwa ipitishe magari ya tani 10 mwisho, lakini wanapitisha magari yenye tani 40. Kwa nini Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi usiwashawishi waitengeneze barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Wananchi wanapata kero kubwa sana ya vumbi, siku moja njoo nikakutembezi. Unapita msululu wa malori 15 vumbi lake ni wimbi kuliko wimbi la mvua.

Mheshimiwa Waziri, naomba sana na ninataka niseme hili ni la mwisho na ninaomba lisikike kwa wananchi wangu kwamba barabara hii itengenezwe kwa kiwango cha lami kuna uwezo mkubwa. Angalau wakiondoka watuachie barabara ya lami, kwa sababu mambo ya madini yamezungumzwa hapa, mimi sikuyazungumzia. Lakini angalau basi wakiondoka watuachie barabara yenye lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii tena. (*Makofi*)

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote ningependa kuipongeza Wizara ya Ujenzi kwa kazi nzuri iliyofanya na hasa naipongeza Serikali ikipitia Wizara hii kwa miradi mikubwa ambayo imetekelizwa na ambayo inatarajiwa kutekelezwa katika kipindi kijacho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napongeza sana mafanikio makubwa tuliyopata katika ujenzi wa daraja la Rufiji, daraja ambalo kwa muda mrefu ilikuwa kama kitendawili. Naamini wenzetu watu wa Kusini kutokana na ujenzi wa daraja hili umaskini utapungua na uchumi wao utakua kama Mwenyezi Mungu alivyowajalia kuwa na maeneo yenyе rutuba nzuri. (*Makofī*)

Mheshimiwa Spika, nichukue tena nafasi hii kuipongeza Wizara ya Ujenzi kwa ule mpango wa barabara ambazo zitatuwezesha sisi watu wa Pwani kuweza kusafiri kwa barabara kufika Dodoma, Singida na kwa watani zetu Tabora na Mwanza. Nadhani sasa usafiri wa treni utakuwa siyo usafiri peke yake. (*Makofī*)

Mheshimiwa Spika, hapo hapo Wizara ya Ujenzi imetusaidia sana akinamama kwa kuhakikisha Wakandarasi wanawaajiri wanawake wenzetu. Namshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake na watendaji wake kwa kutilia mkazo hilo la kuajiri akinamama na kweli akinamama wanafanya kazi nzuri kama inavyojitokeza. (*Makofī*)

Mheshimiwa Spika, mimi kwa kweli leo nimesimama hasa kuleta salaam za wana Dar es Salaam hususan wananchi wa Kigamboni. Wananchi wa Dar es Salaam wanasema Jiji limekua na Kigamboni ya miaka 60 ambayo ilikuwa ikitumia *ferry boat* (Pantoni) sasa kwa kweli imepitwa na wakati. (*Makofī*)

Mheshimiwa Spika, mimi nilitegemea katika *speech* ya Mheshimiwa Waziri kungekuwa angalau na kipengele chochote kinachozungumzia utaratibu wa kufikiria kujengewa daraja pale Magogoni, daraja ambalo litaondoa matumizi ya kutumia vivuko. Kwa hali ilivyo sasa hivi vivuko vilivyokuwepo yaani kivuko cha Alina na kivuko cha Kigamboni ni vivuko ambavyo havina hali nzuri. Unaweza ukapanda kivuko wakati mwingine kikafika katikati kikasimama, kwa wale ambao hawakielewi vizuri wanaanza kutaharaki pale, lakini kwa kweli hali siyo nzuri. Ni kweli Serikali imejithidi imejenga mandhari nzuri, pande zote mbili ukienda utashangaa. Kuna hali nzuri sana katika zile sehemu za kukata tiketi, kwa kweli *infrastructure* yake pale ni nzuri sana. Lakini hatari kubwa iko katika vile vivuko. Kivuko ambacho ndiyo kikubwa zaidi cha Kigamboni sasa kimeanza nacho kuharibika na kinapakia watu wengi, magari mazito, kwa hiyo Serikali ilifikirie hilo. (*Makofī*)

Mheshimiwa Spika, Kigamboni sasa hivi kutokana na sensa ya mwaka 2002 ina watu wanaofikia 24,000, lakini kule Kigamboni bado kuna ongezeko kubwa la shughuli za kiuchumi kama utalii, kilimo cha mbogamboga na matunda na uvuvi. Kwa hiyo watu wanaokwenda Kigamboni ni wengi sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kutokana na wingi wa watu, ipo haja *movement* ya kutoka Kigamboni kuja upande mwingine wa Jiji iwe kama mji mmoja tuwe tunapita tu. Nchi zingine tumeona madaraja kama hayo ambayo yanafunguka. Nakumbuka hapo nyuma kulikuwa na mazungumzo kuhusu daraja naona yamekufa. Namwomba

Mheshimiwa Waziri katika majibu yake atwambie kuna mipango gani ambayo wanaifikiria kuondoa tatizo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijamaliza hilo la Dar es Salaam, ningependa pia kuzungumzia kuhusu barabara za kule Kigamboni. Daraja lile likishatengenezwa hata kama ni kivuko ukishashuka unaingia kwenye barabara nzuri sana kabla hujafika Mjimwema ukiishia hapo ni tatizo kubwa. Wizara ilijitahidi ikajenga barabara za changarawe, lakini wananchi wa kule wanaiomba Serikali itengeneze ile barabara kwa kiwango cha lami ambayo itengenezwa kwa kiwango cha changarawe, kwa sababu kwa muda mfupi barabara ile imeshaharibika tena kama vile haikutengenezwa.

Barabara hiyo ni ile inayoanzia Mjimwema kwenda Mwongozo, Gezaulole, Somagira, Kimbiji, Buyuni na Pemba-Mnazi, tunaomba itengeneze hiyo barabara kwa kiwango cha lami ili isiwe kero ya kila mara, kwa vile kule mvua huwa zinanyesha kwa wingi. Pia kuna hii barabara hii ya kuanzia Kibanda kwenda Kisarawe II wananchi wangeshukuru sana kama ingetengenezwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nivuke kidogo niende kwa majirani zetu wa Mafia. Waheshimiwa Wabunge wengi wa Pwani nadhani wameishalizungumzia hili suala la Mafia.

Mafia ni kisiwa kimoja kizuri sana. Kina mandhari nzuri sana, tatizo kubwa ni gati, lile gati likitengenezwa hata yale maswali yanayokuwa yakiulizwa hapa Bungeni kuhusu vifaa vyta ujenzi kutofika kule. Lile gati likitengenezwa vifaa vyta ujenzi vitafika kwa sababu watu watakuwa tayari kwenda kuchukua *tender* za kujenga zile infrastructure za kule Mafia, lakini tatizo kubwa ni gati.

Kwa wale waliokuwepo hapa Bungeni miaka iliyopita walimsikia Mbunge mmoja wa Mafia mpaka alitaka kuomba awe Mheshimiwa Rais wa Mafia ili aweze kutengeneza hilo gati na mimi naungana mkono na wenzangu wanaotoka Mafia kwamba wakati umefika sasa Mafia nao wafikiriwe kwa sababu maendeleo yao yanabakia hapo hapo wanashindwa kuendelea kutokana na kutokuwa na gati ya kuweza kupelekeea vifaa vyta ujenzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa Mafia kama miezi miwili iliyopita nilisikitika, niko kwenye gari la *DC* mafuta yanauzwa kwenye vikopo, kwa sababu dizeli na petroli inaletwa na madau kutoka nchi kavu.

Kwa hiyo, hawawezi kuyasafirisha kwenye tanki yanaletwa kwenye madebe, halafu yanawekwa kwenye duka nje, mnaenda mnanunua mafuta. Kweli Kisiwa ambacho kinajulikana dunia nzima, wana utajiri mkubwa wa chini ya bahari, watu wanatoka nchi mbalimbali kuja kupata *Ph.D.* pale katika masomo yanayohusu viumbwe vyta baharini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naona upo umuhimu mkubwa wa kuendeleza Kisiwa kile. Nilienda na wawekeza kule walisikitika sana kwani hata ile *air strip* ya pale

ina hali mbaya sana. Kwa hiyo, tuwasaidie wenzetu wa Mafia sasa kwa kuwajengea lile gati la Mafia na hivyo kufungua maendeleo ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kwamba kwanza niipongeze Serikali kwa ujenzi wa barabara nyingi katika Jiji letu la Dar es Salaam na hivyo kuufanya mji upendeze na kila anayekuja Dar es Salaam analisifia Jiji la Dar es Salaam anaulinganisha na Nairobi, anaulinganisha na maeneo chungu nzima. Sisi wana Dar es Salaam tunajitahidi tunaweka mji wetu safi na ndiyo maana tunapata sifa.

Lakini pamoja na usafi ule pita usiku katika Jiji la Dar es Salaam lina giza nzito sana. Ukiachia zile taa zilikuwa nje majengo, taa za barabarani nyingi haziwaki na sehemu nyingi hakuna taa na ujambazi kwa sababu hakuna taa unaendelea. Najua siyo jukumu moja kwa moja la Wizara ya Ujenzi la kuweka taa, lakini sisi Dar es Salaam tunaomba Wizara iweke katika mipango yake fungu la kuweza kutusaidia Jiji la Dar es Salaam kueneza taa katika Jiji lile ili lifanane na Majiji mengine yaliyopo duniani hasa hapa Afrika ili tuweze na sisi kufanana nao na pia kupunguza matatizo ya ujambazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hata zile taa tulizokuwa nazo kutokana na *tariff* kuwa kubwa sana za *TANESCO* tunashindwa taa zile kuwasha zote. Unakuta nyingine zinawaka na nyingine haziwaki. Kwa hiyo, tunaomba Waziri ya Ujenzi iingilie kati suala hilo ili utusaidie tuweze na sisi kulifanya Jiji letu liwake kama Majiji mengine na hivyo lipendeze.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa kweli kwa leo, yangu yalikuwa ni hayo na nitamshukuru Mheshimiwa Waziri hasa akizungumzia suala la Kigamboni. Baada ya hapo napenda kuunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana.

**MHE. KILONSTI M. M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuzungumzia hoja ya Wizara ya Ujenzi. Kwanza kabisa naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika Wizara ile. Kwa kweli ni kazi nzuri wanayoifanya na mimi naunga hoja mkono. (*Makofî*)

Barabara kama wengi wanavyoizungumzia katika Bunge hili, barabara ni maendeleo. Kama ulivyo umeme na kama unataka kupanga kwa ajili ya barabara lazima uangalie uchumi wote *in totality*. Mimi nafikiri kwa kiwango fulani wamejitahidi sana kuangalia hayo. Wameangalia Kusini wakajenga barabara zikafika Makao Makuu. Wakaangalia Makao Makuu ili yafike kwenye ziwa lingine kubwa wakaliona, iko barabara, kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa kazi nzuri waliyofanya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini tunachohitaji katika nchi hii kama ninavyosema kwamba ni vizuri ukaangalia barabara *in totality* tunahitaji *A Road Construction Programme* ambayo inaiangalia *economy* yote kwa ujumla kisha inapanga *in line with literacy endowment* za nchi hii. Inasema tunataka kujenga barabara fulani inatoka

Mtwara inakwenda Lindi ikishatoka Lindi inakwenda Songea halafu inakwenda Mchuchuma because tuna target Mchuchuma. (*Makofi*)

Lakini pia tunasema tunataka kujenga kwa mfano kiwanja fulani cha ndege kwa sababu tunataka ku- *capture market* fulani. Nitatoa mfano, hivi sasa ndege kubwa zinazotoka Kongo zinakuja kununua chakula Mkoa wa Kigoma, zinatua pale kwa shida sana. Uwanja wa ndege wa Kigoma kama ungejengwa nchi hii ingepata fedha nyingi sana kama uwanja ule ungejengwa. Lakini pili, *port* ya Kigoma kama ingejengwa tung-*capture* biashara nyingi sana ya Kongo, Burundi, Zambia na nchi zingine na tungefanya biashara nzuri sana. Tungeweza kuitumia reli yetu vizuri zaidi na reli hiyo ikasaidiwa na barabara itakayojengwa hii inayokwenda mpaka Shinyanga, ikatoka Shinyanga ikapita Kahama ikiwa ni nzuri zaidi na ikafika mpaka Kigoma na ikaenda mpaka Burundi kupitia Ngara. Haya yote yangeweza kuinua kipato chetu cha *export earning*. Fedha za ujenzi wa barabara zipo na utaratibu wa fedha ni mzuri. Kwa hiyo, kama ukitumiwa kwa mipango iliyopo tungeweza kwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukizungumzia habari ya barabara kutoka Tabora kwenda Kigoma. Hii barabara imo katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Miaka kumi sasa inakwisha hatuoni mpango madhubuti wa kufungua Mikoa ya Tabora na Kigoma ili kuwepo na *Inter Virginal Communication System*. Huwezi kusema unakwenda Kigoma leo hii mwezi wa nne mvua zikinyesha sana usafiri kati ya Tabora na Kigoma unakoma. Watu wanakwenda wanalala njiani siku nne, tano maana mle mote ni *floods* zimejaa. Sasa *alternative* iliyokuwepo ni hiyo ya kujenga barabara. Tena tungeomba tujengewe barabara ya lami kutoka Tabora kwenda Kigoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaposema kwamba ni vizuri tukawa na mpango madhubuti wa barabara katika nchi ambao unatueleza. Mimi nimekuwa nasoma hiki kitabu cha Mipango ya 2003/04. Ninaona pale mapato, ukarabati wa barabara na kule mwisho wanaonyesha barabara ambazo zimeombewa fedha.

Kusema kweli *you* .....kama utapata hizo fedha ili uweze kujenga hiyo barabara. Maana nasema hivyo kwa sababu nina *experience* na barabara ya kwangu. Mwandiga/Manyovu karibu itafika miaka 20 sasa tunaizungumza hapa. Mwaka 2002 nilizungumza, rafiki yangu Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi akafikiri namshambulia bila sababu.

Mimi nilichokuwa nasema hii barabara iko kwenye mpango wa kujengwa kwa miaka mingi haijengwi, leo unaniambia Kigoma tumejenga barabara, mimi sielewi unaposema tumejenga barabara Kigoma. Mimi nakuzungumzia barabara ambayo ina *short distance from a 100 kms. to 40* wewe unaniambia tumeweka barabara kadhaa. Ndicho nilichokuwa nasema.

Namshukuru nilipozungumza naye mwaka 2003 akaniambia tumetenga fedha, kwenye kitabu sizioni, lakini ameniambia zimetengwa karibu shilingi milioni 600 angalau kurekebisha sehemu korofu katika barabara ile, namshukuru sana. Lakini naomba niseme hivi Mkoa wa Kigoma ni mkoa ambao kwa kiwango kikubwa

umepunjwa kwa kuwa na barabara chache za mkoa (*Regional Roads*) zinazohudumiwa na Serikali Kuu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*). Ziko barabara chache sana. Wilaya ya Kasulu peke yake ina watu wengi katika maeneo ya mpakani na nchi jirani ya Burundi ambapo biashara kubwa hufanyika kati ya Kasulu na vijiji vya mpakani mwa nchi ya Burundi. Ukiambiwa uende kule utashangaa sana maana unapita porini au kwenye mahandaki.

Aidha, shughuli za ulinzi wa Mpaka huhitaji barabara za uhakika ili kuvifiki vijiji hivyo viliyyoko mpakani. Lakini ukiwaangalia wale askari wetu hata ukisikia watu wetu wanapigwa risasi, wanapigwa risasi kwa sababu wale wakija hata kukimbia ili waweze kwenda kuokoa zile risasi zinalia sio rahisi hawezi kukimbia kwa haraka sana.

Mheshimiwa Spika, naamini rafiki yangu Mheshimiwa Waziri Mkuu anafahamu. Maana kile Kijiji anakifahamu ni Mpakani, ukiangalia hivi Burundi unaiona. Yeye amefika kule na hata juzi mimi nimefika wananiuliza hasa Waziri Mkuu atarudi lini maana hakuzungumza, tunataka azungumze na salamu zetu amezipeleka kwa Rais.

Sasa Waziri Mkuu nikamwambia mimi hajazungumza na mimi ila nitakapokwenda nitasema. Sasa kwa sababu namwona na mimi niko hapa nimeona nilisema hilo ili nimkumbushe Mheshimiwa Waziri Mkuu apeleke salamu hizo, Barabara zile umeziona. Maeneo yaliyo na matatizo la barabara ni katika Tarafa ya Muyama ambayo kipindi kinachokuja Waziri Mkuu atakapotembelea kule nitampeleka. Iko barabara ya Kisili mpaka Buhigwe ambayo ni barabara ya Mkoa. Imeishia katikati ya Wilaya na hii barabara sio kama inatakiwa iishie pale, inatakiwa iendelee na ndiyo barabara ilikuwa inatumiwa na mabasi siku za nyuma. Lakini ina-*hang only 20 kilometres* ndiyo Barabara ya Mkoa. Unaambiwa bwana barabara zako zote bwana zimepata fedha lakini maendeleo yatakuwa ya kilomita 20 toka ukoloni mimi nasoma Shule ya Msingi naiona hiyo tu. Kweli tutaendelea?

Mheshimiwa Spika, barabara hii inatakiwa iende mpaka Tarafa ya Muyama. Ikitoka Tarafa ya Muyama iende mpaka Migongo, Mugera na ifike Kijiji cha Kitanga katika Wilaya ya Kasulu, Jimbo la Kasulu Mashariki. Ndiyo ingekuwa Barabara ya Mkoa ambayo itakuwa ni kilomita zaidi ya 70. Hapo watu wangeweza wakaitumia barabara ile wakafika, lakini ukifika hizo kilomita 20 baada ya hapo hata madaraja yenye ni taabu kupita, hayapitiki ni vichochoro tu.

Sasa mimi ninachomwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kupandisha baadhi ya hadhi za Barabara za Wilaya ziweze kuwa Barabara za Mkoa. Mimi najua sio hii haiko Kasulu tu, iko katika mikoa mingi. Haiwezekani Halmashauri zenye uwezo mdogo kuweza kuhifadhi au kuziendeleza barabara hizo kwa kiwango kinachotakiwa. Ziko barabara nyingi ambazo baadaye nitakuja kuziorodhesha na nitazzungumza katika *Road Board* na tukizungumza katika *Road Board* nitampelekea Mheshimiwa Waziri na mimi nina imani atazipandisha hadi kwa utaratibu anaouelewa yeye.

Aidha, barabara ya Kasulu - Kabanga - Msambala - Mwanga - Kasumo mpaka Muyamo ni barabara muhimu sana kwa sababu inaunganisha Vijiji vingi na Makao

Makuu ya Wilaya na pia hospitali maarufu ya Kabanga ambayo ni ya *Mission Catholic* inayohudumia watu wengi sana katika Mkoa wa Kigoma. Lakini ukitoka Kasulu kilomita 5 ukafika Kabanga baada ya hapo hupiti. Kwa hiyo, wale wengine wanaotoka lazima wazunguke waje Kasulu ili wafike kwenye hospitali ile yenye huduma muhimu sana kwa mkoa huo. Barabara nyingine ni ile inayotoka Muyamo kupitia Vijiji vya Buhoro hadi Makao Makuu ya Tarafa ya Makele. Hizi ndizo barabara muhimu sana katika Wilaya Kasulu na ambazo zinaweza kutusaidia sana katika kuboresha maendeleo ya mji wetu.

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho naomba niseme hivi katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri ameodrodhesha barabara ya Uvinza mpaka Malagarasi. Lakini sisi kitu kinachotuunganisha na kitakachofanya ule mkoa ambao kila wakati tumeuita *sleeping giants* tunataka kuwa na uwezo wa kuwasiliana na wenzetu wa Tabora. Tuunganishwe na wenzetu wa Tabora ili na sisi tupate nafasi ya kuuza vile tunavyolima. Kigoma kilo moja ya nyanya ni shilingi 100/=. Kwa sababu hatuna mahali pa kuuza.

**MBUNGE FULANI:** Uza Burundi

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI:** Burundi kuna vita hatuwezi kwenda na wala sisi hatuwaruhusu watu kwenda Burundi. Ukisema tupeleke Rukwa, Rukwa hatuwezi .

**MBUNGE FULANI:** Kongo je?

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI:** Kongo kuna vita. Ni taabu tupu, *port* nayo ile watu hawawezi kuleta meli zao maana zitaumia. Lakini *planning* ndiyo kama hiyo kama *port* ya Kigoma ingekuwa imetengezwa tungeweza ku-generate zaidi dola milioni 60 kwa mwaka. Kama *Kigoma Airport* ingejengwa, ndege nyingi zingekuja pale na ile ingekuwa *another money spinner* ya nchi hii kwa upande wa utalii na upande wa mambo mengine *we are the only ones* katika sehemu hii ambao tuna utalii wa *chimpanzee*, watu wengi wanapenda kuangalia *chimpanzee*, sokwe mtu. Maana haya ndiyo tuliyo nayo na ndiyo lazima tujivunie kwa sababu hatuna lingine la kujivunia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri tunavyozungumza haya sio tu tunazungumzia lakini tungependa yawekwe katika mipango na ndiyo maana katika mazungumzo yangu yote nimekuwa nasema ninapenda *tu-disband the so called planing and privatisation ministry* au sijui *commission*. Nina sababu na hoja za msingi. Maana tunahitaji *a plan even for us*. Hawa hawakupanga vizuri *we will have things, we will have engineers* kule ambao watasema *no, your plans are not enough*, sio nzuri.

Kwa hiyo, watatumbia lakini leo kila mmoja anapanga vyake. Nimezungumzia habari ya *serious inter-ministerial collaboration* katika nchi hii. *It is after 30 years because each plan to invest with its own ministry and it is better.*

Mheshimiwa Spika, mimi nasema tungefanya zaidi hata kama tunafanya vizuri mimi nikiwa na mtoto akawa anafanya kazi anakuwa wa kumi nitamwambia nataka uwe wa tano kwa nini usiwe. Sasa mimi sisemi kwa sababu wale ndugu zangu pale mimi niko huku, hapana. Mimi nasema ili tuwe na *a better system* ya *planning* na watu wetu *wa-gain from that planning*. Mimi nina imani haya yakifanyika tutaweza kufanikiwa ili tufanye biashara tunahitaji barabara nzuri. Utafanyaje biashara huna barabara nzuri. Kwa hiyo, ni *top priority* katika *planning* za maendeleo ndiyo maana hata katika *economic operation* za Afrika, *we have serious infracturings* ambazo hazipo na hatuwezi kufanikiwa. Maana lazima ziwepo ili tufanye biashara kwa kushirikiana pamoja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba nizidi kuwapongeza, wamefanya kazi nzuri na hiyo kazi nzuri naiomba waiendeleze ili waweke mipango mizuri zaidi inayochukua nchi nzima. Tukisema tunataka barabara kutoka Tanga kwenda Musoma kweli hiyo barabara iwepo ili tusafiri vizuri, watu wa Musoma waje Dar es Salaam kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niishie hapo niunge hoja mkono mia kwa mia. (*Makofî*)

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja ya Wizara ya Ujenzi. Nianze kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tatu inayoongoza na Mheshimiwa Benjamin Mkapa wa CCM kwa utendaji mzuri wa kazi na wenye nidhamu ambao kwa kweli umesababisha wahisani na wafadhilli waliokuwa wamesitisha kutusaidia kuendelea kutusaidia hasa katika sekta ya barabara. Yote tunayoyasema kwa kumsifu Mheshimiwa John Magufuli ni matokeo ya nidhamu ya Serikali kwa ujumla kwamba tumeweza tena kuaminiwa. Naipongeza sana na nampongeza Mheshimiwa Rais. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuwashukuru Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi na Mheshimiwa Lucas Selelii, ambao wameweka wazi dhana ya mipango na ujenzi wa barabara katika maeneo hususan kwa nia ya kuinua na kuibua uchumi wa maeneo na kuondoa umaskini. Hili ndilo linatakiwa liwe lengo katika mipango yetu kwamba tuweze kuibua maeneo ambayo tunaweza kuyaita *sleeping giants* kama Mkoa wa Kigoma ulivyo.

Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwa kweli aweze kuweka nia ya madhubuti sio ya kujenga barabara ya kutoka Uvinza kwenda Malagarasi kama ilivyoonyeshwa katika hotuba bali iwe ni ya kujenga barabara kutoka Kigoma kwenda Tabora kwa sababu ndio njia tu inayoweza kuiunganisha Mkoa wa Kigoma ikaunganishwa na *the rest of the country*, chini ya hapo Kigoma itabaki bado imefungwa. Kwa hiyo, naiomba Wizara kwa makusudi kabisa itenye fedha za kutosha kuweza kuijenga. Katika kitabu nimeona wameandika Uvinza/Malagarasi, hii haitoshi tunaomba iwe ni Kigoma kwenda Tabora ili tuungane na Tabora. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika kitabu cha hotuba ukurasa wa 74 Mheshimiwa Waziri ametenga fedha kwa ajili ya barabara ya kutoka Nyakanazi kwenda Kigoma. Ameiita

kwamba ni *periodic maintenance*. Naomba tena nitamke kwamba barabara hii ya kutoka Kigoma kupitia Nyakanazi ndiyo njia pekee kwa hivi sasa ambayo inaunganisha Mkoa wa Kigoma na *the rest of the country* na *actually* hata Burundi na wapi ni lazima upite Nyakanazi. Sasa kwa miaka miwili iliyopita barabara hii ilikuwa imejengwa na ilikuwa ni nzuri bahati mbaya Mkoa wa Kigoma, labda kwa bahati nzuri kuna mvua nyingi sana. Leo hii barabara haipitiki. Najua wafadhili wanakuja na *terms* zao kwamba watajenga barabara kwa kiwango cha changarawe na *beggars cannot be choosers*, nakubali.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba kabisa kwa nia ya kuokoa fedha za hawa wafadhili na kwa *seriousness* katika maendeleo kwamba Serikali iwashawishi wafadhili na wahisani kwamba ujenzi wa barabara kuu kama hii ya Nyakanazi kwenda Kigoma kwa kutumia changarawe au mchanga imepitwa na wakati na ni hasara. Kwa sababu kila baada ya masika, moja, barabara hiyo lazima itengenezwe upya.

Sasa ningependa niishauri Serikali kwamba wakubaliane na hawa wafadhili kwamba hizi barabara zijengwe kwa kiwango cha lami. Kwa sababu hata ukijenga kilomita 5 unakuwa na hakika kwamba baada ya msimu hutarudi tena hapo. Kuliko kila mwaka tuwe tunatumia fedha nyingi kukarabati *periodic maintenance, spot maintenance* ya nini. Afadhalu tuwe na hakika kwamba tumetoka Kigoma Mjini tumefika Kidahwe barabara inapitika kwa kipindi chote. Tutakapokuwa tunaomba fedha tutakuwa tunaomba fedha za kuendelea mbele, hiki kipande tumesahau.

Mheshimiwa Spika, ilivyo hivi sasa ni kwamba lazima kila mwaka tuombe fedha kwa sababu mvua ikinyesha barabara imeshabomoka. Si utaratibu mzuri wa kuhifadhi barabara zetu na kutumia raslimali. Hata kama tunaomba, tuwaambie kwamba tunachokitaka sisi ni hiki. Huwezi kuwa una njaa unahitaji ugali, mtu akakuambia kwamba mimi nitakupa keki ukakimbilia ukapiga makofii, kwa sababu ile keki haitakusaidia. Kwa hiyo, naiomba Wizara hii ichukue kwa makusudi kabisa kuwashawishi wafadhili na wahisani kwamba tuanze utaratibu wa kujenga barabara hizi kwa lami na sio kwa changarawe na michanga ambayo inabomolewa kila baada ya msimu wa mvua.

Mheshimiwa Spika, wote tu mashahidi wa taabu na adha wanazozipata wananchi wetu wakati wa bomoa bomoa ya barabara ili kupanua barabara au kujenga barabara mpya. Nadhani niamini kwamba Serikali na Wizara kwa ujumla itakuwa na kitu tunaweza kukiita *Road Master Plan* katika nchi na watakuwa wanajua barabara zitapita wapi kwa sababu huwezi kupanga kwa miaka miwili au mitatu unavyotaka kuendeleza nchi.

Sasa inakuwa kama tunavizia wananchi wamejenga ili tubomoe. Hivi kwa nini hiyo *Road Reserve* isijulikane mapema na mipaka ikawekwa kuonyesha kwamba hii ni *reserve* ya barabara, barabara itakuja kupita eneo hili, ili mwananchi asishawishike kujenga katika hayo maeneo mapema. Hivi sasa ilivyo ni kwamba tunavizia mwananchi amejenga na sisi tunataka kupitisha barabara kana kwamba tunamkomoa. Hivi kwa nini tusionyeshe kwamba hapa mita hizi 10 usijenge na tukaweka alama ya wazi, tukaweka mabango kwamba ni eneo la barabara.

Mheshimiwa Spika, lakini cha kusikitisha zaidi ni dhana ya baada ya kubomoa. Unabomoa majengo wananchi kama watafidiwa *alhamdullilah*, hawakufidiwa wanapata taabu ya kuhama na kwenda kujenga kwingine. Lakini inapita miaka pale ambako pamebomolewa bado kitu hakijafanyika. Hivi tunataka kuweka picha ya aina gani, hivi kwa nini kama umeshajiandaa kwa nini usibomoe moja kwa moja na kuanza kujenga hapa itaonyesha *seriousness*. Lakini unabomoa unakaa miaka mitano wanaanza tena wananchi kuja kuvamia eneo lile lile ulilowafukuza, kwa sababu hakuna kinachoendelea.

Naiomba Serikali na Wizara kwa ujumla kwamba pale tunapokuwa tumeanza kubomoa mipango yetu iwe thabiti tubomoe na kuanza kufanya kazi na hapo mwananchi wa kawaida ataaelewa kwamba ameondolewa kwa sababu ya barabara hii ambayo imewekwa hatagombana na Serikali kwa sababu ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme tu kwamba Serikali imekuwa kwa nyakati mbalimbali inaunda Tume. Tume zinatoa mapendekezo na kuwasilisha Serikalini. Lakini kwa mara nyingi sana Serikali imekuwa inasita kutekeleza yale ambayo yamependekezwa na Tume ambazo zimeundwa. Hii inatuletea matatizo kwa sababu *you have to study* maana yake unaunda Tume ili ufanye nini kama sio upate mapendekezo na utekeleze. Nalizungumza hili kwa kulingana na Tume ambazo ziliundwa kwa ajili ya kuangalia uwezekano wa kuwauzia wafanyakazi nyumba za Serikali. Tulikuwa na Tume ya Mheshimiwa Basil Mramba, Mheshimiwa Amon Nsekela, nadhani zilikuwa Tume tatu, zote tangu hiyo miaka zilipendekeza watumishi wa Serikali wauziwe nyumba walizokuwa wanaishi. Leo inaonekana kwamba ni geni kwa sababu Serikali ilipata kigugumizi katika kutekeleza yale ambayo Serikali yenewe ilizituma Tume zitekeleze.

Sasa hiki kigugumizi kinatufikisha hapa leo tunakuja kuonekana kwamba tunafanya kitu kipyä kabisa wakati ilishapendekezwa miaka 30 iliyopita. Sasa ni vyema Serikali ikawa *serious* inapouna Tume inataka ushauri basi yale mashauri wanayopewa watekeleze mara moja sio kungojea miaka ipite itatuletea matatizo mbele ya safari. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini kingine pamoja na matatizo ambayo yamejitokeza, mimi nashauri kwamba Wakala wa Majengo (*TBA*) haiwezi kujenga nyumba za kutosha kwa kutegemea fedha zitakazotokana na makato watakayokuwa wanakatwa hawa waliouziwa nyumba. Kwa sababu ni kwa kipindi.

Kwa hiyo, nashauri Serikali itenye fedha za makusudi kabisa kuiongezea *TBA* ili iweze kujenga nyumba kwa ajili ya watumishi ambao hawana nyumba. Pia maana yake siku hizi wamepata viwanja *TBA* na inajenga eneo moja. Sasa tunajenga kama *Barracks*. Nina hakika hakuna Waziri atakayependa kutazama na Waziri jirani yake watakayokuwa wamejenga. Kwa hiyo, ni vyema viwanja hivi vikatawanywa katika sehemu mbalimbali ili tusijenge *barracks*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nataka na mimi niulizie hivi Wizara kweli iko *serious?* Maana yake mimi najua haina fedha za kutosha kutekeleza ujenzi wa barabara zote. Hivi

huu mpango wa *BOT*, nini msimamo wa Serikali kuhusu *BOT*. Hivi haiwezekani tukajenga Daraja la Kigamboni kutumia *BOT*. Hivi haiwezekani tukajenga barabara ya kutoka Tabora kwenda Kigoma kutumia *BOT*. Maana yake kama fedha hazipo basi tutangaze tuweke masharti ya *BOT* yawe wazi ili wawekezaji waweze kuja. Wakati tunajadili hotuba ya Waziri wa Kilimo na Chakula, tuliambiwa baadhi ya fedha za *STABEX* zitaingizwa katika ujenzi wa barabara ambazo zitajengwa katika maeneo ya uzalishaji wa zao la kahawa.

Sasa nataka nifahamu Wizara ya Ujenzi imeshirikishwa vipi katika hili suala zima na kama wameshaainisha hizo barabara, nalisema hili kwa makusudi kwa sababu zisije fedha hizo zikalenga katika maeneo yaliyozoleka na kusahau maeneo ya Bukiriro, Muhange, Muguzu katika jimbo la Buyungu kwa sababu na wao wanalima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002 tulimsifia sana Mheshimiwa John Magufuli kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kukamata magari na vifaa vyta Serikali vilivyokuwa vimesajiliwa kwa majina ya watu binafsi. Nampongeza sana kwa kazi hiyo aliyoifanya na ninaomba aendelee kuifanya.

Lakini ningependa kufahamu hivi ni watu wangapi ambao wamethibitika kwamba walikuwa wametumia mali za Serikali wakaziandika kwa majina yao na wamefanywa nini ili tujue Serikali imepoteza kiasi gani na Serikali imeweza kuwafanyia nini hawa watu, si hatua za kinidhamu tu za kunyang'anywa gari wamefanywa nini, wamefikishwa Mahakamani? Na kama sio kwa nini bado haiko hivyo?

Mheshimiwa Spika, mwisho nilzungumze hili la barabara ambazo ni za mipakani kama Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, alivyozungumza. Hizi barabara zimeachiwa Halmashauri. Lakini kwa hakika hizi barabara ni muhimu sana kwa faida ya ulinzi na usalama wa Taifa letu. Huwezi kuzungumza usalama kama hizi barabara hazitakuwa zimetengenezwa, barabara zinazolekea mipakani. Barabara ya kutoka Kibondo kwenda mpaka Mukulazi na Kisulu.

Barabara ya kutoka Kibondo kupita Mugunzu kwenda Bukiriro, barabara ya kutoka Kakonko kwenda mpaka Muhange, barabara ya kutoka Kakonko kwenda mpaka Nyabibuye, hizi ni barabara za mipakani na kwa bahati mbaya kwa Mkoa wa Kigoma barabara zinazohudumiwa na Mkoa ni chache sana kutokana na kwamba tunapakana na Hifadhi ya Taifa ya Muyovozi. Sasa, ninaishauri Serikali na Wizara kwa ujumla ielekeze nguvu zake katika kutengeneza barabara ambazo zipo mpakani.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, Mheshimiwa Anatory Choya, amesema kwamba iundwe Tume Maalum ya Kuchunguza Uuzaji wa Nyumba za Serikali.

Naomba nikubaliane na Kamati ya Miundombinu kama ilivyoshauri katika ukurasa wa 9 kifungu cha 5.8.1, kwamba Serikali ifanye tathmini ya zoezi zima ili kubainisha kasoro zilizojitokeza katika uuzaaji wa nyumba za Serikali. Nadhani hakuna sababu ya kuunda Tume Maalum, hili tu litakuwa limetusaidia kwamba tutaweza kujua hali halisi ya zoezi zima limefikia wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie katika hoja ya Wizara ya Ujenzi na napenda kuanza kwa kusema ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa sababu nyingi tu, mojawapo ni kwamba Wizara hii inafanya kazi nzuri sana kwani imebadilisha sura za barabara katika nchi hii na wengine tunapozungumza na Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kweli wanatusikiliza. Kwa hiyo, napenda niwapongeze kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia, napenda niwapongeze kwa sababu ya kutoa hotuba safi, fupi, yenyе kina na malengo ambayo yanaeleweka. Vile vile, nawapongeza kwa sababu ya kuanzisha ujenzi wa barabara ya kutoka Pugu - Kisarawe, kilomita 6 ambazo nimekuwa nikizipigia kelele tangu mwaka 1996 mpaka ikafika mahali nikaanza kutolewana na baadhi ya marafiki zangu ndani ya Serikali. Sasa, barabara hii imeanza kujengwa, pamoja na kwamba zipo kasoro ambazo nitazieleza huku mbele, lakini Wananchi wa Kisarawe wanasema wanaishukuru Wizara kwa kuanza kutekeleza jambo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama hotuba inavyoonyesha katika Ibara ya 33 na 35, pia, nawapongeza kwa kutekeleza azma ya kupambana na umaskini kwa kuhusisha nguvu za Wananchi katika ujenzi wa barabara. Kule kwetu Kisarawe tayari Wananchi wamehusishwa kama Makandarasi wadogo wadogo chini ya mradi wa *DANIDA* na sasa hivi wameanza kufundisha Makandarasi Wanawake ambao wameanza kufanya kazi. Napenda niwapongeze kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, yapo mapungufu ambayo ningependa niyataje kwa maana ya kuishauri Wizara ili iweze kuimarisha kazi zake na tuweze kuisifu zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni Ugawaji wa Fedha za Mfuko wa Barabara. Katika ugawaji wa fedha hizo za Mfuko wa Barabara zinazokwenda kwenye barabara za Mikoa na Serikali Kuu sina tatizo, naona utaoji unakwenda sawa sawa, lakini kasi ya ugawaji na viwango vinavyokwenda katika Halmashauri sasa hivi vimeanza kupungua na nashindwa kuelewa sababu ni nini! Kwa vile Serikali imeongeza ukusanyaji wa kodi na kwa vile Wahisani wametusamehe na wanaendelea kutusamehe madeni, tegemeo langu lilikuwa kwamba magawio kwenye barabara za Wilayani na Vijijini yangeongezeka, lakini nadhani kasi hiyo sasa hivi imepungua.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kuelezea juu ya Matengenezo ya Barabara za Mikoa. Pamoja na kwamba *TANROADS* inajaribu kufanya kazi nzuri, lakini nadhani kuna mahali pengine panahitaji kuimarishwa zaidi. Kwenye barabara ambazo

zinafanyiwa matengenezo ya kawaida badala ya kuzitengeneza, barabara zile huwa zinachongwa na mvua ikinyesha baada ya muda mchache tu tayari zinakuwa mifereji.

Kwa hiyo, fedha za utengenezaji ambazo zinatumika kwa barabara hizi, zinatumika kwa njia ambayo inaonekana siyo sahihi. Hivyo basi, nashauri angalau tutengeneze maeneo mafupi, lakini kwa kuziba mashimo vizuri, kujaza udongo na kuweka matuta ili kusudi barabara ile isiwe njia ya maji wakati mvua inanyesha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tatu, kuna ujenzi wa barabara kwa kutumia changarawe. Barabara zile zinaonekana ni imara, lakini mara baada ya ujenzi kumalizika, hazidumu! Mvua ikishanyesha tu changarawe zinaoshwa na matokeo yake yanakuja mashimo na mashimo ya barabara za changarawe ni mabaya zaidi kuliko mchangano au udongo wa kawaida. Naishauri Serikali wajitahidi kadri iwezekanavyo, ni bora watengeneze maeneo mafupi kwa kuweka lami, kuliko kuiwekea barabara changarawe.

Mheshimiwa Spika, kule Kisarawe na Mkuranga kuna barabara mbili, barabara inayotoka Pugu mpaka Kijiji cha Msanga kwa Kisarawe na barabara inayotoka Mkuranga mpaka Kisiju. Barabara hizi zimejengwa kwenye mwaka 1999 kwa kiwango cha changarawe, sasa hivi ukienda utakuta si barabara tena na fedha iliyotumika pale inaonekana kwamba imesahaulika! Najua kwamba fedha hazitoshi, lakini namshauri Mheshimiwa Waziri kwamba, tutazame uwezekano wa kutengeneza barabara masafa mafupi kwa lami, kuliko kutengeneza masafa marefu kwa changarawe ambapo barabara hizo zinakuwa hazidumu.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kwamba tukifanya hivyo fedha zinazotumika zitakuwa zimetumika vizuri na Wananchi wataona kwamba kweli wana barabara ambazo zinadumu.

Mheshimiwa Spika, nne, ni Makandarasi wasio na uwezo. Kwa bahati nzuri hili Mheshimiwa Waziri amelitambua na limeelezwa vizuri sana katika Ibara ya 39 ya hotuba yake na Kamati ya Miundombinu imelitambua vile vile, imelieleza vizuri chini ya Ibara ya 3.2, kwamba wapo Makandarasi ambao uwezo wao ni mdogo. Sasa kama Makandarasi hao uwezo wao ni mdogo tunapowapa *contracts* ni vizuri pale wanaposhindwa vipengele vyta *contract* vitumike. Kama Mkandarasi hawezibasi ni bora kumsimamisha kuliko kuendelea kumlea tu!

Mheshimiwa Spika, ninafahamu Mheshimiwa Waziri anakuwa mkali sana pale ambapo Mkandarasi hafanyi kazi vizuri. Najua kwamba Mheshimiwa Waziri hajafika katika Wilaya ya Kisarawe, lakini napenda nimwalike aje nimwonyeshe kazi inayofanyiwa na Makandarasi anayetengeneza zile kilomita 6 kutoka Pugu mpaka Kisarawe.

Sasa hivi ni miezi sita imepita kila wakati anaweka udongo, mvua ikinyesha inauondoa, anaweka mwingine, anabomoa tu! Jambo hili litatuchukua muda mrefu sana na siamini kama barabara hii inaweza kujengwa vizuri kama vile ilivyotegemewa chini

ya Mkandarasi huyu! Sina ugomvi na Mkandarasi huyo, lakini nadhani uwezo wake haulingani na kazi aliyopewa.

Mheshimiwa Spika, lakini inawezekana kukawa na sababu nyingine na ambayo nimeiona, kwamba utoaji wa fedha katika Mikataba hii unakuwa hauendi sawasawa na mategemo yenye. Kwa mfano, ile barabara ya Pugu - Kisarawe mwaka uliopita wa 2002/2003 ilitengewa shilingi milioni 640 mwaka huu 2003/2004 nimeona katika kielelezo namba 6 imetengewa shilingi milioni 250. Kwa mujibu wa Wataalam wa Ujenzi wa barabara, kilomita moja inagharimu siyo chini ya shilingi milioni 300, je, hizi shilingi milioni 890 zitajenga hizo kilomita sita?

Mheshimiwa Spika, inawezekana kabisa pengine kushindwa kwa Mkandarasi ni kwa sababu hapewi fedha za kutosha. Kwa kuwa sitapata nafasi ya kuchangia wakati wa Kamati ya Matumizi ya Bunge Zima, kwa kuwa nitakuwa nimesafiri, ningependa wakati Mheshimiwa Waziri ana-*windup* awahakikishie Wananchi wa Kisarawe kwamba barabara hii itamalizwa kwa muda uliopangwa kwa sababu inaonekana Mkandarasi huyo uwezo wake ni mdogo na pia fedha inayotolewa hailingani na ukubwa wa eneo lenyewe.

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kutenga shilingi milioni 450 kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya kuunganisha kati ya Kisarawe na Kiluvya, barabara ambayo itasaidia sana mawasiliano baina ya Wilaya yetu na Makao Makuu ya Mkoa kule Kibaha. Lakini napenda kusema kwamba, kwenye mwaka 1998 au 1999 hivi, barabara hii ilitengewa fedha za matayarisho, lakini hazikutolewa! Sasa, hizi shilingi milioni 450 zilizopangwa katika Bajeti hii ni mategemo yangu kwamba zitatolewa na kazi hiyo itafanywa ili barabara hii iwapunguzie Wananchi wa Kisarawe adha ya kuzunguka mpaka Dar es Salaam kwenda kuonana na Watendaji wa Makao Makuu ya Mkoa. Mambo haya yakitekelezwa ninaamini kabisa watakuwa wametusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa sina maneno mengi sana, nia yangu ni kwanza kumpongeeza Waziri kwa kutekeleza yale ambayo yameshindikana kwa miaka mingi na kumshauri kuweka uimara katika maeneo ambayo bado yanaonyesha yanarudisha nyuma jitihada za Wizara.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nashukuru na ninaunga tena mkono hoja hii. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nikiri kabisa kwamba naunga hoja hii mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nimpongeze sana Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa John Magufuli, Naibu wake Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Katibu

Mkuu wake na Watendaji wake wote, kwa kweli sasa imefikia mahali tunaona kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inafanya kile ambacho Wananchi wanakitegemea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwenye macho haambiwi tazama na mwenye masikio haambiwi sikia! Kwa dira ya Wizara ya Ujenzi, sasa hivi tunaona kwamba ukipita kila mahali kuna shughuli za ujenzi zinazoendelea kwa nchi nzima. Hii ni changamoto katika kukua kwa uchumi wa nchi fulani. Sasa, Tanzania uchumi wetu unakua pamoja na vigezo vya namna hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupongeza jitihada hizi za Mheshimiwa Waziri na timu yake, vile vile, sina budi nipongeze kazi inayofanywa na Wakala wa Barabara (*TANROADS*). Toka kuanzishwa kwa *TANROADS* kazi zinaonekana na mfano ni Mkoa wa Mwanza kwani kumekuwa na mabadiliko makubwa sana ya utendaji kazi kupitia Wakala wa Barabara. Napenda kuwapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio ya *TANROADS*, labda ni vizuri tuangalie ni namna gani tunaweza kuhuisha (*harmonize*) kuhusu shughuli zao. Utakuta *TANROADS* wanafanya kazi kwa barabara za Mikoa, lakini bado kwa barabara za Wilaya *standard* zake ziko chini sana. Tatizo linakuja kwamba wanatengeneza barabara katika Halmashauri za Wilaya bila kuwashirikisha Wahandisi wa Wilaya. Kwa hiyo, kunakuwa hakuna linkage yoyote ambayo inaweza ikamfanya Mhandisi wa Wilaya naye akawa *accountable* kama *part of the process*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashauri tupanue wigo wa Wakala wa Barabara ili wigo huo sasa ushughulikie barabara za Mikoa na zile ambazo ziko Vijijiini. Haya mambo ya fedha kufikia kwenye Halmashauri mara nyingi unakuta *standard* ya barabara inakuwa hairidhishi na ningependa tuichukulie hii kama changamoto kwa kuangalia mafanikio ya *TANROADS*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo naomba sasa nzungumzie kuhusu barabara ya Nyanguge - Musoma. Barabara hii ilijengwa zaidi ya miaka ishirini iliyopita, lakini hadi leo hii haijawekewa tabaka jingine la lami juu yake (*resealing*) matokeo yake barabara hiyo imekuwa na mashimo mengi sana.

Mheshimiwa Spika, ninaamini unaifahamu zaidi barabara hiyo kwa sababu ukifika Mwanza unaona ni bora kwenda kwa *boat* kuliko kutumia barabara ile ya kwenda mpaka Kibara kwa sababu siyo nzuri. Nashauri barabara hii tuiwekee tabaka jingine la lami ili iendelee kudumu na kutoa huduma. Barabara hii ni ya siku nyingi na inafanya kazi vizuri sana, lakini kila wanapoziba, viraka vinabanduka! Kwa hiyo, kuna haja ya kutenga fedha ili barabara hiyo ifanyiwe ukarabati wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, barabara hiyo sasa hivi inakumbwa na matatizo ya ajali nyingi. Nadhani mnasikia kwenye Vyombo vya Habari na nikiwa kama Mbunge wa eneo husika nimekuwa nikishuhudia ajali nyingi sana za mabasi kugonga watu, ng'ombe na kuharibu mali za wananchi. Nadhani ajali hizo zinatokea kwa sababu barabara hiyo

haina *road signs*. Sasa unakuta magari mfano *Fuso* na mabasi yanakwenda kwa *speed* kupita kiasi.

Kwa hiyo, yakipita kwenye msongamano wa watu ni kuwapitia tu! Jambo hili linatia huruma sana kuona Wananchi wengi wanapoteza maisha na mali zao. Ninaomba sana Wizara ya Ujenzi ijaribu kutazama suala hili na kuchukua tahadhari za haraka.

Mheshimiwa Spika, pia, barabara hii haina vizingiti nya kupunguza mwendo (*road bumps*). Siku hizi kuna Vijiji vikubwa, vina msongamano wa watu, haya magari yanakuja yakiwa yameweka *full speed*, matokeo yake ni kwamba wananchi wengi aidha, wanakoswa koswa kugongwa au wanagongwa na magari haya na pengine yanaleta usumbufu mkubwa sana. Kwa hiyo, naomba sana suala hili lizingatiwe.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu vivuko nya ng'ombe. Huwezi ukasema kwamba una barabara na usiweke vivuko nya ng'ombe. Ziwa liko upande wa kushoto na watu wanaishi upande wa kulia, kwa hiyo, ni lazima ng'ombe watoke upande wa kulia kwenda kunywa maji ziwani. Sasa, kunapokuwa hakuna vivuko ni hatari kubwa sana! Kwanza barabara kuu yenewe inachimbika na vile vile, ni hatari hata kwa mifugo hiyo. Kwa hiyo, naomba vivuko hivyo viwekwe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, napenda kusifia uamuzi wa Serikali wa kuwauzia Watumishi wake nyumba. Ni uamuzi mzuri na kwa kweli Serikali iliamua toka siku nyingi na sasa hivi imetekeleza.

Napenda kushauri kwamba tuunde Mfuko maalum wa kuongeza fedha kila mwaka. Tuwe tunaongeza fedha kwenye Mfuko huo kama ilivyo kwenye Mfuko wa Barabara. Pia, kila mwaka watumishi kadhaa wa umma wanaokuwa na *access* kwenye Mfuko huo wajengewe nyumba na kukopeshwa. Hali hii itawasaidia sana Watumishi wote ambao wanahitaji kupewa mkopo, si baadhi tu ya Watumishi ambao wanaishi kwenye nyumba chache za Serikali, tupanue wigo. Hali hii itawasaidia sana Watumishi wa Serikali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge tumekopeshwa magari, lakini tunafanya kazi za umma. Hebu jiulize, mkopo nichukue mimi, halafu nikafanye kazi za umma, wakati mtumishi mwengine wa umma anakopeshwa gari na anakopeshwa nyumba! Mambo kama haya nadhani sasa hivi tujaribu ku-*harmonize*, kwamba sote ni watumishi wa umma, pengine tunaweza kuwekwa tu katika categories mbalimbali Watumishi wa umma wanakuwa na magari ya Serikali ambayo yanakuwa *full service* na Serikali, lakini Mbunge leo ukimwongeza posho kidogo Wananchi wanalamika! Hiyo posho inakwenda kwa wananchi vile vile! (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nadhani kuna haja ya kuangalia suala hili kwa umakini sana. Tusianze tu kuuliza kwa nini Mbunge apewe posho kubwa kuliko Watumishi wengine? Wanasema, aaah, ni lazima ifuate *scale* za Watumishi wote! Lakini inapofikia masuala kama hayo ya mafao mazuri, Mbunge anaambiwa, wewe kaa pembeni kwanza! Napenda

kushauri kwamba kuna haja ya kuangalia suala hili kwa upana wake ili kusudi mafao hayo yaweze kugusa watumishi wote wa umma na waweze kupata huduma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hizi zote ni nguzo tatu ambazo wote tunazifahamu, ni kwa nini nguzo mbili zifikiriwe zaidi na moja isifikiriwe? Nadhani hii iwe ni kama changamoto kwetu sote. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Sawa sawa.

**MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA:** Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuzungumzia kuhusu nyumba za *National Housing*. Nadhani madhumuni yake makubwa ni kuwasaidia watumishi wa Serikali.

Sasa, ni kwa nini tuisiwa kipaumbele wao ndiyo wapange zile nyumba? Kwanza ofisi nyingi zipo Mjini, lakini wanaopanga kwenye nyumba hizo ni watu ambao ni wafanyabiashara na wana uwezo wa kujenga nyumba nyingine!

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini tusitathmini na kutoa mapendekezo ni watu gani ambao wanatakiwa kutumia/kupangishwa nyumba hizo za *National Housing*? Tunatoa kipaumbele kwa watumishi wa Serikali kama mojawapo ya changamoto. Watumishi hawa hawana mishahara mikubwa, unategemea watafanya nini? Wafanyabiashara wana uwezo wa kujenga nyumba mahali popote wanapotaka, lakini wameng'ang'ana kurundikana kuishi katika hizo nyumba! Kuna haja ya kuwa wazi na kuelezana ukweli kwamba linalofaa tulifanye kwa mujibu huu na kwa nafasi hii ambayo kila mmoja atawenza kunufaika nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe changamoto kwa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Gideon Cheyo, kwamba kuna haja ya pengine kutazama suala la nyumba za *National Housing* ili wasaidiwe zaidi watumishi wa Serikali ambao ndiyo wanahitaji zaidi. Hao wengine wameishi miaka nenda rudi, wanarithishana tu hizo nyumba, anatoka fulani anamrithisha mwanaae, ndugu zake na kadhalika, lakini wana uwezo wa kujenga nyumba nyingine! Ni vema watumishi wa Serikali tuwaangalie katika jicho la namna hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nizungumzie kuhusu Jiji la Mwanza. Jiji hilo sasa hivi limejengeka na linaendelea kujengeka, barabara nyingi zilikuwa ni za vumbi, lakini napenda nilihakikishie Bunge lako Tukufu, kwamba mpaka karibu na Mjini sasa hivi lami imeanza kuingia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakumbuka tulikutana *airport* wakati fulani ukasema kwamba: "Sitaki kwenda Mjini kwa sababu ya vumbi!" Najua huo ulikuwa ni utani tu, lakini barabara sasa zinajengwa na ni kazi nzuri inayofanywa na Chama Cha Mapinduzi, safi sana. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo moja ambalo tunalifanya ni kufanya vitu nusu nusu na pengine labda ni kwa sababu ya fedha tunazopata kutoka kwa wahisani zinakuwa

hazitoshii, lakini kuna haja ya kuangalia namna gani unaposema kwamba hili ni Jiji. Jiji la Mwanza, lisaidiwe kupata miundombinu mahsusii ya kufanana fanana na Jiji.

Mheshimiwa Spika, katika Jiji la Mwanza sasa hivi tunajenga barabara lakini hakuna taa hata za kuongozea magari. Sasa hivi pale Mwanza kuna msongamano mkubwa sana wa magari katika ile barabara ya Nyerere. Lakini vile vile barabara inayokwenda uwanja wa ndege, nina imani nayo itakuwa na msongamano mkubwa wa magari.

Nadhani ni vema kama kuna mipango mahsusii ya Wizara isaidie Jiji la Mwanza, kwa sababu haina maana kujenga barabara halafu bado ukawa huja-solve baadhi ya matatizo ambayo wananchi wanaendelea kukabiliana nayo! Napenda Jiji la Mwanza lifanane na Jiji kwa hadhi ya Jiji.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka wakati ule wenzetu wa Dar es Salaam baada ya kuwa limeshatangazwa kuwa ni Jiji na likapata huduma mbalimbali, hata Wahisani wengine waliwekeza fedha na hii ilisaidia sana Jiji hilo kuweza kukua na kupanuka vizuri zaidi. Naomba jitihada hizo hizo pamoja na nguvu za Serikali zielekezwe katika kulisaidia Jiji la Mwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia kuhusu *Board of Materials Management*. Wenzetu wa Kambi ya Upinzani nadhani labda walikuwa hawajafanya utafiti wa kutosha, jana walizungumza kwamba ni Bodi ambayo haina Viongozi na haifanyi kazi vizuri! Nadhani hawakuwa na taarifa za kutosha na pengine nasikitika kusema kwamba hawafuatilii hata takwimu na taarifa kwenye Vyombo vya Habari!

Bodi hii inafanya kazi vizuri sana na taaluma ya ugavi hapa nchini imeanza kupata thamani tofauti na zamani. Sasa watu wanajua kwamba unapozungumzia fedha, si fedha tu unazoweza kuhesabu, vifaa ni fedha tena ambazo ni kubwa zaidi. Naomba Serikali iwekeze jitihada za makusudi katika kuisaidia bodi hii, ili iweze kukamilisha malengo yake na kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria na. 9 ya mwaka 1981. (*Makofi*)

Kwa kweli Waziri Mheshimiwa John Magufuli, amejitahidi sana kuisaidia bodi hii kinyume na huko nyuma ambako haikupata usimamizi wa karibu wa Wizara. Ninaamini kwamba katika Bajeti hii Mheshimiwa Waziri ameweze kutenga fedha kwa ajili ya Bodi hiyo. Naomba sasa iwe ni msisitizo kwa Serikali yetu yote, tusiwaangalie wanataaluma kwa kuangalia baadhi na baadhi yao tukawakejeli! Nadhani kila taaluma ina msingi mkubwa sana katika kuchochea maendeleo ya Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, kabla muda wangu haujaisha napenda sasa niishukuru sana Wizara ya Ujenzi kwamba barabara za Jimbo la Busega zimeanza kuonekana kama ni barabara kwa sababu zinajengwa na hata ninapokuwa Jimboni ninatembea kifua mbele na kwa jeuri kabisa na kusema: "Sasa mnaona jinsi CCM inavyofanya kazi." (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, zamani wenzangu wa Upinzani, majirani zangu wa Chama cha *UDP* walikuwa wanatucheka sana, wanasema: "Ukiwa katika barabara za *UDP*, unalala usingizi, lakini ukiingia za CCM unaamka!" Walikuwa hawasemi ni barabara za Tanzania au za Wilaya, lakini sasa kibao kimegeuka! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jana walisema kwamba: "Ooh barabara fulani eti haina Mkandarasi wa kutosha." Si sahihi, Serikali yetu haibagui, inajenga barabara kwa kuzingatia umuhimu wa kila barabara na bila kujali kwamba hii ni barabara na iko chini ya nani, kwa sababu inaangalia Watanzania wote na mambo ya siasa yanafuatia baadaye. Lengo la Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni kuhakikisha kwamba inamtazama Mtanzania popote pale alipo bila kujali Itikadi yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, nazidi kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, lakini nina ombi. Pamoja na kutenga fedha kidogo kwa ajili ya barabara ya Lamadi - Mkula - Sapiwi na Nyashimo - Shigala - Ngasamo...

(*Hapa kengele illia kuashiria muda wa Mzungumzaji kumalizika*)

**MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA:** Mheshimiwa Spika, naunga hoja hii mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**MHE. PHILIP A. MAGANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Awali ya yote napenda kuungana na wenzangu waliotangulia kwa kuwapongeza sana kwa kazi nzuri waliofanya, Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa John Magufuli, Naibu wake Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Katibu Mkuu wake Ndugu John Kijazi, ambaye kabla ya kuwa Katibu Mkuu katika Wizara hii alikuwa ni *Regional Engineer* wa Mkoa wa Lindi, kwa hiyo anaewela sana matatizo ya kule. Ninawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwape raha wafanyakazi wa Wizara hii. Nawapongeza sana katika mipango yao ya ujenzi wa barabara ya kutoka Dar es Salaam - Lindi - Mnazi Mmoja. Kwa kweli ujenzi wa barabara hii umefanya ndoto imekuwa kweli! Kwa mara ya kwanza wananchi wa Mikoa ya Kusini baada ya ujenzi wa barabara hii kumalizika, watajisikia na wao kuwa ni sehemu ya Tanzania, kwani kabla ya hapo walikuwa wanaitwa Watanganyika na hata wale Maafisa wa Serikali waliokuwa wanapelekwa Mikoa ya Kusini, walikuwa hawapendi kwa sababu ilikuwa inaunda Tanganyika, lakini naamini kwa hatua hii ambayo Serikali ya Awamu ya Tatu imechukua, baada ya muda si mrefu sana Maafisa ambao watakwenda kule watakuwa sehemu nyingine ya Tanzania na siyo Tanganyika tena. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hatua za awali ambazo amezichukua katika azma ya ujenzi wa barabara ya *Mtwara Corridor*. Kama alivyoeleza kwenye kitabu chake, hatua za kwanza zimeishachukuliwa kwa kupata fedha ambazo sasa hivi zinafanyiwa uchambuzi yakinifu ambao bila shaka wakimaliza

itafuatia hatua za ujenzi. Nawapongeza sana kwa hatua hizo na tatu, napenda kumpongeza Waziri na Wizara yake kwa uamuzi walioufanya wa kuifanya barabara ya kutoka Nanganga - Ruangwa - Mandawa - Milola - Ngongo na kurudi Lindi kuwa barabara ya Mkao.

Lindi kuwa barabara ya Mkao ilipandishwa *grade*. Nzuri zaidi kabla sijatoka Lindi niliambiwa na *Manager* wa *TANROAD* Mkao, kwamba barabara hiyo sasa tupatiwe fedha kutoka *OPEC* na kwamba itapanuliwa na kuwekwa kokoto na hivyo kupandishwa daraja kuwa sasa kiwango cha changarawe kama anavyosema Mheshimiwa Waziri mwenyewe. Nampongeza sana kwa hatua hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna barabara nyingine ambayo imechukuliwa kama barabara ya Mkao ambayo ni muhimu sana kwa Wakazi wa Ruangwa, Nachingwea na pengine Masasi, kwa wale ambao wanataka kufika Dar es Salaam kwa haraka. Barabara hii ni barabara ambayo inatoka Ruangwa kupitia Mbekenyela, Namichiga, Nambilanje na Nanjilinji katika Wilaya ya Kilwa, Likawage mpaka Nangurukuru. Barabara hii ni barabara ambayo inaharakisha sana safari ya kuja Dar es Salaam kwa wale ambao wanatoka Masasi, Nachengwea na Ruangwa kwa kiwango cha km 100 kwa saa. Nashukuru na kuipongeza Wizara kwa hilo. Lakini vile vile ningeomba sasa kwa barabara hiyo Waziri ahitimishe ahadi ambayo ilitolewa huko nyuma kabla yeye hajawa Waziri kwamba, Daraja la Mbwemkulu, ambalo linaunganisha Kijiji cha Nambilambi na Nanjilinji litawekwa daraja lile ambalo likikuwa limehamishwa kwenye Mto Mbwemkulu kati ya Mandawa na Lindi. Naomba hilo litimizwe, najua daraja lile ni mali ya Serikali ya Taifa zima na siyo mali ya Mkao, lakini kwa sababu liko pale tayari tungeshukuru sana kama walivyoahidi kwamba, daraja hili lingehamishiwa katika sehemu ya juu ya Mbwemkulu ili barabara hiyo iweze kupitika wakati wowote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nirudie kwenye suala la ujenzi wa barabara hususan *maintenance* ya barabara. Wabunge waliotangulia wamezungumza sana suala hili la *maintenance* ya barabara na mimi ningependa kuongezea kwamba, kujenga barabara ni kitu kimoja kizuri, lakini kujenga barabara peke yake si hatua nzuri sana kama hakuna hatua thabiti zinazochukuliwa za kukarabati mara kwa mara, ndiyo maana unakuta barabara zinaanza kuharibika muda siyo mrefu baada ya kujengwa kwa kiwango cha lami.

Zamani katika Wizara hiyo, naamini mpaka sasa katika *TANROAD*, kulikuwa na kada ya Maofisa wanaoitwa *Road Inspectors*. Watu hao kazi yao kubwa ilikuwa ni kukagua barabara *regularly* na kuhakikisha kwamba, *infrastructure* ambayo imewekwa ipo *in place*, kama inatakiwa ukarabati basi unaandaliwa mpango wa kukarabati. Kwa hiyo, sina hakika sana kama kada hiyo hivi sasa ipo. Lakini kama haipo nani anafanya kazi ya *inspection* ya barabara? Najua Mheshimiwa Waziri yuko makini sana katika ukaguzi wa barabara, lakini kwa kweli siyo kazi yake ni kazi ya makada wenyewe ambao wamewekwa *special* kwa ajili ya shughuli hiyo.

Mimi nitatoa mfano, ilipokuwa inajengwa barabara kutoka Dar es Salaam mpaka Tunduma na Kampuni ya *Nello Teer* kwa mfano, walikuwa wameweka miundombinu ya

kutengenezea kokoto au changarawe, mojawapo ilikuwa ni ya Mikese ambayo baada ya barabara kutengenezwa niliamini kwamba, ingechukuliwa na Serikali ili waweze kuendeleza kutengeneza changarawe au kokoto kwa ajili ya *maintainance* ya barabara hizi. Lakini kwa bahati mbaya ile *facility* ambayo ilijengwa pale, mitambo yake imeonza sasa hivi nadhani haifai tena. Hiyo ni moja tu, tunakuwa na zingine ambazo unawenza kuona huko njiani sehemu za Kongwa na kadhalika, ambazo zimeachwa na Makandarasi waliotangulia kuiachia Serikali iweze kuendeleza kazi ambayo ilianza, lakini Serikali imetelekeza yote hiyo na kuacha inaharibika. Kwa kweli huu ni uharibifu wa mali ya umma. Naomba sana Wizara husika ingekuwa inajali *facilities* hizi ili ziwawezeshe katika ukarabati barabara mara kwa mara.

Mfano mwagine wa ukosefu wa ukarabati wa barabara ambao Waheshimiwa Wabunge wakati tunakwenda kila siku Dar es Salaam tunapoendesha magari yetu tunapitia kutoka hapa Dodoma mpaka Dar es Salaam ni Daraja la Dumila pale njia panda ya kwenda Magoli. Daraja lile mimi nilikuwa naliangalia miaka mitano iliyopita, mchanga unazidi kuongezeka mwaka hadi mwaka, ile *capacity* ya daraja ya kupitisha maji sasa hivi imepungua sana. Mimi naamini msimu unaokuja maji yatajaa mpaka juu. Mwaka huu tumenusurika kwa sababu ya ukame. Kungekuwa na mvua za kawaida mimi naamini kabisa mwaka huu maji yangejaa na daraja lingekuwa limezibwa kabisa na maji yangepita juu ya barabara. Kujenga dajara ni *very expensive*, kwa hiyo, naomba Wizara husika wafanye utaratibu wa kufukua ule mchanga ambao unaziba daraja na kuhakikisha kwamba, maji au mafuriko ambayo yanakuja kuleta mchanga yote yanapita chini ya daraja, vinginevyo sehemu ile yote itakuwa imeharibika kabisa na kutakuwa hakuna mawasiliano kati ya Dar es Salaam na Dodoma. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni hilo hilo juu ya *maintenance* ya barabara hasa uharibifu unaofanywa na madreva wenye magari makubwa. Barabara zinajengwa kwa gharama kubwa sana lakini utaona watumiaji wa barabara hizi wenye magari makubwa hawajali kabisa katika matumizi yake. Magari wanaya-park ovyo ovyo barabarani, wanapita pembezoni na hivyo kuharibu ile *collar* ya barabara na najua wanataka *collar* sehemu ya pembedi na hivyo kuanzisha makorongo ambayo baadaye yanaharibu kabisa mfumo wa barabara.

Mbaya zaidi umekuwa kama ni mtindo wa madreva, mimi nadhani ni mtindo wa kuvunja madaraja kwa makusudi, ninavyoona. Daraja limejengwa vizuri sana zile *edges* zipo wazi, lakini anakuja dreva anagonga zile *edges*, anakwenda zake. Mimi natoa rai kwamba, watu wenye tabia kama hiyo wapate adhabu na watakiwe ku-*repair* madaraja haya ambayo wameyaharibu na kama hawana fedha basi wafilisiwe kwa sababu hatuwezi kukubali fedha za wananchi ziwe zinatumika kuweka miundombinu hii halafu anakuja mtu mmoja anaharibu kwa dakika moja au mbili. Kwa kweli hili naomba Wizara iweke mikakati mizuri ya kusimamia na kama itabidi iwekwe sheria kali, kuwataka hawa ambao wanafanya uharibifu kama huo walipe gharama zote za *maintenance* ya barabara na kuja ku-*repair* huo uharibifu ambao wamefanya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nisingependa kugongewa kengele ya pili, lakini napenda tena kuchukua nafasi hii, kuishukuru Wizara ya Ujenzi, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya na

wanaendelea kuifanya na kuwaomba waendelee na moyo huo ili baada ya muda si mrefu kama anavyosema mwenyewe, watu waweze kuendesha magari ya taxi ndogo ndogo badala ya mashangingi kutoka Mtwara, Masasi, Ruangwa, wakati wameva suti safi mpaka wanapofika Mwanza, bila kubadili nguo, kwenda *night club* pale. Naamini kwamba siku hiyo haiko mbali sana.

Baada ya kusema hayo, napenda kurudia kusema kwamba, naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie machache. Mengi yameshasemwa jana, leo sasa tuko hatua za mwisho na mimi niweze kuchangia machache sana. Kwanza, niwaunge mkono wote walioongea kwa kuwapa pongezi, kumshukuru Waziri na timu yake ya watalaam, pamoja na Naibu Waziri. Naunga mkono hoja hii kwa hiyo na mimi nawapa pongezi kama zile au mara tatu yake. (*Makofi*)

Sasa katika kuchangia kwangu nadhani nitakuwa na maeneo machache tu. Kwanza kabisa, ni *TANROADS* ambayo bado ina utata wa kueleweka wanachofanya. Wanachofanya tunajua wanajenga barabara, lakini uhusiano wao na wenzao wanaojenga barabara pia hauko wazi kama wale *District Engineers* wako wengi na *TANROAD* amechukua *Regional Roads*, lakini haijulishi wanahusiana vipi na yule anayeitwa *District Engineer*, ndiyo mwenye kazi za kila siku katika Wilaya. Nadhani hii ingekuwa wazi halafu na wote tuweze kusaidia katika mazungumzo.

La pili, kwa *TANROAD* ilivyo sasa hivi itaelekea kuwa ni *temporary*. Fedha za misaada zikiisha wale wahisani wakiondoka na nadhani *TANROAD* itakuwa imekwisha tutarudi kwenye *Regional Engineer*. Nasema hivyo kwa sababu imeshatokea mara nyingi tulikuwa na ile *Integrated Rural Road*, ilipokwisha awamu ya kwanza na hata sijui awamu ya pili kama ilikwisha, tukaingia mradi mwengine wa *PEHCOL*. *PEHCOL* walileta *World Bank* na ule wa kwanza world bank ilipokwisha au ilivyokwisha au bado ipo hatuna uhakika. Lakini kwa kweli haipo na haipo *unsermoniously* wanaondoka na mradi unakwisha.

Sasa nashauri *TANROAD* iundwe katika mfumo kama wa *TRA* kwa ajili ya umuhimu wa sekta hiyo ya barabara na uchukuzi, nilidhani kuwa ingetengezewa mfumo kama wa *TRA* ni jirani na Wizara na lakini pembeni ikapewa mamlaka na majukumu na fedha za kutosha iwe siyo shirika, siyo Wizara hapo katikati, lakini ina uwezo wa kufanya kazi zake kwa ubora zaidi kama wanavyofanya *TRA*. Watakuwa na matatizo ya hapa na pale lakini bado tunaweza kuya-control na kujua na kupanga kuwa unakwenda wapi toka ulipo, kesho utafanya nini na mwaka ujao au miaka mitano, kumi, utafanya nini na kwa urahisi zaidi. Lakini kama ilivyo sasa tunafanya zile tu za sasa hivi na mara baada ya kupitisha Bajeti wanaanza kuandaa ya mwaka kesho. Kwa hiyo, ni kila siku kwa kila siku badala ya upangaji wa muda mrefu.

La pili nililotaka niongelee ni barabara zinazounganisha nchi kwa nchi kama vile barabara zetu nyingi. Tuseme sisi tulivyokaa kama daraja *either* daraja linakwenda *West*

toka *East* na toka *North* kwenda *South*. Kwa hiyo, tukitaka kuunganisha *Southern Africa* kama ni *Mozambique*, *Zambia*, *South Africa* yenyewe, *Zimbabwe*, *Kenya*, *Uganda* na nchi za Kaskazini sharti zipite *Tanzania* waende huku. Sasa katika hilo na sisi tuanze kufanya mfumo wetu wa barabara, tuanze kuziweka hizi kuwa ni za *international* na kuwa zitatusukuma *either* biashara au *service* lakini zote ziwe zinaleta fedha katika nchi yetu. Kwa hiyo, katika *North to South* ziko kama tatu hivi, ningependa kuongeza kwenye ramani ya Wizara pale ukurasa (0) naona ziko nyingi *red, blue, yellow*, lakini hizo tatu ni zile wenzangu wamezitaja zinatokea *Mombasa*, *Tanga* kupitia huko *Saadani*, *Pangani*, kuja *Dar es Salaam*, *Lindi* iingie *Mozambique* na zile zitakwenda mpaka *Cape Town*. Sasa kwa upande wa *Tanzania* zimejengwa bado vipande tu kama hiyo ya kutoka *Tanga* kuja *Bagamoyo*, ukifunga ile umeshafika *Mtwara*. Labda miaka miwili mitatu ijayo. Hiyo moja.

Nyingine ni ile ya kutoka *Nairobi* au ilikuwa inatoka *Cape to Cairo*. Sasa kwa sehemu ya *Tanzania* imeshajengwa upande wa *Namanga* mpaka *Arusha*, lakini bado vipande viwili tu vinaudhi vya *Arusha - Dodoma - Iringa*. Tukishafunga hizo tumeshafika *Cape Town* kwa lami. Lakini zaidi ya hiyo, siyo lazima tuwe hiyo ya *Cape Town* ya zamani, labda tuwe na *Cape Town* mpya ukifika pale *Makambako* unakwenda kusini *Songea*, ukifika *Songea* unavuka *Mto Ruvuna* ni kilometra kidogo tu labda kama km 80 unaweka daraja na daraja hilo lipo, lilikuwepo na waliahidi kuwa litarudishwa wakiwa *Mozambique* wako tayari. Basi ile utafika *Lichinga* ni *Headquarter* ya *Nyasa Province* ya *Mozambique*. Ukgusa *Lichanga* umeshafika *Cape Town*. Ya pili hiyo.

Ya tatu nafikiria toka *Mwanza* kuja *Tabora* ukifika *Sikunge* unakatisha *Chunya - Mbeya*. Ukihafika *Mbeya* umeshafika nchi za *Kusini*. Kama unataka *Zambia* na *Zimbabwe* utapita hiyo *Cape Town to Cairo*, ukitaka *Mozambique* utapita hiyo niliyosema ya *Songea*. Kwa hiyo, nilidhani niongeze hizo tatu kwa ajili ya biashara au *service* kwa majirani lakini ni *service* ambayo tunaweza *ku-charge* fedha tukapata *revenue* ya kutosha. (*Makofifi*)

Lingine nilitaka kukumbusha kuwa tulikuwa na mradi mwaka 1996 wa kujenga Daraja la kutoka *Songea* kwenda *Mitomoni* kwenda *Mozambique*. Sasa *Mozambique* hawakuwa tayari kwa kuwa bado hatukuwa tumeamua kuhusu *unit bridge*. Lakini bahati nzuri kwa bidii ya *Waziri John Magufuli*, wamesaini *memo of understanding* nadhani mwishoni mwa mwaka 2002 . Kwa sasa na wao wako *ready* kujenga lile daraja na upande wao wameshajenga barabara toka *Lichinga* mpaka hapo kwenye Daraja ambayo haikuwepo. Sasa wameshajenga pamoja na *Migration* na *Custom* na kadhalika. Sasa hilo ni ombi kwa *Waziri* kuwa atusaidie daraja na fedha za kutengenezea ile barabara zirudi ili tuunganishe iwe barabara moja mpaka *Mozambique* kwa kuwa sasa hivi hatuna namna ya kwenda *Mozambique* kuna mto, kwenda *Malawi* kuna ziwa. Kwa hiyo, tupo hapo hapo tunakuwa tunakwenda na kurudi sehemu hii. (*Makofifi*)

Halafu lingine nilitaka kuzungumzia kwa ufupi nalo ni kuunganisha *Mkoa* wa *Ruvuma* na *Mkoa* wa *Morogoro*. Sisi tuna bahati nzuri tunayo *Morogoro* inafika mpaka karibu ya kijiji changu cha *Madaba*. Lakini hatuna barabara ya kukatisha toka *Ruvuma* au

Songea kuja Morogoro kwa namna yoyote ile, tukitaka kuja Morogoro aidha tupite Iringa tuzunguke tuingilie Morogoro kwa upande wa Magharibi badala ya kuingilia Morogoro kwa upande wa kusini tuliko sisi. Hivyo tukitaka kufika kuna njia nyingine ni hiyo sasa inayochongwa Lindi tupandie Kilwa, tutokee Rufiji halafu tuje Morogoro ili tuanze upya tufike Dar es Salaam kwenda Morogoro. (*Makofi*)

Basi tunaomba kuwa sisi wenyewe Wabunge wa Ruvuma na Morogoro tunaopakana tunayo Kamati yetu tunazungumzia kila mwaka, tunajaribu kufanya kwa mkono kuwahamasisha wananchi wetu wafanye kwa mkono labda ningeomba kuwa Wizara itufikirie kutupa nguvu kama kuchanga tutachanga lakini sidhani kama tutamaliza muda wa miaka michache, itachukua miaka mingi sana mpaka kutoboa hiyo njia, kama wanawenza kutusaidia angalau madaraja au *buldozer* hata sisi tutachangia mafuta ikibidi, lakini hasa tunahitaji msaada tuunganishwe *Songea to Morogoro* kupitia Malinyi na Kitanda. Vijiji hivyo viwili vikiunganishwa, sisi tutakuwa tayari tumeshaunganika na majirani zetu wa Morogoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka niseme hayo machache. Kwa kuwa naona *time* imekwisha, sitaki kengele ya pili inigongee na nitashukuru sana na zaidi nazidi kuwapongeza na kuwatakia afya njema na kheri na wawe na juhudhi hiso hiso Wizara ya Ujenzi tufike huko tunakokwenda. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, nami niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Ujenzi. Nami pia nampongeza Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa John Pombe Magufuli, pamoja na Naibu Waziri, kwa hotuba nzuri na fupi. Pia napenda kuwapongeza Wataalam waliotayarisha hotuba hii. Awali ya yote, ningependa kusema ninaunga mkono hotuba hiyo kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Baada ya kusema hayo, naomba sasa nianze kuchangia kama ifuatavyo: Naipongeza Serikali kwa kukamilisha ujenzi wa Daraja la Mto Rufiji. Hivi sasa usafiri wa kutoka Mikoa ya Kusini - Lindi na Mtwara kuja Dar es Salaam *and vice versa* umekuwa rahisi mno. Magari yanachukua muda mfupi kuwasili Dar es Salaam hivi sasa. Kwa kuwa kukamilika kwa daraja hili ni hatua kubwa sana katika ujenzi wa barabara iendayo Mikoa ya Kusini, namwomba Mheshimiwa Waziri, aandae taratibu za kuzindua daraja hilo mapema iwezekanavyo. Hii itawasaidia wananchi wetu kuelewa nini Serikali ya Chama cha Mapinduzi inafanya. Pia nataka kuku hakikishia kwamba, hata Vyama vyta Upinzani, daraja hilo sasa wanaanza kulitumia na linawafikisha hapa bila matatizo. Katika kufanya hivyo, naamini kabisa mwaka 2005, CCM itashinda kwa kishindo mara dufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kukamilika kwa daraja hilo, namwomba Mheshimiwa Waziri, aendelee kufuatilia kwa karibu zaidi makandarasi waliopewa barabara hiyo kwenye sehemu zilizobaki, asisite kuchukua hatua kali kwa wale makandarasi watakaokwamisha mradi huo kukamilika kwa wakati muafaka.

Baada ya kueleza hayo sasa ningependa kuelezea machache kuhusu barabara zinazokwenda katika Jimbo langu la Liwale. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa kutujali Wana-Liwale, kwa kuiboresha siku hadi siku barabara inayotoka Nangurukuru kwenda Liwale. Barabara hiyo ni fupi mno ukilinganisha kutoka Nangurukuru kwenda Lindi hadi kufika Liwale. Ni barabara ya manufaa kwa wafanyabiashara na ni ya manufaa kwa wananchi kwa ujumla, kwa kuwa bidhaa zinazosafirishwa katika barabara hiyo ambayo ni fupi zinapatikana kwa bei nafuu kwa wananchi wa Liwale. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu Waziri, asichoke tunapokuwa tunamfutilia kwa karibu zaidi kuhusu kuiboresha barabara hiyosiku hadi siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza *Manager* wa Mkoa wa TANROAD Lindi, kwa ushirikiano tunaopata kuhusu utengenezaji wa barabara hiyo. Pia ningependa kutoa shukrani ambazo wamezitoa wananchi wa Liwale kwa ujenzi wa haraka wa Daraja la Mto wa Mihumu, daraja hilo linaitwa Daraja la Kibutuka. Daraja hilo liliharibika ghafla mapema Januari, baada ya kupeleka taarifa kwa Mheshimiwa Waziri kuitia kwa Naibu wake, alinihakikishia daraja hilo litatengenezwa kwa muda mfupi. Kilichotokea ni kwamba, daraja hilo lilijengwa kwa muda wa wiki mbili hadi tatu likawa limekamilika, haijawahi kutokea! (*Makofi*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, nakushukuru na wananchi wa Liwale wanakushukuru na usichoke kutusaidia, *I salute you. (Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo pia ningeomba Mheshimiwa Waziri, atusaidie Wana-Liwale, anapoboresha barabara zetu kusema kweli siyo kwamba ni suala la barabara peke yake. Barabara ya Nangurukuru kwenda Liwale ikiwa nzuri, barabara ya kutoka Nachingwea kwenda Liwale ikiwa nzuri, kutokana na hali halisi ilivyo katika eneo hilo kwani tuna wanyamaporu wakali, inapotokea kwamba barabara ni mbaya na usiku unasi mama kwa kuangalia ile barabara madhara yake ni makubwa sana kwa maisha ya binadamu.

Kwa hiyo, tunakushukuru sana, umeokoa sana maisha ya Wana-Liwale, tunapotumia barabara ile inakuwa haina vikwazo maeneo yale ambayo yalikuwa na vikwazo. Tunakushukuru sana, umetuokoa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Liwale imefungika iko pembezoni kwa hiyo ni muhimu sana ikafikika kwa njia ya barabara, kama siyo ile ya Nangurukuru kwenda Liwale, basi ile ya kutoka Nachingwea kwenda Liwale. Hivyo, ni muhimu kwa kuwa pia hatuna mawasiliano mengine yoyote hata ya simu hatuna bali tunategemea barabara hiyo. Ili kutukomboa zaidi Mheshimiwa Waziri, nakuomba kuna barabara ya asili ambayo inatoka Liwale inapita Lilombe na kwenda Tunduru, ningeweza kumtembelea Naibu Spika wangu kwa urahisi sana kwa kutumia barabara hiyo. Hapo kikwazo kikubwa ni Daraja la Mto Ruhuhu ambalo liko Lilombe. Nimejaribu kuwasiliana na Naibu Waziri kwa suala hilo, nadhani limeshakufikia Mheshimiwa Waziri. Tunakuomba wananchi wamenituma nikukumbushe maombi hayo kwa njia hii ya kuchangia katika hotuba yako. Nadhani maombi haya yamefika kwa wahusika. (*Makofi*)

Pia kuna barabara ambayo inatuunganisha sisi na Ruangwa inatoka Liwale - Mirui kwenda Wilaya ya Ruangwa na hapo pia tukipewa daraja, Waziri wetu wa Ujenzi, atakuwa ametusaidia sana na kutuokoa sisi tusijione tuko pembezoni. Pia kuna barabara ya asili nyingine ambayo pia naomba ushauriane na jirani yako Mheshimiwa Zakia Meghji, kwa kuwa hii inahusu maliasili. Hii inatoka katika Wilaya ya Mahenge, Ulanga inapitia Ndapata hadi kufika Liwale. Nadhani kwa hili Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, namwomba pia asaidie kwa kuwa watu wa Liwale, Ulanga, Mahenge hao ni ndugu. Kuboreshwa kwa barabara hii itatusaidia sisi hata kukimbiza mwenge kutoka Mkoa wa Morogoro kwenda Liwale moja kwa moja Mkoa wa Lindi. (*Makofi*)

Baada ya kuyasema hayo, ningependa kurejea tena kwa kusema naunga mkono hoja hii na namshukuru Mheshimiwa Waziri John Magufuli, Naibu Waziri, Wataalam wake, pamoja na wote wanaotusaidia kwa Jimbo la Liwale. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. CAPT. THEODOS KASAPIRA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba niungane na wenzangu kwa niaba ya Watanzania hasa wale wa Jimbo la Ulanga Mashariki, niunge mkono kwa dhati kabisa hotuba ya Mheshimiwa Waziri John Magufuli. Naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Mimi nina sababu moja kubwa kabla zijaendelea na hii ni kwamba, ni mara ya kwanza kuona hotuba ya Waziri ambayo imegusa Mikoa yote 21 ya Tanzania Bara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii, Mheshimiwa Waziri Magufuli, kwa uwezo aliokuwanao na jinsi anavyoifahamu Tanzania, amegusa kila Mkoa Tanzania Bara na kama ungempa uwezo wa kuzungumzia nchi nzima angegusa Mikoa yote 26. Sasa mimi ndio huwa nasema hawa ndio wanaitwa *ma-comrade*. Kwamba huyu ndio *comrade*, wengine wote ni ndugu tu. *Comrade* ni mtu ambaye unakufa naye. Hotuba yake inazungumzia kila Mkoa. Imegusa kila Wilaya lakini utakuta Mahenge, utakuta Kilosa, utakuta Mikumi, kwa hiyo nasema kwa kweli nina sababu kubwa ya kusema naunga mkono mia kwa mia hotuba hii. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana ndugu yangu Mwenegoha, ambaye ni Msaidizi mkubwa sana wa Mheshimiwa Waziri, nampongeza ndugu Kijazi, pamoja na timu yake nzuri. Timu yenu ni nzuri sana kwa sababu kuna wachapakazi, akina John Ndunguru, Mkurugenzi wa Ufundı katika nchi hii, yuko na *Comrade* mwингine Patrick Mfugala, anashughulikia barabara. Timu ni nzuri sana. Timu hii ni ushahidi mwингine wa pili kwamba, hawa wote tangu Waziri wao mpaka Katibu Mkuu wametokana ndani ya Wizara yenye, ndio maana ile *teamwork* inakuwa ni kubwa zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kutamka vitu vichache ambavyo vimegusa Jimbo langu la Uchaguzi la Ulanga Mashariki. Wizara hii wametupatia Wilaya ya Ulanga, Pantoni mpya na ya kisasa katika Mto Kilombero. Nasema ya kisasa kwa sababu Mto ule tulikuwa tunavuka kwa muda wa dakika 45. Baada ya kuweka Pantoni mpya tunavuka kwa dakika mbili. Haijapata kutokeea. Unavuka unafika mahali huamini,

unaangalia itarudi tena dakika mbili? Tulikwishazoea, dakika 45. Nasema kwa kweli ni mafanikio makubwa, mazuri chini ya *Comrade* Magufuli. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pili, nashukuru sana kwa matengenezo ya barabara kutoka Mahenge - Chilombola - Mwaya - Mbuga, barabara nzuri ambayo hivi sasa imetengenezwa kwa mkopo kutoka *ADB*. Namshukuru sana Mama yangu Meghji, ameisimamia kweli kazi hiyo, lakini pamoja na ushirikiano mzuri wa Wizara hizo mbili, hii kazi sasa hivi inafanyika na inaendelea vizuri mno. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru katika kitabu hiki ukurasa wa 64 wametenga fedha kutengeneza barabara ya kutoka Mwaya - Ngongo mpaka Luhombero. Barabara hii ni tatizo kubwa, lakini kwa jinsi nilivyosema mapema, kwamba Mheshimiwa Waziri Magufuli, anaijua nchi hii, basi anajua kuna tatizo la Mwaya - Ngongo - Luhombero na iko ukurasa wa 64.

Mheshimiwa Spika, ipo kazi moja ambayo hivi sasa inaendelea, nayo ni kuweka lami mlima ambao ni mkorofî sana, mlima unaofanya ufile Mahenge Mjini, mlima wa Ndororo na mlima mdogo wa Nyani. Sasa naomba tu baadaye Mheshimiwa Waziri, anisaidie kwa sababu habari ambazo ninazo mpaka juzi ni kwamba, kazi ya kuweka lami inakwenda polepole kidogo. Halafu nimetazama sana kwenye hotuba hii hasa majedwali mbalimbali sikuweza kuona pesa zinazoendeleza ukamilifu wa lami hiyo.

Kuna kero moja ambayo naomba Wizara inisaidie. Nayo ni kwamba, kutoka Mahenge Mjini kwenda Tarafa ya Mwaya ambako hivi sasa inatengenezwa barabara ya kisasa kuna eneo la mlima Bangayao. Tarafa hii ya Mwaya ina Kata nane na Tarafa hii ya Mwaya ndio sehemu kubwa ya msitu wa Selous na wawindaji, *I mean* watalii, kila mwaka wanakwenda kuwinda eneo hilo. Sasa mlima huu wa Bangayao ni mlima ambao una matatizo makubwa sana wakati wa masika hasa kwa utelezi.

Mheshimiwa Spika, ninakumbuka mwaka 1999 wakati nimekuja Bungeni nilimwona Mheshimiwa Waziri, akiwa na nafasi hiyo hiyo katika Wizara ya Ujenzi, nafasi ya Naibu Waziri na Ndugu Kijazi, wakatenga fedha kutengeneza mlima huo wa Bangayao. Sasa ombi langu kuitia kwako naomba Mheshimiwa Waziri, atusaidie kuweka lami sehemu korofî kwa mlima Bangayao. Atakuwa ametengeneza sehemu korofî lami mlima Ndororo kufika Makao Makuu ya Wilaya na anatoa tena viongozi na watalii kwenda kwenye mbuga ya Selous lakini mlima wa Bangayao atakuwa amegusagusa sehemu korofî kwa utaratibu wa kuweka lami. Hiyo ndio kero kubwa sana na ndio kero iliyobakia katika Jimbo langu. Sasa timu hiyo ya Magufuli imenikumbusha yale mazungumzo aliyosema Rais wangu *Commander in Chief* Benjamin Mkapa kwamba, anatengeneza Askari wa Miavuli, sasa jibu lake ni John Magufuli, ndio jibu lake. (*Makofi*)

Anatengeneza Maaskari wa miavuli. Leo hii barabara kama ninavyosema *Comrade* hapa, inagusa nchi nzima. Kwa hiyo, nasema hebu kamilisha basi *Comrade*, Bangayao. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, niseme jambo moja nalo ni kwamba, ni kweli kabisa kwamba Wilaya ya Ulanga utaingilia hapo hapo kwenda Mahenge na utarudia hapo hapo. Nilisema siku moja kwamba, kwa kweli kiusalama, kiulinzi si vizuri sana rafiki yako, adui yako, ajue unakwenda njia hiyo hiyo na unarudi njia hiyo hiyo. Huna hakika kwamba ata-*lay ambush* wapi, kwa sababu huna njia nyingine.

Kwa hiyo, napenda kusema alichozungumza Mheshimiwa Mbunge wa Liwale, ni kweli ipo njia ya kutoka Mahenge kwenda Liwale, ambayo hivi sasa wananchi wanaitumia na wananchi wanasantikizwa na Askari wa Wanyamapori, kama Mheshimiwa Meghji alivyojieleza hapa jana. Njia ile ni nzuri sana, haina matatizo. Sasa angalia ukitoka Liwale kwenda Nachingwea ni Kilometra 80, ukitoka Nachingwea kwenda Lindi ni kilometra 90, ukutoka Lindi kwenda Kilwa 120, ukitoka Kilwa kwenda Dar es Salaam kilometra 180. Kuna Kilometra 470. Lakini ukitoka Mahenge kuja Dar es Salaam ni kilometra 300. Kwa hiyo, yule anayetoka Mahenge kuja Dar es Salaam atafika mapema kuliko anayetoka Lindi, Nachingwea na Mtwara. Ndipo ninaposema hivi kwa nini hawa Watanzania wa Liwale na Lindi, Ulanga wasipate barabara hii?

Hebu niwaachie Wizara ya Ujenzi wakubaliane na Wizara ya Maliasili wafanye kinachowezekana, hatuzungumzii habari ya wanyama, tunazungumzia wanapita watu wa Wilaya mbili tu, wa Liwale na wa Mahenge ambaa sasa ndio wanaopita. Kwa hiyo, tatizo wala sio sera, tatizo ni utaratibu tu kwamba Wizara hizi mbili wanakaa wanamaliza kazi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, nimepata moyo sana kwa jinsi ambavyo Mheshimiwa Waziri alivyoweza kutenga fedha kwa ajili ya barabara inayoendelea kushughulikiwa kutoka Lupiro, Mtimbila, Malinyi, Kilosampepo, kuelekea Songea. Ni nzuri sana na sisi kama Wabunge kama alivyooleza Mheshimiwa Mbilinyi, ni kweli kabisa tunazungumzia uwezekano wa njia ya kutoka Songea kuja Wilaya ya Ulanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mapema kwamba, kwa Askari wa Mwavuli, ambaye ana uwezo wa kukutoa Dodoma na kukupeleka Cairo kwa hakika, unafika Cairo unapata kahawa pale na mtu huyu ni safi. Kwa hiyo, wewe ni Askari wa Mwavuli wa uhakika kabisa. Ukiingia kwenye *jet* yake una hakika utafika. Ombi langu ni moja tu kwamba, timu ya Wizara ya Ujenzi imsaidie. Haipendezi hata kidogo kwa Waziri kufuta Wakandarasi 200. Amejitosa huyu! Anazungumzia maisha ya watu! Mumsaidie! Akifuta Wakandarasi 200 mumsaidie lugha iwe ni moja sio kama anafuta Wakandarasi 200, Mkuu wa Idara mwagine Wizarani anakwenda kumwambia Mkandarasi kwamba ni Waziri Magufuli bwana amekufuta. (*Makofi*)

Msaidieni huyu. Haiwezekani huyu Kiongozi huyu anapanda gari kuja Kituo cha Kibaha kutazama namna gani mizani inafanya kazi. Sasa hii maana yake ni kwamba, mna mtu ambaye na sisi wenzeni tunawaangalia ni namna gani mnamsaidia huyu *Comrade*. Tunawaangalia namna gani mnamsaidia! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutamka rasmi kwamba, kwa kweli naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. FRANK G. MAGOBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie katika hotuba ya Waziri Magufuli. Lakini mimi ningewapongeza wataalam wa Wizara hiyo, kwa hotuba yao nzuri ambayo wamemwandalia Waziri wao. Ila ningempongeza Waziri na Naibu wake, kwa kutekeleza hizi hotuba ambazo zinatayarishwa na wataalam wake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Waziri Magufuli amekuwa mstari wa mbele kutekeleza yale ambayo anayasema hapa na kwa kweli sina sababu yoyote ya kutokumpongeza. Kwa kufanya hivyo, nitakuwa namnyima haki za kibinadamu. Nakubali kabisa kwamba, pesa za Serikali zinafanya kazi hasa katika Wizara ya Ujenzi. Naamini aliyosema Mheshimiwa Mbunge mmoja jana kwamba, sehemu yenye upinzani ni vyema tukashirikiana na Serikali tukafanya kazi kwa maendeleo ya nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuna maneno machache yanayosemwa kwamba, binadamu tunapoumbwa tunakuwa na kasoro mbalimbali. Kila mtu ana kasoro zake. Unaweza ukawa wewe una kasoro ya kutokujua kusoma au kasoro ya kutokujua cha kufanya, lakini nasema yote haya ni mambo ya Mungu. Lakini nasema kasoro zinazojitokeza katika utekelezaji wa kazi ni budi tumsaidie mtu ambaye anasimamia zile shughuli badala ya kumlaumu. Namshukuru pia Mheshimiwa Magufuli kwa sababu anapokea ushauri na anafanya kazi kwa ushauri baada ya kuona kuna kasoro anazopokea anazifanya kazi na hatimaye kufanikisha yale ambayo anatakiwa kuyafanya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Magayane, amezungumza vizuri hapa kwamba Wizara ya Ujenzi ijithidi kuweka alama za barabara hasa tunazoita *reserve roads*. Sasa mimi nisingeweza kurudia tena kulizungumza hilo kwa sababu Mheshimiwa Magayane, amezungumza vizuri sana. Lakini nasema kwamba, kwa upande wangu mimi nimepata hasara kidogo kuanzia Chuo cha Uhasibu Mbagala, Mtoni kwa Azizi Ali, Chalambe hadi Kongowe. Kwa kukosekana kuweka alama za barabarani kumesababisha wananchi wangu kupata hasara kubwa ya kubomoa nyumba zao ambao sasa wanapisha ujenzi wa barabara hiyo.

Kwanza, niipongeze Serikali kwa uamuzi huo wa kutaka kupanua barabara hiyo na kwa sababu pia inasidia kuchangia uchumi na barabara hiyo inakwenda mpaka Mtwara, ni barabara kubwa mno. Sasa wananchi wa Mbagala wamelalamika kwa sababu Serikali imefanya wajibu wake wa kuwaambia wananchi wabomoe nyumba ili waweeze kufikisha barabara. Lakini wananchi hao wamenitura wanasema kwamba, nimwombe Waziri au niiombe Serikali kwamba, wahusika wote waliohusika kuwapa vibali vya ujenzi kwenye hizi barabara wachukuliwe hatua mara moja kwa kutoa hasara hiyo. (*Makofî*)

Kwanza, wamewatia hasara kubwa wananchi wangu wa Mbagala na Kigamboni kwa ujumla na pia wameitia aibu Serikali ya Tanzania ambayo inafanya kazi yake vizuri wakati mwengine. Haiwezekani ukijua kabisa kwamba, eneo hili ni la *reserve roads* lakini unatoa kibali ukiwa wewe ndio msimamizi wa shughuli za Serikali katika maeneo

yale, unatoa vibali watu wanajenga nyumba. Baada ya miaka kadhaa nyumba zile zinakuja kubomolewa ambayo sasa inakuwa ni hasara kwa Watanzania ambao kutokana na hali ya umaskini wamekuwa na hali mbaya sana kiasi ambacho sasa hivi hawajui pa kwenda.

Mheshimiwa Spika, wananchi wangu wanaiomba Serikali kama kuna uwezekano, basi wapewe fidia au kama sio fidia, basi kitu cha kufuta machozi. Kama hakuna kifuta machozi, basi wanaomba wapatiwe viwanja kwa ajili ya ujenzi kwa sababu baada ya kubomolewa nyumba zao wananchi hao hawajapewa hata eneo la kujenga nyumba zao, hawajui waende wapi.

Pili, wananchi hawa wanaomba ikiwezekana basi baada ya kupewa viwanja hivyo, wasaidiwe pia mabati kwa ajili ya ujenzi wa nyumba zao watakapopata viwanja hivyo kwa sababu sasa hivi hawana uwezo wa kujenga nyumba kwa sababu sasa hivi hawana hela na kwa kweli hawana hela kwa sababu waliokuwemo wamejenga humo ni watu ambaao wanategemea nyumba hizo kufanyabiashara zao, lakini hali yao sasa hivi imekuwa ni mbaya mno. Sasa toka wamebomolewa nyumba zao hawajapewa viwanja na wala hawajui waende wapi. Matokeo yake wameingia kwenye nyumba za majirani zao ndio wanajihifadhi. Kwa hiyo, naiomba Serikali kuitia Wizara ya Ujenzi, wananchi hawa wapewe viwanja na pia wasaidiwe katika ujenzi wa nyumba zao.

Mheshimiwa Spika, itakuwa hatukuwatendea haki wananchi hao kama wale waliohusika wapo na wanajulikana kama hawatachukuliwa hatua za kinidhamu kwa kuwatia hasara wananchi hao wa Jimbo la Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye suala la daraja, daraja limezungumzwa na Mheshimiwa Sophia Simba, amegusia pia, nampongeza kwa sababu naona anakaribia kwenye Jimbo langu, sio mbaya. Namkaribisha aje afanye kazi na mimi kwa faida ya maendeleo ya wananchi. (*Kicheko/Makofit*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli daraja la Kigamboni linazungumzwa kila wakati na nimekuwa nikizungumza mara kwa mara mkielewa kabisa kwamba, nina nia nzuri. Mimi nilishasema siku zote kwamba ninapozungumzia ujenzi wa daraja la Kigamboni, sizungumzii kwa faida yangu mimi. Mimi sivuki pale. Mimi nakaa Mbagala lakini kule nazungumzia kwa faida ya Watanzania na Watanzania ni nchi yenye. Kwa sababu daraja lile likijengwa litainua uchumi mkubwa katika Jimbo hilo na Dar es Salaam nzima na Tanzania nzima kwa sababu kule kuna watalii wengi ambao wameshajenga mahoteli yao, sasa vitu vingi wamevikosa. Hakuna barabara, daraja halijajengwa na mbaya zaidi barabara ambayo inakwenda kwenye mahoteli yao hazina lami na zina kiwango cha kokoto na sasa hivi hali imekuwa mbaya zaidi katika barabara hizo. Barabara hiyo ni kutoka Mji Mwema kwenda Pemba Mnazi, Kimbiji, Yaleyale Puna, kote huku kuna mahoteli ya kitalii.

Mheshimiwa Spika, ni hivi karibuni ilijengwa barabara kwa kiwango cha kokoto kutoka Kibada kwenye Kisarawe II. Mpaka sasa hivi hiyo barabara haina hata mwaka lakini imeshakuwa ni mbaya zaidi. Hiyo barabara sehemu za ukingo imebomoka kwa

sababu inawezekana wataalam waliopewa hiyo kazi hawakuwa makini katika kufanya kazi yao. Naomba Mheshimiwa Waziri, hiyo barabara aifuatilie kama alivyokuwa akifuatilia sehemu nyingine. Sisi hatuna sababu ya kudai lami kwa Serikali haina pesa, lakini hata kiwango cha kokoto basi, angalau ipitike kwa muda wa miaka mitano kuliko kutengeneza leo, keshokutwa barabara inakuwa haipitiki, inakuwa haina maana hata moja. Ninaomba mkandarasi aliyefanya kazi hiyo, kama hajalipwa naomba asilipwe kwanza mpaka nipaye maelezo ya kutosha na kama amelipwa, basi hao waliosaini mkataba wao mimi naomba tuonane nao wanieleze kwa nini walisaini mkataba ule na vinginevyo nitataka maelezo ya kutosha. Tusifanye kazi ya kubahatisha! Ndio maana nikasema kuna kasoro mbalimbali ambazo lazima tuziseme Waziri afanye kazi yake vizuri na kama kuna watu ambao wanam-*double cross*, tuwajue ni akina nani.

Mheshimiwa Spika, suala la kivuko cha Kigamboni limezungumzwa pia na Mheshimiwa Sophia Simba, mimi nitazungumzia kwenye kero. Kivuko nashukuru kwamba kinafanyiwa matengenezo mara kwa mara kwa sababu ndio hali tuliyonayo na nashukuru kuwa wananchi wanapata huduma ya kivuko mara kwa mara. Lakini kuna kero pale. Kero ya pale ni ratiba ya kivuko kile haijulikani vizuri. Kivuko hicho kimesababisha wafanyakazi wengi wa Serikali na wa Mashirika na hasa wanaofanya kazi kwa Wahindi kufukuzwa kazi kwa sababu ratiba yake ya asubuhi haijulikani na kuna Wafanyakabiashara wengi na wakulima wengi ambao wanatoka sehemu ya Puna, Pemba Mnazi, Mwongozo, Kimbiji ambao wanalima na wanapovuna mazao yao wanauza Kariakoo kwa sababu kule Kigamboni hakuna soko. Matokeo yake wakulima wangu hao huwa wanavuka saa saba usiku kuja ng'ambo ya Mji kusubiri alfajiri kwenda kuuza mazao yao sokoni, kwa sababu kivuko kinalala huku Mjini, hakivuki kule. Sasa matokeo yake kumekuwa na ugomvi wa ndoa zao kuvunjia mara kwa mara kwa sababu mwanaume anahama kulala huku kila siku kwa sababu lengo ni kufanya biashara. Anahama kila siku analala ng'ambo ya pili, yule mwanamke haelewi anajua kwamba kuna nyumba ndogo zimebekwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuokoa na kunusuru ndoa za watu, ningeshauri kivuko kiwe na ratiba nzuri. Ijulikane kwamba, ratiba hiyo ya kivuko cha kwanza kitakuwa saa ngapi. Kwa mfano, wananchi wangu wameniomba kwamba, niombe badala ya kufikisha saa saba iwe ni *twenty four hours* wavuke watu pale. Kwa sababu hii utapunguza na itasaidia kwa wafanyakabiashara na wakulima kupeleka mazao yao mapema Kariakoo, kwa sababu wakichelewa kupeleka mazao yao, wanawakuta wale wanunuzi wakubwa wameshaondoka na matokeo yake mazao yale yanauzwa kwa bei ya chini sana na ni hasara. (*Makofî*)

Kwa hiyo, ningeshauri Serikali kwa kweli kile kivuko kisiwekewe masharti, kiwekwe saa 24 kuwavusha wananchi. Kwanza kuna masuala ya akina mama ambao wanapopata uchungu, wanahitaji kwenda hospitali. Kule hospitali bado inategemewa kujengwa, inabidi wavuke. Sasa ikifika saa saba kivuko kama hakuna, mtu anaweza kujifungulia ndani ya bahari, kitu ambacho hakina maana. Kwa nini? Kama kivuko kipo, kiwekwe utaratibu mzuri ili *Captain* atakayefanya uzembe katika kuvusha ajulikane. Sasa hivi huwezi ukamlamu kiongozi yejote pale kwa sababu utaratibu hakuna. Haya

mambo ambayo tunayaona yananyanya wananchi tuyaseme kwa sababu ni mambo ya msingi sana.

Mheshimiwa Spika, kero nyingine ni kwa wananchi wangu wanaovuka kwa baiskeli. Baiskeli inatozwa Shilingi mia na abiria Shilingi mia kivuko hicho hicho kimoja. Hivyo ningeomba kimojawapo katika hivyo vyote iondolewe. Kama mtu ana baiskeli kwa mfano ana gari unalipia gari, dreva, unavuka ukiwa kwenye gari yako hulipi, sasa kwa nini baiskeli itozwe nauli? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kibaya zaidi baiskeli ikiwa na mzigo mkubwa, basi inatozwa mara mbili, yaani mwenye baiskeli na mzigo ule. Kwa hiyo, ningeomba hizo kero ndogo ndogo ambazo zinайдhalilisha Serikali ziondolewe. Hizi kazi kama tunesema tunaondoa kero, basi hizo ni kero ambazo zinasumbua wananchi. Kwa hiyo, naomba hili suala lifuatiliwe kwa makini, kero hizo za wananchi hasa wanaovusha mazao yao wapunguziwe matatizo yao katika kuwapunguzia hizo gharama. Kama ni nauli, iwe nauli ya baiskeli, basi iwe ni baiskeli na kama ni mtu avushwe kwa nauli ile ile kuliko kufanya vitu ambavyo vinakuwa vinatumiza vichwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuzungumzia hivyo lakini naiomba Serikali kwamba, barabara ya kuanzia Mji Mwema kwenda Kimbiji, Mwongozo, Yaleyalepuna, Pemba Mnazi na sehemu mbalimbali itengenezwe kwa kiwango cha lami kwa sababu toka imejengwa barabara ya kutoka Kigamboni - Feri kwenda mpaka Mji Mwema ndio mwisho ilipoishia lami, sasa kwenda huko mbele hakuna lami. Sasa hivi wakati wa mvua wananchi wangu wanapata taabu sana kupata usafiri kwa sababu magari yanaogopa kwenda kule kutokana na barabara mbaya na wanajua gharama za matengenezo ya magari siku hizi ni kubwa. Kwa hiyo, mtu hawezi kupeleka gari yake katika hali hiyo.

Kwa hiyo, wameniomba nimwombe Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Magufuli na Serikali kwa ujumla, Waziri Magufuli rafiki yangu hawezi kuniangusha, naomba kipande kile kiwekwe lami. Si kwa kuja kunifurahisha tu mimi lakini kwa sababu sasa hivi tunawashirikisha wananchi, tuyazungumze yale yanayokera. Si kwa faida yangu, lakini yale ambayo ni kero ya wananchi tuyazungumze. Kile ni kipande kidogo sana, nadhani ni kilometra hata sabini hazifiki, wawekewe lami *at least* wapate unafuu wa kusafirisha mazao yao. Tunaposema wananchi walime, basi tuwawekee masoko jirani na kama hakuna soko jirani wanakwenda mbali, kuna maana gani sasa? Maana yake zile gharama za ukulima pamoja na mbolea, tena unachukua usafiri wa muda mrefu si ajabu njiani ukapata hasara, hakuna maana ya kusema umemsaidia mkulima huyu. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Magufuli, ili urafiki wetu usipinguliwe, kile kipande kiwekwe lami hata kwa kutumia njia ya aina yoyote, naomba unisaidie.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ni barabara hii ambayo nilikuwa naizungumzia ya kutoka Uhasibu mpaka Kongowe, kama nilivyosema. Mimi nashindwa kuelewa ni taratibu gani ambazo zinafanyika sasa hivi, maana yake badala ya kujenga barabara tunaona inachimbwa mifereji. Ni nini sasa hicho? Zile fedha ambazo zingechimba mifereji, basi zifanyiwe kazi nyingine. Kama ni kuamua kuchimba upande mmoja ili barabara ipanuke, tufanye hivyo kwa sababu Mheshimiwa Magufuli, nilimwambia

mwaka jana kwamba, naomba uje nyumbani kwangu ulale lakini uje na mke wako mpaka asubuhi tuamke pamoja kwenda kazini uone adha tunayoipata kutoka Kongowe mpaka Uhasibu. Tunapata matatizo makubwa na kuna Maofisa wako wengi wanakaa kule. Sio kwamba hawajui, wanajua. Si ajabu hawajkwambia tu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi niliona lengo la Serikali kubomoa barabara ile lilikuwa ni zuri, lakini kama haishughulikiwi maana yake ni nini. Sasa leo wananchi wananiuliza kwamba, Mheshimiwa ilitushauri tuvunje nyumba, tumevenja, sasa mbona tena tunaona vitu vya ajabu kwenye barabara hiyo? Nashindwa kuwajibu! Lazima nikwambie ukweli, nashindwa kuwajibu kwa sababu ni kero ambayo naona si nzuri. Ni afadhali tungewatahadharisha kwamba, jamani ifikapo mwaka kesho mwezi wa Kumi nyumba hizo mvunje kwa sababu kipindi hiki tunajiandaa kutafuta pesa kwa ajili ya ujenzi wa barabara. Lakini haikufanyika hivyo, matokeo yake tukawashauri wananchi bomoeni nyumba jamani, kwa maana Serikali inataka kupanua barabara. Wananchi wakabomoa nyumba zao kwa hiari yao kabisa bila ugomvi. Sasa wameona kitu hakifanyiki wameanza kunishutumu mimi kwamba, nimewatapeli au nimewasaliti, kitu ambacho sio kizuri. Mimi siwezi kuwasaliti wananchi wangu, nahitaji wananchi wangu niwawekee mazingira mazuri. Unapokuwa kiongozi, lazima uwekewe mazingira mazuri ya uongozi wako ili unapotoka pale ujue kwamba, ulikuwa unaongoza na umefanikiwa nini katika uongozi wako.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ningeomba Serikali iliangalie hilo. Naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja ya Waziri wa Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, kwa mawasilisho yake mazuri sana ya Bajeti. Vile vile nichukue nafasi hii nimpongeze Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwenegoha, kwa kazi nzuri ya kumsaidia Mheshimiwa Waziri katika kuiendesha Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile niwapongeze kuanzia Katibu Mkuu wa Wizara, Wakurugenzi na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Ujenzi, kwa kuandaa Bajeti nzuri lakini vile vile kwa kuhakikisha kuwa barabara zetu nchini zinatengenezwa.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii ni nzuri sana kama nilivyosema na mimi nashawishika mapema kabisa kuiunga mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mchango wangu nitaelekeza kwenye barabara zilizoko katika Jimbo langu la Nanyumbu kwa kuamini kabisa kuwa Waheshimiwa Wabunge wengine wamezisemea zile barabara ambazo ziko katika maeneo mengine. Nianze kwa kuzungumzia barabara kuu inayotoka Masasi kwenda Tunduru na barabara hii ikiwa ni sehemu ya barabara kuu kutoka Mtwara - Masasi - Tunduru - Songera - Mbambabay.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ni kero kubwa sana kwa wananchi wanaosafiri kati ya Masasi na Tunduru hasa wakati wa kifuku. Barabara hii huwa haipitiki kirahisi kutokana na utelezi na magari mengi hushindwa kupita, kwa hiyo, wananchi hukosa usafiri wakati wa kifuku. Sasa ningeomba Serikali iangalie barabara hii angalau kuifanyia matengenezo kwa kiwango cha changarawe ili kuweza kupidisha magari wakati wa mvua. Ningeomba kabisa kwamba Serikali ianze kutengeneza zile sehemu ambazo ni korofii ili kuhakikisha barabara hii inapitika kipindi chote cha mwaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia barabara hiyo, naomba sasa nizungumzie barabara nyingine ya Nangomba-Nanyumbu-Masuguru-Mtambasuala na ile barabara ya kutoka Mangaka kwenda Nanyumbu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, barabara hii ni barabara ya Mkoa na mara nyingi nimejaribu kuizungumzia sana hapa Bungeni, lakini kwa matumaini makubwa Mheshimiwa Waziri alisema kwamba, barabara hii ingefanyiwa matengenezo. Ajabu ni kwamba, barabara hii kwa miaka mingi hakuna matengenezo yoyote ambayo yamefanyika. Kwa hiyo, sehemu zingine kwa kweli ni mbaya na hazipitiki. Kwa mfano, eneo la Mangaka, pale palianza na ujenzi wa mifereji kando kando ya barabara lakini kwa bahati mbaya mifereji ile haikumalizika na sasa mifereji hiyo inaharibu barabara yenewe.

Kwa hiyo, huhatarisha kwa kweli maisha ya wananchi ambao wanaitumia barabara hiyo. Kwa hiyo, naomba sehemu hii ile mifereji ikamilishwe ili barabara iwe nzuri na magari yapite kwa usalama.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie barabara za Wilaya na Vijiji ambazo ziko kwenye Jimbo langu la Nanyumbu. Kwanza kabisa, barabara ya kutoka Masasi kwenda Chakama-Nandete-Nakole hadi Chivirikiti. Nashukuru Serikali kwamba, barabara hii baada ya kilio changu sasa imeanza kutengenezwa ila naomba tu barabara hii itengenezwe ikiwa ni pamoja na madaraja ambayo yapo ndani ya barabara hii ambayo kwa kweli ni madaraja mabovu na madaraja mengine yanapitika kwa taabu sana.

Lakini vile vile ningeomba barabara ya kutoka Chitowe-Maratani hadi Songambele nayo itengenezwe na barabara hii vile vile kuna madaraja ambayo hayapitiki kirahisi. Sasa madaraja haya naomba yaimarishwe ili yaweze kupidika bila wasi wasi wowote. Lakini vile kuna barabara ya kutoka Nakole kupidia Mikuva hadi Kijiji cha Ngupe. Barabara hii ni muhimu vile kwa kuunganisha Kata za Nandete na Maratani. Kwa hiyo, naomba Serikali kwamba barabara hii iweze kuitengeneza ikiwa ni pamoja na matengenezo ya madaraja yake.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine ambayo napenda kuizungumzia na ambayo imesahaulika kwa muda mrefu ni ile barabara ya kutoka kwenye shamba la mifugo la Nangaramo kwenda kwenye barabara kuu inayotoka Masasi kwenda Tunduru. Barabara hii kwa kweli haipitiki kutokana na mashimo. Kwa hiyo, naomba barabara hii nayo itengenezwehasa kwa kuzingatia kuwa pale Nangaramo ni sehemu ambapo ni muhimu

kiuchumi na watu wangependa kuwa na mawasiliano mazuri kwa ajili ya kujipatia mifugo.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine ambayo ni kero kubwa kwa wananchi ni ile inayotoka Mangaka kuptitia Sengenya-Mkumbaru na kuelekea Matekwe katika Wilaya ya Nachingwea. Barabara hii nayo inapita kwenye maeneo muhimu sana kiuchumi na naomba Serikali iitengeneze kwa sababu ni tegemeo kubwa sana kwa wananchi wa Matekwe ambao sasa hivi wanakuja Mangaka kama ndiyo kituo chao cha kupatia bidhaa za madukani.

Barabara nyingine ambayo iko kwenye hali mbaya na imesahaulika kwa muda mrefu ni ile barabara ya kutoka Nanyumbu kwenda Namijati-Chilunda hadi Mbangara Mbuyuni, ni barabara ambayo ni muhimu vile vile kiuchumi na inategemewa sana na wananchi wengi hasa wa Kata za Nanyumbu, Kata ya Mkonona. Kwa hiyo, naomba barabara hii nayo ifanyiwe matengenezo ili iweze kupitika kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, barabara zingine ambazo ziko kwenye hali mbaya ni ile barabara ya kutoka Michiga kuptitia Nakopi kwenda Napacho hadi Mpombe. Barabara hii vile vile iko kwenye hali mbaya na hasa baada ya daraja la Mto Lukwamba kuzolewa na maji katika msimu huu uliopita. Kwa hiyo, naomba jithada zifanyike. Kwanza kurudisha daraja lile la Mto Lukwamba, kwa sababu sasa Vijiji vya Mpombe, Ndechela na sehemu kubwa ya hifadhi ya Lukwika-Lumesule imetengwa kwa kukosa mawasiliano baada ya daraja hilo kuzolewa na maji. Nina hakika wakati wa masika au kifuku, wananchi hawa watashindwa kuvuka Mto Lukwamba kwa kukosa daraja.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna barabara inayounganisha Kata ya Chipuputa kuptitia Chimika, Kazamoyo hadi Napacho. Barabara hii nayo naomba itengenezwe ikiwa ni pamoja na ujenzi wa daraja kwenye Mto Lukwika.

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kuzungumzia barabara iliyokuwa ya ulinzi. Barabara hii inaanzia Mto Mbangara upande wa Mashariki na inaishia kwenye Mto Lumesule upande wa Magharibi na ni barabara muhimu siyo kiulinzi sasa ila ni muhimu kiuchumi. Kwa sababu kwanza barabara hii inapita kando kando ya Mto Ruvuma, eneo ambalo kwa kweli linafaa sana kwa kilimo cha umwagiliaji maji.

Lakini vile vile inapita katika maeneo ambayo yanafaa kwa shughuli za uvuvi na wananchi wengi wanategemea sana shughuli za uvuvi ili kujipatia fedha au kuondokana na umaskini. Lakini vile vile barabara hiyo inapita kando kando ya hifadhi ya Lukwika/Lumesule. Hifadhi ambayo imeonekana kuwa na wanyama wengi. Hivyo kuwa kivutio kikubwa kwa utalii. Naomba barabara hii ambayo inakosa madaraja muhimu, makalvati kadhaa ambayo yaliondolewa huko nyuma baada ya shughuli za ulinzi kwisha itengenezwe upya ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa madaraja ya mito kama Mto Mbangara, Lukwika, Lukwamba yanajengwa na yale ya mito midogo midogo nayo yanaimarishwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya machache, naomba nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii lakini vile vile niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Ila nitamke tena kuwa ninaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Spika na mimi naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika hoja hii. Pia naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Timu nzima pale Wizarani, kwa kazi kubwa waliyoifanya. Nina ushahidi toka umeonekana humu humu ndani kama kazi haifanyiki basi Wabunge wengi wanaosimama humu ndani wanakuwa wanafoka sana. (*Makofi*)

Lakini nilikuwa ninaongea na wenzangu mbona Bunge hili limetulia sana katika kuchangia hoja hii? Lakini ni ushahidi tosha kwamba, kazi imefanyika na imeonekana na ndiyo maana watu wote wameridhika. Tunakuomba kwamba pamoja na michango ya kutokuwa mikali sana usije ukajiamini sana unakokwenda mbele basi ukajiamini, ukafanya vibaya zaidi. Tunakuomba uendelee kwa kasi hiyo ulioanza kwa kweli unatuwekea sisi Wabunge wenzako pazuri na kwa kazi hii kubwa unaoifanya sisi tunakuhakikishia kwamba, tutarudi tena humu ndani mwaka 2005, kwa kazi kubwa unayoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri, kero kubwa kwa wananchi ni barabara na pia nichukue nafasi hii Mheshimiwa Spika, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa ziara yake ya Mkoa wa Mtwara. Kwa kweli alifanya ziara ya aina ya kipekee na pia nimshukuru sana alipofanya ziara ndani ya Mkoa wa Mtwara alizungukia Jimbo langu la Newala, kulikuwa na Semina ya Bodi ya Wakandarasi Masasi, lakini alitoka Massasi akaenda Newala, akatoka Newala akaja Mtwara, akatoka Mtwara akaenda Lindi, akatoka Lindi kwenda Kilwa, akapita Pwani mpaka Dar es Salaam. Sasa hii inadhihirisha kabisa kazi yako unayoifanya nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, alipokuwepo Jimboni kwangu alifanya kikao na akakutana na Baraza la Wazee Jimboni kwangu Newala na kero kubwa waliyomwambia Mheshimiwa Waziri ni barabara ya kutoka Newala, Kitangari kuja Mtama. Kwa kweli ni kero kubwa sana hiyo barabara. Namshukuru Mheshimiwa Waziri, aliwhahakikishia Baraza la Wazee la Wilaya ya Newala kwamba, kwa kweli Mheshimiwa Mbunge ameshaniletea tatizo hilo na tunalifanyia kazi na baada ya muda si mrefu tatizo hilo litaondoka.

Lakini nimkumbushe tu Mheshimiwa Waziri, mwaka 2002, nilisimama hapa nikakuomba kuhusu barabara hii ya kutoka Mtama-Kitangari mpaka Newala. Kwa kweli ni kero sana. Mheshimiwa Waziri, hii barabara takribani miaka mitano sasa hivi haijafanyiwa ukarabati wa aina yoyote. Sasa kwa kweli *just imagine* kwamba, barabara ambayo haijafanyiwa matengenezo ya aina yoyote kwa kipindi cha miaka mitano hali ya hiyo barabara inakuwaje. Mwaka 2002 ulinikubaliana kwamba, utanisaidia lakini mwaka umeisha Mheshimiwa Waziri na mimi nilijikanyaga nikaenda kwa wapiga kura wangu, nikawaeleza kwamba, Mheshimiwa Waziri kakubali kututengenezea hii barabara.

Sasa Mheshimiwa Waziri, kwa kweli hali imekuwa mbaya jimboni kwangu wakati wanaponiuliza kwamba sasa imekuwaje na mwaka umepita? Sasa naomba Mheshimiwa Waziri unilinde ili unisaidie tena angalau. Ninajua majibu yapo kwamba, tupitie kwenye *Road Fund* ya Mkoa tuwasiliane na Meneja wa Mkoa, majibu yapo lakini Mheshimiwa Waziri hali halisi unaijua ilivyo. Sasa mimi natoa ombi maalum kwako uweze kunisaidia barabara ya kutoka Mtama-Kitangari mpaka Newala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri, hii barabara inawagusa sana watu wa Newala.

**SPIKA:** Elekeza maneno yako kwa Spika.

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimwambie Mhehsimiwa Waziri kwamba, hii barabara inawagusa sana watu wa Newala. Kwa kweli wananchi wa Wilaya ya Newala wanategemea sana Hospitali ya Nyangao. Ile hospitali kwa njia fupi iliyokuwepo ya kuweza kupita ni kutoka Newala kuja Kitangari-Mtama kwenda Nyangao. Sasa hivi wanazunguka kwenda Masasi kuja Ndanda mpaka kurudi tena Nyangao. Kwa hiyo, ninakuomba sana uweze kunisaidia barabara hiyo ili tuondoe kero hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze kwa usimamizi wa hali ya juu wa kuweza kufanikisha mpaka pale tulipofikia katika ujenzi wa daraja la Mto Rufiji. Kwa kweli ile ni historia uliyotuvekea na uliyojiwekea kwa kuweza kufanikisha kuweza kumalizia daraja lile la Mto Rufiji. Lakini tu niongelee kidogo Mheshimiwa Waziri, ni kweli sasa hivi baada ya saa 12 jioni abiria hawaruhusiwi kuvuka katika lile daraja kwa usalama kwa sababu hamna taa.

Mheshimiwa Spika, inakuwa ni kero sana kwa akina mama na watoto. Kuna mabasi ambayo yanatoka Mtwara kwa bahati mbaya wanapata *break down* barabarani, sasa *ile break down* ikitokea lile *bus* linachelewa na kuweza kufika labda saa moja au saa mbili pale katika daraja la Mto Rufiji. Sasa inapaswa wale watoto na akina mama walale pale lakini inakuwa ni kero sana. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri naye aangalie kwamba, angalau wafikishe muda wa mwisho wa kuvuka pale iwe saa 4 za usiku, si kutoka Dar es Salaam lakini angalau wale abiria wanaotoka Lindi/Mtwara basi waweze kupita pale angalau mwisho iwe saa 4 za usiku waweze kupita pale kutokana na matatizo ya magari yakiharibika barabarani. (*Makofi*)

Pia Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, alipofanya ziara yake alipita kwenye eneo linaitwa Chipite. Alipopita pale kutokana na hali halisi aliyojionea pale akamwagiza Meneja wa Mkoa kwamba, nakuagiza ndani ya siku nne, nataka sehemu hii ipitike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siyo ndani ya siku nne, ndani ya siku mbili na nusu paliweza kufanikiwa na kutengenezwa pale. Kwa kweli wananchi wa Mkoa mzima wa Mtwara wanampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kauli yake aliyoitoa hiyo ya Chipite na palirekebishwa. Sasa tunachoona ajabu ni kwamba, wanasesma hawana hela. Lakini Mheshimiwa Waziri, alipopita pale alipoagiza ndani ya siku mbili na nusu kazi ilifanyika.

Sasa sijui hizo hela zilipatikana wapi, alitoa Mheshimiwa Waziri au vipi sijui. Lakini tunaomba atusaidie hivyo hivyo anavyotusaidia. Pia nimshukuru alipofanya ziara yake alipotoka Newala kuja Mtwara, hali ya ile barabara alipoiona akaagiza nayo kwamba ifanyiwe marekebisho. Kwa kweli tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa kazi kubwa inayofanyika sasa hivi katika ile barabara ya kutoka Newala kuja Mtwara kila mwaka, ile barabara walichokuwa wanafanya ni kuchonga tu na greda.

Hali halisi ya ile barabara ikawa sasa kila siku inadidimia kwenda chini. Lakini kwa maagizo yake Mheshimiwa Waziri, sasa hivi ile barabara haichongwi tena isipokuwa inamwagwa kifusi na kunyanyuliwa tuta kubwa sana. Kwa hiyo, tunakushukuru sana kwa hilo Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

Lingine tena Mheshimiwa Spika, nimwombe tu Mheshimiwa Waziri tena kwamba, kuna barabara ya kutoka Masasi kwenda Mapili, ya Newala na kuja Nanguruwe Newala. Hawa watu wako Mto Ruvuma kule bondeni chini kabisa. Wale wananchi wamefanya kazi kubwa sana, wamejitolea kuweza kupasua mawe makubwa milimani na kuweza kufanikisha kutengeneza ile barabara lakini wameshindwa, kuna mawe makubwa ambayo yapo pale sasa hivi hawawezi kuyavunja yale mawe na pakaweza kupitika.

Meneja wa Mkoa wa *TANROAD* Mtwara, alikwenda na timu yake ya wataalam kuangalia pale na baada ya kuangalia wao wametuomba kwamba sisi tuombe kuititia Mfuko wa *TASAF*. Lakini kwa bahati mbaya sisi Newala hatujabahatika kupata *TASAF*. Namwomba Mheshimiwa Waziri, aliangalie atatusaidia vipi, kwa kweli nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Lulindi, ambaye ndiyo Mbunge wa Mapili ya Masasi, kwa kazi kubwa aliyofanya kuandika barua na kuweza kushawishi timu nzima ya wataalam kwenda kuangalia pale, kwa kweli amefanya kazi kubwa sana mpaka hapa tulipofikia. Sasa tunakuomba Mheshimiwa Waziri, uliangalie jambo hilo ili uweze kutusaidia. Ni gharama ndogo sana iliyobaki.

Kwa kweli wale watu wamefanya kazi kubwa sana na kama hatukuwasaidia, basi hawatakuwa na moyo tena wa kuweza kujitolea na kufanya kazi kama hiyo. Pia nimalizie tu kwa kusema kwamba, ninarudia tena kumwomba Mheshimiwa Waziri kwamba, nimesimama zaidi kuchangia katika hoja hii kwa sababu ninataka kumwomba sana Mheshimiwa Waziri kuhusu barabara ya kutoka Mtama kwenda Kitangari mpaka Newala. Ninakuomba sana hiyo barabara uiangalie kwa hali yoyote uweze kutusaidia ili angalau mwaka huu basi iwepo ndani ya mpango wa kuweza kutengenezwa barabara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia niseme tu kwamba, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Kwa hayo, machache nashukuru sana. (*Makofi*)

## **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara ya Ujenzi, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Naomba juhudi hizi nzuri ziendelezwe.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba kuunga mkono hoja ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kupongeza hatua ya kufuta Makandarasi wasiofanya kazi nzuri. Ukaguzi wa kazi za Makandarasi naomba ufanyike mara kwa mara ili watimize wajibu wao na kubaini wasiofanya kazi vizuri ili wachukuliwe hatua. Kwa kuwa baadhi ya Mikoa hakuna Makandarasi wenyewe ujuzi, utaratibu wa kufundisha Makandarasi Mikoani uendelee ili kila Mkoa uweze kuwa na Makandarasi wanaoweza kupewa kazi ya ujenzi wa barabara katika Mikoa husika.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Dodoma - Manyoni - Singida naomba kuishukuru na kuipongeza Serikali kwa hatua iliyofikia ya kuwekeana saini na Makandarasi kwa ajili ya kuanza kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Kukamilika kujengwa kwa barabara hii kutakuza uchumi katika maeneo husika lakini vile vile mawasiliano yataboreshwa sana. Naitakia kazi njema na utekelezaji wa mradi huu na sisi kama Waheshimiwa Wabunge, tunaahidi kutoa ushirikiano wetu ili mradi uweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Manyoni - Itigi - Tabora, imefanyiwa kazi nzuri mpaka sasa ukilinganisha na hapo zamani. Naomba sehemu ambazo bado kama vile mpakani mwa Tabora na Singida (Itigi) ambayo ni kipande cha kama kilomita mbili ambazo zinahitaji kuwekewa changarawe na kushindiliwa. Sehemu nyingine ni kipande cha kati ya Kitopeni na Bangayeyega, sehemu hii inahitaji kujazwa changarawe katika sehemu zenye mashimo na zile ambazo wakati wa masika huwa zina utelezi na sehemu nyingine ni ndogo ndogo sana zinahitaji kuwekewa changarawe ili kuondoa utelezi. Kama hizi kazi zikifanyika barabara hii itapitika mwaka mzima bila matatizo kwa sababu imefanyiwa kazi nzuri kama nilivyosema hapo mwanzoni.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Itigi - Rungwa, naishukuru sana Wizara ya Ujenzi, kwa nia yake nzuri ya kuikarabati barabara hii kwa kiwango cha lami. Ninaamini kwa juhudhi inayofanywa lengo litafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara hii haijafanyiwa matengenezo kwa muda mrefu, naomba Wizara iendelee kuifanyia matengenezo maeneo korofii kati ya Rungwa na Kuitamila hasa sehemu ya mbuga (*Black Cotton Soil*) na Kidongo Chekundu ambazo huwa zina utelezi na mashimo hasa wakati wa masika na kufanya magari yashindwe kupita. Sehemu nyingine ni kati ya Mwamagembe na Kiyombo na ile kati ya Doroto na Kambi ya Mkaa ambayo ina mashimo makubwa. Wizara inajitahidi kufanya kazi ila barabara ni ndefu sana. Kwa kuwa kuna ahadi ya kufanyiwa matengenezo kwa fedha ya mkopo wa *ADB*, naomba Wizara ifuatilie ili hiyo fedha iweze kutumika kufanya matengenezo yatakayowezesha kupitika muda wote.

Mheshimiwa Spika, napongeza na kuunga mkono mipango yote ya matengenezo ya barabara katika Jimbo langu, Wilaya, Mikoa na nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wa Wizara, kwa kazi nzito na nzuri ya kuhakikisha barabara zetu zinakuwa bora na zinalenga kuibua uchumi wa maeneo mbalimbali na hatimaye kuinua Pato la Taifa. Naomba muendelee na *spirit* hiyo hiyo. Kazi kwa hakika unaichapa.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba nitoe ushauri wangu juu ya barabara kuu iendayo Zambia (*Highway*) inayopita katikati ya Jimbo langu la Mbeya Mjini. Eneo la mzunguko wa Mafati limekuwa chanzo cha ajali nyingi na kupotea kwa maisha ya watu na vifaa. Eneo hili la Mwanjelwa ni *business centre* kubwa katika Jiji la Mbeya na pia eneo hili ni pito kuu la wananchi toka Kata ya Iyela yenye watu zaidi ya 25,000, ndiyo Kata kubwa zaidi ndani ya Jiji la Mbeya. Pia zipo Shule za *Samora Secondary, TIA College, ARAGE ACADEMY* na pia Kiwanja cha Ndege cha sasa. Hivyo unaweza kuona jinsi gani eneo hili ni pito kuu la wananchi na wanafunzi wengi wa Mji huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri ifuatavyo:-

1. *Short Term Solution:* Kuweka taa za kuongozea magari ili kupunguza ajali kama ilivyo sasa.
2. Kujenga daraja la juu (*flyway*) kama ilivyo Manzese, pia inaweza kujengwa kwa vyuma ili kutoa nafasi kwa *pedestrians* na magari yaendayo katikati ya Mji.
3. *Long Term Solution:* Kuwe na *Diversion* ya barabara hii kuu ili ianzie njia panda ya Ilomba, Mwakibete, Pambogo, Nzovwe, Inyala, *Mbeya Technical College* na hatimaye kuungana tena maeneo ya Iwambi viwandani.

Mheshimiwa Spika, tatu, napendekeza eneo la Hospitali ya Rufaa Wazazi Meta ijengwe *Round About* ili kupunguza ajali hasa mahali ambapo *Tunduma Road* inakutana na *highway* toka Mwanjelwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni matarajio yangu kuwa Mheshimiwa Waziri atanipatia majibu ya dhati, nafikiri pia nina swali la namna hii. Napendezwa na utendaji wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wake, kwa kuleta hotuba safi Bungeni kuhusu Bajeti ya mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, mimi ni shahidi kwamba, utekelezaji wa Mradi Maalum wa Barabara kuu umeanza kutekelezwa hasa katika Mradi wa Dar es Salaam - Kibiti - Lindi - Mingoyo. Karibu katika eneo lote kazi zimeanza, inatia moyo.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri na Wizara yake waendelee hivyo hivyo ili kazi hii ya muda mrefu iweze kukamilika katika kipindi hiki hiki chetu cha uongozi yaani miaka 2000 - 2005. Isipokamilika kazi hii hatuwezi kuwa na uhakika endapo Serikali itakayofuata itaupa mradi huu umuhimu unaostahili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza haya, ningependa nimwarifu Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kuwa barabara ya Mtwara - Masasi iliharibiwa sana wakati wa mvua za *El-Nino* mwaka 1990. Baadhi ya sehemu zimerekebishwa na baadhi yake hasa madaraja bado. Kuna sehemu korofi ambayo kama ikiachwa hivi hivi basi uzuri wote wa barabara ya Dar es Salaam - Lindi - Masasi utakuwa na dosari kubwa. Sehemu hiyo ni Chipite au Nkwera. Mahali hapo toka mwaka 1990 panapitika kwa taabu sana wakati wa masika.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2001 nililiza swali hapa Bungeni na Mheshimiwa Waziri, akajibu kuwa, mpango wa ukarabati wa sehemu hii ya Chipite ulikuwa mbioni kwa majadiliano na Serikali ya Japan na kwa kutumia fedha za hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nimeangalia katika vitabu vya Makadirio na Matumizi *volume II* na *IV* sikuona mradi huu umewekwa wapi. Naomba Mheshimiwa Waziri, anithibitishie kwamba mpango wa kukarabati sehemu ya Chipite kama bado upo na utatekelezwa mwaka gani. Ni muhimu mpango huo utekelezwe katika kipindi hiki hiki la sivyo tutakuwa na barabara inayopitika mwaka wote lakini ikajirudia hali ya kujifunga wakati wa masika na hivyo hadithi ya barabara ya Kibiti - Lindi kujirudia rudia bila sababu yoyote.

Mheshimiwa Spika, ingawa suala la *Mtwara Development Corridor (MDC)* nililizungumza kwa uchungu wakati nikichangia hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, bado naomba jawabu toka kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, kwa kuwa ye ye ndiye Mwenyekiti wa Ukanda huu wa Maendeleo. Namhimiza aanzishe *Secretariat* itakayoendesha na kuhamasisha suala la *MDC* na napendekeza Makao Makuu ya *Secretariat* yaye Mtwara Mjini. *Secretariat* hii ndiyo itakayohimiza na kusimamia mradi wa ujenzi wa barabara ya Mtwara - Masasi - Songea - *Mbamba Bay*, mradi wa ujenzi wa daraja la Umoja kati ya Tanzania na Msumbiji, Mradi wa Uzalishaji Makaa ya Mawe Mchuchuma, Mradi wa Gesi ya *Mnazi Bay* na Msimbati na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, endapo Serikali ipo *serious* kwa mipango hii ni lazima ione umuhimu wa kuwa na *Secretariat* Mtwara. Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, ana kazi nyingi sana ni rahisi kwake kusahau miradi mingine muhimu kwetu wananchi.

Mheshimiwa Spika, zoezi la kuuza nyumba za Serikali linamtia doa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi bila sababu. Utekelezaji wa zoezi zima halikufanyika kwa uwazi na Utawala Bora. Ni kweli kuna baadhi ya nyumba zimekarabatiwa kwa fedha nyingi za umma (walipa kodi) na kuuziwa viongozi kwa bei ya kutupwa. Suala hili mimi naliona linaihusu Serikali na Utawala Bora zaidi kuliko Wizara yenyewe. Serikali yenyewe iunde chombo cha kuchunguza jambo hili ili kurejesha imani kwa wananchi wengi ambaao wanaona viongozi wamepeana nyumba za umma.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha na kuunga mkono hoja.

**MHE. SUMRI A. S. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kwanza, Jimbo la Mpanda Magharibi limebakia nyuma kwa muda mrefu. Mimi ombi langu ni barabara ya Mkao, Mpanda - Karema. Barabara hii ni muhimu sana kwa vile inaunganisha eneo la Ziwa Tanganyika. Eneo hili ni tajiri sana kwa kilimo, madini na uvuvi lakini barabara zake hazipitiki, hata barabara hii ya Mkao nayo ni mbaya sana. Eneo hili kiusalama ni *delicate* mno hasa ukitilia maanani kwamba, Karema inapakana na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Eneo hili ni kimbilio la wakimbizi na kiusalama linavamiwa sana na majambazi, hivyo barabara hii ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, pili, barabara kuu ya Mpanda - Uvinza imekwishaachwa bila matengenezo yoyote yale. Hivi sasa hakuna mawasiliano ya usafiri kwa wananchi wetu katika eneo hilo na ni kero kubwa. Barabara hii ipo katika eneo wanaloaka wakimbizi wa Burundi na ina uzalishaji mkubwa wa chakula na biashara kubwa. Aidha, kiusalama ni muhimu sana. Kwa vile ni barabara kuu naomba iangaliwe angalau itengenezwe kwa kiwango cha kipitika tu.

Mheshimiwa Spika, tatu, barabara ya Mkao toka Mpanda - Mwese. Mwese kuna kilimo kikubwa cha kahawa na pia uzalishaji mkubwa wa migomba, mahindi na maharage. Sehemu hii ni muhimu sana kwa kuwa ndiyo njia pekee itumikayo kwa usafiri yaani barabara moja tu, umbali wake ni km. 67 hadi Mwese na hadi Ziwa Tanganyika Mkao wa Kigoma ni km. 108. Ombi langu ni kuitengeneza angalau ifike Mwese maana eneo la Kigoma linahitaji matengenezo makubwa na gharama kubwa mno.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba mliokoe Jimbo la Mpanda Magharibi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara ya Ujenzi na natoa pongezi sana kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri ya kuboresha miundombinu ya barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuwezesha kujengwa barabara yetu ya Mwanza - *Shinyanga Border* - Tinde - Isaka - Nzega. Nawapongeza sana Serikali kwa kutekeleza mradi huu ambao ulikuwa hadithi tangu tumejitawala na leo ni miaka 43, barabara hii itasaidia kuboresha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika sherehe za Usalama Barabarani zilizofanyika Mkoani Shinyanga Kitaifa, tulionyeshwa utaratibu wa kupima na kucheki magari na kampuni moja ya *SGS* unaotumiwa Ulaya kupima kuoza kwa magari chini kwa sababu ya chumvi chumvi (*Chassis Rot*), ambao mara nyingi unaweza kuleta madhara ya ajali. Magari

yanayoonekana kuoza sana *chassis* ni vyema yakasimamishwa kutumika. Nilikuwa nashauri sana kama inawezekana pamoja na kupima barabara zetu uzito wa magari, ni vyema kwa usalama zaidi ili kuzuia ajali.

Mheshimiwa Spika, nashauri pia kuwa Serikali ifungue maeneo ambayo hayana barabara ili kufungua uchumi hasa maeneo ambayo hayana barabara za kuunganisha Wilaya na Mikoa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pia kutokana na ukame wa mara kwa mara katika Mikoa ya Ziwa, nashauri barabara ya kutoka Shinyanga - Tabora - Ipole - Mpanda ili chakula cha Mkoa wa Rukwa kiweze kutufikia Mikoa ya Ziwa, ikiwezekana barabara hii iwekwe lami kwa siku za usoni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na kuwatakitia utekelezaji mwema wa Bajeti yenu ya mwaka 2003/2004.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, Mgawanyo wa Fedha za Barabara, Mkoa wa Arusha.

Mheshimiwa Spika, *release No. 9*, tarehe 2 Aprili, 2003, Sh. 140.219 milioni. Maelezo ya kazi inayotarajiwa kufanyika kutumia fedha hizi ni Sh. 20 milioni tu kwa barabara ya Losingai - Orkasemat. Maelezo ya matumizi ya fedha nyingine yalihitajika.

Mheshimiwa Spika, *release No. 10*, tarehe 16 Mei, 2003, *release No. 11*, tarehe 23 Juni, 2003 na *release No. 12*, tarehe 23 Juni, 2003 jumla ni Sh. 508.566 milioni. Naambiwa kuwa pia kumekuwa na *releases* nyingine kabla ya tarehe 30 Juni, 2003. Sasa matumizi ya fedha hizi yameelekezwa kwenye barabara zipi hasa? Kwa mwaka 2002/2003 barabara za Mkoa - Wilayani Mbulu hazikufanyiwa matengenezo, matengenezo yameishia Kilimapunda mpakani mwa Wilaya ya Karatu na Mbulu. Tunafahamu hadi tarehe 30 Juni, 2003 Karatu - Mbulu - Dongobesh - Kidarafa ilistahili kupata mgao kutoka Mkoa wa Arusha. Ni matumaini yetu kuwa basi hizi *releases* za mwishoni zitasaidia sehemu zilizo korofii sana katika barabara ya Kilimapunda - Dongobesh - Kidarafa.

Mheshimiwa Spika, kama Katibu wa Wabunge wa Mkoa mpya wa Manyara, tunakuomba utekeleze masharti ya Sheria ya ku-reconstitute *Regional Road Board* - Manyara na Mkuu wa Mkoa aarifiwe haraka ili aitishe Kikao cha Bodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri.

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hotuba ya Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa John Magufuli, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha na safu yote ya uongozi Wizarani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri, napenda kuipongeza Wizara nzima kwa kazi nzuri ya matengenezo, ukarabati na kuhudumia sekta ya barabara Mijini na Vijiji hasa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2000 hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ameonyesha uwezo mkubwa wa utendaji kazi na hasa kwenye kurudisha nidhamu Wizarani kwake na hasa kwa Makandarasi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupongeza, napendekeza kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, kuishusha hiyo nidhamu kwenye Wizara yake ngazi ya Wilaya hususan *TANROADS* na hasa ukizingatia mabadiliko ya taratibu za matumizi ya mafungu ya fedha toka Wizarani (Hazina) kwa kuhamishia matumizi hayo moja kwa moja Wilayani.

Mheshimiwa Spika, ningeshauri kuwe na ushirikishwaji kamili pia wa Waheshimiwa Wabunge, hasa kwenye matumizi ya maendeleo kama vile ujenzi na barabara. Ushirikishwaji huo uanzie kwenye hatua zote muhimu za awali. Kuanzia hatua ya utangazaji zabuni, uteuzi wa Makandarasi na hatua ya mwisho ya kumlipa Mkandarasi baada ya *consultants* kusaini *certificate* ya malipo kwa sababu moja tu muhimu ya kuainisha malipo na hali halisi ya matengenezo/kazi iliyofanyika ili kuepusha ubadhirifu wa mali na kuhimiza kabisa maendeleo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. IDDI M. SIMBA:** Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi na kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri, ningependa kufikisha salamu nyingi za kheri kutoka kwangu na kwa wananchi wa Jimbo la Ilala.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Mungu awabariki.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Barabara za Magharibi. Katika mifumo yote iliyopo nchini huu ndio mfumo ambao utekelezaji wake uko nyuma pamoja na juhudhi zilizoanza Tunduma - Sumbawanga na Nyakanazi kwenda Kigoma. Sehemu ambayo bado haijashughulikiwa katika Mkoa wa Kigoma na Rukwa ni kubwa mno. Tunaomba Wizara itilie maanani eneo hili.

Mheshimiwa Spika, pili, barabara ya Mkoa ya kutoka Bandari ya Kasanga - Ziwa Tanganyika kuititia Matai - Mwimbi, Kalembe, Ilonga Namchinka katika Wilaya ya Mbozi hadi kona ya Kakozi, barabara kuu ya Tunduma - Sumbawanga, hii itasaidia sementi ya Mbeya kufika kwa urahisi Rwanda, Burundi, *DRC*, Kalemie na hivyo kukuza biashara ya bidhaa nyingine pia.

Mheshimiwa Spika, tatu, Ukosefu wa Vifaa vya Ujenzi Mkoa wa Rukwa na Kigoma. Kazi ya ukandarasi katika Mikoa ya Rukwa na Kigoma ni ngumu mno kwa

sababu ya ukosefu wa vifaa vya ujenzi ingawa ni sera ya Serikali kuwawezesha wazalendo kuingia katika Sekta ya Ujenzi, wengi wameitikia wito huo na wanapata Kandarasi Mkoa wa Rukwa na Kigoma tatizo ni upatikanaji wa vifaa vya ujenzi wa barabara. Vipo vichache vya wafanyabiashara binafsi baada ya *PEHCOL* kufilisiwa. Vifaa hivyo vichache vinagombaniwa sana na Wakandarasi hivyo husubiriana sana na huchukua muda mrefu kukamilisha Kandarasi zilizotolewa.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iwasaide Wakandarasi na au wafanyabiashara wanaoweza kukopeshwa vifaa vya ujenzi wa barabara mfano *caterpillar, earth movers, wheel loaders graders* na *compactors* ili ziwepo Rukwa na au Kigoma ili Wakandarasi waweze kuwa na sehemu ya kukodisha vifaa hivyo. Hii itapunguza gharama tunazopata kukodisha vifaa toka Morogoro, Iringa na Mbeya.

Mheshimiwa Spika, nne, hivi Serikali yetu haiwezi kuwa wabunifu kuwa na *ferry boat* katika Ziwa Tanganyika yenyewe uwezo wa kubeba mabehewa ya treni ili yaweze kufikishwa Kalemie *DRC* na Bunjumbura Burundi ili yapakiliwe huko huko na kuletwala ili kuunganishia katika reli yetu ya Kati Kigoma, njia hii itarahisisha upakiaji na upakuaji. Pili, wafanyabiashara wa *DRC* na Burundi wanaweza kuombwa kununua mabehewa yao yatakayofikishwa hadi nchini mwao lakini yakipitishwa katika reli yetu na kulipia fedha nyingi nchini mwetu.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa mchango wangu katika Wizara hii, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na wataalam wote wa Wizara hii, kwa kazi yao nzuri ya uwajibikaji mzuri ambao Watanzania tunaushuhudia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uwajibikaji huo nashauri sana Wizara ielekeze nguvu zake zote katika Mkoa wa Kusini kwa sababu ndiko kiliko kilio kikubwa cha wananchi na hasa katika kuboresha mavuno ya asili ambayo yapo huko hivyo inapaswa miundombinu ipolekwe haraka.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara hii pia ifikirie daraja la Kigamboni kwani limo katika mpango gani wa utekelezaji kwani kuna umuhimu wa kutosha katika kulifikiria hasa katika karne hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada ya Wizara hii naomba Wizara ifikirie teknolojia mpya ya ujenzi wa barabara za Dar es Salaam kwani msangamano wa magari umekuwa mkubwa mno.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa nyumba za watumishi, Wizara lazima iunde miundombinu mizuri ya kuwasaidia watumishi katika kuwajengea na kuwakopesha nyumba kwa bei ya utumishi. Hii ni kwa sababu ya kiwango, mshahara mdogo, hivyo inapaswa Wizara iwaangalie watumishi kwa lengo la kuwasaidia na sio biashara. Pamoja

na kuimarisha vipimo vya uzito vya barabarani lakini bado yapo malalamiko juu ya Maafisa wa Usimamizi wa vipimo hivyo kwa sababu Wizara haina nia ya kuwasumbua wateja lakini usumbufu upo na Wizara ifanye uchunguzi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, wapo Wakandarasi wa kienyeji wa ndani mimi nahisi kwa wakati huu Wizara inapaswa iwawezeshe sio tu kifedha bali pia kuwapatia utaalam ili angalau waweze kusaidia ujenzi au ukarabati mdogo mdogo wa ndani.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara katika kuhakiki magari na vyombo vya ujenzi katika sera ya Kiserikali, kwani hii imeonyesha bayana kwamba Wizara inajua inachokifanya ila tu bado Wizara inayo nafasi ya kueleza umma kama ilivyoanza hapo awali juu ya zoezi hili linavyoendelea.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naishauri Wizara pamoja na Mheshimiwa Waziri kwamba, wawe karibu sana na wananchi katika kutoa elimu juu ya maendeleo na umuhimu wa utatuzi wa barabara ili kutotoa nafasi ya malalamiko yasiyo na misingi hatimaye kupoteza sifa ya kazi nzuri ya Wizara ya Ujenzi. Ahsante.

Mheshimiwa Spika, naunga tena mkono hoja.

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja hii bila shida yoyote. Pamoja na kuunga mkono naomba hoja zifuatazo zijibiwe:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Serikali iliahidi kujenga Daraja la Kolo ambalo liliharibika na bado halijajengwa. Sasa daraja hilo litajengwa lini?

Mheshimiwa Spika, pili, barabara ya Iringa - Dodoma - Babati - Minjingu itaanza kujengwa lini kwa lami? Naomba maelezo zaidi maana wananchi hawaelewii. Halafu haijapangiwa fedha zozote.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iongeze fedha za matengenezo ya kawaida ili sehemu ya Kondoa - Bereko ijengwe maana bado ni mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, tatu, wakati tunasubiri barabara ya Mnenia - Masange - Kisese - Kikore, bado kuchukuliwa na Mkoa, naomba msaada wako wa fedha kidogo ili kufungua hiyo njia. Njia hiyo ni muhimu sana lakini Halmashauri ya Kondoa haina uwezo. Tafadhali kuititia *TANROAD* naomba msaada kutoka kwako.

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani nyingi sana.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri. Aidha, nampongeza Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Wizara. Pongezi za kipekee ni kwa Wahandisi wanawake. Kazi ya Wahandisi wanawake ni ya kijasiri sana na pia kazi ya Wizara ni makini sana. Bajeti ya Wizara imeandaliwa kisayansi na inatekelezeka.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Dodoma - Kondoa - Arusha, ni muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi. Kondoa inakosa mapato kutokana na utalii kwani barabara ina sehemu kubwa na nyingi ambazo ni korofsi. Wakati wa mvua barabara hii haipitiki hasa kati ya Dodoma na Kondoa. Tunaomba barabara hii itengenezwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kwa furaha kuchukua nafasi hii kuchangia katika hoja hii iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, sina budi kumpongeza Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa John Magufuli, Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu Kijazi na wafanyakazi wengine wote wa Wizara hiyo.

Natoa pongezi hizo sio kwa hotuba kuandikwa na kusomwa vizuri tu, bali kwa kazi kubwa sana Wizara hii inayofanya ya kujenga na kuunganisha nchi yetu yote kwa mtandao wa barabara. Hakika mcheza kwao hutunzwa hata hongera ni tuzo. Azma ya Wizara ya Ujenzi ya kuunganisha kwa barabara za uhakika Makao Makuu ya Mikoa yote hapa nchini ni uamuza wa busara sana na pengine tulichelewa. Mpango huu utasisimua uchumi katika Mikoa yote na kuharakisha maendeleo kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa barabara, pamoja na kazi nzuri ya ujenzi wa barabarani nchini, suala la ukarabati ni la msingi sana. Mara nyingi barabara zimetengenezwa vizuri sana lakini kwa kuwa hatuna utamaduni wa kuzikarabati baada ya muda mfupi barabara hizo hurejea katika hali duni mno. Ndiyo sababu napenda nishauri kwamba, ni muhimu Wizara ianzishe tena kwa haraka mpango unaofanana na ule wa zamani wa *PWD* kwa ajili ya kazi ndogo za ukarabati wa barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, hakuna lazima kurudia utaratibu ule wa zamani bali Wizara inaweza hata kukubaliana na Vijiji mbalimbali kwa gharama ndogo sana na barabara zetu ziangaliwe mara kwa mara. Mifereji ya pembeni mwa barabara ikiziba, maji ya mvua yakipita katika barabara au yakikata barabara baada ya muda mfupi baadaye hutokea maafa makubwa kwa barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, Matengenezo ya Barabara kwa Mikono. Napenda kuishauri Wizara ya Ujenzi kuruhusu baadhi ya barabara zake hasa zile za changarawe kutengenezwa kwa mikono. Uzoefu tulionao ni kwamba, barabara zinazotengenezwa kwa mikono maeneo ya Vijiji ni nzuri sana na pia kuokoa fedha nyingi badala ya kutengenezwa kwa mitambo mikubwa. Kwanza mitambo mingi hutokea Mijini ambapo usafiri pekee hadi kufikia katika eneo husika hutumia fedha nyingi kabla ya kazi kuanza. Pili, kazi ya kutumia mikono ya watu husaidia kupunguza umaskini kwa vile fedha watakazolipwa zitatumwiwa na familia.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Magamba - Malindi - Mlalo na Malindi - Nkelei - Lukozi - Mtate, sina sababu ya kutoipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri ya matengenezo ya barabara hizi. Hata hivyo, barabara hizi za changarawe na za Mkoa zimo katika

utaratibu ule ule wa matengenezo ya maeneo korofii (*Spot Improvement*), badala ya ukarabati kamilifu na timilifu. Itakumbukwa kwamba, barabara hizi zilipatwa na msukosuko mkubwa mwaka 1991 na 1993 katika mafuriko ya maporomoko katika Jimbo langu la Mlalo kiasi kwamba, changarawe nyingi zilizolewa na maji. Hivyo mpango wa matengenezo ya maeneo korofii hausaidii sana mvua inaponyesha. Naomba barabara hizo zirudishiwe changarawe uwezo upatikanapo.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mkomazi - Mnazi - Umba, naishukuru sana Wizara hii na Mheshimiwa Waziri mhusika, kwa kusikiliza na kujali. Ni miaka mingi sasa nimekuwa nikililia ujenzi wa daraja la Mkundi hatimaye Wizara imesikia kilio chetu. Wananchi wa Tarafa ya Umba wanashukuru sana. Hata hivyo, bado sijaona ahadi ya Mheshimiwa Waziri kwa barua ya fedha ya matengenezo ya barabara hiyo. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri, aliahidi na ni mtu mkweli, naomba anieleweshe barabara hiyo imetengewa kiasi gani cha fedha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. SALOME J. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia hoja iliyomezani. Kwanza nienze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake yote, kwa kazi nzuri katika mwaka unaoisha sasa 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, katika Wizara zinazofanya kazi ya kuonekana, na kuthubutu kutenda kazi bila woga au kuoneana aibu katika uwajibikaji ni Wizara hii. Ninawapongeza kwa kukamilisha barabara kadhaa nchini na kuendelea kujenga nyingine kwa mfano daraja la Mto Rufiji na barabara yake ya kwenda Mikoa ya Kusini. Kukamilika kwa barabara na daraja kutafanya Mikoa ya Kusini kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Maendeleo ya nchi hii hayawezi kukamilika endapo kuna Mikoa au sehemu ya nchi inakuwa bado katika giza.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi barabara hufuata pia watu na maendeleo. Hapa nina maana kuwa barabara ni lazima ipanuliwe na kupewa vipambio vyake kwa mfano *traffic lights* pale ongezeko la watu linapoonekana kwa mfano, barabara za *New Bagamoyo* Dar es Salaam. Barabara hii sasa ni kero hasa kwa mlologo wa magari (*ques*), asubuhi na jioni, kupanuliwa kwa barabara hii kumekawia mno. Tusingoje mpaka watu wapate mateso. Barabara hii hata sasa inahitaji *traffic lights* katika makutano ya *New Bagamoyo* na inayokwenda Kijiji cha TPDC (karibu na *Celtel Head Office*) na vilevile *New Bagamoyo Road* na Sam Nujoma.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuzungumzia kuhusu *bumps* au matuta ya barabarani. Ni kweli matatu yapo kwa usalama hasa waenda kwa miguu, lakini vilevile yale ambayo hayakutengenezwa vizuri ni kero na hatari kwa waendesha magari. Hivi ni kwa nini matuta hupishana kwa vipimo? Ni kwa nini Wizara isitoe vipimo vinavyofanana nchi nzima, ili kuepusha ajali na kero? Ninaomba niambiwe *standard* ya matuta. Vilevile ni kwa nini hakuna *warning* kabla ya kuyafikia matuta barabarani?

Mheshimiwa Spika, ningependa Mheshimiwa Waziri anapofanya majumuisho atuelezee dhana ya eneo la barabara *reserve* na hasa hasa hivi karibuni walipopiga "X" kila bango hata shule, hospitali na ofisi za Taasisi mbalimbali, katika Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro na Arusha. Je, kulikuwa na ulazima huo? *Was this the best way* ya kufanya zoezi hili? Je, kulitolewa *notice* yoyote? Nitaomba kupata maelezo kuhusu zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara ya Ujenzi, kwa kazi nzuri ambayo imeshaonyesha mafanikio makubwa kwenye sekta ya usafiri. Pia nawapongeza kwa hotuba nzuri ya Bajeti ya Wizara. Napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kiambatanisho Na. 8 ukurasa wa 82 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kinaonyesha mishahara ya *TANROADS* 2003/2004, Sh. bilioni 3.85 rounded. Kwenye *volume II (Supply Votes) Vote 47 Programmer 60 page 147 subvote 6001 -280700 Transfers and subsidy - Non-profit Organization* imepewa Sh. 3.85 rounded *FY 2003/2004*, hii haikupata fedha 2001/2002 au 2002/2003. Je, haya mawili yana uhusiano, mishahara ya *TANROADS* na *Transfers/Subsidy Non-profit Organization?* Hii *Non-profit Organization* ni ipi na kwa nini mwaka huu na siyo pia miaka miwili iliyopita.

Ukilinganisha mishahara ya *TANROADS* na Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ambayo ni Sh.3.89 bilioni, *Vote 53 in Volume II page (xiii)*, ni vigumu kuelewa. Sijui Wizara inaweza kufafanua kidogo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. AISHA O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua nafasi hii kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Pili, Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa John Magufuli, Mbunge wa Biharamilo na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mbunge wa Morogoro Kusini, kwa hotuba nzuri waliyoiwasilisha . Nawapongeza pia Katibu Mkuu, *Engineer John Kijazi* na watalaaam wake wote. Baada ya pongezi hizo nitachangia katika maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuimarika kwa Wakala wa Barabara (*TANROADS*), napongeza Serikali kwa juhudzi zake za kuhakikisha kuwa miundombinu kama barabara ni suala linalotiliwa kipaumbele. Kazi nzuri tumeionna chini ya Uwakala wa *TANROADS*. Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, bado kilio kikubwa tunakiweka kwako kwenye barabara inayounganisha Wilaya ya Handeni na Kilindi na Wilaya ya Korogwe kwa kiwango cha lami. Mheshimiwa Waziri katika Bajeti iliyopita, kilio hiki tulikielekeza kwako, hata kabla ya Wilaya ya Handeni kuigawa. Umuhimu wa Wilaya za Handeni/Kilindi unafahamu sana kwani ndizo Wilaya Mkoani Tanga ambazo

zinalima mazao ya chakula na biashara ambayo si kwamba inalisha Mkoa wa Tanga na Mikoa jirani ya Arusha, Dodoma, Dar es Salaam, Pwani, Morogoro na kadhalika, bali hata nchi jirani zikiwemo Kenya.

Mheshimiwa Spika, kuwapatia barabara ya Korogwe - Handeni na Handeni-Mkata kwa kiwango cha lami na Handeni - Kilindi utakuwa umetuokoa wananchi wa Handeni/Kilindi na kuwapa maendeleo. Naamini Mheshimiwa Waziri, uwezo huo uno. Nakutakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wako, ili mpate nguvu za kuisaidia Handeni.

Mheshimiwa Spika, kupungua kwa tatizo la kuzidisha uzito wa magari katika barabara zetu. Naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kusimamia uzito wa magari kwa kutumia vyombo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, namshauri Mheshimiwa Waziri, alitupie macho tatizo la mizani pale Tanga-Kange. Mizani ya pale inaleta malalamiko sana kwa baadhi ya wawekezaji na wasafirishaji wa mizigo. Mizani ile ina ubora mdogo. Ni vizuri wataalam walitupie macho. Vilevile mizani hii inaleta utata kwa baadhi ya wawekezaji kwani wanapotoa malighafi bandarini, baadhi ya viwanda vilivyo ndani ya Mji wa Tanga, wanapotoa malighafi bandarini huwa mizigo yao haipimwi kwa vile viwanda viko ndani ya mji, hivyo hata kama mizigo umezidi hakuna wa kuwabana wale wenye viwanda nje ya Mji wa Tanga na ili wafike viwandani ni lazima wapitie katika ile mizani na kuna wakati huleta malalamiko ya uzito wa mizigo unaopita pale kwenye mizani, toka bandarini ambako huwa wakati wa kupakua mizigo huwa unapimwa na ukifika pale kwenye mizani huonekana umezidi au umepungua na hivyo wakati mwingine ukizidi wanatozwa faini!

Mheshimiwa Spika, nimwulize Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, hivi inakuweje wengine watoe mizigo bandarini na kupita moja kwa moja hadi kiwandani bila kuitia kwenye mizani, *of course* hawana sababu kwani viwanda viko nyuma (ndani) ya mji kabla ya kufika kwenye mizani. Nani atajua kama mizigo umezidi au la vipi muwekezaji huyu aliye nje ya mji alazimike kuitia kwenye mizani na wawekezaji wengine hawalazimiki? Hii inaonyesha kuwa tatizo la baadhi ya wanaviwanda kuona wananyimwa haki!

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ili kupunguza malalamiko haya, ingelikuwa vema *either* mizani iwekwe pale bandarini ili wote wapimiwe au wote wasipitishe kwenye mizani malighafi wale wanaotoa mizigo kwenda viwandani. Nini ushauri wako?

Mwisho, nakupongezeni wote na nawaombea kila la kheri msisahau barabara ya Korogwe-Handeni-Mkata kwa kiwango cha lami kwa maendeleo ya Handeni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri sana inayofanywa na Wizara ya Ujenzi.

Utekelezaji wa kazi nyingi unatupa nguvu sisi sote kama Serikali, pamoja na Chama chetu cha Mapinduzi.

Moja, nashukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chilonwa, kwa kuiweka kwenye mpango barabara yetu muhimu sana ya Chenene-Itiso hadi Izava. Barabara hii ni muhimu sana kwa huduma za kusafirisha chakula kutoka ukanda wa uzalishaji mahindi hadi Mjini Dodoma kwenye soko.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba barabara hii ya Chenene-Itiso hadi Izava inaweza kuunganishwa na barabara nyingine ambayo nayo iko kwenye mpango wa matengenezo. Barabara hiyo ni ya *Hogoro Junction* hadi Dosidosi. Kutoka Izava hadi Dosidosi ni kama kilomita 12 hivi. Kwa hiyo, hizi kilomita 12 zikifanyiwa matengenezo itatuwezesha kuwa na barabara moja inayounganisha barabara kuu mbili yaani Dodoma-Kondo-Arusha (Chenene-Itiso-Izava) na barabara kuu ya Dodoma-Morogoro-Dar es Salaam (*Horogo Junction -Dosidosi - Izava*).

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iangalie uwezekano wa kuunganisha barabara hizi mbili kwa kukifanyia matengenezo kipande cha kilomita 12 cha kutoka Dosidosi hadi Izava ili barabara hii iwe ya mzunguko.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Wizara hii na ninawatakitia kila la kheri.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja ya Wizara hii yafuatayo:-

Moja, awali napenda kuchangia kwa kuwapongeza kwa kazi nzuri inayofanyika, hasa ujenzi wa barabara ya Makuyuni-Ngorongoro Gate ambao unaendelea vizuri sana. Pongezi kwa wahusika wote.

Pili, katika mipango na utekelezaji wa 2002/2003 na sasa katika mpango wa 2003/2004, barabara ya Makuyuni - Lalago ambayo tangu mwaka 1996 imekuwepo kwenye hotuba na hata kufanyiwa utafiti wa awali imefutika. Naomba Mheshimiwa Waziri, afafanue kumetokea nini na kama mradi huu muhimu ambao unaunganisha Mkao wa Arusha na Shinyanga na Ukanda wa Ziwa kwa ujumla sasa utaanza lini. Ni vizuri Mheshimiwa Waziri, akaliarifu Bunge kuhusu matokea ya *survey* ya awali.

Tatu, kwa kuwa *Arusha Regional Road Board* imewasilisha Wizarani muda mrefu sasa, ombi la barabara ya Karatu - Mataala kuititia Qanded (Eyasi) kuwekwa chini ya usimamizi wa *TANROADS (Arusha Region)*, kwa vile ni barabara muhimu kiuchumi na kijamii inayounganisha Mkao wa Shinyanga (Meatu) na Mkao wa Arusha (Karatu); ni lini sasa barabara hiyo itaanza kuhudumiwa kama barabara ya Mkao chini ya *TANROADS*, hasa ikizingatiwa kuwa sasa Mkao wa Arusha una barabara moja tu ya Mkao ambayo ni Karatu-Mbulu. Napenda Mheshimiwa Waziri atupe matumaini kuhusu jambo hili ambalo limekuwa kilio cha wananchi hasa wa Eyasi, ambao wanazalisha karibu asilimia 60 ya vitunguu vyote nchini.

Nne, katika majedwali 7(d) - (h) *unpaved Regional Roads*, barabara ya Karatu - Dareda ambayo miaka yote imekuwa barabara ya Mkoa chini ya TANROADS, mwaka huu haionekani wala kwa *spot improvement*, wala *periodic maintenance*. Je, Serikali inatoa kauli gani kwa barabara hii muhimu inayounganisha Mkoa wa Arusha na Manyara, ambayo haiko kwenye hali nzuri na kwa uzoefu mwezi Desemba na Januari kila mwaka ina hatari ya kujifunga kutokana na mvua za vuli. Je, zimetengwa fedha kiasi gani na zimebekwa chini ya kasma ipi baada ya kutoonekana kwenye majedwali yaliyotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani za dhati, narudia kuwapongeza tena kwa kazi nzuri.

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu Waziri na watendaji wake wote. Kazi waliyoifanya katika kipindi kilichopita ni kubwa, inaonekana na ni *practical* waendelee hivyo hivyo.

Sasa basi nilileta *proposal* kuhusu ujenzi wa barabara ya Mkata-Handeni - Korogwe kwa kiwango cha lami. *Proposal* hiyo ambayo niliigharamia kwa kupeleka wataalam nadhani nitoe picha kamili ya hali ya uchumi na jamii. Katika eneo tajwa, najua *proposal* hiyo nimesha-submit Wizarani lakini bado sijapata *feedback*. Ningeshukuru sasa mkianza programu ya kutengeneza barabara hiyo hata kwa awamu.

Awamu ya kwanza inaweza kuwa Mkata-Handeni au Korogwe-Handeni . *Either* inaweze kuwa ni awamu ya utekelezaji. Mafanikio na usanisi tunaona sasa. Wizara ya Ujenzi ni vyema nasi tukafaidika nao hususan wananchi wa Jimbo la Handeni yenye Makao Makuu pekee Mkoani isiyokuwa na barabara ya lami.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuendelea na utengenezaji wa barabara ya Dodoma, Singida, Igunga, Shinyanga, hadi Mwanza. Kukamilika kwa barabara hii kutakuza uchumi katika nchi yetu na kurahisisha mawasiliano.

Nampongeza Mheshimiwa Waziri, pia kwa mashirikiano yake makubwa ambayo anayafanya na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, naomba aendelee hivyo hivyo. Sisi kwetu tunaona kuwa ushirikiano huo unajenga mshikamano na unaimarisha zaidi Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu magari ya Serikali. Napongeza juhudhi za Serikali za kuhakikisha kuwa magari yote ya Serikali kuwa na namba zinazolewaka (Serikalini). Miaka ya nyuma Serikali iliwhali kupunguza magari yake na kuwa na idadi maalum tu ya magari, lakini baadhi ya Wizara na Taasisi za Serikali zimekuwa na magari mengi zaidi na kusababisha matumizi makubwa kwa sababu ya kuyahudumia magari hayo. Serikali

inaliangalia vipi suala hili? Serikali pia ilikuwa na magari maalum kwa matumizi yake ili kusaidia uingiaji wa *spare* za magari hayo badala ya mtindo wa sasa unaotumika kwa kila asasi kuhusu aina gari inayotaka .

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Wizara kwa mashirikiano makubwa baina ya Waheshimiwa Wabunge na Wizara na naomba utaratibu huo uendelee.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa, Mheshimiwa John Magufuli, Waziri wa Ujenzi, kwa hotuba yake nzuri sana, inayoeleweka vizuri na yenyen takwimu muhimu.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Naibu Waziri wa Ujenzi, *Engineer* John Kijazi, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wakuu wote wa Wizara ya Ujenzi kwa utendaji wao wenye ufanisi ambao umeijengea Wizara hii heshima kubwa humu Bungeni. Endeleeni na juhudhi hizo na tutaendelea kuenzi kazi zenu nzuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. PROF. PIUS P. MBAWALA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa John Magufuli, pamoja na pongezi hizi naomba Mheshimiwa Waziri atupie jicho yafuatayo:-

Moja, barabara ya Lingusenguse -Lusewa-Mkongo hadi Mtwara Pachani. Barabara hii imetajwa katika kitabu cha makisio ukurasa wa 65 chini ya *Ruvuma Regional Road*, ujenzi wa madaraja unaenda polepole na sio kwa kasi tunayopendelea. Tutashukuru sana iwapo ujenzi wa tuta la barabara hii lingekamilika haraka kabla ya 2005. Hii ni njia iliyosahauliwa sana ingawa ni njia ya Mkoa ya miaka mingi sana. Inapita katika eneo la Jimbo langu la Namtumbo (*No. II Ruvuma Region*). Njia hii ni mbaya sana. Tafadhali utembelee barabara hii ili ipate msukumo wa kukamilika mapema. Natanguliza shukrani.

Pili, ujenzi wa barabara ya Songea - Kitanda iunganishwe na *Regional Road* ya Lupilo Kilosa kwa Mpepo - Mto Londo hadi Kitanda. Katika kitabu chako barabara hii ipo ukurasa 68 (*No.28 Morogoro Region*).

Barabara ya kitanda hadi Kilosa kwa Mpepo zikifanyiwa mchoro wakati wa 2003/2004 itasaidia sana kuanza kujengwa kwanza madaraja wakati wa 2004/2005 na hivyo mambo kukamilika kabla ya mwaka 2005. Hii itasaidia kuimarisha kilimo kati ya kwa Mpepo na Kitanda. Aidha, shughuli za utalii zitaimarishwa maana Kitanda ni eneo la watalii hivyo itafupisha usafiri baina ya Wilaya na Namtumbo. *Engineer* Kilowoko Wizarani, anaifahamu barabara hii kwa ukamilifu sana. Natanguliza shukrani.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa mikakati ya ujenzi wa barabara nchini na uamuzi wa kuunganisha Makao Makuu ya Mikoa yote kwa barabara za lami (ukurasa wa 5). Pongezi sana sana.

Moja, barabara toka Njombe hadi Lupembe ni *Trunk Road* tunaomba *extension* toka Lupembe hadi Taweta na Mlimba ili kuunganisha Mikoa ya Ruvuma na Mbeya na Mkoa wa Morogoro kupitia Bonde la Kilombero. Barabara toka Lupembe hadi Taweta ilijengwa mwaka 1999 na NGO iitwayo *PADA*, lakini haikukamilika upanuzi na kalvati. Tunaomba msaada wa fedha na utaalam ili barabara hii iweze kutumika. Kwa sasa haitumiki. Pia tunaomba iwe *Trunk Road* kutoka Njombe hadi Taweta-Mlimba. Ombi hili pia lililetwa na Mkoa (Bodi ya Mkoa)

Pili, kwa kutumia fedha za *Road Toll* na Fedha za Halmashauri ya Wilaya, imejenga madaraja 6 kati ya (Makambako) Lyamtieni hadi Ikondo kupitia Itipingu, Upami, Lole, Ninga, Limahadi Ikondo. Ukosefu wa fedha umesababisha Wilaya ishindwe kupanua barabara hii ya (Makambako) Lyamtieni-Ikondo, mpaka sasa barabara hii haipitiki licha ya wananchi kukwetua barabara hii kwa majembe. Tafadhalii sana tusaidie upanuzi.

Tatu, barabara ya Makambako - East Road. Barabara hii ina umbali wa kilomita 60 tu kutoka Makambako hadi Ilevelo eneo lenye ardhi nzuri kwa kilimo. Ni eneo ambalo watu wanataka kuhamia ili kuendeleza kilimo. Kwa sasa watu wanatumia kilomita 260 kwenda Ilevelo kupitia Lupembe au kilomita 242 kufika Ilevelo kupitia Mgololo (Idete) wakati barabara ya Makambako- Ilevelo ni kilomita 60 tu. Wananchi wa vijiji vya Makambako na Mufindi kwa kushirikiana wamekwetua barabara hii ya Makambako -Ilevelo na inapitika kwa miguu na baiskeli. Tunaomba msaada wa kitaalam na fedha ili kujenga madaraja madogo 4 ili barabara hii iweze kutumika. Eneo la Ilevelo ni muhimu sana kiuchumi. Natumaini kilio chetu kitasikilizwa. Barabara hii itawahudumia wananchi wa Wilaya ya Mufindi na Njombe na kuwaunganisha na soko kuu la mazao la Makambako.

**MHE. BATILDA S. BURIAN:** Mheshimiwa Spika, naomba kuungana na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri John Magufuli, Naibu Waziri wake, pamoja na timu nzima ya Wizara yake, kwa kazi nzuri sana waliiyofanya ya kutoa hotuba hii nzuri sana. Hata hivyo, pamoja na pongezi hizi napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Moja, ujenzi wa barabara. Napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri, kwa jitihada zake binafsi kwa kushirikiana na timu ya Wizara yake katika kuendeleza mitandao ya barabara hapa nchini. Kusema kweli jitihada hizi zimeifanya nchi yetu kufaidika zaidi katika miradi ya E.A.C. kushinda nchi za jirani zetu. Hii ni kutohana na kuwepo kwa dira na malengo ya dhahiri na mipango mizuri katika Wizara. Kwangu ni zito na inaweza kunipelekea kutoa shilingi.

Pili, jambo lingine ni mpangilio mzima wa ujenzi wa nyumba hizo. Napendekeza Wizara hii ipatiwe maeneo mazuri, ili nyumba zitakazojengwa ziwe na mpango mzuri na

*facilities*, muhimu kama vile maeneo ya kuchezea watoto, *shopping center* na kadhalika. Mfano ni nyumba zilizojengwa Arusha *AGM Complex*.

Tatu, Mheshimiwa Spika, pia ningeshauri Serikali iangalie umuhimu wa kujenga majengo ya Wizara kwa zile Wizara ambazo zinapanga majengo kwa Mashirika mbalimbali. Fedha nyingi sana za Serikali zinapotea kwenye kulipia kodi za pango. Napendekeza Wakala wa Majengo wahuishwe ili waweze kujenga majengo kwa ajili ya Ofisi za Wizara, kama vile Wizara ya Viwanda na Biashara ambao wanapanga katika jengo la Ushirika. Hata hivyo, napenda kushauri kwamba, katika kujenga barabara za *Highways*, ni vizuri basi kukawa na ushirikiano wa karibu na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, ili kuweka vituo vya dharura (*Emergency Points Stops*), kwa ajili ya kupata mawasiliano. Hii itasaidia kupata taarifa za ajili, *breakdowns*, ujambazi, ujangili na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuzungumzia kuhusu shughuli za Wakala wa Majengo. Kwanza kabisa, napongeza jitihada za Wizara kwa kujenga nyumba kwa ajili ya kuwauzia watumishi wa Serikali. Jambo hili ni zuri sana ila naomba Serikali ihakikishe kwamba, watumishi wote watafaidika na hakutakuwa na upendeleo au uonevu.

Pili, kumetokea tatizo la maeneo ya kujenga nyumba hizo za watumishi. Mimi nimeguswa sana kwa upande wa Arusha, kwani Wizara imechukua eneo la shule ya Msingi Themi na kujenga nyumba hizo. Shule hii ndipo niliposomea, hivyo naomba Mheshimiwa Waziri, anielezee suala hili na utatuzi wa tatizo hili wakati wa kujibu hoja hapa Bungeni. Pia naomba anijibu kimaandishi kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, napenda kusema kwamba, nitaunga mkono hoja iwapo nitapatiwa majibu mazuri ya kuniridhisha kuhusu masuala niliyotaka ufanuzi. Ahsante.

**MHE. ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa John Magufuli, Waziri wa Ujenzi, kwa kuonesha moyo na tabia ya kutekeleza ahadi anazoziveka. Alinieleza angetuma wataalam wa *TANROADS* wa Mkoa wa Tanga na Mkoa wa Morogoro kufanya *survey*. Nafurahi kukujulisha wataalam hao walikuja na wamekwishafanya *survey* ya barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya mchango huu ni kuomba kukueleza umuhimu wa barabara hii. Kihistoria, barabara hii ndiyo iliyokuwa barabara kuu ya kwenda Mikoa ya Kaskazini kutoka Dar es Salaam na pia ndiyo iliyokuwa barabara Kuu kwenda Mikoa ya Nyanda za Juu kutoka Dar es Salaam hadi nchi za jirani za Malawi na Zambia. Kwa wakati huo, hii ndiyo iliyokuwa barabara kuu iliyokuwa inakwenda Kaskazini mwa nchi yetu na Mikoa ya Nyanda za Juu na mpaka nchi za jirani za Malawi na Zambia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu huu wa kihistoria barabara hii kiuchumi ni muhimu sana kwa sababu inapitia katikati ya vijiji vingi vyenye ardhi nzuri ya kilimo

cha mazao ya biashara na chakula. Iwapo barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami, itasaidia sana kupanua kilimo cha mazao ya biashara na mazao ya chakula.

Mheshimiwa Spika, vijiji ambavyo barabara hii inapitia vinalima mazao ya kahawa, pamba, korosho, mahindi, mpunga, ndizi, mtama, maharage, miti ya matunda ya machungwa, miembe, mbogamboga na aina ya mbogamboga zinazolimwa ni *organic vegetables*. Aidha, hata mazao ya chakula pia nayo ni *organic crops* kwa sababu wakulima hawatumii *industrial fertilizers and other chemicals*, katika kilimo cha mazao yao. Mazao yote yanayolimwa kwa kutumia njia ya *organic*, yana soko kubwa sana katika masoko ya Ulaya na kwa hiyo, yatatuingizia fedha za kigeni nyingi.

Mheshimiwa Spika, umuhimu mwengine wa ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami, unapatikana kwa kupitia eneo la mashamba ya miwa. Shamba la Miwa la Kampuni ya Kilombero, ambalo kwa sasa linazalisha sukari tani 100,000 na kutokana na malengo yao wanategemea baada ya miaka michache ijayo Kampuni hii ya Kilombero inategemewa kuzalisha tani 200,000.

Vilevile Mheshimiwa Spika, shamba la miwa la Mtibwa kwa sasa linazalisha tani 45,000 za sukari na wanategemea katika miaka michache uzalishaji wa sukari katika Kampuni hii ya Mtibwa kufikia kuzalisha sukari tani 120,000. Pamoja na uzalishaji wa sukari wa Kampuni hizo mbili, nimepata habari za kuaminika kuwa mwekezaji wa mashamba ya miwa ya Kampuni ya Mtibwa ana mipango ya kuanzisha kilimo cha miwa itakayotoa *Organic Sugar* katika moja ya mashamba yake.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa *almost all consumers in the world prefer organic crops*. Kama nilivyoeleza mazao yote, *vegetables* zote na matunda yote yanayolimwa *along side this road are all organic*. Kwa maana hii kiuchumi kwa kufungua na kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami, itaongeza pato la uchumi wa Taifa letu kwa asilimia kubwa. Pia lipo shamba la Dizungu la miwa na hivi sasa shamba la miwa la Dakawa chini ya mwekezaji wa Kampuni ya Sukari ya Mtwa. Mashamba haya mawili pamoja na shamba la Mtibwa na shamba la Kilombero, uzalishaji wa sukari utafikia tani 400,000.

Mheshimiwa Spika, mtandao wa barabara hii pia unapita maeneo yenye mifugo mingi sana. Kufuatia Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, bidhaa za ngozi za ng'ombe zimekekewa mipango ya kudhibitiwa. Kwa ajili hii mifugo yote iliyomo katika mtandao wa barabara hii eneo la Kilosa itaongeza pato la uchumi wa Taifa letu. Lakini kubwa zaidi ni ule uamuzi wa Serikali wa kubaki na eneo hekta 20,000 katika shamba la mifugo la *Mkata Ranch* kwa ajili ya kukuzia mifugo ya mfano na eneo lote litatolewa hekta 4,000 kwa kila mtu bure kwa wananchi kwa ajili ya kuendeleza mifugo bora ya kisasa. Utekelezaji wa uamuzi huu utaongeza idadi ya wafugaji na wakulima kufuga ng'ombe bora.

Mheshimiwa Spika, hali hii itapelekea Mji wa Kimamba ambao barabara hii nashauri kupendekeza ipitie, patakuwa na kiwanda cha *ku-process* maziwa na ngozi kwa sababu eneo litakalobaki baada ya hekta 20,000 kutengwa litakuwa na ukubwa wa hekta

220,000. Hilo ni eneo kubwa sana ambalo litawezesha barabara hii kuwa kichocheo cha uendelezaji wa mifugo na mazao ya chakula.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa kabla ya shamba la mifugo kugawiwa, eneo hili linapopita barabara hii upande wa Kilosa kuna jumla ya ng'ombe wanaokadiriwa kuwa 300,000 hivyo, kama eneo la hekta 220,000 litatolewa eneo hili linakadiriwa kuwa na ng'ombe karibu 700,000.

Mheshimiwa Spika, kiuchumi barabara hii italipa gharama zake za ujenzi kwa kiwango cha lami katika kipindi kifupi sana kwa sababu barabara itasaidia ukuaji wa uchumi wetu kwa kutumika kusafirisha mazao ya chakula, mazao ya mbogamboga na matunda na kutumika kusafirisha sukari na mifugo pamoja na mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, faida nyingine ya ujenzi kwa kiwango cha lami barabara hii inapatikana na kuondoa tatizo kubwa linalosababisha kupungua kwa wanyamapor kwa kuwepo kwa barabara kuu ya lami inayopita katikati ya Hifadhi ya Taifa ya Mikumi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la barabara kuu ya lami inayopita katikati ya Hifadhi ya Taifa ya Mikumi limo katika makundi matatu yeye athari za ajali, kiuchumi na kimazingira kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ajali nyingi hutokea kwa magari kugonga wanyamapor waliopo ndani ya Hifadhi ya Mikumi ambapo hali hii inapoteza wanyamapor wengi kutokana na kugongwa na kukanyagwa. Kwa mfano, Tembo, Simba, Chui, Twiga, Nyati, Pundamilia, Swala, Nyoka, Mijusi na wengineo. Katika vifo hivi vinavyosababishwa kwa kugongwa au kukanyagwa, jambo baya zaidi ni wale wanyama kama Simba kuacha utamaduni wao wa asili wa kuwinda, kuua na kula yule mnyama waliyemuwinda.

Sasa Simba katika eneo la barabarani kwa sababu ya uwingi wa mizoga Simba wameacha ile mila na desturi yao ya Simba jike kuwinda kukamata na kumwita Simba dume kula mnyamapor aliyemuua. Jambo hili si mzaha. Ukipenda unaweza kwenda kituo cha *TANAPA* pale Mikumi, kuthibitisha haya ninayosema, inawezekana kimtzamo jambo hili likawa la kuchakesha.

Mheshimiwa Spika, lakini unataka kupata mawazo ni njia zipi zitawezesha wanyamapor wakawa endelevu katika uchumi wa Taifa letu. Hivyo, mambo ambayo yanaweza kuchochea wanyamapor hasa katika Hifadhi ya Mikumi kutoweka pale watakapoona hata mila na desturi zao hazitekelezeki. Hivyo, ni muhimu tujenge mkakati kwa kulinda mila na desturi za wanyamapor. Katika barabara ya Mikumi kwa sasa kila siku wanakufa wanyamapor watano kwa kugongwa au kukanyagwa na mbaya zaidi mara nyingi hutokea wanyamapor wanaogongwa na kufa huwa majike na tena wenye mimba. Pia watu wengi hupoteza maisha yao kutokana na ajali za magari na wanyamapor.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine baya zaidi ni pale tabia ya wanyamaporini apoharibika kutokana na baadhi ya wasafiri wa kutoka nchi za jirani wanapowalisha wanyamaporiv yakula vyao ambavyo vimwekwa sumu ya aina ya ulevi. Wanyamapori wanapolewa wanabebwa na kuwapeleka kwoa bila shaka wanawachukua ili wakawaweke kwenye *zoo* zao.

Kitendo hiki kinachangia sana kupunguza mno idadi ya wingi wa wanyamaporikatika Hifadhi yetu. Napenda ieleweke kwa kuwa Hifadhi ya Mikumi kwa ukubwa wa eneo ni ya tatu katika nchi yetu itakuwa jambo la kijinga kabisa kama wanyamaporiwetu wote watatoweka. Ukiangalia sababu kubwa ni barabara ya Mikumi ambayo kuibadilisha wake ni jambo ambalo limo ndani ya uwezo wa Serikali.

Mheshimwia Spika, baadhi ya wanyamaporivaliopo katika Hifadhi ya Mbuga ya Mikumi husafiri hadi kwenye Milima ya *Eastern Mountain ARC*, ambayo ina viumbe hai wa kipekee na hawapatikani kwingine kokote duniani.

Kwa mfano, katika Msitu wa Mandege uliopo Kilosa, ameonekana kinyonga mwenye pembe mbili. Katika hali hii tuna kila sababu ya kulazimika kutunza Hifadhi ya Mbuga ya Mikumi, kwa kuelewa na kuamini umuhimu wa wanyamaporikatika uchumiwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, uchafuzi wa mazingira (*Pollution*), kutokana na wasafiri wanaopita kwenye maeneo hayo ya barabara ya Mikumi. Wasafiri hawa hutupa mifuko ya *plastic*, chupa za maji waliyokwisha kunywa, makopo ya pombe za bia na soda. Bila kufahamu madhara ya kula vitu hivyo, wanyamapori wanakula vitu hivyo vinashindwa kuwa *digested*, yaani vinashindwa kubadilika tumboni na hatimae kusababisha vifo kwa wanyamaporihao.

Vifo vya aina hii vinatokea mara kwa mara kwa sababu mabasi ya abiria yanapitakatika barabara ya Mikumi ambayo inapita katikati ya Hifadhi ya Wanyampori ya Mikumi. Barabara ya Mikumi inatumika na magari mengi na mazito ambayo mengi ni magari ya nchi jirani. Magari hayo mazito yakipita katika barabara hiyo kwenye maeneo ya wanyamaporikwa mingurumo yao na honi zao huwatisha wanyamaporinakuwakosesha amani. Kupita kwa magari katika hifadhi huathiri mienendo ya wanyamaporikutoka sehemu nyingine kutafuta malisho na maji.

Mheshimiwa Spika, kwa hali ya barabara ya Mikumi ilivyo sasa, fedha nyingi za kigeni zinapotea kutokana na wasafiri kutolipa ada za kuangalia wanyamaporii. Hali hii inaweka Taifa letu kushindwa kuelewa umuhimu wa wanyamaporiwetu.

Mheshimiwa Spika, watalii wengi wasio rasmi wanaopita katika barabara ya Mikumi ambayo ipo katikati mwa Hifadhi ya Mikumi hutumia muda wao mwangi katikabarabara ya Mikumi kuchukua mikanda ya video za wanyamaporiwetu bila kulipa fedha za kufanya biashara hiyo. Wakati mwangi husingizia magari yao yameharibika kwa kufungua *bonet* za magari huku wakiendelea kupiga picha za video wanyamaporiwetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hoja za kiuchumi napendekeza barabara ya Mikumi ifungwe.

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwa kifupi kama ifuatavyo:-

Kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Naibu wake, Katibu Mkuu na watendaji wote walio chini yao kwa kazi nzuri sana wanayofanya.

Pili, napendekeza/nashauri/naomba barabara inayochepukia Kisesa kwenda Fela kwa wasafiri wenye magari ambao hawana sababu za kuingia Mwanza mjini ipewe first priority. Kwa mtu anayetoka Magu kwenda Shinyanga na ana haraka kupita Mjini Mwanza ni upotevu mkubwa wa muda.

Tatu, barabara inayopita Magu Mjini (Uhindini) kwenda Mwanza/Musoma bado inatumika sana na mabasi pamoja na malori makubwa. Naomba barabara hii (kama kilometra 1 tu hivi) iwekwe lami maana inaigharimu Halmashauri ya Wilaya ya Magu fedha nyingi sana kuikarabati mara kwa mara. Isitoshe vumbi linalotimuliwa muda wote na mabasi/malori ni a big health hazard. Watu wanaokaaa ama kufanya biashara katika barabara hii wanakabiliwa na hatari kubwa kiafya.

Nne, Sekenke paanziwe kuwekwa lami ya uhakika kama priority ili kupunguza hasara ya uhai wa binadamu wanaopoteza maisha kila mara na upotevu wa mali. Naunga mkono kauli aliyoitao Mheshimiwa Seleli leo hii.

Tano, ubora wa barabara, kuna baadhi ya barabara hapa nchini za Kitaifa, Kimko na Wilaya ambazo zinatengeneza barabara hasa ngazi ya lami, huharibika muda mfupi sana baada ya kutengenezwa. Mfano mzuri ni barabara ya Pamba Road huko Mwanza.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara ya Ujenzi kwa jinsi Wizara hii inavyojitahidi kutekeleza kwa karibu ahadi mbalimbali za kutengeneza barabara Jimboni Songwe. Hivi karibuni imetengenezwa toka mpakani mwa Wilaya ya Mbeya mpaka kijiji cha Galula kwa kuitengeneza vizuri barabara hiyo na pia maeneo mengine kuelekea Mkwajuni - Saza - Makongorosi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ya Ujenzi inisaidie sana tena sana kutengeneza barabara ya Mbalizi - Msangamweru. Kuna lami kidogo ambayo Wizara ilinisaidia maeneo makorofi ambako palikuwa hapapitiki bado eneo lile sio zuri kama kilomita mbili Msangamweru - Mjele. Naomba eneo hilo lililobakia liwekwe lami kwa sababu lina mawe na ni pa baya. Mheshimiwa Naibu Waziri amepita eneo hilo ninalolisema. Linanisonenesha sana ninapopita pale. Ahsante sana kwa kutupatia lami eneo la Msangamweru.

Mheshimiwa Spika, yapo matatizo makubwa ya barabara kutopitika toka Galula kwenda kijiji cha Namkukwe. Mara kwa mara nimekuwa nikiahidiwa hapa lakini hata kwenye hotuba sioni chochote licha ya kuelezwu kuwa eneo hili lingepewa kipaumbele walau matengenezo kidogo kidogo. Hili suala linakuwa kama deni kwa Wizara licha ya majibu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ipo barabara ya Saza - Kapalala hii ni ya Mkoa (*TANROADS*) hata mwaka jana haikutengewa pesa ndiyo maana haikupitika mwaka mzima. Sijui lipotatizo gani kuhusu barabara hii na hii ndiyo barabara ambayo ni rahisi kuunganishwa na Mkoa wa Tabora na Sumbawanga hata Wilaya ya Mpanda kwa kupitia mbuga zile za Lukwati. Hivi kwa nini Wabunge tunasema kila mara hakuna kitu kinachotekelozwa? Eneo lile limefunga kabisa. Naomba Waziri akumbuke sana barabara hizi mbili kama nilivyoziyelea Galula - Namkukwe na Saza - Kapalala kwenda Mpanda. Ebu nisikie mnazungumza kitu gani juu ya haya na hasa kwa nini barabara hizi hazijawekewa pesa licha ya kuzitaja kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuipongeza Wizara ya Ujenzi kwa mipango yake ya uchapakazi katika kuboresha hali ya barabara nchini. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wengine, nawapongezeni sana.

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi ya awali kabisa kuipongeza sana hotuba hii ya matumaini ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi. Namtakia kila la kheri yeze na watendaji wake ili kuitekeleza vizuri bajeti yao hii na ninaunga mkono moja kwa moja. Hata hivyo, naomba kuchangia machache kama ifuatavyo:-

- (i) Ili kuboresha na kuinua uwezo wa Watanzania kumudu kazi za ujenzi hasa Wahandisi na Makandarasi, nashauri pamoja na mbinu zilizopo basi tuisitize suala la Joint-ventures baina ya wageni na wazalendo kama mkakati mahususi. Hii itasaidia vile vile masuala ya technology transfer na kupata zana na vifaa vya ujenzi.
- (ii) Ni vizuri Serikali ikatenga miradi maalum ya barabara ambazo zitatengenezwa kwa utaratibu wa *Build Operate and Transfer (BOT)* na mbinu nyingine ili tukamilishe barabara nyingi zaidi kwa haraka kama inavyowezekana.
- (iii) Naomba Wizara yako ya Ujenzi ishirikiane na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar ili kufanikisha miradi inayofadhiliwa kutoka nje. Hii itasaidia kutekeleza Ilani ya CCM ya kutaka barabara hizi zijengwe haraka kama inavyowezekana.
- (iv) Ombi maalum ni kwa barabara zinazofadhiliwa na *ADB* za Zanzibar na hasa barabara ya Fumba ambayo ina umuhimu maalum kwa Wazanzibar na inapita kwenye Jimbo la Dimani. Umuhimu wa barabara hii ni kuwa itafungua maeneo huru (*EPZ*) ya Fumba kwa hivyo kusaidia kuinua uchumi wa Zanzibar kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba kusema tena naunga mkono hoja hii.

**MHE. OMAR M. ALI:** Mheshimiwa Spika, ninachukua nafasi hii kutoa pongozi zangu kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi kwa hotuba nzuri na yenye maendeleo ya kweli ya Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kunukuu ukurasa 2,3,4 ambao umeelezea majukumu ya Wizara kama aliyooyaeleza Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake hii, ninampongeza sana na ninamtakia mafanikio mazuri na ya salama.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa tano unaelezea Dira ya Wizara. Dira hii ndio mkombozi wa Taifa letu na wananchi kwa ujumla katika kuleta ufanisi wa maendeleo ya kijamii na kiuchumi na hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa kumi na moja unaelezea juu ya mkutano wa wahisani na nchi wanachama wa Afrika Mashariki (*EAC*) uliofanyika Arusha 29/4/2003 ambapo ulifunguliwa na Mheshimiwa Rais Mkapa, ulikuwa na lengo la kutathmini utekelezaji wa mradi wa pamoja wa barabara (*The East African Road Network Project*) ulioanza kutekelezwa na nchi wanachama mwaka 1998 kwa ufadhilli wa wahisani mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ninaipongeza sana Wizara hii ya Ujenzi na ningeiomba sana Serikali kwa mfumo huu huu wa Wizara ya Ujenzi kuweza kuziunganisha nchi hizi tatu hata kwa njia za Bahari na Maziwa yetu nchini kwa kujenga miundo mbinu ya Gati na viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Spika, ninalisema hili kwa eneo zima la Kisiwa chetu cha Pemba ambacho tuko jirani sana na Kenya ambapo kama tutakuwa na Bandari nzuri Wete, Mkoani na Chake-Chake hata katika eneo la Kigomasha itasaidia kuinua uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi anapofanya kazi nzuri sana kwa Taifa letu jambo ambalo linahitajika ni kuungwa mkono na Watanzania wote tukiwemo Waheshimiwa Wabunge, viongozi wa Serikali na vyombo vingine nchini.

Mheshimiwa Spika, kuna umuhimu mkubwa kumpa ushirikiano wa kweli mtu uliyempa mzigo mzito kuufikisha mahali ambapo pamekusudiwa na kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na wahusika wenzake katika Wizara yake wana majukumu makubwa kwa Taifa hili kulifikisha pale tunapokusudia kutaka kulifikisha kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 39 unaelezea vita dhidi ya rushwa. Ninamshukuru Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake amesema: “Kama nilivyoliezea Bunge lako Tukufu katika hotuba yangu ya mwaka 2002/2003 mikakati ya kupiga vita rushwa katika sekta ya ujenzi ambayo Wizara yangu inaendelea kuitekeleza ni pamoja na kutekeleza kwa dhati Sheria ya Manunuzi Na.3 ya Mwaka 2001 (*Public Procurement Act No.3*) ambayo kwa kiasi kikubwa inapunguza mianya ya rushwa katika utoaji wa zabuni za ujenzi, ushauri na ununuzi wa vifaa”.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa mikakati hiyo ya kupiga vita rushwa katika sekta ya ujenzi ambayo ni Wizara yake ndiyo msimamizi mkuu, kwa kutumia Sheria hiyo Na.3 ya mwaka 2001.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Mheshimiwa Waziri anafanya kazi nzuri sana na kwa kweli amenipa matumaini makubwa na kuniondolea hofu moyoni mwangu hasa ninapofuatalia utendaji wake mzuri pale alipoelezea juu ya Sheria hii Na.3 anavyoitumia kupambana na wala rushwa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika kuthibitisha zaidi uwezo wa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwa ujumla ni hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani hapa Bungeni kuhusu Wizara hii ya Ujenzi ambapo ninanukuu katika hotuba yake ukurasa wa kumi na moja ambapo alielezea kuhusu Daraja la Mto Rufiji alisema: "Kambi ya Upinzani inashauri uwepo mkakati wa makusudi wa kulilinda daraja hili maalum la Mto Rufiji kutohana hasa na unyeti wake wa kiuchumi na hata kiutawala wa nchi".

Mheshimiwa Spika, maelezo haya ni ushahidi safi wa uwezo mkubwa ulio makini na uliojaa juhudhi na ukweli wa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwa Taifa hili la Tanzania na kwa Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Magufuli, Waziri wa Ujenzi amebarikiwa na anafanya kazi nzuri yenye kuridhisha umma wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, hakuna kazi nzuri au kitu kizuri ambacho hakitokuwa na kasoro au mapungufu hata kidogo. Kwa hivyo, kwa yale madogo madogo hatunabudi kuyafanya uvumilivu mkubwa na baadaye tumpe ushirikiano wetu kwa dhati.

Mheshimiwa Spika, nataka ninukuu hotuba ya Mheshimiwa Rais Mkapa ya tarehe 31/5/2003 ambapo aliwataka viongozi wa ngazi mbalimbali nchini kuwasaidia wananchi wafikie matarajio yao.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Magufuli anajitahidi kuwasaidia wananchi wafikie matarajio yao kwa nchi nzima. Namtakia mafanikio, maisha marefu na salama hapa duniani, kazi njema na ushirikiano mzuri na wenzake katika Wizara yake, Waheshimiwa wenzake na Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, ninamuomba Mheshimiwa Waziri msaada wake kwa barabara zangu ndani ya Jimbo la Vitongoji. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia.

**MHE. KHERI K. AMEIR:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wapiga kura wangu napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na wafanyakazi waandamizi wa Wizara yake ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, nataka kuongelea barabara za Zanzibar hasa Jimboni kwangu. Jimbo la Matamwe nikizungumzia barabara kutoka Pongwe/Kiwengwa/Pwani Mchangani kuelekea Matamwe (ingawa naelewa suala hili sio la muungano, naelewa Zanzibar katika hili ni lao wenywewe) lakini hata hivyo, kwa uelewa wako na juhudi zako

ambazo nzipongeza, tunaomba ultizame suala hili. Mwaka jana ultienga fungu kwa barabara hizo lakini mwaka huu hatukuona kitu.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 61 wa kitabu chako cha bajeti kasma 4155 (*Road Safety Master Plan*), kuna maelezo ambayo sikupata maana yake hasa ya kifungu hicho.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 11(12) na ukachukua ramani iliyoambatizwa (*Trunk Roads Transport Corridor*) imejielekeza mfumo wa barabara ambao unao mtandao wa EAC (*Road Network Project*) hapakuzingatiwa suala la barabara za Zanzibar ingawa naelewa kuwa Zanzibar imo ndani ya ramani ya kijumuia ndani ya Tanzania lakini hata hivyo nakumbushia endapo limesahauliwa. Zanzibar endapo barabara niliyoitaja hapo awali itashughulikiwa itasaidia sana uchumi wa Zanzibar kwani eneo hilo ni eneo/ukanda wa utalii.

Ninapenda kuungana na baadhi ya wachangiaji waliokupongeza katika ujenzi wa Daraja la Rufiji na kwa kazi nzuri mliyoifanya ya kuunganisha kanda ya Kusini na Mkoa wa Pwani. Lakini sasa elekeza juhud zako kuendeleza ujenzi wa barabara ya Kusini (*Mtwara Corridors*). Ufahamu wangu ni mdogo katika hili lakini kimaelezo hapa Bungeni ni kwamba kuna mwelekeo wa uchumi mkubwa sana utakaosaidia uchumi wa Tanzania. Vile vile nampongeza Mheshimiwa Waziri na naomba uelekeze juhud zako kukamilisha kazi ya kuunganisha barabara Kim-Mikoa kwa Kanda ya Kati kwani barabara itasaidia usafirishaji wa bidhaa kutoka eneo fulani na kupeleka eneo lingine. Hii itasaidia sana kupunguza umaskini na kujenga uwezo kwa wananchi (Watanzania).

Mheshimiwa Spika, lingine ikiwezekana katika kazi hizo Mheshimiwa Waziri afikirie kuwaajiri vijana kwenye ujenzi wa barabara na hata majumba yanayojengwa, ahsante.

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kwa kuwapongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkurugenzi pamoja na wataalam wao wote kwa pamoja kwa kukaa na kupanga bajeti ambayo ni nzuri na yenye kuonesha imani ya kuleta maendeleo na utendaji mzuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi zangu za pekee kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwa kuweza kujitoa mhanga katika kutekeleza kwa dhati Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala bila ya woga wala kujali maneno yanayojitekeza ila ni kujali kazi yake tu.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ifanye jitihada zake kwa nguvu zote kurudisha alama zote za barabarani ambazo kwa kweli Wizara ilijitahidi kuziweka lakini kwa bahati mbaya kwa kuwa wapo wengi ndani ya nchi yetu hawapendelei kuona maendeleo katika nchi hii huzing'oa kwa makusudi ili wafanikiwe yale ambayo yamo ndani ya mawazo yao lakini kwa kuwa Mheshimiwa Waziri uko tayari kuijenga nchi hii basi jitahidi uzirudishe alama hizo.

Mheshimiwa Spika, usajili wa magari ya Serikali ambayo mengi yake baadhi ya watu ambao ni wabadhilifu waliyateka nyara na kuyafanya yao kwa hiyo uamuzi huu wa kuweka usajili mpya wa magari ya aina yote umeweza kuziba ule mwanya ambao walikuwa wakiutumia kwa kufanya ubadhilifu ambao hivi sasa si rahisi kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, suala la makandarasi kwa kweli sasa wameelewa kuwa Wizara ya Ujenzi ni Wizara ambayo ina Waziri ambaye anaelewa kazi yake na kuwa ni mtu ambaye shughuli zake nyingi ziko katika utekelezaji zaidi kuliko kukaa Ofisini ambako huletewa taarifa tu za utendaji lakini kwa bahati nzuri Waziri yeye mwenyewe ndiye mtendaji na mfuatiliaji hata kuweza kuwafukuza wale ambao ni makandarasi wababaishaji. Mheshimiwa Waziri naomba kasi hii isiwe ya muda fulani bali iwe kazi ya siku zote.

Mheshimiwa Spika, baada ya haya machache, napenda kuungana na wenzangu kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR. MAUA A. DAFTARI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Pia nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuimarisha barabara.

Mheshimiwa Spika, naleta ombi langu kwako Mheshimiwa Waziri ili uweze kunisaidia *through IRRP* au sehemu nyingine ujenzi (ufadhili) wa barabara yangu ya Wete-Gando (Pemba). Naelewa suala la barabara si suala la muungano na ningepaswa ombi hilo kulifikisha katika Wizara husika SMZ. Kwa makusudi kabisa na kutokana na hali halisi ya uchumi wetu wa Zanzibar na hali ya barabara hiyo katika kanda hiyo kwa sababu ni sehemu yenye uzalishaji mwangi wa mazao ya kilimo, chakula na biashara, ni kero kubwa kwa wananchi wangu hasa wakati wa mvua. Ni katika uhusiano mwema kati ya Wizara yako, Wizara yangu na ile ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi SMZ ndio naleta ombi hilo, barabara hii haizidi 15km. SMT tumepata misaada mingi tu ya barabara. Hebu mwenzako nisaidie kwa hili dogo sijawahi kukuletea ombi lolote lile ila hili.

Mheshimiwa Spika, Wizara iangalie uwezekano wa kuiboresha barabara ya *Kesange Port - Sumbawanga Mjini* ili iweze kurahisisha usombaji/usafirishaji wa mizigo ndani na nje ya Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Spika, tuimarishe kwa kuweka watu waaminifu katika mizani zinazohamishika na zile ambazo ni fixed.

**MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba ya bajeti yenye takwimu za utekelezaji pamoja na mipango madhubuti. Aidha, pamoja na pongezi hizi, naomba kuainisha masuala yafuatayo:-

- (1) Mafanikio mahsusini yaliyopatikana kufuatia kuwepo muundo wa Wizara.
  - (a) Nakiri kazi nzuri inayofanywa na *TANROAD* na hasa katika Mkoa wa Mwanza kwa kuwa makini na kushirikisha wananchi tukiwemo sisi Waheshimiwa Wabunge

katika utekelezaji wa ujenzi wa barabara katika Mkoa wa Mwanza. Kazi zinazofanywa na makandarasi walio wengi ni zenyenye ubora na kiwango cha kuridhisha. Aidha, katika vikao vyetu vya *Road Board* mambo mengi yanayohusu barabara yamekuwa yakijadiliwa kwa upana na uwazi.

(b) Kuanzishwa kwa taasisi ndani ya Wizara kumesaidia sana kuboresha taaluma na kuchangia katika kuchochaea ubora wa kazi kama *CRB, ERB, A&SRB* na kadhalika. Hii ni changamoto kwa kuhalalisha *value for money*. Haya tu ni baadhi ya mafanikio machache kati ya mengi. Hata hivyo pamoja na haya, nashauri pia yafuatayo yazingatiwe kama siyo kutazamwa kwa umakini.

(i) Ukarabati wa barabara ya Nyanguge - Musoma, barabara hii haijafanyiwa *re-sealing* tangu itengenezwe licha ya kazi ndogo ndogo za kuziba mashimo inayoendelea kufanyika. Ni muhimu sana kipaumbele kitolewe ili kuhakikisha matengenezo haya yanafanyika kwa mwaka huu wa fedha na siyo tu kwa kuendelea kuziba viraka. Aidha, sambamba na ombi hili, barabara hii imekuwa chanzo kikubwa cha ajali, kuuwa watu, kuharibu mali za watu na kadhalika. Barabara hii haina:-

- *Road signs* za kuwasaidia watumiaji wa barabara hii.
- *Road Humps* hazipo sambamba na barabara za Kenya ambapo kila penye *concentration* ya watu kuna tahadhari hiyo.
- Hakuna tahadhari zinazoonyesha njia za mifugo, watoto wa shule (vivuko)
- Hakuna *provision* ya waendao kwa miguu na balskeli hivyo kusababisha msongamano wa watu katika barabara kuu.

Kwa taarifa tu, kumekuwa na ajali za kila mara na kuuwa watu na mifugo katika maeneo ya Kiloleli, Mwamanyili, Nassa, Nyashino, Nyamkoma, Kalemera na Lamadi (katika Wilaya ya Magu). Naiomba sana Wizara iweke kipaumbele kurekebisha kasoro hizo katika barabara hii. Mwaka jana pia nilisema kuhusu tatizo hili na kwamba hata zile *Road humps* zilizowekwa pale Nassa na Lamadi hazifai wala kukidhi mahitaji halisi.

(2) Uuzaji wa nyumba za Serikali, ni mpango mzuri na unalenga kuwasaidia watumishi wa Serikali. Ili uweze kufanikiwa vizuri, nashauri uanzishwe mfuko maalum na uwekewe sheria ili Serikali kila mwaka isaidie kutenga fedha zitakazotumika kujenga nyumba nyingi kwa ajili ya kuwasaidia watumishi wa Serikali/umma. Aidha, nashauri pia suala la *NHC* litazamwe upya ili sehemu kubwa ya nyumba hizo wapewe watumishi wa Serikali wapange badala ya wafanyabiashara amba wengi wao wana mapato makubwa ya kuwawezesha kujenga nyumba zao binafsi ukilinganisha na watumishi wa Serikali.

(3) *NBMM*, tofauti na zamani bodi hii chini ya usimamizi wa karibu wa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi imefanya kazi kubwa sana ikiwemo ya kuitangaza Bodi na kuchochaea taaluma ya ugavi hapa nchini. Zaidi ya watahiniwa 15,000 wamefanya mitihani na kufaulu, zaidi ya watahiniwa 1500 wameshasajiliwa na bodi kwa muda mfupi tu. Hivyo dhana ya ugavi isiangaliwe kwa jicho finyu bali ni totality pamoja na mafanikio. Bodi hii pamoja na mengine yote imeweza:-

- Kuboresha mitaala ya masomo kukidhi mahitaji ya soko;
- Kufanya kaguzi mahsusini kubaini wana taaluma na kuwasajili;
- Kuelimisha umma/waajiri juu ya sifa za kuwa na wana taalum  
katika fani ya ugavi;
- Kufuta kwa baadhi ya wasio na taaluma.

(4) Mwisho, napenda pia kushukuru sana kutengewa fedha kwa ajili ya barabara za Lamadi - Mkula - Sagiwi na Nyashimo - Ngasamo. Nashauri fedha zaidi zitengwe ili kuimarisha barabara hizi muhimu ziweze kupitika kwa muda wote.

**MHE. FAUSTINE K. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Kwa niaba ya wananchi wa Busanda, napenda kutoa shukrani zangu kwa kutenga pesa za kuwezesha kufufua barabara ya Geita - Nyarugusu - Bukoli na Chibingo hadi Bukondo. Kama zitafika zote kama zilivyotengwa barabara hizi zitafunguka. Ahsante sana. Pia napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuanza mikakati ya kuweka lami barabara kutoka Usagara- Geita - Kato hadi Kyamnyolwa. Naomba basi kufikia mwakani Januari kazi ya lami iwe imeanza.

Mheshimiwa Spika, tafadhali Mheshimiwa Waziri wananchi wa Kata za Bukondo, Nyachiluluma na Chigunga, wanaomba uwatembelee japo kwa saa moja. Wananchi wa Nyarugusu na Bukoli, nao wanaomba uwatembelee kwa saa moja. Tafadhali naomba ukubali na uniambie lini utakuja ili niungane na wananchi wa Jimbo langu. Naomba Mheshimiwa Waziri unipe jibu kwani haya ni maombi yao ya muda mrefu.

**MHE. SHAMSA S. MWANGUNGA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na watumishi wote wa Wizara kwa kazi kubwa ya matayarisho ya Bajeti. Bajeti hii ni nzuri sana kwani imefafanua vizuri malengo mbalimbali. Natoa shukrani kwa kuona mmezikumbuka barabara ndogo ndogo za kwenye miji ikiwemo barabara ya Mbande - Kongwa ambapo wakati wa mvua huwa ina usumbufu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na bajeti hii nzuri, ninapenda kutoa pendekezo ya kwamba Halmashauri zetu za Wilaya hazina uwezo kifedha pia kiutalam kushughulikia barabara za Wilayani mwao. Mfano Halmashauri za Wilaya za Mkoa wa Dar es Salaam hazina uwezo wa kujenga barabara nyingi mpya kutokana na wingi wa nyumba mpya zinazojengwa kila leo na Jiji kupanuka sana. Mfano ni barabara za maeneo ya Mbezi Beach, Kimara, Kigamboni na kadhalika. Ningependekeza Kitengo cha *TANROAD* kingepewa jukumu la kujenga barabara muhimu ya mitaa ya miji mikuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pendekezo la nafasi ya Wakurugenzi wa Bodi mbalimbali za Wizara yako, uwafikirie pia wanawake. Idadi ya wanawake iongezeke katika bodi zako. Kwa sasa tuna idadi nzuri tu ya wanawake ambao wana elimu ya ufundi wakiwemo Wahandisi wanawake katika fani mbalimbali. Hii ni kutoka taasisi mbalimbali, Bungeni na asasi zisizo za Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ucheleweshwaji wa kuanza ujenzi wa barabara mbalimbali mojawapo ni tenda za ujenzi zinachukua muda mrefu kufanyiwa uamuzi. Je, Wizara yako inachukua hatua gani au inatoa ushauri gani kwa Serikali Kuu (*Central Tender Board*) kwa ajili ya ukiritimba huu? Naunga mkono bajeti hii, ahsante.

**MHE. NJELU E.M. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, ninaanza kwa kumpongeza Waziri wa Ujenzi kwa kazi nzuri anayoifanya kuimarisha na kuboresha barabara za Tanzania. Ni matumaini yangu kwamba kama jitihada hizi zitaendelezwa, mawasiliano kwa njia ya barabara yatakuwa mazuri sana katika muda mfupi ujao. Aidha, naipongeza Wizara na Serikali kwa ujumla kwa kuiweka barabara ya Mbeya - Chunya - Makongolosi (125km) katika mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami. Barabara hii iliingizwa kwa mara ya kwanza kwenye mpango katika mwaka wa fedha 2001/2002 kwa lengo la kufanya *feasibility study*. Kazi hii ilifanyika na wananchi waliiona na walifurahi sana kwani wao ilikuwa ni dalili kwamba ukombozi wa adha ya barabara mbaya hasa wakati wa mvua ulikuwa unaelekea kufikia mwisho. Katika mwaka wa fedha 2002/2003 shilingi 300 milioni zilitengwa kwa ajili ya *design work*, wananchi ambao wanaulizia mara kwa mara, niliwaeleza kazi iliyokuwa inafanyika na kuwataka wawe na subira kwani programu ya kujenga barabara yao bado ipo. Wengi walitazamia mwaka huu wa fedha Serikali ingezungumzia kukamilika kwa *design work* na hatua za *tendering* zinakuwa kwenye bajeti. Lakini nilichokiona kwenye Bajeti ni fedha kidogo Sh.150 milioni kwa ajili ya *detailed design* ambayo nayo itafanyika kwa asilimia 60 tu ambayo ina maana katika Bajeti ya 2004/2005 ndipo itatengewa fedha za kukamilisha asilimia 40 ya *detailed design*.

Mheshimiwa Spika, kwanza ninashukuru kwamba mradi huu upo kwenye bajeti na hatua za mwanzo za utekelezaji lakini kwa kuzingatia matatizo ya barabara hiyo na kwamba wananchi wamevumilia kwa miaka yote hii, Wizara ingetenga fedha za kutosha kukamilisha *detailed design* katika mwaka huu wa fedha ili kwa mwaka wa fedha 2004/2005 tuone kuanza hatua za kujenga barabara yenyewe. Waziri iwasaidie maelezo na kwa kadri itakavyowezekana aone njia ya kukamilisha detailed design mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo ya awali, Serikali kupitia Wizara hii ilisema barabara ya Mbeya - Makongolosi kujengwa kwa lami ni hatua ya kwanza ya kujenga barabara yote ya Mbeya - Rungwa - Higi. Tunafurahia uamuzi huo wa Serikali lakini hatua hiyo inategemea kuanza kwa barabara ya Mbeya - Makongolosi ndiyo maana ninawasisitiza kuanza kujengwa sehemu hii. Barabara hii ni muhimu kiuchumi.

Serikali imetoa kipaumbele kwa Mikoa ya Kusini Nyanda za Juu kuzalisha mahindi kwa wingi ili kuliokoa Taifa na aibu ya nja. Sawa kabisa! Wakati huo huo Ukanda wa Ziwa unakuwa maarufu kwa migodi mikubwa ya dhahabu ambako kutakuwa na wafanyakazi wengi. Hawa watalishwa mahindi, kwa mujibu wa mkakati wa Serikali, toko Mikoa ya Nyanda za Juu. Barabara fupi kwa kutekeleza azma hiyo ni Mbeya - Rungwa - Higi. Natumaini Waziri atazingatia mtazamo huo wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kabla barabara yote haijajengwa kwa lami inahitaji matengenezo ya mara kwa mara, maeneo ya kutoka Makongolosi hadi Rungwa. Ni muda mrefu maeneo hayo hasa kutoka Kipembawe kwenda Rungwa hayajafanyiwa matengenezo na barabara ni mbaya. Naomba fedha itengwe kwa matengenezo ya kawaida na matengenezo maalum mara kwa mara ili barabara iweze kupitika vizuri wakati wote. Barabara hii ndiyo uhai wa wananchi wa Chunya kwani ndiyo inayowaunganisha na Mbeya, Tabora na Singida.

Mheshimiwa Spika, suala lingine, nimeona wanavunja barabara za lami eneo la Ruvu - Chalinze na Igowa - Mbeya na kuweka viraka. Sehemu wanazovunja ni nzima. Sina hakika kama viraka hivyo ni imara zaidi kuliko lami wanazovunja. Mimi si mtaalam lakini nina wasiwasi ubovu wa barabara utaanzia kwenye viraka hivyo. Nashauri kwanza zoezi hilo lisimame tuone viraka hivyo vitahimili hadi lini.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni usimamizi wakati Serikali inatenga fedha nyingi kutengeneza barabara mpya, usimamizi katika maeneo mengi ni dhaifu. Fedha nyingi inapotea kwa kazi mbovu, mifereji inakuwa juu barabara chini, vifusi havisambazwi vizuri na kuacha matuta matuta barabarani, viraka huwekwa kizembe na kufumuka baada ya muda mfupi. Tatizo la usimamizi likishughulikiwa vizuri, fedha nyingi zitaokolewa na barabara nyingi zitakuwa imara na bora.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na kukutakia mafanikio. Pia nashukuru matengenezo yaliyofanyiwa barabara ya Mbeya - Makongolosi baada ya kuharibika vibaya na mvua msimu uliopita. Meneja wa **TANROAD** Mkoa wa Mbeya anafanya kazi nzuri na akipewa uwezo zaidi na kifedha, nina imani atafanya vizuri zaidi.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, jitihada za Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na wataalam wake zimeonyesha matunda mema katika ujenzi wa barabara, hongera sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengi mazuri, yapo machache ambayo yanahitaji udhibiti.

(a) Ni kweli unawashirikisha Wabunge kuonyesha mgao wa fedha hizo lakini utaalamu wa kudhibiti matumizi na ubora wa barabara kulingana na barabara zilizolimwa bado una utata mkubwa kwa vile maelezo ya matumizi yanatolewa lakini panahitajika utaalam mkubwa wa kulinganisha matumizi na kilichofanyika Wabunge hawana utaalam huo. Naomba Wizara itafute utaratibu wa kufuatilia ukaguzi wa barabara zinazolimwa kwa fedha za Serikali.

(b) Katika Jimbo langu kuna barabara mbili za Mkoa ambazo zinakwenda kwenye maeneo ya uzalishaji wa mpunga, ufuta, ulezi, ufugaji na uvuvi wa samaki Rukwa na kadhalika lakini barabara hizo zimechakaa mno. Wakati wa mvua hakuna urahisi wa

wananchi kufika mjini kutafuta mahitaji yao ya lazima. Tatizo hili ni la muda mrefu sana Mheshimiwa Waziri naomba sana fikiria barabara ya:-

- (i) Igamba - Ivuna- Kamsamba, hata kama ni kwa kuifanyia grading tu tutashukuru.
- (ii) Igamba - Msangano eneo la km. 25 hivi linahitaji kujaza na kusambaza (changarawe) eneo hilo lina utelezi mwingu kiasi kwamba huwezi kusafiri kupita kwa urahisi wakati wa mvua.
- (c) Wizara isimamie kwa karibu sana Mkandarasi wa *Songwe - Tunduma Road* mara nyingi fedha za *Road Toll Fund* zinataja na kutengeneza barabara nyingine tu Mkoa wa Mbeya tena nyingine kwa kurudiwa rudiwa bila kutaja/kutengeneza barabara hizo mbili Jimboni mwangu.

Mheshimiwa Spika, naomba sana barabara ya Igamba - Kamsamba (L. Rukwa) itengenezwe kwa kiwango cha changarawe maeneo korofu na grading maeneo ya kawaida pia *Musangano Road*. Naunga mkono hoja hii, nakupongeza kwa kazi nzuri sana.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, naitakia heri Bajeti ya Mheshimiwa Waziri. Pia napongeza juhudhi zake mwaka jana nilimwombu anisaidie barabara yangu katika Jimbo langu la Mfenesini Zanzibar, tuliishia hivyo hivyo hebu nisaidie pamoja na kwamba nafahamu kuwa siyo ya Muungano.

**MHE. GEORGE L. LUBELEJE:** Mheshimiwa Waziri, pole kwa kazi, habari za siku nyingi, Mpwapwa wote hawajambo wanaendelea kuvuna karanga. Karibu sana Dodoma. Wewe ulikwishapewa kibali cha kuwa mkazi wa Mkoa wa Dodoma mbona unatusahau ndugu zako.

Basi tutaonana baadaye kwa mazungumzo. Hali ya barabara Wilayani Mpwapwa siyo mbaya sana hata Kibalewe Rudi zinatengenzwa bado Mpwapwa - Mlali.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na watendaji wake wa Wizara hiyo. Kazi inayofanywa na Wizara hiyo ni kubwa na inaonekana kwa kila mtu hasa Mkoani Kagera. Ni haki nimpongeze Meneja wa **TANROAD** Mkoa wa Kagera kwa jitihada zake za kutunza barabara za Mkoa wa Kagera. Nampongeza pia Mheshimiwa Waziri kwa uamuzi wa kuanza kuijenga barabara ya Usagara-Bwanga-Chato-Kyamyorwa. Barabara hii ni muhimu sana kwa vile inapita katika maeneo ya uzalishaji wa mpunga, mahindi na zao la biashara la pamba. Aidha, ni njia ya mkato kwa wanaosafiri kutoka Mwanza hadi Bukoba hadi Mwanza. Mkataba wa hatua za awali kujenga barabara hii ilitiwa saini wiki iliyopita. Tuliokuwepo tulishuhudia na tulifurahia sana. Naomba Waziri atakapofanya majumuisho afafanue namna kipande cha barabara ya Bwanga-Biharamulo

kitashughulikiwa maana hata katika majedwali sikuona, lakini wakati huo huo yapo maelezo kuhusu barabara ya Mtukula-Muhutwe-Kagoma-Muleba-Biharamulo-Rusahunga yanaonekana hivyo, hicho kipande cha barabara ya Bwanga hadi Biharamulo kinashughulikiwa pipi?

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu barabara ya Karagwe-Amugakorongo-Rwabaizi-Bugara-Businde-Bugomora-Murongo. Barabara inaambaa mpaka wa nchi yetu na nchi ya Uganda hivyo kwa kweli ingestahili kuwa barabara ya ulinzi. Licha ya hayo, maeneo yote ya barabara hii ni ya wazalishaji wa mahindi, maharage, ndizi na kahawa kwa wingi sana. Mara nyingi kutokana na uwezo mdogo wa Halmashauri barabara hii huwa haitengenezwi kwa kiwango cha kupitika kipindi chote cha mwaka. Kutokana na ubovu wa barabara hii mazao mengi hutoroshwa na kuuzwa nchi jirani kupitia njia za panya. Namwomba Mheshimiwa Waziri afikirie kuichukua barabara hii ili iwe ya Mkoa.

Nazidi kumtakia heri Waziri na timu yake katika utekelezaji wa mpango na bajeti yake aliyowasilisha. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, tulipokuwa kwenye Kamati ya Miundombinu Waziri alisema kuwa barabara ya Mkoa ya Mpwapwa-Gulwe ambayo pia matengenezo yake hufika hadi Kibakwe imo kwenye Bajeti ya mwaka 2003/2004. Lakini nimejitahidi kuitafuta kwenye kitabu cha hotuba lakini sijaiona. Naomba nifahamishwe kwa maandishi wakati wowote kuanzia leo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote wa Wizara hii ya Ujenzi kwa kuwa wazi kwa uendeshaji wa Wizara hii mpaka imefikia kiwango cha utawala bora tunaohubiri kila siku. Naomba nimpongeze pia Naibu Waziri ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini. Yeye binafsi tulimtolea shida ya Wahandisi Wilayani, tunashukuru tumepesta Mhandisi mmoja Bwana Butoto. Dalili inaonyesha kuwa Mhandisi huyu ataisaidia Morogoro.

Mheshimiwa Spika, naomba tushirikiane kwa karibu ili barabara zetu hasa za Kanda za milimani na tambarare ziwe nzuri. Barabara ya Kiswira-Kibungo Juu-Kolelo-Tegetero-Mgozo-Hewe-Lubwe-Tawa-Kinole, naomba ziada rasmi kama ya Ng'aro iongezwe kufikia hadi Kibungo Msituni ije hadi Pangawe.

Barabara za Kongwa-Tununguo-Kiganila hizi ni barabara ambazo baadhi zipo kwa jirani yangu Mheshimiwa Naibu Waziri zilisaulika sana muda mrefu. Naomba sana barabara hizi zikumbukwe. Najua yeye mwenyewe hawezu kusimama na kuomba hapa Bungeni kwani si rahisi. Hivyo mimi natumia nafasi hii kuomba matengenezo ya barabara za Jimbo langu. Barabara hizo ni:-

Kidunda-Ngerengere-Usagara, Msomvizi-Kungwe-Lubungo, Madamu-Kinole-Tegetero-Hewe na Kidugalo-Mdaula-Bwabwa.

Mheshimiwa Spika, barabara za Jimbo la Jirani yangu Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, ni kama ifuatavyo:-

Kiswira-Tawa; Kifiudike -Kibungo Juu; Kongwa-Kilengezi; Nige hadi Ngong'olo. Ingawa barabara hizi zipo chini ya Halmashauri lakini Morogoro Vijijini haina kitu. Naomba ujenzi itusaidie katika barabara hizi tu, nne za Jimbo la Kusini na barabara nne za Jimbo la Kusini Mashariki, naomba kwenye migawo ya fedha mtukomboe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mgawo wa fedha, kifungu kidogo 280561 imepanda toka 50,265,195 mwaka 2001/2002 hadi 526,699,000 mwaka 2003/2004, mara tatu ukilinganisha na maeneo mengine, kiasi hicho ni kikubwa. Zipo idara nydingi muhimu na nyeti katika kitengo cha ugavi *Government Stores, E&M* na kadhalika. Mgawo wao ni mdogo, naomba maelezo kuhusu tofauti hii kubwa.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Old Dar es Salaam. Zamani za kale kabla mimi, wewe Mheshimiwa Waziri na Naibu wako hatujazaliwa barabara hii ya kutoka Morogoro kwenda Dar es Salaam ilipitia Morogoro-Mikese-Ngerengere-Matuli-Kwaba-Ng'ese-Usungura-Mzumbwi-Kisarawe-Pugu-Dar es Salaam. Barabara hii inapitika toka Dar es Salaam hadi Mtoni. Haipitiki toka Mtoni Ruvu-Usungura na Kwaba na kutoka Kwaba hadi Morogoro haipitiki, tunaomba atume wataalam waje.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vivuko vidogo vidogo. Kero kubwa kwa wananchi wa Tununguo-Kidunda hawana vivuko. Hutumia ngalawa za kienyeji. Naomba za kisasa ili zisaidie wananchi hawa. Tutachangia kidogo kama asilimia tano ya bei ya chombo hicho.

**MHE. HERBET J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Naibu wake na watendaji wake wote kwa kuwasilisha hotuba nzuri na mipango mizuri ya Wizara ya Ujenzi hasa kwa mwelekeo wa maendeleo ya barabara kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutoa ushauri na pia kupata maelezo katika maeneo yafuatayo:-

Moja, barabara za Jumuiya ya *EAC-Tanga-Horohoro*, kwa kuwa barabara hii ipo katika mpango wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwa kuwa kazi ya ujenzi wa madaraja bado inaendelea nje ya mpango wa Jumuiya ni vema Wizara ya Ujenzi ikatuthibitishia kwamba kazi hiyo nzuri ya madaraja itaendelea bila kuathiriwa na upatikanaji wa fedha chini ya mpango wa Jumuiya ya *EAC*.

Pili, Wizara ionyeshe ina mpango gani wa tahadhari wa kuendelea na ujenzi wa barabara hiyo katika mpango wa Taifa uliokuwepo iwapo kutakuwa na ucheleweshaji mkubwa wa upatikanaji wa fedha katika mpango wa Jumuiya ya *EAC*.

Mheshimiwa Spika, hali mbaya ya barabara ya Mkoa ya Muheza-Amani yenyeye urefu wa kilomita 1.5 Muheza Mjini. Wilaya ya Muheza haina hata barabara moja ya

Mkoa yenyé lami. Eneo la barabara ya Mkoa hadi Muheza-Amani iliyokuwa na lami zamani lipo katika hali mbaya kiasi kwamba linafanana na mifugo iliyopata ugonjwa wa upele na kuharibika manyoya yake na ngozi. Barua ya Katibu Tawala Mkoa wa Tanga Kumb. Na. R4D/17/VOL III/26 ya tarehe 17 Januari, 2003 ambayo pia Mheshimiwa Waziri anakiri kuipata na kujibu barua hiyo kwa barua yake Kumb. Na. BC 341/476/01/43 ya tarehe 16 Mei, 2003 zinaonyesha kwamba jitihada zingefanywa kutengeneza kwa kiwango cha lami eneo la kilomita 1.5 la barabara hiyo ya Mkoa hadi Muheza Mjini na kwamba barua ya Katibu Tawala Mkoa inakiri kwamba sehemu hiyo ya barabara imeombewa fedha za kuwekewa lami kwa kutumia teknolojia mpya (*Otta Seals*) katika Bajeti ya mwaka ujao wa fedha wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nina uhakika Wizara ya Ujenzi ina nia ya kutekeleza vizuri mipango yake ni vema wananchi wa Muheza wakajua mpango wa utekelezaji wa mpango huo wa eneo la barabara Muheza Mjini katika Bajeti hii ya mwaka huu wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, uwiano wa mipango ya maendeleo ya barabara ya Mkoa wa Tanga. Pamoja na ukweli kwamba Bodi ya Barabara ya Mkoa ndiyo chombo cha maandalizi ya mpango wa maendeleo ya ujenzi wa barabara ya Mkoa bado ipo haja kwa Wizara husika kuona kwamba upo uwiano wa mpango wa Mkoa kwa Wilaya zake. Mpango wa maendeleo wa barabara za Mkoa wa Tanga umeelekea kwa kiasi kikubwa katika barabara za Wilaya ya Lushoto kuliko Wilaya zote zilizobaki yaani Muheza, Handeni, Tanga, Korogwe na Pangani. Utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya wananchi bila kuwa na uwiano unaleta madhara makubwa ya kugawa maeneo kimaendeleo kati ya bora na duni.

Historia inaonyesha Wilaya ya Lushoto kuwa na barabara nyingi za Mkoa kuliko Wilaya zingine. Hata hivyo lazima tugawe fedha hasa za mipango ya maendeleo kwa uwiano ili wale walio duni wapate nafasi ya kuanza kuboreka. Naomba kurudia kwamba Wilaya ya Muheza haina barabara hata moja ya Mkoa yenyé lami na bado hakuna tamko lolote la kuonyesha hatua zilizofikiwa kuweka lami barabara ya Muheza hadi Amani, sehemu ambayo inasaidia sana katika kutoa mchango wa fedha za kigeni kwa mazao yao ya chai na utalii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote niliyochangia bado moja naamini na kuipongeza Wizara ya Ujenzi kwa kazi nzuri iliyofanya katika sekta ya ujenzi (barabara).

Pia Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba hii ya Wizara ya Ujenzi kwa bajeti ya mwaka 2003/2004.

**MHE. ANTHONY M. DIALLO:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni Hongera kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, kwa Bajeti safi.

Mheshimiwa Spika, napendekeza ujenzi wa barabara uzingatie mambo yafuatayo:-

Kwanza, kila umbali wa kilomita hamsini kuwekwe *rest parking* na kuwepo choo cha wanaume na wanawake. Pia kuwekwe *a small shop house* ambapo unaweza kununua maji, mswaki, mkate na kadhalika. Pia upande mmoja wa jengo hilo kuwe na *Cafe* au mgahawa mdogo na pia *bench* la kukalia kama wawili hivi. Majengo hayo na vyoo vikabidhiwe kwa Serikali ya Kijiji au mwanakijiji mmoja kwa masharti ya matumizi yake na uendelevu wa kuwepo matunzo yake.

Pili, barabara kuu zote zipite nje ya Miji na kuzilazimisha Halmashauri kuhakikisha kutoruhusu wananchi kujenga au kuhamia karibu na barabara kuu lakini waweke lami barabara inayoingia Mijini na kutoka. Mfano wa Tarime uwe ndiyo *model* ya maeneo yote ya barabara zinakojengwa hapa nchini. Utaratibu huu utaondoa hali ya kuweka *special bumps* kwenye *highway* zetu. Masharti haya pia yatekelezwe na Halmashauri sehemu za Vijijini. Kwa maeneo ambako haya yameshatokea, basi Wizara ya Ujenzi na TAMISEMI washirikiane kuondoa hali hii na kuzuia isiendelee. Hali ya watu kujenga karibu na barabara ni gharama kubwa hapo baadaye baada ya *environmentalists* watashinikiza barabara zinazopita Mijini ziwekewe *sound barrier* kuzuia *sound* au *noise pollution* kama ilivyotokea huko Ulaya na America katika miaka ya 70 na 80.

Tatu, Wizara iweke taa za barabarani kwenye barabara zinazojengwa na Wizara na *EU* Mjini Mwanza. Barabara za Mjini, *Airport roads* na maeneo ya Igoma, Nyakato na Mabatini kwenye barabara ya Mwanza-Nyaguge na kupitia *Mwanza South*, Butimba, Nyegezi na *Mkolani Area*. Siyo kazi ndogo kufanywa na Halmashauri ya Jiji kwa vile inahitaji kuweka nyaya za *tracking system*. Sehemu nyingine inahitaji kuvunja barabara ili kupitisha nyaya na kadhalika. Wizara imesaidia Jiji la Dar es Salaam kwa vyote hivi, *why not Mwanza? Please avoid double standards.*

Mheshimiwa spika, nne, ili kuokoa barabara mpya za Mwanza kutoharibiwa na magari makubwa, inabidi Wizara isaidie kujenga *inner* na *outer ring roads* kuzunguka Mji wa Mwanza kutoka *Airport Road* kupitia Pasiansi, Nyakato hadi Mkuyuni (*Mwanza South*). Nyingine kutoka Igombe-Buswelu-Igoma-Buhongwa (*Shinyanga Road*). Hii itapunguza *traffic* kuingia Mjini kati na kuanzisha *satellite towns development away from the city centre*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri mara nyingi fedha za barabara zinazokuja Rukwa nyingine hutolewa maelekezo ya barabara ipi itengenezwe. Mara zote tatu tangu mwaka 1995 barabara hutajwa za Sumbawanga na Mpanda tu. Je, ina maana Nkansi kama Wilaya haina barabara za Mkoa? kupitia mchango huu ninaomba ombi maalum la mara kwa mara maelekezo ya fedha zielekezwu barabara ya Mkoa inayounganisha barabara kuu (*track road*) na Makao Makuu ya Wilaya ya Namanyere yaani barabara ya Chala-Namanyere-Mpalamawe yenyе urefu wa kilomita 57 tu.

Mheshimiwa Spika, pia naomba barabara ya Nkundi-Kate na Chala-Namanyere-Kirando na ya mwisho ni ile ya Lyazumbi-Kabwe ili ku-link na Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani nyingi kwa Wizara ya Ujenzi kwa jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali kwa kuondoa kero ya muda mrefu ya wananchi wa Mikoa ya Kusini. Ujenzi wa daraja la Mto Rufiji, Matandu na Mbwemkulu na utiaji saini Mikataba ya ujenzi ya Somanga -Masaninga, Nangurukulu-Mbwemkuru-Lindi-Mingoyo ni ushahidi wa jinsi Serikali ilivyothamini kuondoa kabisa tatizo la barabara ya Kibiti-Lindi-Mingoyo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nimshukuru *Engineer Kijazi* - Katibu Mkuu na *Engineer Partric Mfugale* kwa umakini wao katika kufuatilia mradi wa Kibiti-Lindi. Nawashukuru na kuwapongeza. Napenda kuiomba Serikali ijitahidi kutafuta uwezo na kukamilisha ujenzi wa barabara katika sehemu iliyobakia ya Nyamwage-Somanga.

Mheshimiwa Spika, ningependa vile vile kugusia suala muhimu ambalo nimetumwa na wapiga kura wangu kuhusu uhamishaji mitambo ya ujenzi kutoka Lindi kwenda Mtwara. Tunaomba mpango huo usitishwe kwani utakuwa kero kubwa kwa Wakandarasi wadogo waliopo Lindi. Kama ni lazima vifaa hivyo viwekwe sehemu moja ni vema basi kituo kiwe Lindi Mjini ambako ni kati kati kwa Wilaya zote za Mikoa ya Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, ningependa kumalizia kwa kutoa pongezi kwa watumishi wa *TANROAD* Mkoani Lindi wakiongozwa na *Engineer Nyamuhanga* kwa kazi zao nzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. LEPHY B. GEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwa kuwa tulikuwa na kilio kikubwa sana cha barabara yetu ya kutoka Mpanda hadi Koga. Hivyo nichukue nafasi hii kutoa shukrani hizo kwa kutenga fedha za ndani na za nje kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha moramu na kalveti. Ingawa tunahitaji lami nasema ahsante sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, hii inatupa matumaini makubwa na kwa barabara nyingine zilizobaki.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, kazi inayofanywa na Serikali kuiunganisha Tanzania kwa barabara inastahili pongezi kubwa. Wote tunajua jinsi nchi ilivyokuwa na matatizo ya mawasiliano ya barabara na jinsi Rais

Benjamin Mkapa , alivyoyavalia njuga na kuyatatua. Kwa niaba ya Wanamwanga wote nampongeza yeze binafsi na Serikali yake kwa hatua hizi nzuri sana.

Hivyo Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Waziri wa Ujenzi na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Katibu Mkuu Engineer Kijazi na wataalam wote walioitayarisha bajeti hii kwa kazi nzuri waliyoifanya, hongera sana.

Mheshimiwa Spika, ninayo maomba mawili. Kwanza, katika mwaka 2001 nilimwandikia Waziri wa Ujenzi nikimwomba aangalie upya barabara chache Wilayani Mwanga na azipandishe daraja ili zitengenezwe na Mkoa. Katika majibu yake Mheshimiwa Waziri alinijibu kuwa wakati ule Serikali ilikuwa itathmini na kuziangalia upya barabara zote nchini na kuwa mpaka ifikapo Desemba 2002 atanipatia majibu. Katika jibu hilo alinipatia pia ni vigezo ambavyo vitatumika katika kuipandisha daraja barabara ili iwe ya Mkoa na utengenezaji wake ufanywe na *TANROADS*. Barabara zangu mbili hapo chini, hii ya kwanza na ya tatu zina hivi vigezo vyote.

Mheshimiwa Spika, barabara nilizoziombea kupanda daraja kutoka barabara za Wilaya kuwa barabara za Mkoa ni:-

- \* Kikweni mpaka Usangi, Lomwe kilomita 15. Barabara hii inaunganisha Tarafa nne za Wilaya ya Mwanga na Tarafa ya Usangi ilipo Hospitali ya Wilaya.
- \* Lembeni mpaka Kolomeni yenze urefu wa kilomita 10.
- \* Kisangara hadi Ngujini-Vuchama-Ndambwe mpaka Shighatini.
- \* Mwaniko mpaka Vuchama-Ngofi yenze urefu wa kilomita sita.
- \* Kifula mpaka Masumbeni-Butu.
- \* Mwanga mpaka Kagongo.

Mheshimiwa Spika, naomba nielezwe ni barabara zipi au ipi ambayo tathmini ya Wilaya imeipandisha daraja. Ningependa kueleza kuwa Mwanga ndiyo moja ya Wiaya ambazo zina barabara chache sana zinazoshughulikiwa na *TANROADS* (jumla ya kilomita 121 tu).

Mheshimiwa Spika, pili, Wilaya yangu iliomba daraja mbili za *Beiley* (*2 Beiley Bridges*) ili tuweze kukamilisha barabara ya *Mwanga By-pass*. Wizara ya Ujenzi ilituahidi kuwa mara madaraja hayo yatakapong'olewa kwenye barabara zinazotengenezwa upya, tutapewa daraja hizo. Kwa kuwa muda unakwenda tunapenda kuchukua fursa hii kuiomba Wizara ifanye juhudhi zote itusaidie ili tuweze kukamilisha barabara ya *Mwanga By-pass*.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru tena wote katika Wizara hii na kuunga mkono hoja ya Waziri wa Ujenzi. Ahsante sana.

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Katibu Mkuu Bwana Kijazi na wataalam wenu. Hakika mmezibadilisha sura za barabara kuu za nchi hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo napenda kushauri yafuatayo:-

Kwanza, ugawaji wa fedha za Mfuko wa Barabara kwa ajili ya barabara za Vijijini naona kasi imepungua. Kwa kuwa makusanyo ya kodi yameongezeka sana na Tanzania inaendelea kusamehewa madeni ya Kimataifa ni mategemeo ya wananchi kuwa viwango nya gawio la Mfuko wa Barabara vingeongezeka na utoaji wa mara kwa mara pia ungeongezeka, lakini hivyo sivyo ilivyo. Hali ya mgawo kwa barabara za Kitaifa na Kimko na tofauti kwani bado ni nzuri.

Mheshimiwa Spika, pili, matengenezo ya barabara za Mikoa hasa za Mkoa wa Pwani si mazuri kwani barabara hizo huwa zinachongwa badala ya kuzibwa mashimo. Hivyo kuzifanya barabara kuwa njia rahisi ya maji yaani mifereji. Ingawa kweli matengenezo yanafanywa mara kwa mara, matengenezo ya kuchonga hayasaidii kuzifanya barabara hizo zipitike kwa vipindi virefu kabla ya kurudia matengenezo. Hivyo Serikali inatumia fedha nyingi kwa matengenezo ya mara kwa mara badala ya matengenezo ya kudumu.

Mheshimiwa Spika, tatu, ujenzi wa barabara kwa changarawe. Ingawa barabara za changarawe ni bora zaidi kuliko zile za mchanga na matope, barabara hizo zinakuwa kero zaidi kuliko barabara za kawaida.

Kwa hiyo, Serikali inapoteza fedha nyingi kwa barabara zisizodumu hasa nyakati za mvua ambapo changarawe huwa zinasombwa na maji na kuacha mashimo. Barabara za Pugu-Msanga na Mkuranga-Kisiju ni mifano mizuri. Kwa hiyo namshauri Mheshimiwa Waziri aanze kufikiria ujenzi wa barabara kwa lami ingawa kwa masafa mafupi kila mwaka badala ya changarawe.

Mheshimiwa Spika, nne, makandarasi wasio na uwezo na usimamizi haffifu wa *TANROADS*. Kwa bahati tatizo la ufanisi duni wa baadhi ya Makandarasi Mheshimiwa Waziri analitambua na amelieleza katika Ibara ya 39 kama moja ya matatizo. Mfano upo pale katika barabara ya Pugu-Kisarawe, kandarasi ameshindwa. Inafaa makandarasi kama hawa wasimamishwe. Hali hii pia inamaanisha kushindwa kwa *TANROADS* kusimamia shughuli hizi za ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kutenga shilingi 450 milioni kwa barabara ya Kiluvya-Kisarawe. Lakini sielewi kwa nini barabara ya Pugu-Kisarawe umeitengea shilingi 250 milioni tu na za kujengea kilomita moja na nusu. Barabara yenye urefu wa kilomita sita sasa imepangiwa jumla ya shilingi 890 milioni tu, fedha ambayo kwa jumla haitoshi hata kumaliza nusu ya barabara. Hii

inaashiria kuwa Serikali haiko serious na ujenzi wa barabara hiyo. Nataka nipate maelezo ni jinsi gani barabara hiyo itamalizwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote niliyosema naiunga mkono hoja hii. Nakushukuru.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara kwa hotuba yenye mipango mizuri ya matengenezo ya barabara nchi nzima. Pia nashukuru sana kwa kuamua kufanya matengenezo ya majaribio ya *Otta Seal* kilomita nne katika barabara kuu ya Mji wa Mbanga kwa gharama ya shilingi 365 milioni. Hivyo mimi naiunga mkono hotuba hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ikamilishe matengenezo ya barabara zifuatazo kama ni njia ya kukamilisha ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyowaahidi wananchi wakati wa ziara yake Wilaya ya Mbanga mwaka 1998.

Kwanza, barabara ya ni Chiwindi, *Mbamba Bay*, Liuli, Ngumbo hadi Lituhi. Barabara hii Wizara imeanza kutengeneza sehemu kama kutoka *Mbamba Bay* hadi Ngindo kilomita 12 na Ngido, Liuli, Ngumbo hadi Lituhi bado kwa sehemu kubwa haipitiki wakati wote. Vile vile kipande kutoka Nangombo hadi Ng'ombo imetengenezwa na Ng'ombo hadi Chiwindi bado haipitiki wakati wote.

Pili, barabara ya Mbaha hadi Kigonsera inapitika kwa tabu sana. Kutoka Kigonsera hadi Kilindi na kutoka Kilindi hadi Mbaha haipitiki kabisa wakati wote.

Tatu, barabara ya Lituhi hadi Kitai. Tunashukuru tuta limekamilika lakini kati ya madaraja kumi na nane ni sita tu ndiyo yametengenezwa na mengine yote yanapitika kwa tabu.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali ikamilishe matengenezo ya barabara hizi ndani ya kipindi hiki cha Mheshimiwa Rais wa awamu ya tatu ili kulinda ahadi na kauli nzito aliyoitao kwa wananchi. Barabara hizi zipo katika mradi wa *RUSIRM* lakini mambo yanakwenda polepole sana.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002, Wizara ilitumia fedha nyingi sana kutengeneza barabara ya Mkili hadi Litemba. Barabara hii haitumiki kikamilifu kutokana na kona mbili kali sana na marekebisho mengine madogo madogo. Ingefaa sana Wizara ikafanya marekebisho kwa barabara hii ili iweze kutumika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Songea hadi Mbanga inatengenezwa chini ya mradi wa *RUSIRM*. Lakini sehemu ya barabara ya Mbanga hadi *Mbamba Bay* ilitegemewa itengenezwe na fedha za mkopo kutoka *ADB*. Lakini nimechunguza hotuba ya Mheshimiwa Waziri hakuna mahali popote panapoelezea juu ya sehemu hii ya barabara. Naomba sana kufahamu hali ikoje?

Mheshimiwa Spika, kivuko cha Mto Ruhuhu kinafanya kazi kwa njia ngumu sana kwa kutumia nguvu za watu. Hivyo wakati wa masika na ndipo kinapohitajika sana hakifanyi kazi. Mbaya zaidi waya hupita chini ya maji na huwezi kufahamu usalama wake. Naomba Mheshimiwa Waziri abadilishe njia hii ya kutumia hili pantoni.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maoni yangu kuhusu hali ya utekelezaji wa ugavi wa fedha kwa Wizara ya Ujenzi kwa barabara za Jimboni mwangu kama ifuatavyo:-

Kwanza, mwaka mzima wa 2001/02 sikuwahi kuhudhuria kikao cha Bodi ya Barabara Mkoa wa Mbeya kwa sababu Bodi hiyo iliitishwa wakati Wabunge tukiwa Bungeni. Tabia hii inaonekana kwamba watekelezaji wa barabara wasipate hoja na msukumo wa ukamilikaji wa kazi zilizopangwa huko nyuma.

Pili, barabara ya Mkoa za Ruanda, Iyula hadi Nyimbili, Isansa, Magamba hadi Iporoto (Itaka) bado hazijakamilika. Nilikwishamwona Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi akaniambia nimwambie Meneja wa *TANROAD* aandae profile ili zitengewe fedha katika bajeti ya mwaka huu. Alipokuja Mheshimiwa Naibu Waziri, Meneja alikiri mbele yake kuwa amekwishaandaa tayari. Katika majedwali yote yaliyomo kwenye kitabu cha bajeti wala maelezo yako barabara hizi hazipo. Naomba Meneja *TANROAD* Mbeya anieleze tatizo ni nini kuitia kwako. Aidha, naomba kupata maelezo kwa nini vikao vya Bodi ya Barabara havijali uwakilishi wa Wabunge.

Tatu, katika vikao vya Bodi ya Barabara Mbeya malipo ya sitting allowance ya shilingi 10,000/= ni ndogo mno kwani inawapa gharama kubwa Wabunge na viongozi wengine wa Wilaya, kwani kiasi hicho hakiwezeshi dereva apate posho wala mafuta ya gari za Wabunge. Tunaomba maelezo ili suala hili lisizidishe kutolewana.

Nne, napenda niwapongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa ufuatiliaji wa ujenzi wa barabara za Songwe-Tunduma. Utendaji kazi wa Kampuni ya China ulikuwa mdogo sana. Umejitokeza wizi mkubwa wa dizeli ambao unaweza kuwa pingamizi ya mafanikio ya kazi nzuri. Nimewahi kufanya mazungumzo na wafanyakazi walikiri kabisa na kwamba hata Wachina wanahuksika. Kinachofanyika ni kuwanunulia konyagi Wachina ambao wakinywa wanalewa na kuwapa mwanya wanyonya mafuta waibe bila kizuizi. Naomba kama wapo wawakilishi wa Serikali waweze kufuutilia hili, vinginevyo kazi haitakamilika kutokana na hasara hiyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda niwapongeze Wizara nzima kwa namna mnavyopambana na ulaji rushwa katika zabuni na udhibiti kwa magari makubwa kuzidisha mizigo na kuharibu barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mchango wangu kwa maandishi kwenye Wizara ya Ujenzi kuhusiana na bajeti ya Mheshimiwa Waziri ya mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo nimeielewa. Pia nimpongeze Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Makamishna na watendaji wote kwenye Wizara ya Ujenzi kutoptana na hotuba hiyo ambayo wao wameshiriki kikamilifu kuiandaa. Naomba niwatakie kheri kwenye mipango yao hii ili waitekeleze kwa ukamilifu katika kipindi hiki cha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, kwa moyo wa wazi kabisa naomba nitambue mambo yafuatayo ambayo yametekelezwa na Wizara ya Ujenzi:-

Kwanza, kubaini tatizo ambalo lilikuwa linakua kwa kasi kubwa na kulichukulia hatua polepole za kulipatia ufumbuzi. Nalo ni tabia ya watendaji ya kutokuwa waaminifu juu ya magari ya Serikali ambayo yalikuwa na namba za kiraia kujaribu kuyafanya mali zao kwani magari haya yamekuja kwenye miradi ya Serikali kuititia wahisani mbalimbali. Juhudi iliyofanywa na Wizara ya Ujenzi ya kufuatalia magari hayo na kuhakikisha kwamba yanarudi Serikalini salama inahitaji pongezi nyingi. Naomba tu juhudhi hii iendelee maana haya magari hayajarudi yote.

Pili, hali ya Jiji la Mwanza kwa barabara bado si nzuri. Mradi wa ujenzi wa sehemu ya barabara hizo ambao unafadhiliwa na Umoja wa Nchi za Ulaya (*EU - Countries*) utakamilisha kiasi cha kilomita 54 za kiwango cha lami. Wizara ya Ujenzi imesimama kidete kuona kwamba barabara hizi zinajengwa na kukamilika. Wizara imeweza kudhibiti ujenzi wa barabara hizo *M/S ASTALD ASP* kutoptana na ukorofi alioanza nao juu ya ujenzi wa barabara hizo. Juhudi hii ya kusimamia ujenzi huu kwa karibu imenitia moyo kwamba kazi hii itakamilika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya ya awali, sasa naomba nitoe maoni yangu kwenye bajeti ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Maswa kuititia Lalago-Mhunze na kutokea Kolandoto na kuelekea Shinyanga Mjini ni barabara ya siku nyingi na muhimu sana kimaendeleo kwenye eneo hilo. Kwa hiyo, naiomba Wizara ya ujenzi iitupie macho ili iweze kuimarishwa na kwa ubora wa kutosha. Kama nitaruhusiwa naomba niseme kwamba barabara inayotoka kwenye Mji wa Igunga na kupita ndani kwa ndani hadi kuja kuungana na hiyo itokayo Maswa na kutokea Kolandoto hadi Mji wa Shinyanga nayo ifanyiwe matengenezo ya kutosha. Barabara hii inafupisha sana umbali kwa waendao Shinyanga na Mwanza kutokea Igunga.

Kuna wasafiri wengi wanapenda kutumia kivuko cha Kamanga-Mwanza wakienda Sengerema, Geita, Biharamulo na Kagera-Bukoba. Tatizo la barabara hii ni kutoka Kamanga kwenda Sengerema. Wizara ya Ujenzi kwa nafasi yake naomba ilichukue jambo la kuboresha barabara hii kama jambo la maendeleo kwa wakazi wa eneo hili na kuifanyia matengenezo yanayolingana na matumizi ya barabara hiyo.

Baada ya mambo haya naomba niitakie Wizara ya Ujenzi mafanikio na kwa nafasi hiyo hiyo naomba kuunga mkono hoja hii.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa John Pombe Magufuli na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Hamza Mwenegoha pamoja na Katibu Mkuu Ndugu Kijazi na wataalam wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya katika kuendeleza Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kukiri kwamba Wizara hii inaleta mapinduzi makubwa katika kuibua uchumi wa nchi yetu. Katika hali ya miaka ya nyuma miaka ya 70 na 80 hali ya barabara zetu ilikuwa mbaya sana. Lakini cha kufurahisha leo hii karibu nchi nzima barabara zinajengwa, lazima tukubali kusifia pale inapostahili. Mimi naamini nchi hii baada ya miaka mitano hali ya mawasiliano ya barabara itakuwa nzuri sana. Naomba sana kuipongeza Wizara kwa kujali kilio cha wananchi wa Korogwe kwa kukubali kuondoa tatizo sugu la barabara ya kutoka *New Korogwe-Old Korogwe-Mashewa* hadi Mtoni Bombo. Barabara hii kwa miaka mingi katika eneo la Foroforo ilikuwa haipitiki hasa wakati wa mvua. Lakini Wizara katika mwaka 2002/2003 walitenga fedha maalum za kutengeneza eneo hilo. Nawapongeza sana.

Pamoja na juhudhi hizo bado eneo hilo halijamalizika ninaomba sana Wizara izingatie kuongeza fedha ili kuimalizia yote kilomita 15. Itakuwa ni jambo la kusikitisha iwapo eneo hilo la Foroforo litaendelea kuwa kero. Ni bora nguvu kubwa ikatumika hapo ili tatizo la eneo hilo liishe kabisa. Hii ninamaanisha ziongezwe fedha za kumalizia eneo hilo ili kukamilisha ujenzi wa eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, ombi lingine muhimu ni barabara hiyo ya Korogwe-Mashewa-Mtoni Bombo kutengenezwa maeneo korofu yote. Nikizungumza Korogwe Mashariki ni barabara hiyo kwani inahudumia Kata zote kumi. Pia barabara hiyo inatumika kwenda Tanga kwa kupitia Daluni, Maramba, Mabokweni hadi Tanga Mjini. Kwa hiyo utaona ni barabara muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine ninayoomba ishughulikiwe kwa kiwango cha changarawe ni kutoka *Old Korogwe-Muyuzi* hadi Maguzoni. Barabara hii ni nzuri sana ila inatengenezwa kwa kubabaisha. Inahitajika kuwekwa changarawe. Kinachofanyika kila mwaka ni kuweka vumbi badala ya changarawe. Nimeomba sana na kusisitiza barabara zetu ziwekwe changarawe badala ya kuchongwa tu na kuweka vumbi. Barabara zetu hizi zinapitika wakati wa kiangazi tu. Wakati wa mvua barabara hazipitiki kwa sababu ya kuchonga au kuweka vumbi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, ni bora kutengeneza kilomita chache kidogo kidogo kwa kuweka changarawe kuliko hii tabia ya Makandarasi kuchanga tu. Barabara zetu hazikomai zinakuwa changa kila mara kwa sababu ya kupiga greda au kuchonga. Makandarasi wengi hawapendi kuweka changarawe ila wanapenda kuchonga tu. Ninashauri sana tabia hiyo ikomeshwe.

Mheshimiwa Spika, nianomba daraja la Songea Magoma litengenezwe. Hali yake ni mbaya sana. Wakati wowote mvua kubwa zitakaponyesha daraja hili litaporomoka. Ninapenda kuendelea kushauri kwamba barabara zangu zote mbili Korogwe-Mashewa-Mtoni Bombo hadi Mabokweni na barabara ya Korogwe-Mnyuzi-Maguzoni zitengenezwe katika maeneo korofu tu. Mimi naamini maeneo hayo yaktengenezwa kwa awamu tutafika na barabara yote itakuwa inapitika kwa mwaka mzima wakati wowote. Makandarasi wasimamiwe kwa karibu ili watekeleze inavyopaswa. Makandarasi wengi wanalipwa tu (Serikali na hata Wizara iwe na utaratibu wa kuwadhibiti Makandarasi).

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa niaba yangu na wananchi wa Wilaya ya Korogwe wanaipongeza Wizara kwa kukumbuka kilio chao cha miaka mingi cha kutengeneza kipande cha kutoka *Korogwe Girls* hadi *Old Korogwe* yenyeye urefu wa kilomita tatu. Tunatoa shukrani za dhati na wananchi wanawaombea kila la kheri katika kuleta mafanikio ya Wizara, cha muhimu Mungu awajaalie baraka na maisha marefu.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mpaka hapo ndiyo tumefikia mwisho wa mjadala wa jumla kwa Wizara ya Ujenzi. Kwa hiyo, tukirudi jioni watoa hoja wataanza kujibu, tukianza na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, halafu mtoa hoja mwenyewe Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa John Magufuli.

Baada ya maelezo hayo sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11 jioni.

(*Saa 06.49 mchana Bunge lilifungwa m paka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia*)

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie hoja iliyo mbele yetu ya Wizara ya Ujenzi. Kwa sababu hoja yenyewe ni ya Wizara ya Ujenzi na mimi ni Naibu Waziri wa Ujenzi itakuwa ajabu sana kama suingi mkono hoja hii. Kwa hiyo ninaunga mkono asilimia mia moja. Nisije nikasahau. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa ukiachilia mbali zile za kuja hapa kuwajibika kujibu maswali. Niwapongeze Wabunge wapya walioingia kwenye Bunge hili na wale waliorudi na wale walioingia upya kabisa. Nimpongeze Waheshimiwa Wabunge wawili waliofunga ndoa. Wao wametengeneza historia kabisa katika Bunge hili na *inshallah* Mwenyezi Mungu atawabariki huko mbele wako wengine watakaotengeneza historia hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Magufuli, akiwa Waziri wa Ujenzi sio kwa kumpamba kwa haki kabisa. Matokeo ya hotuba hii ambayo mmeisoma mnayo mkononi naweza kusema ni matokeo ya usikivu na uvumilivu wa Waziri Magufuli. Wale ambao wamekwenda Ofisini kwake aliwapoeka akawasiliza na

pengine akawashauri waandike na wale ambao amewaaahidi asilimia 96 ametekeleza ahadi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mno mno ni desturi yake ya kushirikiana. Mimi nimepata bahati ya kufanya kazi naye mfululizo tangu nimechaguliwa kuwa Naibu Waziri kwa hakika hajawahi nikaenda kwake nikatoa ushauri akaniambia huo sitaki, lugha hiyo hana. Ila mara nydingi ukiona hakubaliani na wewe atakwambia tujadili tena, maana yake nenda karifikirie, lugha ya ustaarabu kabisa na mimi nilipenda hilo. Na hiyo lugha nilifundishwa na Mwalimu wangu, wengi hamjui kama nina Mwalimu mimi hapa amenifundisha Mwalimu Ng'andu. Alinifundisha Shule ya Sekondari. Mheshimiwa Ng'wandu. (*Makofi*)

Lakini jambo lingine la kupendeza juu ya Mheshimiwa Magufuli ni jinsi anavyowathamini watalamu wake. Kama humjui sana Mheshimiwa Magufuli unawenza kusema ni mkali sana, lakini kumbe si mkali ni tabia ya lugha ya Kisukuma tu, Kiswahili nafikiri kinawagongagonga sana. Kwa hiyo anapopata nafasi ya kukatiza maneno anayakatiza. (*Makofi/Kicheko*)

### **WABUNGE FULANI:** Hoja !!!

### **NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Hoja ndiyo hii hii Waziri wa Ujenzi. (*Makofi*)

Nitakuwa siwafanyii haki wataalamu ambao wengine mnatengenezewa barabara tu hamjui wanahuksika vipi. Sasa ni vizuri nikawataja wawili, watatu mkajua jinsi wanavyohusika kwa utengenezaji wa barabara moja kwa moja. Mnamfahamu Ndugu yangu Kijazi, yeye ni Katibu Mkuu na wajibu wake unafahamika wazi wazi. Lakini kuna mtu mmoja ni *quiet giant* mwanamke hodari sana, Mama Rose Mang'enya. Huyu ni Mwenyekiti wa Mfuko wa Barabara. Yeye ndiye anayetoea fedha kwa *TANROAD* kwa kukarabati barabara na *TAMISEMI*. Yeye ndiye anayesema Wilaya fulani Mheshimiwa Waziri haistahili kupelekewa fedha kwa sababu hajjarudisha ripoti. Yeye ndiye anayetoea mkataba wa utengenezaji barabara kwa *TANROAD*. Ni muhimu sana kwetu, hodari lakini ni mtu anayependa sana kushirikiana na wenzake na Wizara. Kwa hiyo, nadhani nisingmfanya haki bila kumzungumzia hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ebu nijibu hoja chache tu za Waheshimiwa Wabunge kwa sababu Waziri wangu yeye atakuja kumalizia hii kazi. Ingekuwa amri yangu kwa jinsi Waheshimiwa Wabunge walivyochangia nilipokuwa nakaa pale nilimwuliza Waziri hivyo nikaseme nini? Si nikisema tu ahsanteni sana, halafu nikae chini. Lakini nimeona si vizuri, ni vizuri nikachangia baadhi ya hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib, Msemaji wa Kambi ya Upinzani yeye alisema tuna mkusanyiko wa Taasisi mbalimbali ndani ya Wizara lakini tuna Makandarasi wasiofaa na tunawapa kazi. Tunazo Taasisi nydingi, Asasi nydingi tunazo pale Wizarani, lakini sio pale. Tunayo Bodi ya Makandarasi inajitegemea, inawajibika Wizarani. Tunayo Bodi ya Menejimenti bahati nzuri Mwenyekiti wake amejibu vizuri sana maelezo hayo. Tunayo Bodi ya Ma-engineer nayo inajitegemea inawajibika Wizarani. Tunayo Bodi ya Wajenzi na Wasanifu wa Majengo naye inajitegemea.

Lakini wote hawa hawapewi kazi wanaotoa wao wote hawatoi kazi kwa Mkandarasi yoyote. Chukua Bodi ya Makandarasi wanaotoa kazi ni watu binafsi, Mashirika ya Umma na Madiwani pamoja na Wabunge huko kwenye Wilaya zetu. Tunatangaza tenda tunawapa wao wanafanya kazi. Inapotokea dosari na sisi sasa tunawajibishwa kwa kutoa taarifa ndipo hapo sasa tunawaambia wao ebu nenda kachunguze Mkandarasi huyu ambaye amechukua kazi hii anaambiwa anafanya kazi yake chini ya kiwango kwa nini. Wao ni Mkandarasi mwenzao, wanakwenda kuchunguza. Kama ni suala la standard watamchukulia hatua wao, kama ni suala la rushwa watatoa taarifa na sisi tunatoa taarifa kwenye vyombo vinavyohusika wanamchukulia hatua. Huku sisi tunamshtaki wao wanamfuta kama Mkandarasi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Spika, hawatoi kazi wao. Inapokuja kwenye masuala ya Halmashauri ni mgogoro zaidi kwa sababu Madiwani wengi na wao Makandarasi. Sasa Mkandarasi anagawa kazi kwenye Kikao cha Halmashauri Kamati ya Fedha, Mkandarasi anageuka kuwa ndiye anayetoa zabuni. Kwanza anaomba zabuni halafu anakwenda kukaa kwenye kikao cha kutoa zabuni, zaidi atajipendelea. Huo ndio mgogoro wa kwanza uko Halmashauri tunajigawia kazi. Hilo lisiposahihishwa fedha zinazotolewa na TAMISEMI hazitaonyesha dalili nzuri kwa barabara za Wilaya.

Niende kwenye hoja nyingine ya Mheshimiwa Mntangi. Yeye amesema hali mbaya ya barabara ya Mkoa ya lami Muheza/Amani kilomita 15 iwekwe lami kwa kutumia teknolojia ya water feel kwa mwaka 2003/2004. Mheshimiwa Mntangi hili limezingatiwa kwa mwaka 2003/2004 lakini barabara ya lami kilomita 1.5 Muheza Mjini itawekwa lami kwa *water feel*. Ukitazama ukurasa 75 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri yenye jedwali Na. 17 utaona ipo hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Dr. Luoga yeye anaomba barabara ya Mbinge/Mbambabay ambayo imetengewa fedha za mkopo kutoka *ADB* lakini hakuona maelezo yaliyotolewa katika hotuba ya Waziri. Mheshimiwa Luoga maelezo yapo katika kiambatanisho 7(i) yapo pale maelezo kabisa ya fedha hiyo.

Mheshimiwa Edson Halinga yeye anasema vikao vya Bodi ya Barabara ya Mkoa visiitishwe wakati Wabunge wakiwa Bungeni ili kukwepa maswali watakayo wauliza watendaji na *sitting allowance* ya shilingi 10,000/= haitoshi. Mimi nakubaliana kabisa na la kwanza kwamba kuitisha vikao vya *Road Board* wakati Wabunge wako Bungeni ni kukwepa kuulizwa madhambi. Kwa mantiki hiyo nachukua nafasi hii kuagiza *Ma-Regional Managers* wawasiliane na Wenyekiti wa vikao hivyo amba ni Wakuu wa Mikoa kwamba vikao vikae wakati Bunge halikai. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juu ya shilingi 10,000/= haitoshi kwa vikao vile kwa hivi sasa tunaomba Waheshimiwa Wabunge wastahimili wapokee zile shilingi 10,000=/. Najua ni ndogo sana na Waswahili husema “Mazoea hujenga tabia, lakini tabia hurekebishika”. Kwa hiyo, wakati ule ambapo mnakwenda kule tunaomba mtumie kama Madiwani wengine wote wanaokuja pale kupokea hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Janguo, yeze anaona kasi ya ugawaji wa fedha za Mfuko wa Barabara imepungua, kasi ya ugawaji imeongezeka kulingana na kabla Bodi ya Mfuko haijaanzishwa, na hivi sasa fedha zinatolewa kwa kila mwezi zinapatikana. Halmashauri iwjibishwe kuweka wazi. Wakurugenzi waweke wazi mapato ya fedha za barabara. Kwa vile mkusanyo wa kodi umeongezeka sana na Serikali imesamehewa madeni mbona fedha za mgao hazongezeki. Ni suala lingine ambalo linafanana na lile na kwa mantiki hiyo basi nimsomee tu jinsi *Road Fund* au Bodi ya Mfuko wa Barabara ilivyopeleka TAMISEMI. Mwaka 2000/2001 walipeleka shilingi 10,846.88 bilioni. Mwaka 2001/2002 walipeleka shilingi 15, 236.40 bilioni. Mwaka 2002/2003 walipeleka 17,886.18 bilioni. Mwaka 2002/2004 tunategemea watapeleka 19,145.5 bilioni. Kwa hiyo, fedha zipo naamini kwamba zinakuja tafadhalini mhakikishe ile *priority* yenu ya kipaumbele za barabara zinafuatwa.

Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, yeze ameuliza juu ya barabara ya Msata/ Handeni/Korogwe iwekewe lami. Wazo zuri, lakini uwezo hakuna, pamoja na hiyo asubuhi leo nilikuwa nimejibu swalii la Mheshimiwa Christopher Semanini Wegga juu ya barabara hiyo na nimesema hatua gani zinaendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Salome Mbatia anasema yeze barabara ya Dar es Salaam/Bagamoyo ipanuliwe kupunguza msongamano. Barabara hii ipo kwenye mpango wa kupanuliwa chini ya *Master Plan* ya barabara za Jiji la Dar es Salaam kwa ufadhili wa Serikali ya Japan kuanzia Kiwanda cha *Saruji Wazo Hill* hadi Mbagala. Kwa hiyo, kama una kibanda hapo njiani kianze kukiwekea *X* wewe mwenyewe. Mheshimiwa Elizabeth Batenga yeze aliomba barabara ya Karagwe, Mugakorongo/Rwambahizi/Bugala/Busindi/Bukomola/Mulongo inastahili kuwa ya ulinzi. Halmashauri inashindwa kuhudumia, naomba Waziri afikirie kuichukua. Wizara inapitia upya ordinance ambayo itajumuisha barabara za kupanda madaraja kufuatilia vigezo vilivyowekwa na barabara hii pia itaangaliwa. Prof. Mwaga yeze anazungumzia barabara ya Mpwapwa/Gulwe hadi Kibakwe haionekani kwenye kitabu. Anaomba maelezo. Barabara hiyo ipo na imejumuishwa kwenye mpango wa matengenezo ya kilomita 282 za Mkoa wa Dodoma kwa mwaka 2003/2004. Ukiangalia kiambatanisho namba 7 (d) ukurasa 73 utaikuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga yeze anauliza *TANROADS* wapewe jukumu la kujenga barabara ya miji mikuu na ya Wilaya. Hili ningeiomba nilizungumzie kidogo. *TANROADS* wameanza mwaka 2001/2002 bado wako katika hatua mbalimbali za kujipanga. Waheshimiwa Wabunge pamoja na kwamba wanafanya kazi nzuri sana *TANROADS* tuwaache basi tuone wamejipanga vizuri kweli kweli. Tukiwabebesa mzigo wa barabara za Wilaya halafu tukaenda kwenye barabara za Vijijini na wakashindwa tutarudi pale pale kuanza kuwasema kumbe wenzetu walipokuwa ndiyo kwanza wanajifunza kusimamia kutumia viambaza na ndoo sisi tulidhani wanakimbia. Mimi nafikiri ni vizuri tuwaache kwanza *TANROADS* wafanye kazi hizi kwa sababu bado tuna kazi kubwa sana ya barabara za udongo kugeuka kuwa barabara za changarawe na barabara za changarawe kuwa barabara za lami na bado tuna kazi kubwa sana ya kuunganisha mikoa kadhaa iweze kuunganishwa kwa barabara za

lami katika nchi hii. Kazi hizi zote za kusimamiwa zitasimamiwa na *TANROADS* pamoja na ukarabati wa barabara ambapo zipo sasa.

Mimi ningewaomba Waheshimiwa Wabunge tuwaachie hii *TANROADS* hii kazi tuliowapa waifanye kwa uhakika tutakuwa na barabara nzuri sana kulikoni tukiwaongeza mzigo. Najua nimekwishatembelea baadhi ya Halmashauri tatizo ni Ma-*Engineer* wa Wilaya. Hakuna Ma-*Engineer* wa Wilaya. Anaweza kuwepo mjenzi wa nyumba ndio anakuwa mjenzi wa barabara. Ni bahati mbaya sana nimewakuta wawili watatu na nikuzungumza nao anasema Mzee habari ya barabara mimi sijui. Lakini huyu *Engineer* wa Wilaya, ni kwa sababu ya ukosefu tu wa kutokupata Ma-*Engineer* wa Wilaya. Lakini sasa hivi Chuo Kikuu kinaendelea kutupa Ma-*Engineer*. Nina hakika baada ya miaka mitano vijana hawa watakuwa wameingia huku na wamejaza nafasi. Bahati nzuri mkiangalia sura za wale kule watendaji wetu kama hawa hapa ndio wazee basi hao waliobakia huko ni vijana mno. Ndio kwa kawaida mwenye madaraka huwa mtu mzima. (*Makofii*)

Sasa hapo mimi simwoni mtu mzima unaweza kuona sura zile zote zimenawiri, bado changa. Sasa huko ni wachanga zaidi, kwa hiyo wana muda, wana nafasi ya kufanya kazi hizi vizuri sana na wataendelea kufanya. Mimi naomba tustahimili tuwaachie wafanye Halmashauri na wapokee fedha wajibike kutumia fedha hizi kwa barabara tu, bado Wakurugenzi fulani fulani hawaoni umuhimu wa kutumia fedha za barabara kwa barabara tu wanapenda kupeana posho. Sasa tuna tatizo kubwa sana kwamba kodi ya maendeleo ambayo ndiyo ilikuwa fedha inaingia pale mahesabu yao wanayajua wao sasa haipo na hiyo fedha italetwa. Kwa hiyo tusipokuwa macho kwenye Halmashauri tuna hatari ya kunyang'anywa hata hizi fedha za TAMISEMI. Kwa sababu zikitumika vibaya tu basi mtapata athari ya kusimamishwa. Hii mkitaka kujua vizuri mwulizeni Mheshimiwa Msabaha na Mheshimiwa Mbunge wa Bagamoyo wao walisimamishiwa fedha hizi kwa muda wa miezi mitano kwa sababu Wakurugenzi wao walizitumia fedha hizo kwa kazi zingine kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kujibu hoja hizi za baadhi ya Wabunge mimi naomba nirudie mwito wangu kwa mwaka jana. Nitarudia mpaka tukakubaliane. Tutaendelea kutengeneza barabara za udongo na barabara za changarawe kila mwaka mpaka tutakapokuja kugundua hali halisi kwamba hatuendi mbali kwa sababu moja tu. Wakati tunajua kuna mikoa kadhaa haijaunganishwa kwa barabara za lami bado sisi watu binafsi tunataka vibarabara vyetu vidogo vitengenezwe kwa lami. Tusipokuwa tayari kufanya hii kazi Kitaifa hatumsaidii sana Waziri. Kupanga kwamba sasa wakati umefika barabara zile ambazo zinatakiwa ziunganishe mikoa ile ambayo haijaunganishwa na lami tuunganishe tusiendelee kuomba barabara zetu zitengenezwe kwa lami. Mwombe barabara zipitike ili mikoa mingine hii nayo yote tuunganishe kwa lami ndiyo mapinduzi halisi ya uchumi yatapatikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya aibu kubwa ambayo kila siku inatusuta Waheshimiwa Wabunge wote wakati tunakaa kwenye vikao ni kumuona Mbunge wa Kusini inabidi apite Morogoro badala ya kupitia Iringa kwa sababu hakuna lami. Sasa mikakati lazima tukakubaliane kwamba utafika wakati Wizara italetwa hoja kwamba

barabara hizi sasa tutatumia fedha zetu ama za wafadhili kwa kujenga barabara ya mikoa hii michache mitano iliyobakia ipate lami kwa makusudi. Hili ninawaomba na naendelea kuomba kwa sababu wakati Waziri atakapoleta hii msishtuke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize kwa hadithi ndogo sana aliyenihadithia mjomba wangu. Mjomba wangu alinihadithia hadithi ya Pete ya Binti Mfalme wa Uginingi. Waliosoma *ESSOPO* wataijua na wale waliosoma Abunuwasvi vijana kama mimi wataijua. Kulikuwa na Binti Mfalme na yule Mfalme wa Ugining alitoa agizo moja tu anayetaka kumwoa Binti yake akachukue pete Makao Makuu ya Uginingi. Aah Maruhani naam !!! Lakini kufika kule lazima upitie mahali utamkuta Bibi kizee amejaajia tongotongo mchafu wa kupindukia, huyo ndio kigezo chako cha kwanza. Wakapita vijana wengi masharti anakwambia ebu nilambe basi nikuone wewe unayenizungumzisha. Mchafu huyo hawamtaki. Alipopita kijana mmoja akamlamba akamwambia sasa ninakuona. Ukienda kwenye Mji wa Majini ukiwakuta wamenyamaza kimya ujue wako macho, usidhubutu kuingia mjini kwao. Lakini ukiwakuta wanapiga kelele kinyume chake huyo mwizi, huyo pumbavu huyo kamata, huyo anakuja, hao wamelala. Ukiwakuta kimya huko ndiko kwenye utaalam, kila mtu anafanya jambo lake, wako macho. Wataalamu wote wako macho. Kwa sababu ya kufuatilia ushauri ule kijana huyo alipofika pale akawakuta kimya akajua hawa wako macho akangoja walipolala akaenda kuchukua pete ya Binti Mfalme akaja akaoa.

Kwa hiyo, mkiingia pale Wizarani Ujenzi mkifika mambo kimya wale wakubwa wanafanya kazi. Ndio, wako kazini. Zamani palikuwa na kelele kelele sana pale sasa hivi ukiingia ni kimya Ofisini. Usiogope kuingia Ofisi ya Waziri, Naibu Waziri wala ya Katibu Mkuu, unakaribishwa njoo useme tatizo lako na sisi tutakusikiliza. Wale waliokuja kwetu tulipokosa chai na biskuti angalau tumewapa chai bila biskuti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda na mimi nikushukuru na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kupata nafasi ili niweze kuchangia hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Waliochangia ni Waheshimiwa Wabunge 24 walichangia wakati Wizara zingine zilipokuwa zikiwasilisha hoja zake. Orodha ya Wabunge waliochangia kwa maandishi ni 93. Waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni wakati wa hoja yangu wako 28.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nianze kuwataja waliochangia. Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Alhaji Shaweji Abdallah, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mheshimiwa Dr. Batilda S. Burian, Mheshimiwa Prof. Pius P. Mbawala, Mheshimiwa Semindu K. Pawa, Mheshimiwa Herbert J. Mtangi, Mheshimiwa Anthony M. Diallo, Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami, Mheshimiwa Mohammed A. Abdulaziz, Mheshimiwa Lephy B. Gembe, Mheshimiwa Dr. Thadeus M. Luoga, Mheshimiwa Stephen M. Kazi, Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe, Mheshimiwa Edson M. Halinga, Mheshimiwa Athuman S. M. Janguo, Mheshimiwa Leonard N. Derefa, Mheshimiwa

Philip S. Marmo, Mheshimiwa Benson M. Mpesa, Mheshimiwa Ludovick J. Mwananza, Mheshimiwa Ismail J. R. Iwatta na Mheshimiwa Sumri A. S. Mohammed.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Charles H. Kagonji, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Khalid S. Suru, Mheshimiwa Zabein M. Mhita, Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, Mheshimiwa Eliachim J. Simpasa, Mheshimiwa Paul E. Ntwina, Mheshimiwa Remidius Edington Kissassi, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, Mheshimiwa Dr. Chegeni R. Masunga, Mheshimiwa Faustine K. Rwilomba na Mheshimiwa Talala B. Mbise.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Dr. Aisha O. Kigoda, Mheshimiwa Idd M. Simba, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mheshimiwa Prof. Daimon M. Mwaga, Mheshimiwa Shamsa S. Mwangunga, Mheshimiwa Njelu E. M. Kasaka, Mheshimiwa Hezekiah N. Chibulunje, Mheshimiwa Joel N. Bendera, Mheshimiwa Abu T. Kiwanga, Mheshimiwa Salome J. Mbatia, Mheshimiwa Dr. Aaron D. Chiduo, Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mheshimiwa Sijamini Mohamed Shaame, Mheshimiwa Margaret A. Mkanga, Mheshimiwa Stanley H. Kolimba, Mheshimiwa Abdullah S. Lutavi, Mheshimiwa Mgana I. Msindai na Mheshimiwa Karim Said Othman.

Pamoja na hao ni Mheshimiwa Ireneus N. Ngwatura, Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mheshimiwa Major Jesse J. Makundi, Mheshimiwa Dr. Hussein A. Mwinyi, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Benedicto M. Mutungirehi, Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. R. Msabaha, Mheshimiwa Arcado D. Ntagazwa, Mheshimiwa Mbarouk K. Mwandoro, Mheshimiwa Monica N. Mbega, Mheshimiwa Abdullatif Hussein Ismail, Mheshimiwa Mwanaidi Hassan Makame, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mheshimiwa Frank M. Mussati, Mheshimiwa Jumanne H. Nguli, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Bernadine R. Ndaboine, Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa, Mheshimiwa Balozi Dr. Pius Y. Ng'wandu, Mheshimiwa Omar S. Chubi, Mheshimiwa Hasnain M. Murji, Mheshimiwa Aridi M. Uledi, Mheshimiwa Prof. Juma A. Kapuya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Zakia H. Meghji, Mheshimiwa Samwel M. Chitalilo, Mheshimiwa Dr. James A. Msekela, Mheshimiwa Harith B. Mwapachu, Mheshimiwa Mizengo K. P. Pinda, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mheshimiwa Joseph J. Mungai na Mheshimiwa Christopher S. Wegga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Ibrahim W. Marwa, Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Halima O. Kimbau, Mheshimiwa Abdulkarim E. H. Shah, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Dr. Milton M. Mahanga, Mheshimiwa Anatory K. Choya, Mheshimiwa John L. Mwakipesile,

Mheshimiwa Oscar T. Mloka, Mheshimiwa Dr. Thadeus M. Luoga, Mheshimiwa John E. Singo, Mheshimiwa Samwel M. Chitalilo na Mheshimiwa Emmanuel E. Kipole. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Sophia M. Simba, Mheshimiwa Kilontsi M. M. Mporogomyi, Mheshimiwa Beatus R. Magayane, Mheshimiwa Athumani S. M. Janguo, Mheshimiwa Dr. Chegeni R. Masunga, Mheshimiwa Philip A. Magani, Mheshimiwa Prof. Simon M. Mbilinyi, Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, Mheshimiwa Capt. Theodos J. Kasapira, Mheshimiwa Frank G. Magoba, Mheshimiwa Aridi M. Uledi, Mheshimiwa Hasnain M. Murji na Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliota michango yao hapa Bungeni kwa maandishi na kwa kuzungumza. Kwa kutambua kwamba muda niliopewa ni mfupi sana sitaweza kujibu hoja zote zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge waliochangia, ambao ni zaidi ya 109. Lakini napenda kusema wazi kwamba, hoja zao zote tumezipokea, tutazijibu kwa maandishi kabla kikao hiki cha Bunge hakijaisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu nizungumzie mambo ya jumla. Sisi Wizara ya Ujenzi, kama alivyozungumza Mheshimiwa Naibu Waziri, tuna nia kubwa ya kuhakikisha kwamba barabara nyingi zinajengwa kwa kiwango cha lami na hasa baada ya kutambua kwamba barabara zinapojengwa kwa kiwango cha changarawe zinadumu kwa muda mfupi na kwa kweli barabara hizi zinakuwa ni za gharama kubwa kwa Taifa. Kwa hiyo, mipango ipo, tutasaidiana na Wafadhili ili kuhakikisha kwamba barabara nyingi za Kitaifa na zile zinazounganisha nchi yetu na nchi jirani zinajengwa kwa kiwango cha lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miradi ya *East Africa Cooperation's*, Tanzania tuna jumla ya kilomita 4,880 ambazo zimeombwa, kati ya kilomita 10,700 ambazo zinahusisha nchi zote za Afrika Mashariki. Tumeomba jumla ya Dola za Marekani 1,700 ambazo ndizo zitahusika katika barabara hizi. Lakini pia katika kuhakikisha kwamba barabara za Tanzania zinakua kwa kiwango cha lami, tumechukua zaidi ya kilomita 6,000 ambazo tumeziweka kwenye mpango wa *NEPAD*. Kwa hiyo, tuna matumaini kwamba kulingana na fedha ambazo pia zinatengwa na Serikali kwa ujumla, simu moja barabara zetu zote zitakuwa ni za kiwango cha lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, barabara ya kutoka Mtwara - Dar es Salaam - Mwanza, *program* yote ipo na inaendelea vizuri kwa sababu karibu kila mahali sasa kuna Makandarasi. Ukianzia Nangurukuru - Mbwemkulu - Mingoyo kuna jumla ya kilomita 190, pale kuna Makandarasi wawili ambao wanafanya kazi kwa gharama za Serikali ya nchi yetu. Pia, Somanga kuna Makandarasi wanafanya kazi. Daraja la Malagalasi linafanya kazi. Vile vile, daraja la Rufiji liko kwenye hatua za mwisho za matengenezo. Lakini pia tumepata fedha kutoka Kuwait Fund jumla ya Shilingi 20 bilioni ambazo zitaunganisha Dar es salaam - Ndundu na Ndundu - Somanga, katika sehemu iliyokuwa imebaki. Kwa hiyo, unaweza kuona kwamba barabara ya lami itapatikana kabla ya mwaka 2005/2006 kutoka Dar es Salaam hadi Mtwara. (*Makofi*)

Kwa upande wa Dar es Salaam kwenda Mwanza mtaona kwamba barabara ya Dar es Salaam - Mlandizi imekwishakamilika na jumla ya Shilingi 30 bilioni zilitumika. Kwa sasa hivi kuna ujenzi ambao unaendelea wa kutoka Chalinze - Melela ambapo kuna jumla ya Shilingi 33 bilioni ambazo zinatumika na Mkandarasi anaendelea na kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi ujao wa Agosti 2003, tutasaini Mkataba ili kutangaza *tender* kwa ajili ya kuweka *resealing* kutoka Morogoro - Dodoma ambapo kuna jumla ya Shilingi 40 bilioni ambazo zimetolewa na *European Union*. Kutoka Dodoma - Manyoni, Mkandarasi amekwishaanza kazi kwa fedha zinazotolewa na Serikali na jumla ya Shilingi 43 bilioni zimetolewa. Kutoka Manyoni - Singida napo kuna Mkandarasi, *SIETCO* amekwishateuliwa na amekwishaanza kufanya *mobilization*. Kutoka Singida - Shelui ambapo kuna jumla ya kilomita 110, kwa sasa kuna tender ambazo zinaweza kutangazwa mwishoni mwa mwezi huu na fedha zile zimetolewa na *World Bank* kwa ajili ya kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoka Shelui - Nzega ambapo kuna jumla ya kilomita 108, kwa sasa hivi kuna Mkandarasi ambaye anafanya kazi na fedha hizo zimetolewa na *African Development Bank - ADB*. Barabara ya Shelui - Tinde - Isaka - Shinyanga border ambapo kuna jumla ya kilomita 170, tumesaini Mkataba na European Union zaidi ya Shilingi 50 bilioni zitumika, Mkandarasi amekwishapatiaka na anatakiwa kuanza mobilization kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za Mwanza zinaendelea vizuri. Barabara ya kutoka Mutukula - Muhutwe - Kagoma ambapo kuna jumla ya kilomita 130, kuna Makandarasi wanaendelea kufanya kazi kwa kiwango cha lami. Mwezi ujao wa Agosti, 2003 tunategemea kutangaza tender nyingine kwa ujenzi wa lami kutoka Kagoma - Muleba - Biharamulo - Lusahunga ambapo kuna jumla ya kilomita 154 na mradi ule una zaidi ya Shilingi 24 bilioni ambazo zitahitajika katika kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali ya hivyo, tuna program ambayo tumeiweka katika miradi ya *NEPAD* na ya *East Africa Cooperation's* kwa barabara za kutoka Nyakanazi - Kasulu - Kigoma - Mpanda - Tunduma, katika ujenzi wa kiwango cha lami. Miradi hii tumeiweka katika *program* ya *NEPAD* pamoja na *East Africa Cooperation* ili kusudi fedha zitakopatikana kuwe na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami ikiwa ni pamoja na ile barabara ya Mwandiga - Manyovu, pamoja na kwamba sasa hivi tunaitengeneza katika kiwango cha changarawe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za kuanza *feasibility study* katika barabara ya kutoka Tunduma - Sumbawanga zimekwishaanza chini ya ufadhili wa *World Bank*. Kwa hiyo, tunaendelea hivyo, lakini hii ni katika kuhakikisha kwamba tunajitahidi kutengeneza barabara nyingi kwa kiwango cha lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tumeeleza kwamba kuna barabara ya kutoka Mtwara - *Mbamba bay*, *design* inafanyika kwa barabara hiyo. Tunategemea *design* hiyo

itakamilika kwenye mwezi Septemba, 2003 na kuna jumla ya Shilingi 1.0 bilioni ambazo zimetolewa na *Kuwait Fund*. Barabara ya kutoka Makuyuni - Ngorongoro gate, ujenzi wa kilomita 77 unaendelea na kuna jumla ya Shilingi 24 bilioni ambazo zimetolewa na ujenzi uko kwenye hatua nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano barabara nydingine ya kutoka Minjingu - Dodoma - Iringa, ni sehemu pekee ambayo imebaki katika barabara za *Great North Road*. Barabara ile iko kwenye *first priority* ya barabara za *East Africa Cooperation's*. Lakini pia, kwa sababu sasa Serikali imeanza kutenga fedha zake kwa ajili ya ujenzi wa barabara za lami na kwa vile sasa kuna hatua mbalimbali ambazo zinachukuliwa katika barabara ya *Central Corridor*, kuna uwezekano katika Bajeti ya mwaka kesho kama tutaona Wafadhili wamechelewa kutoa fedha na yenewe tuanze kuijenga kwa kutumia fedha zetu ili Makao Makuu ya Dodoma yaweze kupitika vizuri kwa barabara za lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nydingine ambayo nayo inaendelea kujengwa na tumeweka kwa ajili ya design ni ile ya kutoka Usagara - Busisi - Sengerema - Geita - Kyamiorwa ambayo itaungana na barabara inayotoka Mutukula - Sumbawanga. Lakini pia tumeamua ku-open barabara ambazo zipo katika Mkoa wa Tabora na Mbeya. Ile barabara ya kutoka Mbeya - Chunya, kupitia Makongorosi ambayo itakuja kuungana na barabara ya Singida kwa sehemu ya Itigi na barabara ya kufungua Itigi - Tabora kwa kupitia Kaliua - daraja la Malagalasi - Kigoma, hizo nazo tumeziweka kwenye priority number one na design kwa kiwango cha lami kutoka Itigi - Ipole zile nazo tumeziwekea fedha. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, mnawenza kuona kwamba tuna nia ya *ku-open* nchi nzima katika kutengeneza barabara kwa kiwango cha lami ili tuhakikisha kwamba barabara zote zinaendelea vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu spika, suala lingine la jumla ambalo limezungumzwa hapa ni kuhusu nyumba. Suala hili limezungumzwa kwa muda mrefu na napenda kusema kwamba, suala hili lilianza kuzungumzwa tangu mwaka 1963 wakati Tume ya *ADU* ilipoteuliwa, ikaja Tume ya Nsekela na kadhalika. Tume hizi zote zilikuwa na nia ya kuhakikisha kwamba ni kwa namna gani Watumishi wa Serikali wataweza kupatiwa mkopo kwa ajili ya kujenga nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, uala hili halikuanzia Tanzania tu, bali limekuwa likitumika katika nchi mbalimbali na hii imetokana na kwamba nyumba zilizojengwa na ambazo tunazo ni 6,000 tangu enzi za ukoloni. Nyumba hizi hazikujengwa na Serikali ya Tanzania, bali zilijengwa tangu enzi za ukoloni na katika Bajeti ya karibu miaka mitano, fedha kwa ajili ya kuzifanya maintenance zimekuwa hazitolewi! Kwa hiyo, hizi nyumba zimefikia katika hali mbaya. Nyumba hizi tungeziuza katika market value ni kweli tungeweza kupata fedha nydingi, lakini wale ambao wangenunua si wafanyakazi ambao kwa kweli wengi ni Watanzania na nia yetu ya kuwasaidia wafanyakazi hao isingetimia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuuza nyumba katika nchi hii limeanza siku nyingi. Kwenye mwaka 1972 nyumba 1,900 za National Housing ziliuzwa na waliuziwa wakazi waliokuwemo mle. Kuna nyumba nyingi za *GAPEX, NBC, ATC*, na kadhalika ziliuzwa. Nyumba hizi zote zimekuwa zikiuzwa kwenye *market value* na waliokuwa wanazipata siyo wafanyakazi wa kawaida. Kwa hiyo, tulijua kabisa kwamba hizi nyumba kama tungeziuza katika *market value* tungkuwa tuna-create class ya watu wenye fedha wa kuzinunua hizi nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Sera ya Chama cha Mapinduzi ni kuhakikisha kwamba inajenga uwezo wa Watanzania wote, ndiyo maana tuliamua kuziua nyumba hizi kwa wafanyakazi na fedha zitakazopatikana ni karibu Shilingi 24 bilioni. Fedha hizi badala ya kuzitumia katika shughuli nyingine, zitaendelea kujenga nyumba nyingine na masharti ya zile nyumba ni kwamba, yule anayeuziwa haruhusiwi kuziua hizo nyumba kwa miaka 25! Ni adhabu kubwa sana kwa wafanyakazi, kwa sababu hawezi akaiiza hiyo nyumba mpaka baada ya miaka 25. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa *imagine* kama mtu ana umri wa miaka 50 ukijumlisha na miaka mengine 25 atakuwa na miaka 75 na *life span* ya Mtanzania sasa hivi ni miaka 49. *Obviously* kati ya watakaouziwa hakuna atakayeiuza kwa sababu wote watakuwa wamekwishakufa! Lakini tumeweka masharti mengine kwamba, vile viwanja vyote vilivyo kwenye *prime area* haviuzwi! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niseme kwamba, ninashukuru kwa ushauri mzuri sana uliotolewa na Kamati ya Miundombinu, kwamba zoezi hili tupitie kwa baadhi ya nyumba ambazo inawezekana matatizo yametokea. Napenda niseme kwamba, hili zoezi halikufanywa na Malaika, yapo matatizo ambayo yameanza kujitokeza! Nimeshaambiwa na Mheshimiwa Shekiffu kwamba kuna matatizo kule kwao na tena nimeshaelezwa na Mheshimiwa Marwa. Kwa hiyo, yale mambo ambayo yalikiukwa sisi tutayafulilia na tutatoa taarifa kwa Kamati ya Miundombinu ambayo ndiyo mwakilishi Mkuu katika Bunge hili. (*Makofi*)

(*Hapa umeme ulikatika na kuwaka tena baada ya muda mfupi sana*)

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba 173, nazo tutakuwa makini sana katika kuwagawia wafanyakazi, lakini pia katika Bajeti ya mwaka huu ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeipitisha, tutajenga nyumba zingine 500 katika Mikoa yetu ili kusudi tuwe tunajenga na kuwauzia wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa wito kwa wale wafanyakazi ambao wamenunua nyumba na bado hawajamaliza kulipa na wanachelewa chelewa kulipa. Kwa kweli napenda nitumie nafasi hii kuwaomba walipe, wasipolipa tutawanyang'anya hizo nyumba na tutawagawia wafanyakazi wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Waheshimiwa Wabunge wakichangia wamezungumza kwamba suala hili limewagusa wafanyakazi, lakini pia ingefaa likachukuliwa kwa upana zaidi, hata Waheshimiwa Wabunge siku nyingine nao

wakahusika katika kukopeshwa hizo nyumba. Hilo ni ombi ambalo Serikali imepewa na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu naye amelisikia na ninaamini kwamba suala hilo linaweza kuzungumzika. Kwa sababu hamtapewa bure, mtauziwa kama mnavyouziwa kama mnavyouziwa magari, bado ni utaratibu mzuri na Serikali inaweza ikatoa guarantee kwa hawa Waheshimiwa Wabunge au na kwa watu wengine katika kuendeleza hili suala. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri tumeanza na wafanyakazi, lakini suala hilo linaweza likaongezwa, likahusisha watu wengi zaidi na hii ndiyo maana halisi ya kuwajenga Watanzania na kuwa-empower indigenous kama Waheshimiwa Wabunge wengine ambavyo wamekuwa wakizungumza katika kuwatetea Watanzania wa kweli. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nianze kujibu haraka haraka hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maneno. Mheshimiwa Marwa ambaye alizungumza hapa kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, ametoa ushauri mwangi na nisingependa kuhoji ushauri huo ambao umetolewa na Kamati hiyo, tunauchukua wote na tutaufanya kazi na tutaleta maendeleo ya utekelezaji wake kwa Kamati husika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib; kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, alizungumza maneno mengi na bahati nzuri amezungumzia kuhusu masuala ya siasa na kadhalika. Napenda tu niseme kwamba, baada ya Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib kuteuliwa kama Waziri kivuli wa Wizara ya Ujenzi, nilichofanya nilimpa draft ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi mapema sana. Nilifanya hivyo kwa makusudi ili aweze kupata mchango mzuri na aelewé Wizara ya Ujenzi inavyokwenda kwa sababu yupo katika kujifunza. Kwa bahati mbaya Mheshimiwa Danhi Makanga hayupo hapa, lakini alikuwa amekwishaelewa sana ni namna gani Wizara ya Ujenzi inavyokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Khatib amezungumzia umuhimu wa barabara ninamshukuru sana na amezungumzia barabara za Bagamoyo. Pia, amezungumza kuna taarifa kwamba nyumba za National Housing zilijengwa na kukarabatiwa kwa fedha nyingi, hiyo si kweli. Vile vile, amezungumzia Bodi ya NBMM ni ya watu ambao hawana qualifications! Ninawashukuru sana Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga na Mheshimiwa Dr. Chegeni Masunga, walimjibu na ninafikiri ameelewa. Napenda kusema kwamba Bodi hii inafanya kazi nzuri sana na imetusaidia sana na katika hatua ambazo Bodi hii imechukua, ni pamoja na kufukuza wafanyakazi zaidi ya 253. Kwa hiyo, nilifikiri Mheshimiwa Waziri kivuli huyo angeweza kusifu hizo shughuli zinazofanywa na Bodi hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, amezungumzia kwamba barabara ni duni na hiyo ni kutokana na uongozi usiokuwa na makini! Nilifikiri nilipompa Bajeti yangu angeweza kuangalia na Bajeti za miaka ya nyuma. Bajeti ya mwaka huu ni Shilingi 244.5 bilioni na fedha hizo ni kwa ajili ya kutengeneza barabara tu! Sasa yeye anasema Serikali haiko

makini na kadhalika, nilifikiri kwamba atatoa mawazo ya kusema sasa fedha zitapatikana wapi! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilifikiri unapokuwa na Waziri kivuli wa Wizara yako anaishauri Serikali na nilitegemea kwamba labda angeweza kutushauri ni namna gani ya kupata fedha, hata kama ni kwa maruhani sisi tungezipata hizo fedha ili kusudi tutengeneze barabara, lakini yeche amezungumzia tu kwa kuponda. Nafikiri ukweli unajionyesha kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inafanya kazi nzuri katika kufungua barabara zake. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mohamed Rishedi Abdallah ametoa pongozi nyingi na amezungumzia kuhusu barabara ya Tanga - Horohoro na kuhusu ujenzi wa kivuko cha Mto Wami. Wizara ya Ujenzi imetenga fedha kwa ajili ya kutengeneza kivuko cha Mto Wami ili kusudi kiweze kutumika. Lakini pia tumepokea ushauri wake kwamba, mahali ambapo tunaweza kutengeneza madaraja ni vizuri tukatengeneza madaraja badala ya kutumia *ferry*. Tatizo tulilonalo ni kwamba kutengeneza daraja ni gharama kubwa sana, ukilinganisha na hatua ya mwanzo ya kutengeneza *ferry* mahali pale panapotakiwa. Ushauri wake tumeuzingatia na tutaufanyia kazi, mara uwezo utakapopatikana mahali ambapo panastahili kutengenezwa daraja tutalitengeneza, badala ya kutumia *ferry*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Mheshimiwa Mohamed Rishedi Abdallah, amezungumzia barabara ya Horohoro - Dar es Salaam, kwamba barabara hiyo ni muhimu katika masuala ya kufungua utalii. Tunakubaliana naye kwamba barabara hiyo tunaifanyia kazi na tunajaribu hata kutafuta wawekezaji kwa njia ya *BoT* kama wataweza kukubali barabara hiyo na kuitengeneza kwa kiwango kizuri ili iweze kufungua eneo hilo kiuchumi. Lakini kwa upande wa Tanga - Horohoro kwa sasa hivi madaraja yanatengenezwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia na stage ya pili itakuwa ni kutengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Halima Kimbau, amezungumzia kuhusu umuhimu wa barabara za Mafia. Ni kweli kabisa kwamba fedha nyingi zimekuwa zikitumika kwa ajili ya kutengeneza barabara hizi, lakini pamekuwa na tatizo la upatikanaji wa udongo na hali halisi ya huko Mafia. Alitaka tufafanue kwamba ujenzi wa barabara za Mafia unahusika na barabara ipi? Zile Shilingi 50 milioni zimetengwa kwa kuhusisha barabara ya *Custom - Kiindoni - Utete*. Kwa hiyo, hizi fedha zitatumika kwa sasa hivi, lakini kwa baadaye katika mpango wa mwaka huu tumepanga tutatumwa Wahandisi ili waweze kukagua barabara hiyo yote, tuangalie uwezekano wa kuitengeneza kwa mpango wa lami ya *OTASEAL*, ambayo itadumu kwa muda mrefu na kupunguza gharama za kufanya *maintenance*. Lakini kwa hatua za mwanzo tumetenga hizo Shilingi 50 milioni ambazo zitasaidia katika kuhakikisha kwamba barabara hiyo inatengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Abdulkarim Shah naye alizungumzia kuhusu suala la barabara za Mafia, tutazingatia ushauri wake na tutaangalia ni namna

gani tunaweza tukasaidia Mafia kuweza kupata vifaa kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Said Nkumba amezungumzia kuhusu barabara zake na ametoa shukrani nyingi sana, tunashukuru sana na pia, amesema kwamba ataendelea kuomba. Lakini katika Bajeti ya mwaka huu Mheshimiwa Nkumba amepata fedha nyingi sana ambazo zitahusisha barabara yake. Tunashukuru sana kwa ushauri wake. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Selelii amesema nisife hadi kazi zote za barabara zitakapokamiliaka kwani Bajeti ya mwaka 2001/2002 nilikuwa mahututu! Namshukuru Mungu kwamba ameniombea nisife, lakini naomba na yeze Mheshimiwa Selelii asife kwa sababu nafikiri na yeze hahitaji kufa! Lakini napenda kusema kwamba, ushauri wake kwa sehemu ya Sekenke tumeuzingatia na kwa vile kwa sasa hivi tunatengeneza *alignment* nyingine ya kutoka Singida - Shelui, tumeigawanya katika *packages* tatu tutakapoitangaza kwa ajili ya *tender* na hivyo barabara itatengenezwa na haitapitia kule mahali ambapo magari mengi yanaanguka. Lakini hata hivyo katika hatua za dharula tukiwa tunasubiri ujenzi wa lami kwa sehemu hiyo, tutaziba yale mashimo kwa haraka sana. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dr. Mahanga ameelleza mambo mengi na ninamshukuru sana. Mheshimiwa Anatory Choya amezungumzia kuhusu barabara zake za Wilaya ya Biharamulo na ninamshukuru sana kwa mchango wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa ya Bunge ni kwamba, nilipokuwa nikiangalia fedha zilizotengwa katika barabara za Mheshimiwa Choya, ukurasa wa 74 kiambatanisho 7(e) kuna barabara ya Rusumo - Lusahunga Shilingi 400 milioni, kuna barabara ya Kagoma - Biharamulo Shilingi 120 milioni, barabara ya Biharamulo - Buseresere Shilingi 240 milioni, barabara ya Biharamulo - Buseresere nyingine ambayo pia inaenda kwenye Jimbo lake ni Shilingi 75 milioni.

Katika ukurasa wa 80 ni juu ya *Myobozi bridge* Shilingi 35 milioni, ukurasa wa 85 unazungumzia *Corridor Number 2* na ukurasa wa 86 *Corridor Number 4* unazungumzia barabara za *East Africa Cooperation*. Ukurasa wa 61 kiambatanisho namba 5 unazungumzia juu ya barabara ya Kagoma - Lusahunga na hii barabara inapita Biharamulo pamoja na barabara za Biharamulo Mjini, kuna Shilingi 6.518 bilioni. Barabara ya Bwanga - Biharamulo - Kyamiorwa ile ni barabara ambayo inaunganisha kutoka Usagara - Geita - Bwanga - Biharamulo na *section* nyingine ni kutoka Bwanga - Kyamiorwa. Kwa hiyo, nilipiga hesabu ukitoa ile barabara ya Bwanga - Biharamulo - Kyamiorwa, zile nyingine ambazo zinapita kwenye barabara ya Mheshimiwa Choya ni zaidi ya Shilingi 7.5 bilioni ambazo zimetumika. Kwa hiyo, nafikiri ni katika hali nzuri tu ya kuhakikisha kwamba barabara zikiwemo za Mheshimiwa Choya zitatengenezwa kwa kiwango cha lami. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara ya Mheshimiwa John Mwakipesile ile ya Mbeya - Ibanda - Itungi, tumempa Shilingi 100 milioni ili ziweze kukamilisha zile

kilomita 8 zilizobaki na barabara ya Kasusa - Matema beach tumetoa Shilingi 40 milioni ili ziweze kusaidia kumaliza tatizo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara za Mheshimiwa Mloka tumetoa Shilingi 10 milioni ambazo zitasaidia katika kufanya alignment kwenye ile barabara, lakini huku tukiwa tunafutilia fedha nyingine zikipatikana. Tumegundua kwamba katika kulipa gharama ya barabara hii ziliongezeka *charges* nyingine na kulipwa zaidi ya Shilingi 1.3 bilioni. Lakini tutaendelea kusaidiana kuhakikisha kwamba barabara hii nayo tunaitengeneza ili kusudi iweze kupitika na kutoa usumbufu mkubwa uliopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga amezungumzia mambo mengi ikiwa ni pamoja na barabara zake alizozitaja, tumezingatia na hasa katika mradi wa *RUSIM*. Mheshimiwa John E. Singo naye amezungumzia kuhusu barabara zake, tutafutilia suala hilo ikiwa ni pamoja na barabara nyingine tulizozitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Samwel Chitalilo amezungumzia kuhusu barabara yake ya kutoka Nyamililo - Chitalilo. Barabara ile iko chini ya umiliki wa Halmashauri ya Wilaya na kwa vile Mheshimiwa Ngwilizi yuko hapa na ile ni ahadi ya Waziri Mkuu na ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, nina hakika Mheshimiwa Brigedia Jenerali Hassan Ngwilizi atatekeleza ahadi hiyo ili barabara hiyo itengenezwe. Wananchi wa Sengerema wanachohitaji ni barabara itengenezwe, si kwamba fedha zile za barabara ni lazima zitoke Wizara ya Ujenzi au zitoke Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa , fedha hizo ni za Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kipole ametoa mawazo yake, pia, Mheshimiwa Sophia Simba amezungumzia kuhusu daraja la Kigamboni, tunalifanyia kazi na wenzetu wa *NSSF* ili kusudi tutengeneze daraja linalounganisha. Mheshimiwa Mpologomyi amezungumzia kuhusu barabara zake pamoja na barabara ya Mwandiga - Manyovu. Mheshimiwa Beatus Magayame amesifu mpango wa nyumba na kadhalika. Mheshimiwa Athumanji Janguo ameshajibowi. Mheshimiwa Magani amesifu pamoja na Waheshimiwa wengi sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara ya Mbagala, namshukuru sana Mheshimiwa Frank Magoba ametoa ushirikiano mkubwa sana na napenda niwapongeze sana Wananchi wa Mbagala ambao walibomoa nyumba zao na wale ni watu ambao wanahehimu sana Sheria Namba 167 ya mwaka 1967.

Katika mpango wa mwaka huu 2003/2004 tumetenga Shilingi 800 milioni ambazo zitaanza kujenga kwa kiwango cha lami ile *bureau carriageways* kwenye hiyo barabara. Kwa hiyo, baada ya kikao hiki cha Bajeti tutatangaza *tender*, lakini ukweli ni kwamba hakuna *compensation*. Sheria inasema wazi kwamba ukishavamia barabara huwezi ukalipwa *compensation*. Napenda niseme wazi, pamoja na kwamba Mheshimiwa Magoba ni wa Upinzani, lakini katika suala ili ametoa ushirikiano sana na ninapenda nimpongeze sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Hasnain Murji amezungumzia kuhusu barabara yake ya Mtama - Newala. Barabara hii tutaipa Shilingi 40 milioni kutoka kwenye *routine* ili iweze kutengenezwa. (*Makofi*)

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwamba muda wa mzungumzaji umekwisha*)

Mheshimiwa Naibu Spika, muda umekwisha, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, ushauri wao tutauzingatia. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Toa hoja.

**WAZIRI WA UJENZI:** Ninaomba zile fedha zilizotengwa nizipate na ninaomba kutoa hoja. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Naomba nimpe muda wa kusoma hicho kifungu ni pesa zippi anazoomba ili zieleweke kabisa. Soma vizuri hizo pesa unazoomba.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ya mwaka 2003/2004, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Bajeti ya jumla ya Shilingi 244,588.37 milioni ambapo kati ya fedha hizo Shilingi 114,308.8 milioni ni za hapa na Shilingi 129,879.57 milioni ni za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

### **KAMATI YA MATUMIZI**

#### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **Fungu 47 - Wizara ya Ujenzi**

Kifungu 1001 *Administration and General..Shs1,259,602,400/=*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupewa nafasi hii. Ingawa mimi nimechangia kwa njia ya maandishi ambayo nadhani Wizara haijayasoma, lakini vile vile mchango wangu ulikuwa sambamba na wa Mheshimiwa Elizabeth Batenga ambaye amezungumzia kuhusu barabara ya Kayanga. Hiki kifungu ambacho Mheshimiwa umetaja ni *Vote 47 program* ya 10 *Administration, Sub-Vote. 1001, 250100* sasa nilitaka maelezo Mheshimiwa Waziri, amesema barabara alizosema Mheshimiwa Elizabeth Batenga na ndiyo *exactly* ndivyo nilivyosema mimi kwenye ule mchango wangu kwa maandishi.

*Council ya Wilaya ya Karagwe nimekwisha kuiomba Serikali kwamba barabara ile kwa sababu za kiulinzi na usalama kwa sababu tunapakana na DRC na Ruanda na Uganda na hawatabiliki kwamba barabara ile ndiyo pekee inayoweza kutumika kwa sababu za kiulinzi na kiusalama na haijatengenezwa kwa zaidi ya 30 sasa. Je, Mheshimiwa Waziri ama msaidizi wake ama mtu mwininge licha ya mapendekezo yale yalivyokuja, je, wako tayari kumteua mtu aende aione barabara ili siyo kupokea kwa sababu suala la barabara kila mmoja angependa kujengewa barabara. Je, yuko tayari kuiona na kuona hali halisi ilivyo? Nilitaka tu ahakikishe hiyo. (Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ameshasema barabara ya Halmashauri ya Wilaya halafu anataka mimi ndiyo niende nikaione. Hii barabara ambayo ameitaja na kwa vile ameshaleta maelezo yake kwa maandishi, tutamjibu kwa maandishi na kama patakuwa na uwezekano wa kwenda kuiona sisi hatuna matatizo tutakwenda kuiona.

**MHE. BENEDICTO MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namwomba aache kukasirika. Samahani! Maana anakasirika kwa sababu anachosema sisi tumeandika tumemwambia na tunachosema sisi wala hamuwindi pale mtu kwamba huyu ni Waziri au namna gani, sisi tunachomwambia ni umuhimu wa barabara. Kwa hiyo, suala pale tunaliomba ni kwamba uende pale uone barabara kwa sababu ile Wilaya ndiyo yenye wakazi kuliko hata sehemu nyingine. Mimi sitaki kwenda kwenye hiyo na wala hakuna barabara ya lami pale. Kwa hiyo, tungeomba tukubaliane hilo suala la kusema tukiangalia tutakwenda, aende aione ile barabara.

**MWENYEKITU:** Haya Mheshimiwa Waziri, maana Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi anafahamu alipokarika. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Benedicto Mutungirehi tumetoka Mkao mmoja. Nitawatuma wataalam wakaiangalie hiyo barabara. (*Makofi*)

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba ufanuzi tu au maelezo kuna barabara baada ya kugawa Mkao wa Arusha na Manyara Mheshimiwa Rais alitoa ahadi moja nzito, kwamba atajenga barabara ya kudumu kutoka Makao Makuu ya Mkao wa Manyara kuja Olkestimet na Kibaya nichasisitiza hapa ni barabara kudumu kwa sababu umeelezea hapa kwamba barabara ya udongo na changarawe siyo barabara ya kudumu. Sasa ahadi hiyo ya barabara ya kudumu itaanza lini kwa sababu imeonyesha milioni 130. (*Makofi*)

*(Hapa miophone zilizimika ghafla na kurudia hali ya kawaida)*

Mimi nadhani swali langu limeeleweka kabisa naomba Mheshimiwa Waziri atupe ufanuzi zaidi. (*Makofi*)

**MWENYEKITU:** Naomba zingine zizimwe kila inayowaka izimwe, iweke ya yule anayeongea na sisi hapa.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba katika ukurasa wa 68 tumeizungumzia hii Babati Olkestimet shilingi milioni 130 na ni kweli kabisa kwamba Mheshimiwa Rais, alisema hii barabara ni lazima itengenezwa iwe ya kudumu. Lakini tunachofanya sasa hivi tumekwishatuma wataalam kwa ajili ya kuanza kufanya *feasibility study* pamoja na *design* ile barabara ili kusudi iweze kupatikana barabara ya kudumu. Kwa hiyo, fedha hizi zilizotengwa, ni kwa ajili ya kuifanya tu ipitike wakati tukaandaa hiyo mipango mikubwa ya kuifanya barabara hiyo iwe ya kudumu. (*Makofi*)

**MHE. ANATORY K. CHOYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia jana, nilikusidia kuleta hoja binafsi inayohusu matatizo yaliyojitokeza wakati tulipokuwa tunachangia, lakini kutokana na maelezo sahihi ya ufasaha ambayo yanaonyesha kabisa kwamba sasa hatakukuwepo tena na watu wengine kudandia ile hoja kwa kweli nimefurahishwa ni kwamba hii hoja nilikuwa nimeiandaa ilikuwa na kurasa tatu. Nilivyokuwa nimeiandaa hii hoja kutokana na maelezo haya nimeshapata jibu kwa hiyo ni jukumu tu la kamati inayohusika ya miundombinu kama ilivyotuelezea kuhakikisha kwamba inaleta ile taarifa haraka sana iwezekanavyo. Kwa hiyo, mimi nimeridhika na maelezo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kupewa nafasi hii. Wakati nikichangia jana nilizungumzia wasiwas wangu katika barabara ya Sheluhi - Singida ambazo Mheshimiwa Waziri ametaja kama kilometra 109. Mimi sikukusudia matengenezo ya barabara nzima, nilichokuwa nimekusudia ni matengenezo ya pale mlimali Sekenke. Ule mlima una kilometra kama 7 siyo nyingi sana.

Lakini pale kwenye tatizo ni pale kwenye kilele ni pafupi sana kama nusu kilometra. Sasa Waziri amejibu hapa kwamba tumezingatia, lakini hakutaja hata ni kiasi gani ambacho amezingatia na lini kazi hiyo itafanyika kwa sababu nilisema ajali zinatokea mara kwa mara na watu wanakufa na magari yao yanaharibika. Sasa ni shilingi ngapi na ni lini hiyo kazi itafanyika kurekebisha sehemu hiyo? Wasiwas wangu ni huo. (*Makofi*)

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu anayoizungumza Mheshimiwa Lucas Selelii ni kweli pameshaharibika na wakati tulipokuwa tumekutana leo na wataalam akiwemo Katibu Mkuu tumeshatoa maagizo kwamba Mwandisi wa Singida akaanze kazi hiyo ya kuanza kupaziba. Kwa hiyo, katika kipindi cha wiki moja, au mbili mahali pale patakuwa pameshatengenezwa. (*Makofi*)

**MHE. LUCAS L. SELELI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri. Mimi nilichokuwa nimesema izibwe kwa kiwango cha lami kwa sasa hivi kilichopo ni kiwango cha changarawe na hiyo changarawe ndiyo inayosababisha kuwa vumbi na kusababisha ajali. Sasa niliomba kwamba izibwe kwa kiwango lami angalau km 3. Sasa kama ameagiza kiwango cha lami kwa wiki moja kitu ambacho hakiwezekani. Tender yenye we amesema bado anakusudia kuitisha tender kwa hiyo bado muda mwangi utahitajika. Kitu kitakachofanyika sasa hivi ni kutengeneza

haraka haraka ili paonekane pamfanyika tatizo litarudia pale pale. Mimi niliomba Serikali itengeneze kwa kiwango cha lami angalau km 3. (*Makofi*)

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapanga mipango ya kutengeneza barabara huwa inaangalia pia kuzipoteza fedha. Katika maelezo yangu nilieleza kwamba barabara ya Singida hadi Shelehi yenyе jumla ya km 110 kuna fedha ambazo zimetolewa na World Bank zaidi ya shilingi bilioni 50, tender zimeshatangazwa za pre qualification ili kusudi kumpata mkandarasi atakayeshiriki katika kutengeneza hiyo kazi. Kwa hiyo, kama tutapeleka fedha sasa hivi kwa ajili ya kutengeneza lami na kwa maani nyingine ni re sealing km 1 ni shilingi milioni 200 mpaka 250 kwa hiyo km 3 zitatumika shilingi milioni 750.

Kwa hiyo, kutumia shilingi milioni 750 wakati baada ya mwezi mmoja unatangaza *tender* kwa kutengeneza barabara ambayo wala haitafika sehemu hiyo utakuwa ni upotevu wa fedha. Hiyo barabara imekuwa haifiki. Ni vizuri fedha hizo shilingi milioni 750 zikatumika mahali pengine ambapo napo hapapitiki na ndiyo maana nimesema hiyo barabara tutaitengeneza ili kusudi iendelee kupitika mpaka wakati itakapokuwa inatengenezwa barabara ya lami ambayo nayo haipitii kule. (*Makofi*)

(*Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* .... Shs. 208,083,900/=  
Kifungu 1003 - *Policy and Planinng* .... .. Shs. 224,127,100/=

(*Vifungu Viliviyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko*)

Kifungu 2001 - *Electrical and Mechanical* ....Shs.3, 566,322,600/=

(*Hapa Micro phone zilizimika zote ghafla na kurudia hali ya kawaida*)

**MWENYEKITI:** Inaelekea hiyo line ina matatizo. Mheshimiwa Raynald Mrope uzime hiyo ya mbele hapo ataitumia ile ya nyuma. Hiyo ya nyuma inafanya kazi?

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, anafahamu matatizo tunayopata katika vivuko. Mimi nataka anihakikishie kwa sababu Kivuko cha Pangani ndiyo uchumi wa Pangani na ndiyo siasa ya Pangani. Sasa kuna suala zima la periodic maintenance juu ya Kivuko cha Pangani na kuna suala zima la kupata spares kwa sababu imeshajitokeza kwa kipindi kirefu tumepata matatizo kwenye *propels* za mashine ya kivuko kile. Imechukua muda mrefu kuagizia spares na kule ili kivuko kifanye kazi kwa ufanisi zaidi bila kuwa na *interruption* katika suala zima la uvushaji. Sasa anihakikishie tu kwamba katika bajeti hii amekwishatenga pesa za *periodic maintenance* kwa ajili ya mwaka mzima huu wa bajeti hii pamoja na kuhakikisha kwamba spares zote muhimu ambazo zitahitajika ziwepo katika stores ili tuweze kufanya kazi panapotokea matatizo? Ahsante. (*Makofi*)

**WAZIRI WA UJENZI:** Ni kweli kabisa katika siku za nyuma Kivuko cha Pangani kilipata matatizo na ikabidi *spares* ziagizwe na kutengenezwa. Zile *spares* zilizoagizwa zilikuwa ni mpya na kwa sasa hivi kivuko kinafanya kazi. Kwa hiyo, ile maintenance nyingine ambayo ni kidogo inatakiwa ifanyike kwenye kivuko, itaendelea kufanya kulingana na mapato yanayopatikana kwenye kivuko chenyewe kwa sababu vivuko hivi vinatakiwa vijiendeshe na ndiyo maana mtaona fedha zinazokusanya kutoka sehemu nyingine zinatakiwa pia kusaidia kuhakikisha kwamba vivuko vinafanya kazi. Kwa hiyo, napenda kumhakikishia kwamba Kivuko cha Pangani kitaendelea kufanya kazi.

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3001 - *Supplies and Services* ..... Shs. 1,102,177,600=  
Kifungu 5001 - *Buldings* ..... Shs. 1,403,541,900/=

*(Vifungu Viliviyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 6001- *Trunks Roads*.... .... Shs. 50,663,383,400/=

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikichangia kwa maandishi nilikuwa nimemwuliza Mheshimiwa Waziri juu ya ujenzi au ukarabati wa sehemu moja korofsi sana inaitwa Chipike ambayo ilikuwa imeharibiwa wakati wa mafuriko ya mwaka 1990. Sasa katika kitabu chake anaonyesha kwamba kutakuwa na utaratibu wa kuweka makalvati pale. Lakini pale kwa sababu kuna *land slide* na mafuriko ya mara kwa mara na maji yanafika kwa nguvu sana, mimi nina wasiwasi kwamba hizo kalvati zitakawekwa zinaweza nazo zikazolewa na maji ya mvua.

Sasa kulikuwa na mawazo kwamba barabara hii ingepitishwa pembedi kidogo ikafuata tuta la zamani la reli. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri, anihakikishie katika kuweka hizi kalvati kweli ndiyo litakuwa ni suluhisho la kuduma na hapatakuwa na mafuriko baadaye ya kuweka kuondoa hayo makalvati?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa sehemu ya Chipike katika barabara ya Mnazi mmoja kwenda Masasi huwa ina matatizo na hii inatokana na maporomoko yaliyotokea mwaka 1992. Katika hatua za mwanzo za kuhakikisha kwamba hiyo sehemu inapitika katika kipindi cha mwaka mzima ndiyo maana tumeweka fedha ambazo zitahusisha pia katika kuweka makalvati.

Kuhusu pendekexo lake la kwamba hiyo barabara sasa ipitie kwenye tuta lililokuwa la reli kwa sasa hivi hiyo barabara inafanyiwa *feasibility study* ikihusisha mradi wa kutoka Mtwara, Mnazi Mmoja, Masasi, Songea hadi *Mbamba Bay* ambapo kuna jumla ya shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kufanya hiyo kazi na kuna kampuni tatu zinazoshughulikia hiyo. Kwa hiyo, ripoti ya kampuni inayofanya *feasibility study* watakapoamua kupitisha hiyo hilo tutazingatia.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilipokuwa ninachangia nilizungumzia daraja moja kwenye kijiji cha Choba lilivunjika wakati wa mvua za *El-nino* toka mwaka 1998 sasa nipaye kauli ya Mheshimiwa Waziri. Je, Wizara yake safari hii inaweza ikanitengea fedha ili kukamilisha hilo daraja? Ahsante sana.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda ningependa nipaye ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge hilo Daraja la Choba liko kwenye barabara ipi?

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni barabara ya kutoka Tanga - Pangani ambayo inasimamiwa na *TANROAD* Mkao.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti yetu ya mwaka huu tumetenga fedha kwa ajili ya kutengeneza madaraja. Katika Mkao wa Tanga pia umetengewa fedha kwa kutengeneza madaraja. Kwa hiyo hilo Daraja la Choba litahusika katika kufanyiwa matengenezo.

**MHE. ABDULA SULEIMAN LUTAVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hilo nilipochangia kwenye hoja hii nilionyesha wasiwasini kwamba ile feasibility study ambayo Mheshimiwa Waziri, alii taja inayohusiana na barabara ya kutoka Mtwara kwenda *Mbamba Bay*, nilipozungumzia habari kipande kinachohusika kutoka Mtwara kwenda Masasi kwamba kipande hiki anachokimaanisha ni cha kutoka Mtwara kwenda Masasi kuitia Tandahimba na Newala au anamaanisha kwamba ni kipande kinachotoka Mtwara kwenda Masasi ambacho tayari kina lami sasa hivi tunapozungumza kwamba ndicho kitakachojengwa tena kwa kiwango cha lami. Sasa nilipomwuliza amesema ni kipande kile kile chenye lami ndicho tunachotaka tukijenge kwa kiwango cha lami. Sasa nataka iwekwe sawa sawa hapa. Hii *feasibility study* kweli inazungumzia kipande chenye lami tayari, kwamba tunataku tubandue lami tubandike nyingine, au tunazungumzia kipande ambacho kinahitaji kupata hiyo *elevation* ya *status* kupata lami ili iungane na pale Masasi kuelekea *Mbamba Bay*? Nakushukuru. (*Makofî*)

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Feasibility study* inayofanyika kwanza ina malengo mawili ni kuunganisha Bandari ya Mtwara na Bandari ya Lindi ili ziungane vizuri hadi *Mbamba Bay*. Kwa hiyo, kama malengo hayo yote mawili yanatakiwa yakamilike kwa maana nyingine huwezi ukaanza kufanya *feasibility study* ya barabara ukaanza Lindi, ukaenda Mnazi mmoja, ukaenda Mtwara, Tandahimba, Masasi, *Mbamba Bay*. Pale gharama zinakuwa ni kubwa sana. Kwa hiyo, katika *ku-cover* hayo maeneo yote mawili yaani Bandari ya Lindi na Bandari ya Mtwara ndio maana mapendekezo ya *feasibility study* inayofanywa ni kuanzia Mtwara pamoja na Lindi kuja kupita kwenye hiyo lami ambayo kwa sasa hivi imeharibika sana kwa sehemu ya Chipike inapita Masasi hadi *Mbamba Bay*. Kwenye barabara ya kutoka Mtwara, Tandahimba hadi Masasi yenyewe itaendelea kuwa barabara ya Serikali na itaendelea kufanyiwa matengenezo ya kawaida. (*Makofî*)

**MHE. ABDULA SULEIMAN LUTAVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki naona kinahitaji maelezo zaidi. Wasiwasi wangu ni kwamba hivi tunavyozungumza mimi na Mheshimiwa Waziri inawezekana ikawa hatuelewani. Kwa sababu kwenye hotuba hii Mheshimiwa Waziri, amezungumza habari ya ujenzi wa barabara kutoka Dar es Salaam kupita Lindi kuja Mingoyo. Hicho kipande ninachozungumza sasa kwamba kinafanyiwa tena *feasibility study* kuja kuunganisha na Mnazi mmoja ndiyo kipande tayari kwenye programu hii tunayozungumza ya ujenzi wa barabara ya kutoka Mingoyo kuja Dar es Salaam kwenye hii programu kubwa. Swali langu mimi ni kwamba watu wengi kule kwetu wakisikia hii habari ya *Mtware Corridor* wanavyoolewa ni kwamba Serikali sasa inatazama uwezekano wa kukineemesha kipande kile ambacho kweli kinahitaji kufanyiwa ujenzi.

Sasa mimi nadhani tumeshindwa kuelewana kwa sababu pengine Mheshimiwa Waziri ama jiografia ya kule haimfikii sawa sawa au vipi kwa sababu hicho kipande anachozungumza kiko kwenye barabara anayosema mwenyewe na hicho kipande cha Mtware kuja Mnazi Mmoja hapa ni kipande ambacho hakina maharibiko hayo anayoyataja. Sasa mimi nazungumza kwamba kama barabara ni ile ile ya kutoka Mtware kuja Masasi basi hii ambayo ina lami tayari hatuna haja tena ya kwenda kuweka pesa pale badala ya sisi kuendelea kufanya *maintenance* nyingine inayohitajika ambayo aliomba Mheshimiwa Raynald Mrope, lakini kwa kipande kile ambacho kinahitaji kujengwa basi kijengwa kipate hiyo *status* ya kuwa ni kipande cha lami ili iunganike kuelekea *Mbamba Bay* ndiyo ninachosema. (*Makofi*)

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufanya *feasibility study* siyo kwamba barabara ikishakuwa ya lami haiwezi ikafanyiwa *feasibility study*. Unaweza ukakuta ni barabara ya lami ina upana wa mita sita, ikafanywa *feasibility study* ikawa upana wa saba na nusu nakadhalika. Lakini kwa sababu sasa hivi kitu kinachofanyika ni *feasibility study* na *feasibility study* kwa kawaida wanapoifanya huwa wanaangalia pia barabara ambayo ni fupi zaidi itakayounganisha kutoka Mtware hadi *Mbamba Bay* ambapo kuna jumla ya km zaidi mia sita na kitu. Mimi nafikiri tusubiri matokeo ya *feasibility study* ambayo yatamalizika kwenye mwezi wa 9 au 10 halafu yale mapendekezo tutakapoyaona ndipo tutaamua ni wapi barabara ipite badala ya kuanza sasa hivi kubishana barabara inapita wapi wakati hata *feasibility study* bado haijamalizika. (*Makofi*)

(*Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati bila  
mabadiliko yoyote*)

Kifungu 7001 - *Rural Roads* ..... Shs. 1,262,561,000/=

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyojuu wote sasa Halmashauri zetu zina mzigo mkubwa wa kuhudumia kilometra nyingi za barabara. Nilipokuwa nikizungumza asubuhi hapa nilijaribu kuhoji kwamba sheria iliyokwamisha kuzipandisha hadhi barabara zile zinazostahili hajafikisha hapa sikupata maelezo ni lini itafikishwa hapa Bungeni? Nataka ufanuzi zaidi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Mheshimiwa Emmanuel Kipole, alichangia vizuri kuhusu kupandishwa kwa hadhi kwa baadhi ya barabara za Wilaya. Lakini kwa bahati mbaya sana sikuweza kujibu yote kutoka na muda kwa sababu wakati nikiwa najiandaa kujibu hizo hoja zake kengele imelia na mimi ilibidi niheshimu meza. Lakini suala la kupandisha barabara kutoka kwenye hadhi ya Wilaya au ya Mkoa au ya Taifa ni kazi ambayo imeshafanyiwa kazi katika kipindi cha miaka miwili wakati consultant alipoteuliwa, alitembelea barabara zote.

Lakini hili pia ni suala la kisheria, sheria ya mwaka 1973 ya high way *audience* ambayo inatakiwa ibadilishwe. Kwa hiyo, tutakapoleta Bungeni hiyo sheria baadhi ya barabara zitapanda kutoka kwenye *District Road* kwenda kwenye *Regional Roads*. Lakini kuna baadhi ya barabara kutoka *Regional Roads* zitatelemka kuwa *District Roads*. Hii ni kutoka na hii *assessment* iliyofanyika.

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani kama alivyosema kwamba tayari wameshafanya kazi bado sheria kuletwa hapa Bungeni. Swali langu ni lini sheria itakuja hapa, ili hizi barabara ziweze kupandisha au kushushwa?

**WAZIRI WA UJENZI:** Uchambuzi unafanyika kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa sababu si suala tu la barabara litakaloletwa lakini kuna mambo mengine pia ya mabadiliko ambayo yanatakiwa kufanyika katika sheria hiyo.

Kwa hiyo, mara baada ya kumalizika hizo taratibu zingine zote ikiwa ni pamoja na kupelekwa kwenye *cabinet* italetwa hapa Bungeni. Kwa hiyo, ni vigumu kuahidi ni lini italetwa hapa Bungeni. Lakini kazi inafanyika iwe sheria.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu tumeomba barabara ya kutoka Kikweli kufika Usangi ambayo unaunganisha Tarafa nne za Wilaya ya Mwanga na hospitali ya Wilaya, ipandishwe daraja iwe barabara ya Mkoa kwa sababu uwezo wa mfuko wa barabara kuitengeneza ni mdogo na tulikuwa tuna hamu na shauku kubwa ya kujua kwamba maombi haya yamefikia wapi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya kupandishwa hadhi barabara kutoka kwenye barabara za Wilaya kwenda kwenye barabara za Mikoa yako karibu kila Mkoa, lakini mwenye Mamlaka ya kupandisha hadhi ya barabara sio Waziri wa Ujenzi, ni sheria. Ndio maana nasema sheria itakapoletwa Bungeni na kubadilishwa, kuna baadhi ya barabara zitapandishwa zile zitakazokuwa zime-*qualify* na kuna baadhi ya barabara za Mikoa hata *trunk-roads* zitateremshwa.

Kwa hiyo, mara zitakapoletwa hapa ndipo Waheshimiwa Wabunge watakuwa na muda wa kujadili na kuona ni barabara ipi, na kama barabara hii nayo itakuwa ime-*fulfill* zile *conditions* itapandishwa lakini kwa sasa hivi si Waziri wa Ujenzi mwenye Mamlaka ya kupandisha hadhi ya barabara kwa mujibu wa sheria ya mwaka 1973.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilisema tu hoja mbili, ya kwanza imeshakwisha. Katika kifungu hiki, kwa kazi nzuri wanayoifanya Wizara ya kutujulisha Waheshimiwa Wabunge kwa barua kwamba ni fedha kiasi gani zimetumwa Mikoani na mara nyingi barua hizo zinatutaka tufuatilie fedha hizo.

Sasa namwomba Waziri sijui atakubaliana na hili kwamba kwa sababu ya kutokuwa na muda wa kuzuia wakati mwagine *Regional Board Committees* na kwa sababu wakati wanatuma zile fedha tunakuwa hatuna taarifa, tunakuja kuzipata hapa Bungeni.

Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuwaandikia watu wa *Tanroad* Mikoani kwamba pamoja na barua wanazotuandikia na wao watuandikie jinsi walivyotumia fedha zile na kuzipa Ofisi za kila Mbunge jinsi walivyotumia? (*Makofî*)

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kutoa taarifa za matumizi ya fedha za *road fund* ni katika suala tu la wazi la kuwalishwa Waheshimiwa Wabunge ni namna gani fedha zinatumwa kule Mikoani. Sasa ni namna gani zile fedha zimetumika vibaya au zimetumika vizuri, mimi nilifikiri huwa kuna Vikao vya *Regional Road Board* ambapo Mwenyekiti huwa ni Mkuu wa Mkoa na Makamu Mwenyekiti huwa ni Waheshimiwa Wabunge na Wabunge wote huwa wanahudhuria.

Mimi nilifikiri kama kuna matumizi mabaya ya fedha ambazo zimetumwa na amejua labda kuna mahali fedha zile hazikutumika. Mimi namwomba Mheshimiwa Mbunge atuandikie au anijulishe kwamba katika sehemu fulani walisema fedha zimetumika kiasi fulani na hazikutumika na sisi tutachukua hatua. Ni kama hizo hatua ambazo tumekuwa tukizichukua kwa Watendaji amba ni wabadhirifu. (*Makofî*)

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani labda hatujaelewana kitu kimoja. Mimi ninachosema ni kwamba taarifa tunazozipata hapa wakati mwagine zinakuta tumeshapita kwenye ile mikutano, kwa hiyo tunakuwa hatujui jumla ni fedha kiasi gani zimetoka na kwa mfano labda wamefanya Wizara ya Elimu, kwamba hata kama Kamati ya Shule imetumia vitu ambavyo ni *public lazima* muwajilishe.

Sasa mimi nilichoomba ni kwamba Wizara kwa sababu zoezi lenyewe wala haina inachoficha, na yenyele imeomba kwamba kwenye Wizara hii ya Ujenzi, huko chini sasa ndiko wanakoharibu. Ni suala la yule Meneja wa *Tanroad* kutujulisha kwamba imepokea hela hizi, sasa sisi tunakuja tunalinganisha ile barua tuliyopewa na Mheshimiwa Waziri halafu na yeye alivyotumia kwenye zile barabara zilizoko kwenye Majimbo yetu. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi nashangaa sana kwa nini Mheshimiwa Mutungirehi anataka aandikiwe na *Regional Manager*. Ameandikiwa na Waziri amempa taarifa, anataka tena akaandikiwe na *Regional*

*Engineer*, basi Mheshimiwa Mutungirehi achague moja. Tuwe tunampa taarifa *Regional Engineer* wanamwandikia halafu sisi tuache kumwandikia. (*Kicheko/Makofit*)

Mimi nilifikiri barua ya kutoka kwa Waziri au kwa Naibu Waziri ina uzito zaidi kwa sababu imeandikwa na Serikali. Lakini anataka aende kwa Watendaji. Sasa mimi sikatai Mheshimiwa Mutungirehi kuandikiwa na *Regional Engineer* ila achague, tutakuwa tunampa taarifa *Regional Engineer* na yeye anaandikiwa barua na *Regional Engineer* kwa sababu anaona barua ya *Regional Engineer* ndio anailewa zaidi kuliko barua ya Naibu Waziri na Waziri. (*Kicheko/Makofit*)

**MHE. BENSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia kwangu kwa maandishi nilimwomba Mheshimiwa Waziri angalau anipe tamko tu maana nimemwona mara nyingi juu ya barabara ya Ruanda - Iyula mpaka Nyimbili na ile ya Isansa kuunganisha mpaka Itandu. Sasa hajatamka lolote, sijui imempitia mahali au ningeomba anidhahirishie na anipe imani.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikichangia nilieleza kwamba waliochangia kwa maandishi walikuwa Waheshimiwa Wabunge 93. Kwa hiyo, kulingana na ule muda uliokuwepo nisingeweza kuwajibu Waheshimiwa Wabunge wote.

Lakini napenda niseme tu kwamba nitaangalia hizi barabara ambazo amezitaja Mheshimiwa Halinga baada ya Bunge hili ili kusudi kama hizi barabara zitakuwa ni za Mkoa zinahudumiwa na Wizara yangu, napenda kumthibitishia kwamba tutampa fedha ili ziweze kutengenezwa. (*Makofit*)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati  
Bila Mabadiliko yoyote)*

## **MIPANGO YA MAENDELEO**

### **FUNGU LA 47 - WIZARA YA UJENZI**

Kifungu 1003 - *Policy and Planning* ...Shs. 8,597,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati  
Bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu 6001 - *Trunk Roads* ... ... Shs. 88,997,700,000/=

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vifungu hivi kuna makosa ya uchapishaji yamefanyika na niliomba kwa ruhusa yako labda niyafanyie masahihisho. Kwa taarifa I mean.

**MWENYEKITI:** Endelea Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Katika ukurasa wa 94, *Sub-vote 6001 - Trunk Roads; Project* ya 2352 isisomeke Shelui - Nzega bali isomeke Singida - Shelui.

Ninaendelea ukurasa wa 96, *Project* ya 4112 inasomeka Ilunde - Malagalasi, pale pasomeke Uvinza - Ilunde - Malagalasi. Ukurasa huo huo wa 96, *Project* ya 4115 pasomeke Marangu - Tarakea - Rongai.

Mheshimiwa Mwenyejkiti, ukurasa wa 97, *Project* ya 4115 pameandikwa Chalinze - Melela. Ile Chalinze - Melela ifutwe iwe ni *Procurement of Ukara Ferry*. Halafu *page* hiyo hiyo ya 97 *Project* ya 4167 imeandikwa Shelui - Nzega. Shelui - Nzega imerudiwa rudiwa sana, pale ni mradi unaitwa *Trunk Road Bridges*. Ni madaraja yanayotengenezwa ikiwa ni pamoja na Rukwa na kadhalika.

Ukurasa wa 98, *Project* ya 4177 wameandika *Wazo Hill - Bagamoyo*, hapo ni mradi unaitwa Mkuranga - Kitonga - Kibiti. *Project* ya 4180 wamerudia tena Shelui - Nzega, hapo ni mradi unaitwa Tunduma - Sumbawanga. Ukurasa wa 99 *Project* ya 4183, wamerudia tena *Wazo Hill - Bagamoyo*, hapo ni mradi unaitwa Singida - Babati - Minjingu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa masahihisho.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati  
Bila Mabadiliko yoyote*)

Kifungu 7001 - *Trunk Roads* ... ... Shs. 29,016,770,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati  
Bila Mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)  
**T A A R I F A**

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ujenzi ya Mwaka 2003/2004 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha pamoja na mabadiliko ya majina niliyoyataja. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makisio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Ujenzi ya Mwaka 2003/2004  
yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wote nafikiri wameafiki isipokuwa moja hapa. *(Kicheko)*

**WABUNGE:** Maruhani. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupitisha rasmi Makadirio haya ya Wizara ya Ujenzi ya Mwaka 2003/2004 sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.48 Jioni Bunge lilahirishwa Mpaka Siku ya Ijumaa  
Tarehe 4 Julai, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*